# UCHU

## E. A MUSIBA

# SURA YA KWANZA

ARUSHA

Christopher Temu, ambaye Jumapili hii nyumbani kwake Arusha, alikuwa amefikiwa na ugeni mkubwa kutoka Umoja wa wanaharakati wa Afrika (Pan African Movement PAM) kutoka sehemu mbalimbali za Afrika. Temu alikuwa mwanachama wa chama hicho.

Hii haikuwa mara ya kwanza kwa watu hawa kukutana nyumbani kwa Temu kwani watatu kati yao walikaa nyumbani kwake kwa muda usiopungua miezi sita. Mnamo mwaka 1992 na 1993 walihudhuria mkutano uliofanyika Arusha kuvisuruhisha vikundi mbalimbali vilivyokuwa vikipambana katika mgogoro wa nchi ya Rwanda, ili mgogoro huo umalizike kwa njia ya amani

Kikundi hiki cha PAM. ambacho kilikuwa kinahudhuria kama kikundi cha wapenda amani wa Afrika. Kilikuwa kinaweka shinikizo kwa kila upande uliokuwa unahusika na mgogoro huo ili umalizike kwa amani. PAM ilianzishwa mwanzoni mwa karne ya 19 ikiwa na lengo la kupambana na utumwa, ukoloni mkongwe, ukoloni mamboleo, kupigania haki ya watu weusi na kuhakikisha kuwa waafrika wanaweza kupambanua mambo yao wenyewe.

Hivyo, mara hii kikao kilichokuwa kinafanyika nyumbani kwa Temu kilikuwa cha kutathmini juhudi zote zilizofanywa kuumaliza mgogoro wa Rwanda kwa amani, lakini bila mafanikio. Wakiwa wamekaa kwenye bustani nzuri iliyokuwa nyuma ya nyumba hii iliyojengwa kisasa. Ikiwa kwenye barabara ya Njiro kwenye kilima kidogo ikiuangalia mji wa Arusha kwa upande wa Kijenge. Mkutano uliendelea mchana huu wa saa kumi alasiri huku bia aina ya safari na ndafu, iliyokuwa inachomwa hapohapo kwenye jiko la mkaa vikiendelea kuwa viburudisho vya wageni hawa.

"Ndugu zangu. Fundisho kwa Rwanda ni fundisho kwetu sote, na sisi tukiwa tumejitolea kuona Afrika inajikomboa na kujitawala kwa amani ni lazima tukae chini kulitafakari swala zima la Rwanda tuone makosa yalitokea wapi, na kwanini hali ilifikia hapo ilipofikia na watu zaidi ya milioni moja kuteketea bila Afrika wala dunia kufanya chochote", Jackson Musoke kutoka Uganda ambaye pia ndiye Mwenyekiti wa PAM Kanda ya Afrika Mashariki alieleza.

"Ni kweli kabisa maneno uliyosema, lakini mimi nafikiri wakati mkutano wa amani ulipokuwa unaendelea hapa Arusha. Ukweli wa mambo Rwanda ulikuwa haufahamiki. Na hivyo maamuzi mengi yaliyofanyika hayakuzingatia hali halisi ya mambo ilivyokuwa Rwanda wakati huo. Na ningependa niseme kuwa hata hivi sasa tunavyokaa hapa hali halisi na ukweli wa mambo Rwanda bado haujulikani. Ndio maana Jumuia ya Kimataifa, Umoja wa Mataifa, Umoja wa Nchi Huru za Afrika bado wanafanya maamuzi ambayo yanazidi kuleta matatizo nchini humo, na kuifanya serikali ya sasa iyumbe katika kutekeleza shughuri zake za kuleta amani iliyo ya kweli katika nchi hiyo", Alfred Kimani kutoka Kenya aliongezea.

"Sasa tutafanya nini ili huo ukweli wa mambo uweze kujulikana na matatizo yaliyo mengi katika nchi hiyo yaweze kutatuliwa?", Temu aliuliza.

"Mimi nafikiri tuunde tume ya uchunguzi, ikafanye uchunguzi, ichimbe chanzo cha matatizo Rwanda toka kabla ya uhuru mpaka sasa, na kujaribu kuelewa kabisa tatizo ni nini na nani anahusika na matatzo kwani mimi siamini kuwa tatizo hasa ni kabila tu. Miaka yote tumefikiria hivyo na kujaribu kumaliza tofauti za kikabila lakini mambo bado yako pale pale", Abdul Abakutsi toka Nigeria alijibu.

"Vilevile, kama tatizo ni la kikabila, lazima uchunguzi ufanyike ili ipatikane namna ya kulitatua tatizo hilo maana hatuwezi kukaa tu na kusema kwa sababu ni tatizo la kikabila, basi halina ufumbuzi", Lukaka Makwega kutoka Zambia aliongeza.

"Tulipokuwa hapa kwa ajili ya mkutano wa amani, ilionekana kwamba serikali tawala ndiyo iliyokuwa inachochea ukabila. Swali hapa ni kwanini serikali inachochea ukabila?. Ni kwa sababu inataka kubaki madarakani kwa njia ya gawa utawale au Rais alikuwa na sera za kikabila yeye mwenyewe au kulikuwa na kitu kingine kilichokuwa kinachochea hali hii, maana kinachotisha zaidi ni jinsi mauaji hayo yalivyotokea. Inaonekana kuwa dakika ishirini tu baada ya ndege ilikuwa imemchukua Rais kutunguliwa mauaji yalianza sehemu zote. Hii inaonyesha mauaji yamepangwa kabla. Ina maana ilijulikana kuwa Rais atauawa siku hiyo?. Na kama Rais ndiye aliyepanga mauaji haya, je alijuwa kuwa atauawa, na kwa hiyo akapanga akiuawa alipiziwe kisasi?. Na kama alijuwa atauawa kwani alirudi na ile ndege! Mimi vilevile naanza kukubaliana na wenzangu kuwa huenda kuna mambo zaidi yasiyojulikana ambayo yanaleta matatizo nchini humo. Nami naamini kuwa mambo hayo yakifichuliwa ufumbuzi wa matatizo ya ndugu zetu hao utapatikana haraka", Charles Malisa wa Tanzania alichangia.

"Kuna kitu kingine nilichokisema mwanzoni ambacho kinatisha sana. Jumuia ya Kimataifa haikufanya kitu chochote pamoja na kuona jinsi watu walivyokuwa wakiuawa kinyama. Majeshi ya kulinda amani ya Umoja wa Mataifa yalikuwepo. Na Jeshi la Ufaransa lilikuwemo nchini humo wakati wa mauaji. Nchi kama Marekani ambazo zimejitokeza kama Polisi wa dunia, vilevile haikushtuka. Na kila mtu anakubali kuwa haya yalikuwa mauaji ya kikatili yaliyopangwa kuliko yale ya Hitler aliyowaua Wayahudi. Kwanini hali ilibaki hivi! Na nchi za kiafrika nazo zilikaa tu zikiangalia kabila moja ndani ya nchi ya kiafrika likiangamizwa kabisa ili lisiwepo tena. Jamani hapa kuna sababu na kuna jambo ambalo halieleweki. Uchunguzi ni kitu cha lazima", Musoke alisisitiza.

"Abakutsi ametoa ushauri wa kuunda tume ya uchunguzi, sijui ni tume ya watu wa namna gani anayozungumzia, maana nchi yenyewe ya Rwanda bado iko katika hali ya kivita bado wanauana. Serikali ya sasa bado haina uwezo wa kudhibiti hali ya usalama katika nchi hiyo. Mambo yote bado shagalabagala. Tukisema watu kama sisi twende huko kufanya uchunguzi hakika hatutaambulia kitu kama si kutafuta kuuawa. Uchunguzi ni muhimu lakini lazima tufikirie uchunguzi huu ufanywe namna gani", Makwega alishauri.

Watu wote waliohudhuria kikao hiki walinyamaza kimya wakitafakari kwa kina kuhusu uzito wa suala hili nyeti.

"Lete ndafu na utuongeze vinywaji, tunatakari huku tukilegeza makoo", Temu alimwagiza mtumishi wake. Bia baridi aina ya Safari zikaletwa na mabwana hawa wakaendelea kulegeza makoo na kutafuna ndafu, huku wote wakitafakari mazungumzo yao kwa makini.

Baada ya kimya kirefu Abakotsi alivunja kimya hicho. "Huenda ikawa ni lazima tuunde kikosi cha siri cha upelelezi, kipeleleze kwa sirisiri halafu kituletee taarifa maana serikali zetu zinao vijana wanaoweza kufanya upelelezi kama huo na ukazaa matunda. Kama bwana Makwega alivyosema, tume ya kawaida haiwezi kuambulia kitu, kwani mambo ni magumu huko. Nia yetu ni kupata ufumbuzi na si kupeleka watu wakauawe. Mnasemaje jamani?".

"Hapo umenena, hiyo ndio njia pekee ya kuweza kuingia ndani na kupeleleza kiini cha matatizo hayo. Mimi nakuunga mkono ila tutaiomba serikali gani itupe msaada huo?. Nyinyi wenyewe mliona jinsi serikali zetu zilivyonyamaza na kuacha kana kwamba hazikujua kuwa mauaji yalikuwa yakifanyika Rwanda", Makwega alinena.

"Wote tunakubaliana kuwa njia nzuri ya kupata kiini cha matatizo yaliyosababisha hali ya Rwanda ikafikia pale ni kutuma kikosi cha upelelezi?", Musoke aliuliza.

"Ndiyo", wote walijibu kwa pamoja.

"Basi, tuahirishe mkutano kwa leo, tuonane hapa kesho mchana saa kama hizi ili niweze kuwasiliana na watu fulani fulani ambao naamini wanaweza kutusaidia bila kugongana na serikali zetu", Musoke alisema.

Nyuso za wajumbe, ambazo kwa muda mrefu zilikuwa zikionyesha wasiwasi, zilikunjuka na kuonyesha furaha. Ndipo wote walipokumbuka kuwa Musoke ndiye aliyekuwa Mkuu wa Idara ya Upelelezi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kabla haijavunjika. Hivyo, alijuana na wakuu wa idara hizi katika Afrika Mashariki, na alisemekana hadi sasa alikuwa akiombwa ushauri wa kiupelelezi mara kwa mara.

Baada ya kumaliza vinywaji vyao, wote waliondoka kuelekea kwenye hoteli zao walikofikia. Usiku ule Musoke aliporudi hotelini kwake, pale Mount Meru, aliwapigia simu rafiki zake, yaani wakurugenzi wa upelelezi wa Kenya, Uganda na Tanzania. Alizungumza nao kidiplomasia na kila mmoja alimuomba ushauri na kumweleza sababu za kufanya hivyo. La kusikitisha ni kwamba, kwa vile yeye alikuwa sasa anaongoza chombo ambacho si cha kiserikali, serikali zisingeweza kumsaidia mtu au kikundi cha watu, kwa vile ingeshindwa kujieleza iwapo mkasa wowote wa kiupelelezi ungetokea.

Hilo ndilo lililokuwa jibu la kila mkurugenzi wa upelelezi. Wote waliomba samahani kwa hilo kwani walimheshimu sana, lakini ilikuwa nje ya masharti yao ya kazi, hasa wakati huu ambapo siasa za nchi hizi ni kutoingilia mambo ya ndani ya nchi zingine!

Swala hili lilimkasilisha sana Musoke. Wakati wenzao katika PAM wanapigania Afrika iwe moja, wengine wanadai eti ni kuingilia mambo ya ndani ya nchi nyingine!

"Ole wetu Afrika", Musoke alijililia. Ni wakati alipokaribia kukata tamaa, baada ya kufikiri sana namna ya kuweza kufanya ndipo alipomkumbuka Mzee mmoja mstaafu. Alifikiri huyu angeweza kumtatulia shida yake kwani ni Mzee aliyeisaidia sana Afrika, hasa wakati wa ukombozi wa nchi zilizo kusini mwa Afrika. Yeye alijuana na wapelelezi wengi na maamuzi yake yalikuwa ya pekee, na ndiye aliyekuwa kitovu cha ukombozi Kusini mwa Afrika. Mpaka leo wengi walimjua kwa jina la "Chifu" tu.

Musoke aliangalia ndani ya kitabu chake cha simu, akaipata namba ya Chifu ya nyumbani na kumpigia simu.

Alipoangalia saa ilikuwa yapata saa tano usiku.

"Hallo", alisikia sauti ya Chifu, ikiwa na nguvu kama ya kijana wa miaka thelathini.

"Mzee, shikamoo, Musoke hapa".

"Marahaba Musoke, habari za siku nyingi, nini kinakufaya unipigie simu saa hizi?".

"Umekasirika Mzee?".

"Hapana, shauku".

"Bado tu uko vilevile, utafikiri hujastaafu?".

"Mwili ndio unastaafu lakini nafsi huwa haistaafu maana nafsi haizeeki isipokuwa mwili".

"Ahsante nitazingatia, huo ushauri, maana nami naitwa mzee sasa na nafsi yangu imeanza kukubali".

"Hapana usiruhusu kabisa. Haya, lete habari zinazokufanya umpigie simu mzee kama mimi saa hizi kwanza uko wapi?".

"Niko Arusha".

"Aha, nilifikiri uko Kampala".

"Niko Arusha, Chifu". Ilikuwa ukimwita Chifu mara moja anajuwa kazi imeanza.

"Haya lete hizo habari".

Musoke alimweleza habari zote toka mwanzo mpaka mwisho. Pia alimweleza jinsi idara za upelelezi za serikali zilivyokataa kumsaidia kwa kitu nyeti kama hiki.

"Pole sana", Chifu alimjibu baada ya kuyasikia yote.

"Tatizo lako ni kubwa, la kuangaliwa kwa makini sana. Mimi mwenyewe nimekuwa nikishangazwa sana na mambo yalivyo Rwanda. Enzi zetu sisi tusingeruhusu hali kama hiyo itokee, wewe mwenyewe unajuwa msimamo wetu ulivyokuwa".

"Ndio Chifu, lakini serikali zetu za sasa kila mtu eti na nchi yake, eti hiyo ndio wanaiita demokrasia", Musoke alijibu.

Wakati wanazungumza kwenye simu mawazo ya Chifu yalikuwa yanakwenda kama Kompyuta kutafuta nani angeweza kumsaidia Musoke na Chama chake cha PAM katika azma yao ya kutafuta kiini cha matatizo ya Rwanda. Chifu mwenyewe alikuwa mwana PAM, na aliamini Umoja katika Afrika.

"Jack", Musoke alishituka kusikia Chifu akimuita kwa jina lake la kwanza. Hii ilikuwa na maana amekwisha pata jawabu. "Nafikiri nitakupatia ufumbuzi wa tatizo lako. Mtu mmoja tu katika Afrika hii ambaye anaweza kuifanya kazi yako. Hivi sasa ameacha kazi za kiserikali maana ameowa na anafanya shughuli zake. Lakini kutokana na imani yake katika Umoja wa Afrika anaweza akaifanya kazi hii, huna haja ya kuwa na kikosi, maana yeye pekee ni kikosi. Nitazungumza naye, nipe namba yako ya simu na chumba chako; nitakupigia simu kesho asubuhi".

"Ahsante Chifu, nilijuwa wewe ndiye utakayenimalizia matatizo yangu", Musoke alijibu kisha akampa namba ya simu ya pale hotelini na namba ya chumba. Alipomaliza tu akasikia simu ikikatwa. Akajuwa tayari Mzee yuko kazini.

Chifu alipokata simu ya Musoke, alipiga simu nyingine.

"Hallo".

"Chifu".

"Aha shikamoo".

"Marahaba, tuonane kusho asubuhi, tutastafutahi pamoja pale Kili, kama kawaida.

"Sawa Mzee, kesho", Chifu alijibiwa.

"Kesho, ahsante", Chifu alijibu na kukata simu.

KAZI KWAKO

"Umesikia George Foreman amerudi ulingoni na kutwaa ubingwa", Chifu aliuliza.

"Sikusikia tu, nimeona kwenye televisheni".

"Basi na wewe nataka urudi ulingoni", Chifu anasema kwa tabasamu huku akiupaka mkate wake siagi.

"Mimi! mimi nimeoa na mke wangu ana mimba. Mchezo huo sifanyi, sifanyi ng'o".

Chifu anaangua kicheko kiasi cha kuwafanya watu wote ndani ya chumba cha mkutano wamwangalie.

"Kwani mimi sijui umeoa! Kwani mimi sijui mke wako ana mimba! Najua, lakini nakutaka ulingoni tena. Kwani George Foreman hana mke, hana watoto, mbona karudi ulingoni", Chifu aliendelea kusema kwa kebehi.

"Huenda alikuwa anataka pesa, huenda alikuwa anatafuta sifa, mimi sitaki vitu vyote hivyo, sirudi ng'o", Chifu alielezwa kwa busara.

"Sikiliza nikueleze kwanza. Mimi ndiye niliyekuruhusu uache kazi na kukushauri uoe na nisingependa uharibu ndoa yako. Najua unampenda sana mkeo, sasa nasema nisikilize kwa makini nikueleze, kama utakataa itanibidi niingie mimi mwenyewe ulingoni", Chifu alijibu kwa masikitiko kiasi cha kumfanya mwenzake apoe hasira zake.

"Chifu, hebu nieleze kuna nini? Kitu cha maana namna hiyo, kiasi cha kusema utafanya kazi hiyo mimi nisipokubali? Unajua mimi siwezi kukuruhusu wewe kufanya hivyo.

"Basi sikiliza".

Ilimchukua Chifu saa nzima kumweleza suala la Rwanda na jinsi msimamo wa PAM ulivyohusiana pamoja na vipengele vingine vingi ambavyo hata akina Musoke wasingeweza kumweleza maana hawavijui.

"Unafikiri Serikali ya sasa ya huko haiwezi kufanya kazi hiyo", Chifu aliulizwa.

"Haiwezi. Inahitaji ujuzi wa hali ya juu kufanya kazi hiyo, katika hali ya machafuko namna ile, maana hata wao hawajui nani ni nani katika nchi yao. Hawamwamini mtu yeyote na wao hawaaminiki vilevile na kuweza kupata habari za kina kama zinavyotakiwa, unahitajika ujuzi wa juu sana. Na katika Afrika nzima kama si wewe basi itanibidi mimi mwalimu wako nikaifanye.

"Umenipa mtihani mkubwa sana. Unafikiri kazi kama hii inaweza kuchukua muda gani?".

Chifu alipoulizwa swali hili, moyo wake ilitulia akijuwa kazi itafanywa.

"Inategemea na wewe mwenywe, wiki moja au mbili, mwezi yote yategemea wewe. Kwani Pepe atajifungua lini?".

"Bado ana miezi miwili".

"Nakutakia heri. Nafikiri utamaliza kazi kabla ya hapo. Tafadhali, hafadhari iwe kitu cha kwanza kwako maana huko kuna hatari nyingi, usifanye mchezo kama unataka kumwona mtoto wako", Chifu sasa alikuwa amebadilika na kumwasa mwenzake.

"Nikifa utamlea wewe", Alijibu.

"Sasa nina miaka sabini, nitamlea miaka mingapi mie", Chifu alijibu.

"Wewe ndiye uliyetaka, shauri yako, damu yangu itakuwa juu ya kichwa chako".

"Pole sana. Ndege ya Shirika la Ndege Tanzania inaondoka saa tano na nusu kwenda Kilimanjaro. Tiketi hii hapa, umepatiwa nafasi kwenye ndage hiyo. Musoke mtaonana uwanja wa ndege, atakuja kukupokea, si unamfahamu?".

"Ndio, namfahamu".

"Haya kwa heri. Ukirudi toka Arusha, kabla ya kwenda Kigali, njoo unione nitakuwa tayari na taarifa za kukusaidia kule".

"Asante, nitafanya hivyo.

Chifu alilipa wakaondoka.

Ilikuwa saa tatu na nusu Chifu alipompigia simu Jack Musoke kule Arusha.

"Naam Chifu. Nilikuwa nasubiri huku kiroho kinanidunda. Haya nipashe".

"Willy Gamba ndiye mtu wako, mpokee uwanja wa ndege saa sita na nusu mchana".

Musoke alipigwa na butwa. Hakuweza kujibu kwa ajili ya furaha na msisimko. Hata Chifu alipokata simu hakusikia. Utafikiri kapigwa na radi.

"Willy Gamba! Willy Gamba! Jamani huyu Chifu nitamfanyia nini kwa kumleta willy Gamba! Mungu anatupenda sana Waafrika maana sasa kazi itafanyika", Musoke alijisemea kama kichaa.

Baada ya kuachana na Chifu, Willy Gamba alikwenda tena kwenye ofisi za Shirika la Ndege Tanzania ATC kujua kama kutakuwa na ndege ya kurudi siku ile ile jioni, maana Chifu alimkatia tiketi ya kurudi kesho yake jioni ambayo hakuiafiki. Alitaka arudi siku ile ile.

"Kuna ndege toka Kilimanjaro jioni", Willy alimuuliza kimwana mmoja kati ya vimwana walikuwa kwenye kaunta wakiwashughulikia wateja.

"Hakuna ndege jioni, kuna inayoondoka saa tano na nusu hapa na kuondoka kule saa saba na dakika kumi basi', yule kimwana alijibu huku akimrembulia macho.

"Hakuna ndege ya shirika lingine lolote?".

"Hakuna, labda uchukuwe ya kukodi huko Tanzanair", kimwana alijibu kwa kebehi akijuwa kuwa Willy hawezi kumudu gharama za kukodi ndege.

"Unaweza kunifanyia mpango ili hiyo ndege inichukuwe uwanja wa ndege wa Kilimanjaro saa kumi na mbili jioni?", Willy aliuliza katika hali ya kuomba.

"Sisi haturuhusiwi, sisi tunahusika na kuuza tiketi za ATC tu", yule kimwana alijibu kwa wasiwasi. Willy alitoa kadi yake, na kumweleza. "Mimi ni mteja wenu mzuri sana. Nenda hapo Tanzanair kanikodishie, nitamtuma katibu mahsusi wangu, atakuja kukuona mkalipe na kwa kufanya kazi hiyo na wewe utapata chochote kwani hakuna kazi ya bure siku hizi. Wewe unaitwa nani?".

Akiwa amepigwa na butwa yule msichana alijibu. "Naitwa Mariam".

"Oke, Mariam fanya hiyo kazi kungali mapema, mimi naenda uwanjani kuwahi ndege yenu ya saa tano. Katibu wangu anaitwa Dudu, atakuja kumaliza mambo ya malipo na wewe".

Kabla Mariam hajaanza kulalamika Willy alikuwa amekwisha nyanyuka na kuondoka.

"Wanaume wengine utafikiri wana dawa. Huyu mwanaume kanitia butwa, sasa itanibidi nifanye hiyo kazi yake; nimeshindwa hata kupata mwanya wa kukataa", Mariam alimweleza mwenzake aliyekuwa amekaa karibu naye.

"Hukuona macho yake! Akikuangalia tu roho inadunda, hiyo ndiyo dawa yake, ni mwanaume anayevutia sana, ana sumaku ya kiume, mwanamke hawezi kumkatalia kitu naye anajuwa hivyo", Husna alimjibu Mariam.

Mariam aliondoka na kwenda kumtafutia Willy ndege huku kiroho chake kinarukaruka. "Sijui nitamwona tena yule mwanaume, kaniachia kadi yake, ngoja nitamtafuta", Mariam alifikiri huku akielekea ofisi za Tanzanair.

Willy Gamba alipofika ofisini kwake kwenye jengo la Sukari, Mtaa wa Ohio, ilikuwa saa nne na robo. Dudu aliangalia saa yake na kumwangalia Bosi wake kwa macho ya kumshitaki kuwa kachelewa.

"Shikamoo bosi", Dudu alimsalimia Willy.

"Marahaba, najuwa umeninunia kwani sikuwahi kutimiza miadi na wateja.

"Kumbe unajuwa, na ukafanya makusudi", Dudu alijibu.

"Siyo makusudi, ila ndiyo sababu kuna usemi kuwa, bosi hachelewi kazini, huwa amepita kwenye shughuli kadhaa wa kadha, nami nilipita kwenye shughuli kadha wa kadha. Sasa sikiliza, mimi naondoka kwenda Arusha kwa ndege ya ATC saa tano unusu, nina muda mfupi sana. Kumetokea dharura. Nataka nirudi leo jioni, maana dharura hii inaweza kunifanya nisafiri kwa muda wa wiki kadhaa nje ya nchi. Kwa vile ATC hawana ndege kutoka Kilimanjaro jioni, nimemuomba msichana mmoja aitwaye Mariam pale kwenye ofisi ya mauzo ya ATC anifanyie mpango wa ndege ndogo ya kukodi ya Tanzanair. Hivyo, uende ulipie na ndege iwe kwenye uwanja wa ndege wa Arusha saa kumi na mbili jioni, umeelewa?".

"Nimeelewa bosi, naona kweli dharura, mpaka kukodi ndege, nani atalipia gharama hizi bosi?".

"Nina mteja ambaye atalipia", Willy alijibu.

# SURA YA PILI

Dudu alikwisha fanya kazi na Willy kwenye ofisi yao hii ya watu wawili kwa muda wa miaka mitatu. Hivyo alikwisha mwelewa vizuri Willy na alifurahi sana kufanya kazi na mtu sifa na mwenye roho nzuri kama Willy. Hata siku moja hakupata ugonjwa wa moyo toka kwa bosi wake huyu. Alikuwa mtu tofauti sana na watu wengine ambao Dudu aliwahi kufanya nao kazi.

Baada ya kuacha kazi serikali, ambako alifanya kazi kama mpelelezi, na akawa mpelelezi wa kutegemewa si Tanzania tu bali Afrika nzima, Willy Gamba aliamua kuanzisha ofisi yake binafsi ya upelelezi, hasa iliyohusu mambo ya Bima. Aliamua kuacha kazi akiwa na umri mdogo wa miaka 42 tu. Kwa vile alitaka aoe kwani kazi yake serikalini ilimfanya asafiri sana nje, kitu ambacho kilimfanya asioe maana ndoa yake ingekuwa ya wasiwasi. Hivyo aliomba na kwa shingo upande na baada ya malumbano ya muda mrefu na waajiri wake huku akisaidiwa na Chifu ambaye alikuwa Bosi wake kabla hajastaafu, alikubaliwa kuacha kazi. Ndipo baada ya kuacha kazi, akamwoa mchumba wake ambaye alikuwa amesubiri kwa muda mrefu huku akimvumilia kwa safari zake nyingi.

Huyu mchumba wake aliitwa Pepe. Pepe alikuwa mtoto wa watu, msichana aliyeumbika, mzuri wa sura na tabia, na kwa uzoefu wake mwingi kwa wasichana, Willy aliamua lazima amwoe Pepe na kila wakati alimwambia mama yake ambaye kila siku alikuwa akimpigia kelele aoe, na asipomuoa Pepe basi hataoa tena.

Mama yake Willy alikuwa na wasiwasi sana na Pepe, kutokana na jinsi mtoto yule alivyokuwa mzuri wa sura. Alifikiri kuwa msichana mzuri kiasi kile hawezi kuwa mke wa nyumbani kwani lazima atakuwa na maringo. Lakini Mama yake Willy alikuwa kakosea kabisa. Huyu msichana alikuwa amelelewa kwao, wazazi wake walimlea kwa kumtayarisha ili aje awe mke wa mtu. Walimsomesha vizuri mpaka chuo kikuu, lakini walihakikisha kuwa Pepe anapata mafunzo ya namna ya kuishi na watu na maisha ya ndoa yanapewa kipaumbele. Na kweli pamoja na uzuri usioelezeka wa maumbile ya Pepe, tabia yake ilikuwa nzuri isiyoweza kuelezewa vilevile. Hii ndio inaonyesha kuwa tabia ya mtu haitokani na maumbile yake, bali zaidi inatokana na malezi.

Hivyo, baada ya kuacha kazi, Willy alifanya vitu viwili kwa mara moja. Alianzisha ofisi yake binafsi na akamwoa Pepe. Na hii miaka yao mitatu ya ndoa ilikuwa

miaka mitamu iliyojaa kila aina ya raha, starehe na mapenzi yasiyo kifani. Kila mtu aliyewaona na kujuwa walivyokuwa wanaishi, aliwaonea wivu.

Dudu naye aliajiriwa na Willy alipofungua tu ofisi yake, Chifu ndiye aliyemtafutia mfanyakazi huyu. Hivyo hata ofisini kwake kazi zilifanyika vizuri na kwa uelewano mkubwa. Kweli Willy alikuwa hatoka nje ya Tanzania kikazi, ila tu kwa mapumziko ambayo alisafiri pamoja na Pepe wakitalii nchi nyingi sana, na kumwonyesha dunia ilivyo.

"Kama ndege inaondoka saa tano na nusu itabidi uwahi maana siku hizi msururu wa magari kwenye barabara ya Nyerere ni hatari".

"Kweli kabisa, niitie taksi, AVIS, na uwaeleze waje wanipokee jioni, kama yule dereva wao Ismail yupo ningependa aje yeye".

Ofisi za AVIS zilikuwa ofisi mpya jijini Dar es Salaam na haikuwa mbali na ofisi za Willy. Tangu ianzishwe ilikuwa na uhusiano wa karibu na ofisi ya Willy vilevile meneja wao walikuwa rafiki wa Willy.

"Pepe ana habari", Dudu aliuliza baada ya kuagiza taksi.

"Hajui, na ndio maana ningependa nirudi jioni ili kama nitasafiri nje ya nchi nijuwe nitamwelezaje. Na maelezo ili yaeleweke usiku ndio mzuri, hasa mkiwa ndani ya shuka".

"Au vipi", Dudu alidakia.

"Hivyo akipiga simu mwambie nitachelewa kurudi nyumbani, huenda hadi saa mbili usiku. Pale shuleni kwao kama kawaida ya Dar es Salaam, simu bado haifanyi kazi".

"Nitamweleza baba, usiwe na wasiwasi".

Taksi ilifika. Willy akachukua mkoba wake tayari kuelekea uwanja wa ndege.

"Shikamoo", Ismail alimwamkia Willy.

"Marahaba Ismail, maana sasa abiria tayari wana 'check-in' fanya kila njia sitaki kuachwa na ndege hii".

"Inaondoka saa ngapi?".

"Saa tano u-nusu".

"Dakika hamsini zimebaki, utawahi acha mimi nifanye kazi yangu", Ismail alimjibu Willy wakaondoka.

Kweli Ismail aliijuwa kazi yake maana walipotoka kwenye jengo la Sukari aliingia Mtaa wa Ohio ili kukwepa msururu wa magari, akaingia Barabara ya Titi Mohamed, alipofika Mnazi Mmoja akaingia Mtaa wa Uhuru, halafu Lumbumba na kisha Mtaa wa Lindi tukatokea Ilala na kushika tena Mtaa wa Uhuru, tukaingia Barabara ya Nelson Mandela. Ndipo akashika Barabara ya Nyerere kwenye taa za Tazara, na ndani ya dakika ishirini tulikuwa Uwanja wa Ndege.

"Asante Ismail", Willy aklimshukuru na kumkabidhi shilingi elfu moja kama asante. "Usisahau jioni?".

"Nimeshaelezwa mzee, utanikutwa nakusubiri".

Willy alijulikana sana na wafanyakazi wa ATC na Dahaco, kwenye kaunta ya kujiandikisha kabla ya kuondoka na kwa vile alikuwa na mkoba wake tu walimchukuwa mara moja na kulipia kodi ya kiwanja na kuelekea chumba cha kuondokea.

Ndege ya Shirika la Ndege Tanzania ATC iliondoka Dar es Salaam saa tano na nusu kamili. Willy alikuwa na tiketi ya daraja la kwanza, na alipoingia ndani ya ndege akitafuta mahali pa kukaa alimwona mwalimu wake, mzee Petro Magoti, akimchekea.

"Njoo ukae hapa Willy, habari za siku nyingi?".

"Nzuri, shikamoo", Willy alijibu huku akiuweka mkoba wake chini ya kiti chake.

"Marahaba, nimefurahi kukuona baada ya miaka kama mitatu hivi".

"Asante mwalimu, unajuwa nilikwambia wakati tulipoonana Mwanza kuwa nilikuwa natarajia kuacha kazi ya kuajiriwa ili nijiajiri mwenyewe, sasa tayari nimefanya hivyo. Na pia sasa nimeoa.

"Aha, hongera, nimefurahi sana nikisikia wanafunzi wangu mkiendelea vizuri", Mzee Magoti alijibu.

Mzee Magoti alikuwa Mkuu wa Shule ya Sekondari ambako Willy alisoma. Kwa vile Willy alikuwa na akili nyingi sana darasani, walimu wengi walimpenda sana na kumheshimu. Hata wakati matokeo ya mtihani wa Cambridge wa darasa la kumi na mbili yalipotoka Willy alipata ushindi wa juu kuliko mwanafunzi mwingine yeyote katika Afrika Mashariki na hivyo kuiletea shule ya Mwalimu

Magoti heshima kubwa. Kutokana na matokeo hayo mazuri hata Mwalimu Magoti alipandishwa cheo hata kushika nyadhifa mbalimbali katika Wizara ya Elimu hadi kufikia kuwa Kamishna wa Elimu. Na alipostaafu walimu walimchagua kuwa Mwenyekiti wa Chama chao kama miaka miwili iliyopita.

"Nimekusikia ukiunguruma kwenye magazeti kuhusu matatizo ya walimu", Willy alimzungumzia.

Ndege ilikuwa inaweka speed ili iruke. Hivyo kama ilivyo kwa abiria wengi wakati huu kila mtu hunyamaza kimya akingojea ndege ipae ndipo waendelee na mazungumzo.

"Ndio kijana wangu, hali ni mbaya sana mashuleni mpaka sasa walimu wana mgomo baridi. Watoto hawasomi kabisa, shule ambazo zinasemekana zinasoma, hasa zile za Sekondari, mwalimu anaweza kuingia darasani mara moja kwa wiki. Sasa utasema huku ni kusoma kweli, si hatari kwa maendeleo ya hawa vijana wetu ambao watakuwa viongozi wetu wa baadaye", Magoti alijibu.

"Lakini mzee, wewe ukiwa kiongozi wa walimu si uzungumze nao waelewe athari za kufanya hivyo kwa taifa hili", Willy alimshauri.

"Bwana mdogo, wewe unaweza kumshauri mtu mwenye njaa! Walimu hawa wote wana njaa, ndicho kilio chao. Mishahara ya serikali wewe mwenyewe unaijuwa. Na kutokana na kupanda kwa gharama za maisha, mshahara wa mwalimu wa kawaida anaweza kuutumia kwa siku tatu tu katika mwezi na ukaisha, je, siku ishirini na saba afanyeje?", Mzee Magoti aliuliza.

"Lakini mzee hii inahusu watu wote walioajiriwa serikalini. Wote mishahara yao haitoshi", Willy alijibu.

"Ahaa, sasa unasema. Yote hii inategemea unyeti wa kazi. Ili watu wajiongezee kipato wanahangaika na kufanya shughuli nyingine. Sasa hivi ukienda kwenye maofisi mengi ya serikali hukuti watu, ukiuliza katoka nje kikazi. Kweli kikazi, maana anakwenda kufanya kazi kwenye miradi yake binafsi, iwe kwenda kukamua ng'ombe wake maziwa au kuwatafutia majani, au iwe kwenda kununua bia kwenye kampuni ya bia ili apeleke kwenye kiduka chake pale nyumbani, yote wanasema kaenda nje kikazi. Sasa kwa mwalimu hahitaji kutoka. Mimi nimekuwa mwalimu karibu maisha yangu yote, ualimu ni kazi ambayo unahitaji saa ishirini na nne, siyo kazi unayoweza ukafanya na kazi nyingine, hutaweza kuifanya sawasawa, Saa hii unafundisha. saa hii unasahihisha kazi za wanafunzi, saa hii unatayarisha masomo kwa ajili ya kesho. Kweli kazi ya ualimu ni nyeti inayohitaji muda wako wote.

Sasa walimu nao wanapofanya kama wafanyakazi wengine na kuwa na miradi matokeo yake ndio hayo! wanafunzi hawafundishwi", Mzee Magoti alieleza.

Mhudumu wa ndani ya ndege alifika na kuwauliza watakunywa nini.

"Mimi chai", Mzee Magoti alijibu.

"Na mimi chai", Willy naye pia alijibu.

"Msingependelea bia au pombe nyingine kali", yule msichana aliendelea kuwashawishi.

"Hapana ni mapema mno", Mzee Magoti alijibu huku Willy akitingisha kichwa kukubaliana naye.

Hata kama Willy angependa bia lakini haikuwa heshima mbele ya mzee aliyemheshimu kama huyu kufanya hivyo.

"Haya, chai yenu inatengenezwa.

"Asante", walijibu, tena kwa pamoja. Kisha wakaendelea na mazungumzo yao.

"Sasa Mzee Magoti, si mmeieleza serikali na serikali inajuwa tatizo hili, na athari zake kwa taifa hili! Maana hawa vijana ndio taifa la kesho, na kama hawasomi ina maana karibuni tu tutakuwa na taifa la wajinga. Yaani wakati dunia inaingia kwenye karne ya ishirini na moja, elimu ndio kitu muhimu kwa taifa lolote, ili liweze kwenda sambamba na mataifa mengine katika sayansi na teknolojia: kama maneno unayosema ni kweli basi tuko hatarini", Willy alieleza mawazo yake kwa Mzee Magoti.

"Maneno yako ni kweli kabisa kijana. Na hiki ndicho tunachopigia kelele sisi mpaka sasa hatuelewani na viongozi wakifikiri tunajaribu kuwachochea wananchi. Lakini viongozi wetu hawajali kabisa. Jibu lao kila siku ni kwamba hali ya uchumi ni mbaya, na serikali haina fedha. Lakini sababu kubwa kwa nini hawajali. ni kwa sababu wao na marafiki zao hawaathiriki na tatizo hili walimu hapa nchini, maana wao wanasomesha watoto wao nje. Hivyo hawajali kama watoto hawasomeshwi: wa kwao wanasoma nje na katika shule za hali ya juu", Mzee Magoti alijibu kwa uchungu sana.

"Mzee Magoti umegusa kitu cha hatari sana. Yaani viongozi wetu wamekuwa na ubinafsi. Kwa vile wao wana pesa, basi wanapeleka watoto wao nje na hawajali nini kinawapata watoto wa wakulima na wafanyakazi, ambao hawana uwezo wa kupeleka watoto wao nje".

"Barabara kabisa Willy, lakini zaidi ya hapo wanajenga tabaka la watawala na watawaliwa. Kwa vile watoto wa wakulima na wafanyakazi ambao ndio wengi katika nchi hii, watapata elimu duni, basi hawa watoto wa viongozi na matajiri ambao ni kama asilimia (2%) ya idadi ya watoto wote wa nchi hii, watarudi na elimu nzuri na hivyo ndivyo watakavyoshika madaraka hapo baadaye maana wao watakuwa wamesoma vizuri, na kama ulivyosema ndivyo wataenda sambamba na mataifa mengine. Hii ni hatari kubwa kwa taifa hili", Mzee Magoti alijibu tena kwa uchungu.

"Ina maana viongozi wetu wanaiachia hali hii ya kushuka kwa kiwango cha elimu nchini kwa makusudi kabisa ili wawape watoto wao na wa matajiri nafasi ya kuendelea kuiongoza nchi hii, na kuwanyima watoto wa watu wa kawaida nafasi hii! Kama hii ni kweli, basi tunaelekea kubaya, maana katika nchi hii tangu uhuru watoto wa watu wa kawaida, ambao ndio sisi, serikali ilitupa nafasi nzuri na kutusaidia ili tuinuke na tuweze kuliondoa taifa katika ujinga na kuweza kuinua taifa na familia zetu kutoka katika hali duni", Willy alieleza.

"Nchi imegeuka, ubinafsi umetawala roho za viongozi wetu, wanajifikiria wao tu. Si viongozi wa wananchi tena, ila wanatafuta uongozi kwa faida yao wenyewe. Hata ukiangalia ni viongozi wachache sana kwa sasa ambao sio matajiri. Wanaingia katika uongozi wakiwa hawana kitu, lakini baada ya muda mfupi unawakuta wamejilimbikizia mali. Afadhali wangefanya hivyo halafu wakaendelea kuwasaidia wananchi ili na wao hali zao ziinuke, la hasha, sera zao ni za kuwadidimiza wananchi wawe masikini pamoja na vizazi vyao ili wasiwe na sauti kabisa. Sauti wanataka ibaki yao na vizazi vyao ili wabaki madarakani kama vile wafalme.

"Sikilizeni... tunakaribia kutua kwenye uwanja wa ndege wa Kilimanjaro. Mabibi na mabwana, inuweni viti vyenu wima, fungeni mikanda yenu ya viti tayari kwa kutua", sauti ya msichana ilisema.

"Mzee, basi nitakutafuta ili unielimishe zaidi kuhusu mambo yalivyo katika nchi yetu hii kwa sasa, maana kwa muda mfupi huu nimeelimika kwa kiasi fulani", Willy alimweleza Mzee Magoti maana ndege ilikuwa inaelekea kutua na hivyo wasingekuwa na muda wa kuzungumza zaidi.

Mzee Magoti alitoa kadi yake yenye anwani na simu.

"Basi ukirudi Dar es Salaam, nipigie simu tuonane".

"Asante Mzee".

Ndege ilipogusa chini wote wakawa kimya mpaka iliposimama kabisa.

"Haya kwe heri Mzee Magoti", Willy alimpa mkono. Akachukuwa mkoba wake na akawa wa kwanza kutoka. Alipoiangalia saa yake ilikuwa saa sita na nusu mchana .

Willy aliposhuka kutoka ndani ya ndege, alimkuta Musoke anamsubiri.

"Shikamoo".

"Marahaba, habari za siku nyingi, haujabadirika bado, ila umetia uzito kidogo", Musoke alimweleza Willy.

"Asante, unajua nimeoa, sasa mapochopocho yananimaliza". Wote walicheka na kuelekea kwenye gari ambalo lilikuwa la kukodi lakini Mzee Musoke alikuwa analiendesha mwenyewe.

"Nimefurahi sana umekubali wito".

"Unajua tena Chifu, ni vigumu sana kumkatalia kitu, hasa anachokiamini yeye kuwa ni kitu muhimu".

"Najua, lakini lazima nikushukuru", Musoke alijibu huku kiroho kikizidi kumdunda kwa furaha kwa kuwa na uhakika kuwa Willy yuko naye tayari kwenda kutekeleza kazi hii nyeti, ambayo inaweza kuleta ufumbuzi mkubwa kwa mataifa ya Afrika.

TAFUTA UKWELI

Ilikuwa yapata saa saba unusu. Musoke na Willy walipofika nyumbani kwa Temu. Walimkuta Temu akitembeatembea mbele ya nyumba yake katika bustani huku ameweka mikono yake nyuma. Kwa vile nyumba ilikuwa juu kwenye kilima, na wao walimwona kabla hajawaona mpaka walipopiga honi ya gari ili kufunguliwa lango la mbele. Alipoona ni gari la kukodi la Musoke, mara moja alikimbia na kulifungua lile lango hata askari wake anayelinda nyumba yake hakuwahi mbio za mzee huyu. Hii yote ilionyesha shauku aliyokuwa nayo Temu juu ya suala hili la Rwanda.

"Shikamoo", Willy alimshalimia.

"Marahaba, karibu".

Temu alipeana nao mikono na wote na kuwakaribisha kule uani kwenye bustani ya nyumba.

"Wengine?", Musoke aliuliza.

"Saa nane watafika".

"Vizuri".

Walipokuwa wameketi kule uawani kwenye kivuli kizuri cha miti, Musoke alitumia nafasi hiyo kuwafahamisha.

"Bwana Temu, huyu ni kijana wetu, anaitwa Willy Gamba, sasa hivi anafanyakazi za kujitegemea, lakini alikuwa kwenye idara ya upelelezi ya Tanzania kabla hajaamua kuacha kazi ili ajitegemee. Yeye ameombwa na marafiki zetu wengine aje atusaidie kwenye hili tatizo letu", Musoke alieleza huku Temu akionekana kushikwa na butwaa.

"Na bwana Gamba, huyu ni mzee Temu na ndiye Mkuu wa PAM upande wa Tanzania.

Willy aliinuka na kumpa Temu mkono.

"Mimi siamini macho na masikio yangu", Temu aliendelea kuonyesha kama mtu aliyeshituka sana. "Hivi kweli Willy Gamba yupo! na ni wewe! Hivi ni kweli baba yangu, ni kweli. Mimi siku zote husikia habari za Willy Gamba na huamini kuwa ni hadithi tu, maana mambo ambayo ameyafanya wakati wa ukombozi wa nchi zilizo kusini mwa Afrika tulifikiri ni propaganda tu ya kamati ya ukombozi ya OAU. Kumbe mtu mwenyewe upo na ni kweli. Eehe, ama kweli kuishi kwingi kuona mengi. Basi bwana Musoke, kazi yetu itafanikiwa", Temu alieleza.

"Huyu kijana wetu Mwenyezi Mungu amemjaalia uwezo mkubwa sana katika kazi hii ya upelelezi. Hakuna mtu unayeweza kumlinganisha naye hapa Afrika, sijui huko Ulaya, lakini hata majasusi wa huko Ulaya ndiye aliyekuwa akiyakomesha wakati wote huo. Kwa kweli hata mimi niliposikia amekubali na ni yeye anayekuja basi roho yangu ilitulia, najuwa tutafanikiwa. Hivi kwanini wamekukubalia kustaafu mapema hivi?", Musoke alimuuliza Willy lakini kabla ya kujibu, mhudumu wa pale nyumbani alifika na kutaka kujuwa watakunywa nini.

"Bwana Gamba unataka kunywa nini?, kunywa kitu kidogo, maana huko ndani wanatengeneza chochote cha mchana, sisi wachaga ndizi ndicho chakula chetu, sijui wewe utapendelea?", Temu aliuliza.

"Kinywaji naomba klabu soda, na nitafurahia sana macharari", Willy alijibu huku Temu akicheka na kufurahi kusikia macharari.

"Kumbe unayajuwa eeh basi baba yangu tutakula hayo maana wanaandaa. Na wewe mzee Musoke?".

"Mimi nitakunywa ki-wiski kidogo, unajuwa sisi wazee lazima ushituwe damu kidogo upate joto".

"Sawa kabisa, nenda kalete haraka", Temu alimwagiza mhudumu wake.

"Ehe Willy, kwanini umeruhusiwa kustaafu mapema hivi?, au kwa sababu ya Afrika Kusini kupata uhuru?", Musoke aliuliza tena.

"Hapana, mimi niliomba kustaafu ili niweze kuoa na kuanza maisha ya kifamilia maana kazi hii haifai kama umeoa na una familia. Sasa hivi nimeoa na mke wangu ni mjamzito. Na hata kazi hii nimekubali tu, kwanza kwa sababu na mimi nimeumwa sana na hali hii ya mauaji ya Rwanda na pili kwa sababu Chifu alisema nisipokwenda mimi atakwenda yeye. Na unajuwa bwana Musoke, mimi nisingependa hata kidogo kuruhusu kitu kama hicho".

"Ni kweli kazi hii inahitaji kuweka mawazo yako pamoja, usiwe na fikira zingine, lakini ndivyo hivyo, taifa bado linakuhitaji mara kwa mara kama hivi, ingawaje si sana kama ulivyokuwa jikoni", Musoke alikubaliana na Willy. Mara wakaona wenzao wengine wanaingia na wote wakasimama kuwasalimia.

Temu alichukuwa nafasi ya kuwafahamishe wenzake kwa Willy Gamba. "Hawa ni wana PAM kutoka sehemu mbalimbali za Afrika. Na wamekuja kwa ajili ya kikao hiki cha kutathimini jinsi mambo yalivyokuwa huko Rwanda. Huyu ni bwana Kimani kutoka Kenya, huyo ni Abakusi toka Nigeria, huyu ni Makwega toka Zambia na huyu kijana mwenzio ni Malisa kutoka hapa hapa Tanzania". Kisha akageuka na kumgusa Willy. "Na huyu ndiye mgeni tuliyemtarajia kwa ajili ya kazi yetu. Bwana Willy Gamba.

Kimani na Malisa waliwahi kusikia habari zake nao walishikwa na mshangao kama wa Temu. Musoko alitumia nafasi hiyo kunong'ona na Abakusi na Makwega kuwaeleza Willy Gamba hasa alikuwa mtu wa sifa za namna gani. Bila hata kusema mengi, alipoeleza kazi zake mbili alizofanya na kuutingisha ulimwengu kwa kuwazuia majasusi wa Afrika Kusini tayari wote wakamtambua na kupigwa na butwaa vilevile.

"Wakati mwingine binadamu akili inashindwa kuamini kitu. Mimi nilisikia jinsi mpelelezi wa Afrika alivyoyaangamiza majasusi kule Kinsasa, Zaire, na nikaamini

kuwa zilikuwa hadithi tu. Sasa namuona hapa mtu mwenyewe, akili inashindwa kuamini. Inashangaza", Abakusi alisema.

"Kama Willy Gamba ndiye huyu kijana, basi mambo yetu yameiva", Makwega naye alinena na kutokwa na wasiwasi aliokuwa nao usiku.

Bila kupoteza muda mkutano uliendelea huku wakipata huduma za vinywaji na chakula.

"Nafikiri wasiwasi wetu wote sasa umepungua baada ya kumpata kijana huyu?", Musoke alisema kama vile akitoa maoni ya mkutano.

Wote walitingisha vichwa kama ishara ya kukubali.

Kwa vile kijana huyu yuko hapa, tumpe maelezo tunataka atufanyie nini. Nafikiri mimi niendelee na kama mtu ataona nimepwelea mahala naomba asisite kuongezea, sawa".

"Sawa", wote walimjibu mzee Musoke.

"Bwana Willy, wewe mwenyewe naami unazo habari nyingi kuhusu matukio ya Rwanda. Ila sisi, kama wana PAM tungetaka tupate undani zaidi wa mambo yalivyotokea huko Rwanda mpaka yakafikia yalipofikia na watu zaidi ya milioni moja katika nchi ya watu milioni tano kuteketezwa kwa siku kadhaa tu. Kitu hiki kinatisha na kama hakiwezi kuangaliwa kwa undani na kuthibitiwa inaweza kutokea tena si Rwanda tu bali hata mahali pengine Afrika. Sijui unanielewa?", Musoke alimuuliza Willy.

"Nakuelewa, ila nataka nijie ni nini hasa mnataka mimi nifanye maana kule sasa kuna serikali ya RPF, kuna mashirika ya kimataifa, kuna mashirika yanayotetea haki za binadamu, mnafikiri mimi nitafanya nini zaidi ya watu hawa na wenye uwezo na mapesa mengi nyuma yao, maana na wao wanachunguza kwa kina maovu yaliyotendeka Rwanda", Willy alisema akitaka ufafanuzi zaidi.

"Sawa bwana Gamba, kitu tunachotaka sisi ni uchunguzi wetu wenyewe. Hawa watu wengine wote wanaweza kuwa na nia zao tofauti. Serikali ya RPF ni mhusika kwa kiasi fulani. hatuwezi kupata ukweli asilimia mia toka kwao. Mashirika ya kimataifa yenyewe yanaweza kuwa na ajenda tofauti, tena wanaweza kutoa ripoti kutokana na ajenda yao. Wanaotetea haki za binadamu nao wana mtazamo wao kwa maana ya kuonyesha kuwa kulikuwa na ukiukwaji wa haki za binadamu Rwanda. Sisi tunataka uende zaidi ya pale, ujue kama haki za binadamu zilikiukwa, na kwa nini zilikiukwa, lazima kuna sababu. Mauajiyaliyotokea nini

kiini chake, maana yanaonekana yalikuwa yamepangwa toka mapema. Na vilevile kwanini Afrika na dunia kwa ujumla, ikiwa kimya pamoja na nchi jirani kama Uganda, Tanzania, Zaire na Burundi hazikufanya chochote kuzuia mauaji haya. Tukishajuwa chanzo na sababu zilizofanya mpaka binadamu akafikia kuwa mbaya kuliko mnyama, nafikiri tutakuwa tumejifunza; na hili fundisho litatusaidia kuweka mkakati wa kuzuia kitu kama hicho kitakapotokea. Vilevile tujue namna ya kukidhibiti kabla hakijaleta maafa makubwa kama haya", Musoke alijibu.

"Oke, nimeelewa nini mnataka, nitajitahidi niweze kuchimbua mambo uliyoyataja hapo ili nipate vyanzo vyake", Willy alijibu.

"Lakini haitakuwa kazi lahisi, lazima uwe macho maana ukweli wa mambo haya unaweza kuwa na athari nyingi kwa watu mbalimbali ndani ya Rwanda na pengineko duniani. Kwa hiyo ikijulikana kuwa kuna mtu anatafuta ukweli na ikaonekana kuwa ataupata, basi ujuwe masiha yako yanaweza kuwa hatarini maana mpaka sasa tunaamini kuna watu wanajaribu kufukia ukweli usijulikane. Na hawa watu watakuwa watu hatari. Tafadhali, hadhari ni lazima", Abakusi alimwasa Willy.

"Nitalitazama hilo", Willy alijibu na kuendelea, "Na malipo yangu yatalipwaje, maana sasa ni mfanyabiashara na si mfanyakazi wa serikali tena. Kazi hii nimeichukua binafsi".

"Malipo utalipwa na PAM. Kwa ajili ya kazi hii PAM iliwaomba michango wafanyabiashara wa kiafrika ambao wanaunga mkono msimamo wa PAM na wametoa michango mizuri sana na tukitoka hapa tutapitia hotelini kwangu nikupatie malipo yako. Sijui utahitaji kiasi gani?", Musoke aliuliza.

"Mimi vilevile, kama nilivyosema, naunga mkono madhumuni ya PAM, kwani ni mpaka pale Mwafrika atakapojitambua kuwa lazima azungumze na Waafrika wenzake kupambana na ukoloni mambo leo ndipo atakapokuwa amejikomboa kutoka katika umasikini, ujinga na maradh. Kwa jinsi hiyo na mimi nikiwa mshabiki wa PAM nitaomba nilipwe gharama zangu tu nitakazotumia, lakini utaalamu wangu nautoa bure".

Makofi na kupeana mikono ya shukrani vilisikika.

"Sijui hii kazi unafikiri itachukuwa muda gani?", Kimani aliuliza.

"Mimi nitawafanyia kazi, nipeni muda", Willy alijibu.

"Wiki mbili?", Makwega aliuliza pia.

"Nitajitahidi".

"Basi tuonane hapa baada ya wiki mbili", Musoke aliagiza.

"Sawa".

"Lakini Willy Gamba atakuwa anawasiliana na mimi Kampala kwa kila hatua atakayofikia. Kama ikionekana kazi inakuwa bado baada ya hizo wiki mbili, nitawajulisha", Musoke alieleza.

"Sawa".

"Haya, asanteni sana wazee, tutaonana Mwenyezi Mungu akitujaalia baada ya wiki mbili. Sasa hivi ngoja niende na mzee Musoke akanikamilishie masuala ya mapesa", Willy aliaga huku akiwachekesha.

"Nilitaka kusahau. Tumekupatia nafasi ya kulala Impala, ukienda tu pale mapokezi watakupa funguo, tumelipia kila kitu, kazi kwako. Sijui kama utahitaji usafiri kesho kukupeleka uwanja wa ndege?", Temu alieleza na kuuliza.

"Hapana, nitajitegemea kwenda uwanja wa ndege".

Musoke alipoangalia saa ilikuwa saa kumi na nusu. Willy alipewa mkono wa heri na wajumbe wa PAM huku kila mmoja akimwombea mafanikio na usalama. Willy aliupokea mkono huo wa heri huku naye kimoyomoyo akiomba sala zao ziwe pamoja naye, kwani hawa walikuwa watu wenye roho za ubinadamu, ambao walikuwa wakitumia muda wao kujaribu kuwasaidia wengine bila malipo ya aina yoyote. Kweli Mungu awabariki.

Musoke na Willy aliondoka, wakaelekea Maunt Meru.

"Kesho umesema ndege saa ngapi?", Musoke alimwuliza Willy.

"Saa tatu asubuhi".

"Nije nikupeleke?".

"Hapana, nina marafiki wengi hapa watanipeleka".

"Na leo jioni tunaweza kula pamoja?", Musoke alimkaribisha chakula cha usiku.

"Hapana, nitakwenda kwa dada yangu jioni, alifiwa na mjukuu wake na nilikuwa sijapata nafasi ya kumsalimia na hii ndio nafasi pekee niliyopata".

"Umeua ndege wawili kwa jiwe moja".

"Bila shaka", Willy alijibu huku akijuwa kabisa kuwa angeondoka jioni ile. Willy kama kawaida yake, aliendelea kuonyesha kama angelala Arusha. Hii inaonyesha jinsi ambavyo Willy hamwamini mtu yeyote mara akishakuwa kazini.

"Huwezi kujuwa, kikulacho ki nguoni mwako, uzoefu wa siku nyingi umenifundisha", Willy alijisemea moyoni.

# SURA YA TATU

Walipofika Hoteli ya Mount Meru, walikwenda chumbani kwa Musoke na kuanza kuelezana tena. Kwa vile Musoke naye alikuwa na uzoefu wa siku nyingi na kazi ya upelelezi alijuwa Willy angetaka nini.

"Bwana Gamba, unajuwa kazi hii inaweza ikawa ngumu na ya hatari kuliko hata jinsi tunavyotegemea. Hivyo, jitayarishe kwa yote, nadhani unanielewa?", Musoke alimwuliza.

"Nakuelewa sana, kazi hii naichukulia uzito uleule wa kawaida, sintaipuuza hata chembe. Kwa kawaida uzoefu umenionyesha kuwa kwa kawaida kazi rahisi ndio hugeuka kuwa ngumu sana".

"Vizuri, mimi ninao wenyeji kule Rwanda, ambao nafikiri wanaweza kukusaidia kupata fununu za awali", Musoke alisema na kufungua mkoba wake na kutoa kitabu chake cha anuani. "Yuko rafiki yangu ambaye kwa miaka amekuwa akiipinga siasa ya chama cha MRND. Yeye ni mwanajeshi. Alikuwa kamanda katika jeshi la kumlinda Rais, lakini kwa vile hakukubaliana na sera yao, aliacha na kuanza kwa siri kueneza habari kwa vyombo vinavyotetea haki za binadamu jinsi serikali ya Rwanda ilivyokuwa inavunja haki za binadamu nchini humo. Wakati Rais alipouawa Aprili 6, 1994, yeye alikuwa Nairobi kuonana na Katibu wa Chama cha kutetea Haki za Binadamu ulimwenguni. Hata hivyo, huku nyuma mke wake na watoto wake sita na wapwa wake wawili, wote waliuawa tarehe 7, Aprili. Hii ina maana angekuwepo Kigali na yey vilevile leo angekuwa marehemu. Anakaa Kimihurura nyumba namba 168. Simu yake kwa bahati ni moja ya chache zinazofanyakazi sasa hivi na ni namba 50486. Yeye ni Mhutu.

"Umeishazungumza naye?", Willy aliuliza.

"Nitazubumza naye, tuna uelewano mzuri, na yeye anajuwa mengi kwa watu wachache waliokuwa wanaipinga serikali waliobaki. Na ujuwe huyu mtu alikuwa karibu sana na serikali ya Rwanda, na huenda karibu sana na Rais mpaka kufikia kuwa kamanda wa jeshi lake. Hivyo, anajuwa serikali ilivyoondolewa madarakani na RPF vizuri sana, na ndio sababu vilevile kumtafuta ili kumuua ili kuua ukweli wa mambo".

"Vizuri, nikifika Rwanda nitamtafuta kama nitamhitaji".

"Tumekupangia kwenye hoteli iitwayo Des Mille Collines. Hoteli hii ni maarufu maana wakati wa mauaji watu wengi, hasa wa mataifa ya nje, walijificha hapa na hivyo hata wanyarwanda waliokuwa wanatafuta ili kuuawa kati ya walionusurika ni wale waliobahatika kufika hoteli hapo. Hivyo, nayo itakupa fursa nzuri kupata fununu mbalimbali.

Vilevile ningependa umwone Padre mmoja ambaye tunafahamiana na yeye alinusurika kimiujiza baada ya mapadri, maburuda , watawa na watu wote waliokuwa kwenye kituo hicho cha dini kiitwacho Centre Christus, kuuawa na Wahutu wenye siasa kali. Padri huyu anaitwa Jean Marie Karangwa. Utapata mengi toka kwake vilevile".

"Bado yuko kwenye kituo hicho?", Willy aliuliza.

"Ndio yupo, na anajaribu kukianzisha upya. Na wa mwisho ambaye ningependa umwone ikiwa unahitaji msaada, maana huwezi kujuwa, unaweza kuwa kwenye hatari ambayo inahitaji msaada wa kiserikali, hasa kijeshi. Huyu ni rafiki yangu saana, tumekaa naye jirani mjini Kampala na ni mmoja wa makamanda wa RPF, mtu shupavu kama wewe na msomi kama wewe na kijana wa rika lako. Naamini mkionana mtashibana tu. ana roho safi sana. Anaitwa Col Thomas Rwivanga, namba yake ya simu 60314".

"Asante, nikihitaji msaada wake nitamtafuta", Willy alijibu.

"Utaondoka lini na kwa njia gani?", Musoke aliuliza.

"Mimi kesho kutwa nitakutafuta Kampala nikiwa Kigali kukujulisha nimefika".

Musoke hakuuliza zaidi maana alielewa maana yake. Kisha akatoa bahasha kubwa iliyokuwa na pesa za dola za Kimarekani. Idadi yake haikuzungumzwa, lakini bila shaka ilikuwa maelfu ya madola.

Baada ya kumpa mzigo huo walisimama na kuagana.

"Haya, nakutakia safari njema na kazi njema. Nakuombea heri", Musoke alimshika mkono akionyesha uchungu kidogo.

"Asante sana, tuombe Mungu", Willy alijibu na kuondoka.

Willy alipoachana na Musoke alikodi teksi pale nje ya Mount Meru Hotel na kuelekea Impala. Alipofika Impala alijitambulisha. "Naamini nina nafasi ya chumba hapa, naitwa Willy Gamba.

Msichana wa mapokezi aliangalia kwenye orodha yake ya majina kisha akaliona jina la Willy Gamba.

"Ndio baba, chumba 212", alijibu huku akitoa funguo na kumkabidhi.

"Una mizigo?".

"Hapana, huu mkoba wangu una kila kitu".

"Kila kitu?".

"Kila kitu nakuambia, utashangaa nikiufungua, mrembo zaidi yako atatokea".

Yule msichana akacheka na Willy akapandisha ngazi. Alikifungua chumba na kukuta kidogo lakini kizuri sana. Aliangalia saa yake akaona ilikuwa saa kumi na mbili kasoro robo.

Alikwenda kitandani akatoa blanketi, akaliweka pembeni na kufunua shuka na kutengeneza kama kwamba kulikuwa na mtu aliyelala pale. Kisha, akauweka ufunguo kwenye kufuli la mlango kwa ndani, akachukua mkoba wake. Akafungua mlango na kuurudisha bila kuufunga na funguo kwa vile aliziacha ndani makusudi na kutelemka chini. Alipoangalia pale mapokezi na kuona wapokeaji wapo shughulini, alichepuka na kutoka nje. Akelekea kwenye maegesho ya teksi na kukodi teksi kuelekea uwanja wa ndege wa Arusha.

Ilikuwa yapata saa kumi na mbili na robo alipofika uwanja wa ndege na kukuta ndege imeshatua tayari. Rubani wa ndege alimfuata na kumpokea mkoba wake.

"Habari za jioni?", Rubani alimshalimia.

"Za jioni nzuri asante".

"Huna mzigo zaidi?".

Sina, ni huo huo".

Rubani aliufungua mlango wa ndege hii ya Tanzanair, aina ya Cessina Mark 4, na kumkaribisha abiria wake huyu mmoja, ambaye walikaa pamoja kwenye viti vya mbele, na kisha akawasha injini za ndege, na kuruka.

Baada ya Musoke na Willy Gamba kuondoka nyumbani kwa Temu, kila mtu alitawanyika kuelekea kwenye hoteli yake.

Malisa aliyekuja kwenye mkutano huo akitokea Dar es Salaam, alikuwa amefikia Hoteli ya Sabasaba. Alijulikana sana katika kundi la wasomi na kiserikali alikuwa

mmoja wa watu waliokuwa mstari wa mbele katika kupigania kuwepo Umoja wa Afrika. Hata maafisa wa ngazi za juu serikalini mara nyingi walitafuta ushauri kwake kila walipotaka kuzungumzia swala la Umoja wa Afrika.

Malisa alikuwa msomi na Mhadhili wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam katika kitivo cha Sayansi ya Jamii. Mara hii alipokuwa anakuja kwenye mkutano huu Arusha, Afisa mmoja wa ngazi za juu kabisa serikalini alimwomba amweleze mazungumzo na makubaliano ya mkutano wao, kwani serikali ilipenda kujuwa mambo gani PAM inafikiria kuhusu tatizo la Rwanda ili serikali nayo iweze kusaidia. Huyu Afisa wa serikali alimpa namba zake za simu za nyumbani na kumwomba ampigie baada tu ya mkutano.

Malisa alipofika Hotelini tu, ikawa yapata saa kumi na mbili na robo, alichukua ufunguo wa chumba chake mapokezi na kueleka chumbani. Alipofika chumbani alimwomba opereta wa simu pale hotelini ampatie simu ya Dar es Salaam na kumpa namba.

"Subiri kidogo nitakuita", opereta alimwambia.

"Haya asante, lakini nifanyie haraka maana nataka kutoka nina miadi", Malisa alimwomba opereta.

"Sasa hivi", aliambiwa.

Baada ya muda si mrefu simu iliita chumbani kwa Malisa.

"Hallo".

"Namba yako ya Dar es Salaam inaita", opereta alijibu.

"Haya asante", na akaunganishwa na namba hiyo ya Dar es Salaam ambayo iliendelea kuita.

"Hallo", mtu aliitikia baada ya muda kidogo.

"Hapa ni Arusha, mzee yupo?", Malisa aliuliza.

"Yupo, subiri".

Na baada ya muda kidogo akasikia, "Hallo, nani mwenzangu?".

"Malisa hapa, shikamoo".

"Marahaba, habari ya huko?".

"Salama".

"Vipi mkutano".

"Tumemaliza".

"Ehee, hebu nipe maazimio yenu kwani wazee huku wana shauku ya kusikia".

"Haya tega sikio nikueleze, mambo ni mazuri sana", Malisa alijibu na kumweleza mambo yote tokea mwanzo mpaka mwisho.

"Hizo ni habari njema", yule afisa alijibu na kuendelea. "Willy Gamba ni kijana wetu na ni mtu shupavu. Kwa hakika ataifanikisha hiyo kazi. Na mimi nitawaeleza wazee naamini wataridhika na hatua mliyochukuwa. Mnajua sisi kama serikali ni vigumu kuchukua hatua yoyote dhidi ya nchi nyingine, lakini nyinyi mkiwa umoja usio wa kiserikali mnaweza kutusaidia sana kwa mambo kama haya. Willy amefikia wapi?".

"Yuko hoteli ya Impala chumba namba 212. Huenda mzee si vizuri kumpigia simu sasa hivi tu atashituka", Malisa alijibu.

"Na kweli, ingawa ni kijana wetu basi tuache nyinyi muendelee nae. Asante sana kwa kazi nzuri, na mwanzo mzuri, watu wenye uchungu na Afrika kama nyinyi ndio mtakaoisogeza Afrika mbele katika kuleta maendeleo wakati tukielekea katika karne ya sayansi na teknolojia. Asante sana", yule afisa wa serikali alijibu na kukata simu.

Bila kujua alichokuwa amefanya, Malisa alifurahi sana kusikia sifa alizozitoa mtu huyu mashuhuri katika serikali ya Tanzania, kwa umoja wao. Minongono mingi jijini Dar es Salaam ilikuwa ni kwamba afisa huyu, ambaye watu wengi walipenda kumwita kwa kifupi tu kama 'JKS' alitegemewa kugombea Urais baada ya muda wa Rais wa sasa kumalizika.

Baada ya kukata simu ya Malisa tu, JKS alipiga simu nyingine. Mara hii ilikuwa simu ya masafa marefu, alipga Paris, Ufaransa. Na mara moja ikaitikiwa.

"Hallo, naomba kuzungumza na Jean Yves Francois".

"Subiri kidogo", alijibiwa.

"Hallo Francois, nani anaita?".

"Yaani huwezi kutambua sauti".

"Ah JKS. Ehe, nipe habari".

"Habari nzuri, sijui wewe huko?".

"Huku salama, tunasubiri tu kwa hamu kusikia Umoja wa Mataifa mahakama ya mauaji ya Rwanda ianze lini".

"Nasikia itaanza miezi minne ijayo huko Arusha".

"Aha, majina?", Jean aliuliza.

"Majina ni yaleyale mpaka sasa".

"Kwa hiyo upande wa watu wetu hakuna aliyeguswa?".

"Bado kabisa, ila kumetokea hali ambayo inaweza kutuletea madhara".

"Hali gani?", Jean alihoji kwa shauku.

"Unakumbuka niliwahi kukueleza juu ya chama kiitwacho kwa kifupi PAM?", alimwuliza.

"Nakikumbuka na nimekitafiti vilevile kujua msimamo wake. Wanachama wake wanapigania umoja wa waafrika ili kuleta haraka uhuru wa watu weusi dhidi ya ukoloni mambo leo, ili watu weusi waweze kujiamulia mambo yao wenyewe. Na vilevile walikuwa mojawapo ya makundi yaliyotoa shinikizo katika mkutano wa Arusha ili mgogoro wa Rwanda umalizike kwa njia ya amani. Hata mkutano wa Algers, walikuwepo wawakilishi wao, niliwaona maana nilikuwepo. Haya sema watu kama hawa wanaweza kuleta madhara gani?", Jean aliuliza.

"Wanaweza kuleta madhara makubwa sana", JKS alimjibu na kisha akaanza kueleza kwa kirefu jinsi Malisa alivyomweleza, na hatua ambazo tayari zilikuwa zimechukuliwa.

"Huyu Willy Gamba ni hatari, anaweza kuchambua kila kitu mpaka akafikia ukweli unaweza kukugusa hata wewe", JKS aliasa.

"Lililopo ni kuzuia asiende", Jean alijibu.

"Tutamzuia vipi na hayuko chini yetu?", JKS aliuliza.

"Mbona huelewi, kwani maiti inasafiri?".

"Aha, sasa nimekuelewa, lakini hiyo ni kazi kubwa", JKS alijibu.

"Hiyo ni kazi ndogo kabisa, si umeeleza kuwa mtu wako ameeleza kuwa leo huyo Willy Gamba analala Arusha. Hotel ya Impala na chumba amekupa namba zake, au sikukuelewa vizuri?", Jean aliuliza.

"Ni sawa kabisa, alinipa kila habari bila kuelewa maana yake, na mimi aliponieleza sikuelewa habari hiyo itakuwa muhimu", JKS alijibu.

"Hiyo ilikuwa muhimu sana. Unakumbuka kuwa tuna watu wetu kule Arusha, ambao walikuwa wasafiri na Rais aliyeuawa, lakini kwa ajili ya ujumbe wa Rais wa Burundi hawakwenda na wapo kule Arusha kama wageni wa serikali yako?", Jean aliuliza katika hali ya kukumbusha.

"Hao! hata juzi nilizungumza na kiongozi wao maana alikuwa ametokea Ngala kwenda makambi ya wakimbizi wa Rwanda kwa ajili ya kuwachukuwa vijana kumi muhimu ambao waliingia Tanzania baada ya kufunga kazi kule Rwanda. Alikuwa anataka msaada wangu kwa ajili ya makazi, nami nimewafanyia mpango katika nyumba za mashirika ya serikali pale Arusha na sasa wako salama salimini", JKS alijibu.

"Hiyo ni kazi nzuri sana. Kwa kazi hiyo na kwa habari ulizonipa leo, nitapeleka dola za kimarekani elfu ishirini kwenye akaunti yako kule Uswisi, kufika kesho jioni pesa zitakuwa zimeingia. Na kama kazi hii ya usiku ikifanikiwa dola zingine elfu ishirini zitapelekwa", Jean alimweleza JKS.

"Asante sana, nami nitafanya kazi kwa upande wangu. Nitampigia simu kiongozi wao hapo Arusha, Bwana Phillipe Habimana, atume vijana wawili waimalize hiyo kazi. Umeshatoa agizo, na agizo lako litatimizwa", JKS alijigamba.

"Oke, vizuri; unajuwa vijana wetu wana ujuzi wa hali ya juu, na swala la kuua kwako si swala tena la maana wameishaua sana kiasi kwamba kuua kwao sasa ni sawa na kunywa chai", Jean alijibu huku akiangua kicheko cha kejeli.

"Tena sana, juzi tu kwenye kambi huko Ngala wamemaliza kuua vikaragosi vinavyojipendekeza kwenye serikali mpya, kwa kuwashawishi wakimbizi waanze kurudi ili ionekane serikali ya sasa imeshaleta amani na usalama Rwanda ili iweze kuungwa mkono na jumuia za kimataifa. Ni baada tu ya kumaliza hiyo kazi ndipo Phillipe alipokwenda kuwachukuwa kwa msaada wangu. Hivyo, nikiwaagiza leo, hakika huyu Willy ajihesabu ni marehemu maana bado wana mori kabisa", JKS alijibu.

"Haya basi, nipigie simu kesho, baada ya kumaliza hiyo kazi. Na kama ukisikia habari zingine zozote, fanya kama kawaida na mimi nitafanya kama kawaida yangu", Jean alijibu na kukata simu.

Jean na JKS walikuwa wanafahamiana yapata miaka mitano sasa. Uhusiano wao ulianza wakati JKS alipokuwa na wadhifa wa kuamua juu ya ununuzi wa silaha mbalimbali zilizokuwa zinahitajiwa na serikali ya Tanzania. Jean Yvers Francois alikuwa kijana bado yapata miaka therathini na minane, na alikuwa tayari mfanyabiashara maarufu sana duniani. Alikuwa akifanya biashara ya kuuza silaha katika nchi zinazoendelea, na alimudu sana kupata biashara hiyo kwa urahisi kwa vile watu wengi walisema kuwa alikuwa mtoto wa kiongozi wa ngazi za juu kabisa katika serikali ya Ufaransa.

Kwa kutumia wadhifa wa baba yake na umaarufu aliokuwa nao baba yake katika nchi zinazoendelea, kijana huyu hakukosa biashara hii ya silaha na biashara nyinginezo zilizokuwa zikipita mbele yake. Lakini vilevile alinong'onwa kuwa, kijana huyu alijua kuwazawadia waliompa biashara, hasa viongozi wa ngazi za juu katika nchi za Kiafrika. Kutokana na sifa hii ya kutoa asilimia kumi na zawadi zingine, kijana huyu alikuwa akitafutwa na biashara badala ya yeye kuzitafuta hata ikasemekana kwamba viongozi fulanifulani wa nchi za Kiafrika iliwabidi wazungumze naye kwanza kabla hawajatoa maamuzi yoyote muhimu ya kibiashara.

Kwa hiyo, wakati JKS alipoagizwa na serikali ya Tanzania kutoa zabuni ya kisiri kwa makampuni yanayotengeneza silaha, mara moja alimtafuta Jean, maana viongozi wenzake walishawahi kumweleza kama angetaka kunufaika na wenzake pia wanufaike basi Jean ndiye alikuwa mtu wa kuwasiliana naye. Ingawa wakati huo walikuwa hawafahamiani, lakini JKS alikuwa tayari ana anuani ya Jean kutoka kwa rafiki zake. Hivyo hakusita, akawasiliana naye. Ni baada ya kuwasiliana naye na kufanya biashara ya kwanza ndipo urafiki wa karibu sana ulipoanza kati yao.

Kwa vile Ufaransa ilikuwa na uhusiano wa karibu sana wa kiserikali na serikali ya Rwanda, Jean alijikuta ana uhusiano wa karibu sana na uongozi wa serikali ya nchi hiyo kuliko ilivyokuwa serikali za nchi nyingine za Kiafrika alizokuwa akifanya nazo biashara. Inasemekana kuwa, kwa njia moja ama nyingine, Jean ndiye aliyekuwa mshauri mkuu wa uongozi huo na hakuna uamuzi wowote uliofanyika bila yeye kuhusishwa. Kiuchumi, Jean alimiliki njia zote muhimu za uchumi wa Rwanda kwani uongozi wa serikali ya Rwanda ulimpa uwezo wa kufanya biashara

yoyote aliyoitaka nchini humo, na uongozi huo ulinufaika kwa kujilimbikizia mali, na kumwachia anyonye jasho la wananchi wa Rwanda kwa kununua mazao yao yote kwa bei rahisi na kuwauzia bidhaa kwa bei ghali.

Kwa jinsi hii Rwanda ilimtajirisha Jean na viongozi wa serikali isivyo kifani. Na ndio sababu wakati wa mkutano wa kusuruhisha pande zote za mgogoro wa Rwanda mjini Arusha, Jean alikuwepo. Inasemekana alimtumia sana JKS kujaribu kuipotosha serikali ya Tanzania ili isione ukweli wa mambo ulivyokuwa Rwanda kutokana na urafiki wao wa karibu uliotokana na kupeana bakshishi.

Baada ya Jean kukata simu, JKS alitafuta kitabu chake cha simu na kutafuta simu ya Phillipe Habimana kule Arusha. Baada ya kuipata alimpigia simu.

"Hallo Habimana".

"Habari za leo", JKS alijibu na mara moja Phillipe akaitambua sauti.

"Nzuri mzee, shikamoo".

"Marahaba, sikiliza kwa makini, nina kazi nataka vijana wako wakaifanye usiku huu, tafadhali sitaki makosa ya namna yoyote yafanyike kwani yanaweza kuleta madhara kwa suala lenu zima. Nimeshazungumza na Jean.

JKS alitoa maagizo yake kwa kirefu na akamalizia.

"Narudia tena, mtu huyu ni hatari sana; vijana wako wasifanye mzaha wakafikiria ni mtu wa kawaida, si wa kawaida, hadhari yote ichukuliwe".

"Hamna matatizo mzee, hesabu kazi imekwisha, tuonane kwenye msiba wa Willy Gamba", Phillipe alijigamba.

Ilikuwa saa kumi na mbili alfajiri simu ya JKS ilipolia na kumwamsha usingizini.

"Hallo, nani?", JKS aliuliza huku amebanwa na usingizi.

"Phillipe".

"Ehe, sema", alijibu kwa shauku.

"Matanga hayatakuwepo, mtu wetu hakulala pale, na hata hajulikani kalala wapi, alionekana akiingia lakini hakuna aliyemuona wakati akitoka. Funguo za chumba kaziacha chumbani, Kavurugavuruga kitanda lakini hakukilalia. Tumefanya utafiti

katika hoteli na nyumba zote za kulala wageni Arusha nzima,hayupo. Mtu wako ni mjuzi, naamini maneno yako", Phillipe alimalizia.

"Haya asante, kazi imeanza". JKS alikata simu baada ya kusema.

IV

Baada ya kutelemka Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere, Dar es Salaam, akitokea Arusha alikwenda kwenye ofisi za Tanzaniar za pale uwanjani na kwa bahati alimkuta meneja hajaondoka, hivyo akafanya mipango ya kukodi ndege yao kesho yake alfajiri ili impeleke Kigali. Ingawa ndege zao zilikuwa na kazi nyingi kesho yake, lakini kwa vile ile biashara ya kwenda Kigali ilikuwa nzuri, meneja alimkubalia ila akaomba Willy asaidie kupata ruhusa ya kutuwa kwenye uwanja wa ndege wa Kavihanda wa mjini Kigali. Willy alilipa na kuahidi kuwa angejitahidi kupata hiyo ruhusa. Alipewa kila kitu ambacho kingehitajika kule Kigali ili kibali kipatikane.

Willy alifika nyumbani yapata saa mbili usiku baada ya kupokelewa uwanja wa ndege na kuletwa moja kwa moja nyumbani na Ismail, dereva wa AVIS. Alitoa shilingi elfu tano akampa Ismail kama bakshishi.

"Asante sana mzee, gharama zitawekwa kwenye akaunti yako", Ismail alijibu.

"Kama kawaida. Asante kwa kuja kunipokea na kwa heri", Willy alijibu na kutelemka kwenye gari.

"Kwa heri mzee", Ismail alimwaga.

Pepe alikuwa jikoni akipika wakati Willy alipoingia ndani. Mara alipomwona alitoka jikoni akamkimbilia sebuleni huku akiwa ameshikilia kipande cha nyama.

"Karibu nyumbani bwana wee", kabla Willy hajajibu, Pepe alimkumbatia na kumbusu. Tumbo la Pepe lilipoligusa la Willy, akahisi mtoto akicheza tumboni.

Kitu ambacho kilimwongeza furaha. Willy, bila kujua akadondosha mkoba wake, na kuendelea kumbusu Pepe. Mara Pepe akamsukuma kidogo na kuangalia jikoni asije akaunguza, na kumwekea Willy kile kipande cha nyama alichokuwa ameshikilia mdomoni, kisha alitabasamu na kukimbilia tena jikoni ambako Willy naye alimfuata.

"Siku nyingine utafanya moyo wangu usimame kwa raha unazonipa", Willy alisema akiwa amemshikilia Pepe begani, huku Pepe akikaangiza nyama kwenye chungu.

"Sasa nimpe nani raha kama si wewe mume wangu", Pepe alijibu.

"Kuoa kutamu", Willy alijibu.

"Kutamu sana, kama ukioa ama kuolewa na akupendaye ki-kwelikweli", Pepe alijibu huku akimtupia jicho la mahaba.

Willy alimgeuza na kuanza kumbusu tena.

"Inatosha kwa sasa. Ngoja kwanza nikakuwekee maji uoge, halafu utakuta chakula tayari ndipo unieleze kwanini umechelewa kuja nyumbani", Pepe alieleza.

"Nakwambia kuoa kutamu, najisikia kama mtoto wa miaka mitatu, nilivyokuwa nafanyiwa na Mama Willy", Willy alijibu kwa dhati kabisa kwani kila aliporudi nyumbani Pepe alimfanya ajisikie kama mtoto, na hivyo kusikia raha isiyo kifani.

Baada ya kuoga na kula, huku wakizungumza mambo yao ya kawaida Willy alifikiria jinsi ya kuanza kumweleza Pepe juu ya safari yake.

Ni mpaka walipokwenda kulala ndipo Pepe alipotoa wasiwasi wake. Wakiwa wameingia kitandani na kujifunika shuka, Pepe alijilaza juu ya kifua cha Willy na kuuliza.

"Chifu keshanieleza huenda ukasafiri kesho, mbona husemi?".

"Mara moja Willy alimfikiria Chifu ambavyo alijaribu kumsaidia ili asipate tatizo lolote kuhusu masuala ya nyumbani.

"Nilikuwa najishauri nitaanzaje kukueleza".

"Unaenda kesho lakini", Pepe aliuliza kwa sauti kali kidogo.

"Ndio alfajiri", Willy alijibu kwa unyonge.

"Sawa", Pepe alijibu.

"Sawa ya ukweli au ya hasira?".

"Sawa ya kikwelikweli, naelewa. Naelewa ya kwamba mpaka umekubali kuondoka uniache, kweli ni lazima uende, nami yafaa nikubaliane nawe. Willy nataka uelewa kitu kimoja, najuwa unavyonipenda, na unajuwa ninavyokupenda kwa hiyo uamzi wako ndio uamzi wangu, najuwa lingekuwa jambo la hivihivi tu usingekubali na Chifu asingejaribu kama alivyojaribu kunisihi nikueleze. Nimeelewa. Willy, nakupenda Willy, nakupenda sana", Pepe alisema na kuanza kububujikwa na machozi ambayo yalianguka kifuani kwa Willy.

Kwa mara ya kwanza maishani mwake, Willy naye machozi ya mapenzi yalimtoka. Mara mtoto tumboni kwa Pepe alicheza na mara hii kwa fujo sana, na kwa vile walikuwa wamekumbatiana ndani ya shuka Willy naye alimhisi.

Kitendo hiki cha mtoto kiliwatoa kwenye haya mawazo yao ya majonzi ya kuachana kwa muda na kuwarudisha katika hali yao ya furaha ya kawaida".

"Mtoto hataki tuwe na majonzi", Willy alimnong'oneza mkewe.

"Haswa", Pepe alijibu na kumkumbatia kwa kujibana kabisa kwenye mwili wa mumewe na kuweka mguu wake juu ya mapaja yake.

# SURA YA NNE

KAZI IMEANZA

Baada ya kuzungumza na Phillipe JKS alimpigia simu ofisa mmoja wa usalama aliyekuwa anashughulikia maswala ya uchukuzi wa abiria. JKS ndiye aliyemsaidia sana ofisa huyu kupanda hadi kufikia ofisa usalama mwandamizi.

"Mulamba", JKS aliita baada ya simu kupokelewa.

"Ndiyo, nani mwenzangu?".

"Pole kwa kukuamsha, naona ulikuwa bado umelala, huyu ni JKS".

Mulamba mara moja usingizi ulimtoka na kuinuka kabisa kitandani na kuketi kwenye ncha ya kitanda.

"Ndiyo mzee, hapana nilikuwa nimeamka ila bado nilikuwa najinyooshanyoosha tu kwani jana nilichelewa kulala", alimjibu kwa woga. Ile sauti ya woga ilimfurahisha JKS maana alipenda na kufurahia kutetemekewa.

"Hamna neno, sasa sikiliza, hii ni amri toka juu kuliko hata mimi. Si unamjuwa Willy Gamba?".

"Ndiyo mzee, nani asiyemjua katika fani yetu hii", Mulamba alijibu.

"Amepewa kazi toka ngazi za juu, na jana alienda Arusha na ndege za Shirika la Ndege Tanzania. Kwa vile sasa hayuko tena kwenye ajira ya serikali, hii kazi amepewa nje ya mipango ya kiserikali maana ni kazi nyeti na serikali haitaki itambulike kuwa inahusika. Ila alitakiwa ajulikane yuko wapi kila wakati, lakini toka jana jioni hajulikani aliko. Sasa imeamriwa tutumie ofisi yako tujuwe yuko wapi na ripoti hiyo isiende kwa mtu yeyote ila mimi", JKS alimaliza.

"Hilo nitalifanya sasa hivi mzee, ila nataka kujua alikuwa anatarajia kwenda wapi baada ya kutoka Arusha?", Mulamba aliuliza.

"Baada ya kutoka Arusha alitakiwa kurudi hapa Dar es Salaam, halafu anende Kigali. Kuna ndege ya asubuhi sana ya ATC toka Kilimanjaro ambayo itaondoka saa moja, kama yumo nipe habari, kama hayumo tafiti ujuwe anakuja Dar es Salaam na usafiri gani, nipate habari haraka. Angalia usafiri wote mabasi, malori na kadhalika.

"Usiwe na wasiwasi mzee, nitakujulisha baada ya saa chache, tutampata tu. Tukimpata tumfanyeje?".

"Usifanye chochote, wewe eleza tu yuko wapi".

"Haya, asante".

"Kwa heri", JKS alikata simu.

Baada ya kukata simu ya Mulamba, JKS alipiga simu Paris kwa Jean na kumweleza mambo yaliyotokea Arusha na hadhari aliyokuwa amechukuwa tayari. Jean, akiwa bado na usingizi kwani Paris ilikuwa yapata saa kumi na nusu za asubuhi, tulikuwa tunapishana saa mbili.

"Nataka utakaponipigia tena simu unieleze kuwa tayari keshauawa, vinginevyo usinipigie simu mpaka utakapofanikiwa kazi hiyo. Natuma pesa leo asubuhi kupitia kwa yule rafiki yangu mwenye kampuni ya kitalii ya Concord Tours zikusaidie kukamilisha kazi. Vilevile nitawapigia simu na marafiki zangu wengine huko Afrika Mashariki wakupe msaada wowote utakaohitaji", Jean alimalizia na kukata simu bila bila kumsubiri JKS ajibu.

Kwa mara ya kwanza katika maisha yake JKS alisikia woga. Alizijua nguvu za Jean na akajuwa itabidi atimize hii kazi, vinginevyo mambo yangeweza kumgeukia. Alifikiria jinsi Jean alivyokuwa amemwahidi kumsaidia kuunyakuwa urais wa Tanzania na alikuwa anaujuwa uwezo wa Jean kuifanikisha azma yake hiyo. Na dhamira ya JKS kuwa Rais ilizidi vitu vingine vyote, lakini leo huyu Willy Gamba angeweza kumfanya akose nafasi hii. Asubuhi hii alisikia jasho la baridi likimtiririka mgongoni na kujisemea kwa sauti. "Kwa kila hali lazima aondoke".

Bila kujua amesema kwa sauti kubwa mke wake aliyekuwa amelala bado alishtuka na kuuliza. "Unasemaje?".

"Hapana, sijasema kitu", JKS alijibu.

Mke wake alimjua sana. Hivyo, akanyamaza lakini alijuwa mzee alikuwa anasumbuliwa na kitu fulani.

Willy alitua kwenye uwanja wa ndege wa Mwanza mnamo saa mbili na nusu za asubuhi. Asubuhi kabla hajaondoka nyumbani alimpigia simu rafiki yake mmoja ambaye alikuwa na wadhifa wa juu ndani ya Chama cha Msalaba Mwekundu na kumwomba msaada kati ya ndege zao zilizokuwa Mwanza moja impeleke Kigali.

Willy aliwahi kukisaidia sana Chama hiki, na huyu rafiki yake aliona bahati sana kupata fursa kama hii ili nae alipe angalau fadhila kidogo za Willy kwa yote aliyowahi kuwatendea.

"Bila shaka Willy, sasa hivi nitapiga simu Mwanza na hiyo saa mbili na nusu unayotegemea kufika Mwanza utakuta ndege ndogo ya injini mbili aina ya Cessina yenye namba MMT 3 ikikusubiri. Sisi tunaruhusiwa bila matatizo kutua Kigali kutokana na hali ilivyo Wilayani Ngara. Hivyo, huna haja ya kuhangaika kupata kibali cha kutua, hicho sisi tunacho na utakuta maofisa wetu pale Mwanza wameshawasiliana na Kigali", yule rafiki yake Willy alieleza.

"Nitafurahi sana, na kama vilevile mtawaeleza kuwa mimi ni afisa wenu", Willy aliongezea.

"Bila shaka", rafiki yake alijibu huku akicheka maana alijua Willy haendi Kigali bure.

Kwa hiyo, Willy alipotelemka ndani ya ndege ya kukodi ya Tanzanair alikuta ndege ya Chama cha Msalana Mwekundu iko tayari.

"Ina maana mimi sasa nitarudia hapa?", rubani wa Tanzanair alimuulizia alipomwona anashuka na mfuko wake.

"Ngoja kidogo", Willy alimjibu.

Willy alikwenda mpaka kwenye ile ndege na kumkuta rubani na ofisa mmoja wa Msalaba Mwekundu wakimsubiri Willy.

"Karibu mzee", wote wawili walitamka kwa pamoja Willy akawapa mikono kuwasalimia.

"Asanteni sana", alijibu.

"Sisi tuko tayari, ila tu tunaomba uende na ndugu yetu mmoja ambaye anaenda huko vilevile kikazi", yule afisa alimwambia willy.

Willy alimwangalia yule jamaa, na kumwona ni wa makamu yake na wa umbo lake.

"Sawa, lakini ningeomba aje na ile ndege ndogo ambayo nimekuja nayo ili rubani awe na mtu wa kuzungumza nae, maana hiyo nayo inakuja Kigali, ila kwa sababu lazima ijaze mafuta na kukaguliwa kidogo ndio sababu imebidi mimi nikifika tu

hapa nipate ndege nyingine kwa vile nina miadi maalumu ya kiserikali pale uwanja wa Kigali na mtu ambaye ataondoka saa moja kuanzia sasa", Willy alieleza.

"Basi, vizuri sana. Je, ndege yako ina vibali vyote vya kutua?", yule ofisa aliuliza maana alijua jinsi hali ilivyokuwa uwanjani pale Kigali.

"Hamna taabu, kila kitu kipo", Willy alijibu, kisha akaenda kwa rubani wa ndege yake.

"Sasa ukishajaza mafuta utakuja na yule bwana pale, naye anakuja Kigali. Ukishamshusha tu basi wewe urudi", Willy alimweleza.

Yule rubani alishangaa kwanini wasitumie ndege moja badala ya ndege mbili. Lakini kwa vile haikuwa shughuli yake na kwa vile alikuwa ameagizwa kwenda mpaka Kigali aliamua kubaki ameshangaa lakini atekeleze wajibu wake.

"Sawa mzee", yule rubani alimjibu huku sauti ikionyesha mshangao. Willy alitoa dola mia za kimarekani, akampa.

Tabasamu safi likaonekana usoni mwa rubani.

"Asante sana mzee", alijibu tena na kupeana mikono ya kuagana. Willy alikwenda kwenye ndege, na rubani wa Chama cha Msalaba Mwekundu akaiondoa ndege kuelekea Kigali ikiwa yapata saa tatu kasoro robo. saa za asubuhi.

Ilikuwa saa tatu na dakika kama tano hivi, Mulamba alipompigia simu JKS. JKS alikuwa tayari amefika ofisini.

Simu ya moja kwa moja kwa JKS ililia na haraka akainua. "Nani", aliuliza kwa shauku.

"Mulamba, mzee".

"Haya vipi mmempata?".

"Mzee huyu mtu tumeweza kupata nyendo zake zote, ila hatukuweza kumpata yeye kabisa maana alikuwa hatua moja mbele kila tulipokuwa karibu kumpata".

"Una maana gani, hebu sema mambo ya kueleweka", JKS aliuliza kwa ukali.

"Ndio nilitaka nikupe ripoti kamili mzee. Kutokana na taarifa za uchunguzi wetu, aliondoka Arusha jana kwa ndege ya kukodi ya Tanzanair, hivyo hakulala Arusha ila alilala hapa Dar es Salaam. Leo asubuhi ameondoka Dar es Salaam kwa ndege hiyo hiyo ya kukodi ya Tanzaniair na anaelekea Kigali. Habari za watu wangu

nilizozipata hivi punde ni kwamba ameondoka Mwanza mnamo saa tatu kamili kuelekea Kigali. Hali ndivyo ilivyo mzee. Sijui tukusaidie nini tena?", Mulamba aliuliza.

"Ndege hiyo ya Tanzaniar ni namba ngapi?", JKS aliuliza.

"Namba zake ni MHZT 12".

"Sawa basi asante, nikikuhitaji nitakutafuta".

"Haya, asante mzee", Mulamba alijibu huku akipumua kwani alikuwa amejawa na wasiwasi angetakiwa kufanya nini tena kwani hakutaka kazi yoyote ya kuhusiana na Willy Gamba, maana mtu huyu alikuwa ni moto wa kuotea mbali. Alibaki anashangaa tu hasa ni nini kilikuwa kinatokea kati ya serikali na Willy Gamba.

JKS alijishika kichwa na kujua kazi imekuwa ngumu na yeye peke yake asingeiweza. Huyu Willy Gamba alikuwa kweli kabisa mtu wa hatari na hakika kuwapo kwake Rwanda kungezua balaa, lazima kila njia ifanyike kabla hajaleta madhara. Hakukuwa na njia nyingine ila kurudi kwa Jean maana yeye alikuwa na uwezo mkubwa kufanya mambo Rwanda kuliko yeye. Uwezo wa JKS uliishia ndani ya mipaka ya Tanzania, isipokuwa tu propagada ya kisiasa ndio angeweza kusaidia kokote ulimwenguni kwani alikubalika sana duniani kote kisiasa. Ingawaje Jean alikuwa amemwamru ampigie simu ikiwa Willy ameshauawa, lakini JKS alionelea afadhali atukanwe kuliko kunyamaza. Aliinua simu akampigia Jean kwenye simu yake ya kutembea nayo (Mobile).

"Hallo", Jean alijibu baada ya kupokea.

"JKS hapa".

"Ehe, mambo mazuri?", Jean aliuliza kwa shauku.

"Hapana, mambo yanazidi kuwa magumu", JKS alijibu na akamweleza jinsi sasa Willy Gamba alivyokuwa anaelekea Kigali.

"Mbona mtu huyu nitampenda", Jean alijibu kwa kejeli.

JKS alinyamaza. Hakuwa na la kusema.

"Hapa kweli tunashughulika na mtu mjuzi, huyo anatakiwa apambane na watu wenye ujuzi kama yeye. Basi niachie huyo mtu kwa sasa. Nitarudi kwako baadae, nipe hiyo namba ya ndege na maelezo mengine yote kuhusu hiyo ndege na huyo mtu wako", Jean alimalizia.

JKS alimpa maelezo yote huku akifurahi kuwa Jean ameelewa na hakuweza kumkasirikia. Baada ya kumpa maelezo JKS alikata simu na kuinuka kitini na kwenda kusimama dirishani mwa ofisi yake na kuwaangalia ndege aina ya tausi waliokuwa wakicheza nje tu ya dirisha lake.

Mara mawazo yake yakarudi kwa Willy Gamba. Kuuawa kwa Willy ndio kupata kwake Urais, maana huyu mtu asipouawa anaweza kuchokonoa ukweli wa mambo na kuleta kashifa ambayo ingeweza kumgusa hata yeye kwani JKS alikuwa mmoja wa watu waliokuwa wanahusika na swala zima la Rwanda, tokea maswala ya kisiasa mpaka kufikia mauaji. Na serikali ya Tanzania ilikuwa imeweka mambo yote yahusuyo Rwanda chini yake na ofisi yake kwa vile aliaminika kuwa ni kiongozi mwadilifu.

Baada ya kukata simu ya JKS, Jean alipiga simu Rwanda kwa rafiki yake alikuwa ndani ya Jeshi la RPF. Baada ya RPF kushika madaraka Rwanda, Col. Gatabazi alikuwa wa kwanza kupata simu iliyofanya kazi. Hii yote ilikuwa kwa hisani ya Jean ambaye alikuwa na uhusiano wa karibu na mkuu wa jeshi la Ufaransa lililokuwa Rwanda pamoja na mkuu wa Idara ya Usalama wa Nje wa Ufaransa (DGSE). Inasemekana kuwa Jean ndiye aliyewasaidia hata kupata vyeo hivi kutokana na kuwa kwake karibu na uongozi wa juu wa serikali ya Ufaransa.

Jean alikuwa kama ndiye mshauri mkuu wa serikali ya Ufaransa kuhusu maswala ya Rwanda. Kutokana na kuwa kwake karibu na Rais pamoja na watu wote muhimu ndani na nje ya serikali ya Rwanda. Kwa hiyo baada ya Kigali kuangukia mikononi mwa RPF tu na maofisa wa jeshi hilo kujinyakulia nyumba za kukaa zilizokimbiwa na maofisa wa serikali ya MNRD. Col. Gatabazi ambaye siku zote alijulikana kama mkereketwa mkubwa wa RPF, hakuwa mkereketwa ila msaliti na ndiye aliyekuwa akitoa siri zote za RPF kwa Jean, na Jean akazitoa kwa rafiki zake wa serikali ya MNRD. Kwa hiyo, baada ya kupata nyumba tu Jean alihakikisha kuwa Col. Gatabazi anapata simu ili kila kilichokuwa kinaendelea ndani ya RPF kimfikie.

Kutokana na huo uhaini wake Col. Gatabazi alijipenyeza na kujiweka karibu kabisa na kiongozi wa RPF na akaaminika sana. Inasemekana alikuwa Mhutu, lakini mama yake alikuwa Mtutsi. Baba yake alifariki akiwa na umri wa miaka miwili na akakulia kwa mjomba wake na kwa vile alikuwa amechukuwa umbo la mama yake alitambuliwa kama Mtutsi tu. Ila yeye alijuwa ni Mhutu na inasemekana aliwahi kuambiwa kuwa baba yake aliuawa na wajomba zake kwa vile hawakutaka dada yao aolewe na Mhutu. Hivi kinyongo alikuwa nacho moyoni

na ndio sababu alipopata nafasi ya kuwasaliti Watutsi alifanya hivyo kwa moyo mmoja.

Baada ya serikali ya MNRD kuanguka na RPF kuingia, Jean alimhakikishia Col. Gatabazi kuwa serikali hiyo isingeweza kukaa madarakani kwa muda mrefu kwani ingepinduliwa na yeye angeiongoza serikali inayofuata. Jean alimhakikishia kuwa serikali ya Ufaransa isingeiruhusu serikali ya RPF ikae madarakani kwani viongozi wake walikuwa na mwelekeo wa Kiingereza kwa kukaa kwao Uganda na hivyo wangeathiri nguvu (influence) ya Ufaransa ndani ya Rwanda kitu ambacho Ufaransa isingekiruhusu kabisa. Kwa hiyo kwa kushirikiana na viongozi wa serikali ya MNRD waliokimbia na watu wengine walio ndani kama Col. Gatabazi kwa msaada wa serikali ya Ufaransa. Jean alikuwa anatayarisha jeshi la kuivamia tena Rwanda na kuchukua madaraka toka kwa RPF. Kwa hiyo, Col. Gatabazi alikuwa anajitayarisha kuwaggeuka wenzake mara wakati wa kufanya hivyo utakapofika.

Col. Gatabazi alikuwa anataka kutoka nyumbani kwenda ofisini kwake, Merridian Hotel, ambako ndiko ofisi zake zilikuwa kwani ndiye aliyekuwa anashughulikia uratibu wa shughuli zote za vikosi mbalimbali vya jeshi la RPF na kuripoti kwa mkuu wa majeshi.

Simu ililia. Hallo Col. Gatabazi?".

"Jean".

"Mbona leo unanipigia simu saa hizi? Saa zetu unazijuwa", Col. Gatabazi aliuliza.

"Kuna dharura", Jean alijibu na kumweleza juu ya Willy Gamba na athari za kuwa kwake Kigali.

"Hivyo ni vizuri hiyo ndege yake ingetunguliwa ikiwa hewani iwe mwisho wa tatizo la huyu mtu maana toka jana anatusumbua, nafikiri hiyo ndio njia rahisi", Jean alimalizia.

"Si Tanzania italalamika sana na kwa sasa hivi serikali ya RPF inataka sana kueleweka vizuri, hasa kwa serikali kama ya Tanzania", Col. Gatabazi alijibu kwa njia ya kuuliza swali.

"Usijali, Tanzania inaunga mkono kwa kusema hiyo ndege iliruka anga zetu bila ruhusa hata haikutoa habari huko Tanzania kama ilikuwa inakuja Kigali. Hilo niachie mimi na wewe utasikia itakavyokuwa maana utacheka", Jean alijibu.

"Basi ngoja niwahi kwani watatua kwenye dakika thelathini zijazo kutokana na maelezo yako ya saa walizoondoka mjini Mwanza".

"Asante, kwa heri, ila nipigie simu baada ya tukio".

"Sawa", Col. Gatabazi alijibu.

Ndege ya Chama Cha Msalaba Mwekundu ilitua kwenye uwanja wa ndege wa Kayibanda mjini Kigali yapata saa nne kamili. Willy Gamba alichukua mkoba wake na kutelemka.

"Asante", Willy alimshukuru rubani na kumpa dola mia za kimarekani.

"Asante sana mzee", yule rubani alishukuru na kufunga mlango tayari kwa kuruka tena.

Willy alikwenda moja kwa moja kwenye jengo la uwanja wa ndege na kuelekea Uhamiaji. Ulinzi uwanjani ulikuwa bado mkali lakini kwa sababu alikuja kwa ndege ya Chama Cha Msalaba Mwekundu na alikuwa amefanyiwa mpango na rafiki yake Dar es Salaam aje apokelewe na mmoja wa maafisa wa Msalaba Mwekundu walioko Kigali, yeye akiwa kama Afisa wa habari wa Msalaba Mwekundu kimataifa na ndivyo Chifu alivyomtayarishia pasipoti aliyoikuta nyumbani, taratibu zake pale uwanja wa ndege zilikwenda haraka bila kipingamizi chochote.

Katika pasipoti yake hii jina lake lilikuwa George Mambo.

Alipojitokeza tu nje, alimkuta mwenyeji wake aliyekuwa amevaa beji ya Msalaba Mwekundu na kwa vile na yeye toka alipotua tu aliweka beji aliyokuwa amepewa na Msalaba Mwekundu wakatambuana mara moja.

"Bwana George Mambo natumai", yule mwenyeji wake alisema huku akitoa mkono wa salamu.

"Ndio mimi. Habari zako", Willy alijibu na kusalimu.

"Nzuri, mimi naitwa Vicent Nyemazi, ni afisa wa habari hapa, na mimi ni Mhutu ila mimi siyo Mhutu mwenye siasa kali", Vicent alijibu huku akitabasamu.

"Vizuri sana na pole kwa yote yaliyotokea hapa nchini kwenu".

"Asante sana, ndio hali ya dunia. Gari nimeegesha hapo mbele", Vicent alieleza.

"Mkahawa wa hapa umefunguliwa?", Willy aliuliza.

"Ndio, uko wazi".

"Unajuwa nimeondoka asubuhi sana, sijanywa hata chai na ndege zetu kama unavyojuwa si kama ndege za abiria, hamna chochote hata kikombe cha chai", Willy alijibu huku akiangalia saa yake.

"Sawa, twende hapa kuna mkahawa mzuri, na hali imeanza kurudi kama zamani, hivyo vitu vingi vinaendelea kama kawaida.

Walipanda juu kwenye mkahawa na willy aliagiza kahawa na kipande cha mkate na Vicent akaagiza kahawa peke yake. Willy aliangalia saa yake kwa chati kabisa, akajuwa ile ndege ya Tanzanair ilikuwa karibu kutua, na alitaka tu kuona kama kungeweza kuwa na fununu za kuja kwake. Hii ilikuwa hadhari tu kwani aliamini hakuna mtu ambaye angeweza kujua kuwa anakuja kwa jinsi alivyokuwa ameondoka Dar es Salaam kisirisiri.

"Ah, vipi hali ya huko Ngara, nasikia hali ya wakimbizi ni mbaya sana, yaani chakula, maji na madawa ni taabu", Vicent aliuliza.

"Ni kweli hali ni mbaya, jumuiya ya kimataifa inajaribu kusaidia lakini wakimbizi ni wengi mno. Fikiria watu kama wa mji huu mnamo wiki moja watengeneze mji mwingine ambao haukuwepo kabisa, ambako ni porini tu hakuna huduma za kijamii za aina...". Kabla Willy hajamaliza kueleza mlio mkubwa ulitokea na mara ukatokea mlipuko. Willy na Vicent walikimbilia dirishani kuangalia kwenye uwanja wa ndege ambako ndiko mlipuko ulikotokea. Kwenye barabara zinakoondokea na kutua ndege wakaona vipande vya ndege vimesambaa na kuwaka moto.

"Kazi imeanza", Willy alisema na kumvuta Vicent mkono. Wakakimbilia chini kuangalia kwani vishindo vya kukimbia uwanjani vilisikika kutoka kila pahala.

Walipofika chini na kuelekea uwanjani walikuta magari ya jeshi aina ya Landrover yakiwa yamejaa askari yakielekea pale mabaki ya ndege yalipoangukia na wengine wakija huku kwenye jengo la uwanja ili kuzuia watu wasiende kule uwanjani.

Vicent na Willy walionyesha beji zao za Msalaba Mwekundu wakiomba wafike kwenye tukio lakini walikataliwa na askari ambao kwa sasa walikuwa wamechachamaa. Willy aligundua kuwa kumbe walishajua atafika na maskini yule rubani na afisa wa Msalaba Mwekundu waliuawa kwa kufikiri ni yeye. Willy alimshukuru Mungu kwa kumfanya afikiri na kufanya kama alivyofanya.

Kweli kama Msoke alivyosema, kazi hii tayari ilionyesha kuwa ni ya hatari. Ila kilichomshangaza Willy ni jinsi yule mtu aliyeshambulia ndege ya Tanzanair alivyojuwa kuwa yeye angekuwemo mle ndani ya ile ndege. Hii ilionyesha kuwa kati ya wale maafisa wa PAM miongoni mwao kulikuwa na msaliti, lakini kwa sasa hakukuwa na haja ya kufikiria hicho ila kufanya kilichomleta Kigali. Huyu msaliti angetafutwa baadaye. Jinsi ile ndege ilivyokuwa imepigwa na kombora. Willy alijua kabisa kuwa hakuna mabaki ya binadamu ambayo yangeweza kutambuliwa, kwani kombora lililotumika lilikuwa kubwa wakati ndege yenyewe ilikuwa ndogo.

"Twende zetu, nipeleke hotelini, acha wanajeshi wafanye kazi yao", Willy alimvuta Vicent wakaondoka huku wakisesera kuelekea kwenye gari la Vicent.

"Kwanini wameipiga ile ndege?", Vicent aliuliza huku akifungua mlango wa gari.

"Huenda ilikuwa na hatari, bado unajuwa mambo hayajatengamaa hapa", Willy alijibu.

"Unafikia hoteli gani?".

"Nafikiri jaribu Meridian Hotel kama kuna nafasi", Willy alijibu na kuikacha Hotel Des Mille Collines aliyokuwa amepangiwa na rafiki za Musoke, kwani sasa hakukuwa tena na kumwamini mtu yeyote kwa vile hakujuwa nani alikuwa ametoa amri ya kupigwa kombora ndege aliyopaswa kuwemo na huyo mtu alikuwa anajuwa habari kiasi gani kumhusu yeye Willy.

"Sawa, pale hotelini wanatua na watu wetu kutoka mataifa ya nje wako pale. Na vilevile pana usalama maana ofisi zingine za jeshi ziko pale, na maafisa wengine wa jeshi wanakaa pale", Vicent alimweleza Willy. Wakati wakielekea Meridian Hotel walikutana na magari madogo ya jeshi, kama matatu, yakielekea uwanja wa ndege. Willy aliona wengi walikuwa maofisa wa vyeo vya juu na akahisi walikuwa wanakwenda kutathimini tukio lililotokea.

Walipofika Meridian walikuwa watu wako vikundi vikundi wakizungumza, bila saka walikuwa wamepata habari za tukio la uwanja wa ndege. Vicent likwenda mapokezi na kuzungumza na mmoja wa wafanyakazi wa pale ambaye alionekana kumfahamu sana, na baada ya muda kidogo Willy aliitwa kujaza fomu za kupatiwa chumba. Baada ya kupewa funguo alichukua mkoba wake na vicent akamweleza kuwa atamsubiri kwenye mkahawa wa hoteli.

"Si utataka twende ofisini?", Vicent aliuliza.

"Bila shaka", Willy alijibu.

"Basi utanikuta hapo kwenye mkahawa".

"Asante", Willy alijibu na kuelekea kwenye ngazi kwani alikuwa ameelezwa lifti zilikuwa hazifanyi kazi. Alikuwa amepewa chumba namba 412, ghorofa ya nne.

V

Baada ya Col. Gatabazi kuhakikisha kuwa hakuna kitu kilichobaki ndani ya ndege na ndege yenyewe, alielekea nyumbani kwake ili akampashe habari Jean. Alipompata Jean alimweleza. "Kazi tayari, mtu wako hata mfupa haukuonekana, kawa hewa".

"Safi sana, hakika mimi hupenda mtu wa vitendo na siyo maneno", Jean alijibu.

"Lililobaki ni la kujieleza kwanini tumeipiga hiyo ndege, lakini tayari mkuu nimemwandikia taarifa safi ambayo hawezi kuwa na mashaka nayo. Wasiwasi wangu Tanzania tu", Col. Gatabazi alieleza.

"Nilikwambia Tanzania niachie mimi. Tuongee jioni. Kama kawaida mzigo mwingine unatua leo, na ni shehena kubwa", Jean alijibu na kabla Col. Gatabazi hajajibu alikata simu.

Baada ya kukata simu ya Col. Gatabazi. Jean alimpigia simu JKS, Dar es Salaam. JKS, aliyekuwa na wasiwasi mkubwa aliipokea simu haraka ilipolia. "Nani".

"Jean hapa. Kigali Bingo!!, mambo safi".

# SURA YA TANO

MIGUU YA NYOKA

Willy alipowasili kwa Col. Thomas Rwivanga, alimkuta anamsubiri. willy alikuwa amemweleza kuwa angekuwa anaendesha gari la Msalaba Mwekundu na angekuja peke yake bila  Vicent. Col. Rwivanga alikuwa amemweleza njia ya kupita mpaka huko nyumbani kwake, Kimihurura.

Col. Rwivanga aliposikia mwungurumo wa gari alitoka nje na kwenda kumpokea Willy.

"Habari yako?", Col. Rwivanga alimsalimia Willy huku akimpa mkono.

"Safi, na wewe?", Willy alimjibu.

"Safi kabisa, nafurahi sana kuonana na wewe, Mzee Musoke amenieleza habari zako, nami nilikuwa na shauku kubwa ya kukutana nawe. Karibu ndani", Col. Rwivanga alimkaribisha Willy.

"Asante sana, nimekaribia", Willy alijibu huku akiingia ndani na kuketi.

"Nikupe kinywaji gani?|".

"Klabu soda inatosha", Willy alijibu.

Col. Rwivanga alileta Klabu soda mbili na kuzifungua, wakaanza kunywa.

"Ehee, habari ya maisha?", Col. Rwivanga aliuliza.

"Safi, naamini Mzee Musoke amekueleza kwanini niko hapa".

"Ndio amenieleza".

"Imebidi nikuone mapema maana kuna jambo lililotokea ambalo linaonyesha kuwa katika uongozi wenu kuna mtu aliyejuwa kuwa mimi nimo ndeani ya ile ndege iliyotunguliwa leo asubuhi, akiwa na nia ya kuniua, bahati nzuri sikuwemo ila nilitakiwa kuwemo kwenye ndege hiyo. Na ninafikiri yeyote yule aliyeagiza hiyo ndege itunguliwe anaamini kuwa mimi sasa ni marehemu", Willy alimweleza Col. Rwivanga ambaye wakati huo alikuwa akimwangalia kwa mshangao mkubwa.

"Hivi swala unaloijia hapa ni nyeti kiasi hicho, mpaka wanataka kukuua! Mimi Mzee Musoke aliponieleza, sikutegemea kama kunaweza kuwa na hatari yoyote,

maana wewe unakuja kutathimini tu hali ya mambo yalivyotokea mpaka kufikia watu wengi namna ile kuuawa. Lakini sasa inaonekana kuja kwako kumetia watu wasiwasi na wameamua kukumaliza kabisa hata hujaanza huo uchunguzi. Ndugu Gamba hii inaonekana kuna jambo kubwa ambalo hata sisi hatulifahamu. Hii ni hatari na ni hatari kubwa", Col. Rwivanga alijibu.

"Je, unaweza kujuwa ni nani au ni vipi ile ndege ilitunguliwa?, Huenda tukaanzia hapo ndipo tutajuwa hasa ni nani anahusika na kwa sababu gani?", willy aliuliza.

"Taarifa niliyopata kuhusu tukio hilo kwenye kikao cha makamanda wa jeshi, ambayo imetolewa na Col. Gatabazi, ambaye ndiye mkuu wa utawala jeshini, inasema ndege hiyo ilipoitwa kwenye rada ijitambulishe haikufanya hivyo. Kwa hiyo Luteni Silasi Biniga, ambaye ndiye anaongoza wanajeshi wanaolinda uwanja alimtaarifu Meja Juvenal Mukama, Mkuu wa Kikosi cha Mizinga kinacholinda mji huu, ambaye alitoa amri kuwa kama inakaribia kutua na bado haitoi taarifa yoyote itunguliwe. Na ndivyo ilivyofanyika. Baada ya kujuwa kuwa ilikuwa ndege ya kukodi ya kampuni ya kukodisha ndege ya Kitanzania, habari zilipelekwa Dar es Salaam, na habari tulizopata toka Wizara ya mambo ya Nje ya Tanzania ni kwamba ndege hiyo ilikuwa imekodiwa na mtu mmoja kwa jina la Juma Omari aliyejitambulisha kama mwandishi wa habari na masuala yote ya kupata vibali vya kutua alifanya mwenyewe. Hivyo, serikali ya Tanzania inaunga mkono kutunguliwa kwa ndege hiyo ambayo imeingia anga ya watu bila kibali wala kujitambulisha na huku rubani na kampuni hiyo ikijuwa hali ya hatari iliyomo nchini Rwanda. Taarifa hiyo tumeipata jioni hii na serikali ya Tanzania imezidi kusema itaichukulia hatua kampuni hiyo ya ndege kwani inaweza kuwa inatumiwa na maadui wa Rwanda na kuweza kuleta uhusiano mbaya kati ya nchi zetu rafiki", Col. Rwivanga alieleza na ukawa ni wakati wa Willy kushangazwa na maelezo hayo.

"Rafiki yangu, hapa kuna jambo kubwa maana sababu ya kutunguliwa ndege hii ni moja tu, ambayo ni kutaka kuniua mimi. Lakini sasa maelezo ya makamanda wenu. Col. Gatabazi na maelezo kutoka Dar es Salaam, yamenichanganya kabisa na nahisi kuna kitu kikubwa tusichokijua", Willy alijibu.

"Sasa tufanye nini?", Col. Rwivanga alimwuliza.

"Kwanza, nataka aliyetaka kuniua aendelee kufikiri kwamba ameniua. Pili, huenda huyu Lt. Silasi Biniga anaweza akawa na habari zinazoweza kutusaidia kufumbua hiki kitendawili hivyo anafaa kuonwa na kuulizwa", Willy alijibu.

"Basi niache huyu mimi nitamwuliza", Col. Rwivanga alijibu.

"Hapana, niachie mimi, swala hili linaweza kuwa vilevile linaugusa uongozi wenu. Mimi nikiwa mtu baki naweza kupata ukweli bila kuleta kasheshe sasa hivi. Ni lazima tujitahidi tujue undani wa jambo hili maana ni zito. Naomba tu unieleze huyu Luteni Biniga anakaa wapi nami nitaenda kumwona", Willy alijibu.

"Inaweza kuwa hatari kwako, unajuwa hawa watu ni wanajeshi safi", Col. Rwivanga alimwasa Willy.

"Usijali, hatari ndio jina la kazi yangu", Willy alijibu.

Wote wakacheka, maana Musoke alikwishampa Col. Rwivanga maelezo kamilifu kuhusu Willy na uwezo wake.

"Sawa, huyu Luteni Biniga anakaa barabara ya tatu tu kutoka hapa kwangu, sehemu hiihii ya Kamihurura". Kisha akamweleza mtaa na nyumba ilipo.

"Sasa hivi naanza kushangaa, wakati wanajeshi wa cheo chake wengi bado wako kambini na wengine wako huko Ndera ambako ndiko kuna nyumba za maofisa wa ngazi ya chini yeye anakaa sehemu ambayo wanakaa maofisa wa ngazi za juu. Sijui huenda ikawa tu bahati yake", Col. Rwivanga alisema kama vile anajisemea mwenyewe.

"Nafikiri nikionana naye nitajua. Naona niende kama saa tatu hivi. Nitaacha gari hapa na kwenda kwa miguu", Willy alisema.

"Uamzi wako. Kwa vile bado kuna muda mpaka saa tatu ngoja nitengeneze chakula kidogo", Col. Rwivanga alieleza.

"Na mimi nitakusaidia kupika, kupika ni moja ya starehe zangu", Willy alieleza huku wakiinuka kuelekea jikoni.

Willy alipofika kwenye nyumba ya Luteni Biniga taa za ndani zilikuwa zikiwaka. Nyumba hii ilikuwa imezungushiwa ua kama alivyokuwa ameelezwa na Col. Rwivanga. Badala ya kubisha hodi langoni aliamua kupita kwenye uchochoro, akapanda ukuta kisha akatumbukia ndani. Alitambaa chini kwa chini mpaka akaufikia ukuta wa nyumba hii. Dirisha la nyuma lilikuwa limefungwa, hivyo aliendelea kuambaa na ukuta. Ndipo aliposikia sauti za watu wakizungumza na kucheka. Alichungulia dirishani na kuwaona watu watatu. Wanaume wawili na mwanamke mmoja. Mazungumzo yao yalikuwa kwa lugha ya Kifaransa, ambayo

Willy aliielewa vizuri sana, mazungumzo yao ndiyo yaliyomshitua na kumweka chonjo.

"Kazi mimi nimeifanya kwa ustadi mkubwa. Hiyo pesa kweli iko kwenye akaunti yangu Nairobi?", mmoja wa wale vijana alimwuliza yule mwanamke.

"Siyo wewe tu, nyote kesho pigeni simu kwenye benki zenu. Mambo safi. Nimeelezwa na wakala wa mlipaji kuwa pesa zimetumwa kwa njia ya 'swift' na tayari ziko kwenye akaunti zenu", yule mwanamke alijibu.

"Mimi nilihitaji kulipwa dola laki moja. Ndizo zilizotumwa na kuwekwa kwenye akaunti yangu?", yule mwanaume wa pili aliuliza.

"Ndio. Sasa kwenye akaunti yako kuna dola laki tatu. Zimeingia pamoja na zile za malipo ya kuwatorosha wale makamanda wa Intarahamwe kwenda Zaire", yule mwanamke alijibu.

"Kama kesho nikijuwa pesa yangu yote hiyo iko benki, basi mimi nitatoroka kwenda Kenya. Halafu Afrika Kusini. Sitaki kukaa hapa tena, tusije tukabainika kuwa tuko kwenye upinzani", mwanaume wa pili alisema.

Hapa Willy aliamini kuwa wakati wa kukabiliana ana kwa ana na watu hawa ulikuwa umefika kwani walionekana kana kwamba wanataka kuondoka. Mawazo na akili ya Willy yalivutika sana kwa yule mwanamke kuliko hata kwa wale wanaume wawili ambao alihisi ni Luteni Silasi Biniga na Juvinali Mukama. Alipogeuka tu kutaka kwenda kubisha hodi kwenye mlango wa mbele, alijikuta akiuangalia mtutu wa bunduku kubwa aina ya 'Sub Machine Gun'.

"Usisogee hata hatua moja. Hapohapo ulipo weka mikono yako juu, geuka nyuma na utembee kuelekea mlango wa mbele ya nyumba hii", Willy alimrishwa na yule askari na kutii amri kama alivyokuwa ameamriwa.

"Nani huyo tena", Silasi Biniga aliuliza katika hali ya mshangao.

"Nini Ananie", Juvinali naye aliuliza.

"Inkotanyi", Ananie alijibu.

"Bibiane wewe nenda. Sisi ngoja tujuwe huyu mtu ni nani?", Juvenali alimweleza yule mwanamke huku yeye na Luteni Biniga wakichukuwa bastola zao na kutoka nje kwenda kumkabiri mtu huyu aliyekuja kuwapeleleza ili kabla hawajamuua wajuwe ni nani na anajuwa nini kuhusu wao. Wakati Bibiane anatoka ndani

alikutana na Willy pamoja na mtu aliyemkamata, wakiwa wamefika mbele ya nyumba, kwenye mlango wa mbele.

"Simama hapo", Ananie alimwamru Willy huku akiwa bado ameweka mikono yake kichwani. Bibiane alipotoka nje alimwangalia Willy. Willy naye akamtazama. Kulikuwa na mwanga wa kutosha kuweza kumtambua mtu. Bibiane alimwemweseka kwa Willy kisha akalekea kwenye lango kubwa la kutokea nje na kutokomea gizani.

"Luteni Biniga..., lazima mtu huyu ni Inkotanyi, amekuja kupeleleza kuhusu tukio la leo", Ananie alimwambia Luteni Biniga walipotoka nje pamoja na Juvinali. Luteni Biniga alimwangalia Willy na kwa sura yake akabaini kuwa mtu huyu hakuwa Mnyarwanda. Bila kuchelewa Luteni Biniga alimpiga Willy kwa kitako cha bastola kwenye paji la uso na Willy akaanguka chini. Alipoanguka Juvinali naye alimpiga teke la tumboni. Willy alipotaka kuinuka alipigwa teke la ubavuni. Ni hapa ambapo mambo yaligeuka. Baada ya Juvinali kutupa teke kali lililompata Willy vilivyo ubavuni. Willy akahisi amevunjika mbavu, kama sumaku.

Willy aliunasa mguu wa Juvinali kabla haujarudi na kuupinda, kisha akauvuta upande wake, haraka sana akamlalia juu. Hii yote ilitokea kwa haraka mno kiasi cha kuwatatanisha Luteni Biniga na Ananie wasijuwe wafanye nini kwani wangefyatua risasi wangemuua Juvinali. Bastola ya Juvinali ilianguka chini karibu yao. Tena kwa kutumia nguvu zote alizokuwa nazo Willy alimrusha Juvinali kwa Ananie aliyekuwa kama hatua mbili kutoka pale walipokuwa. Juvinali akamkumba Ananie, wakaanguka huku bunduki ya Ananie ikitema risasi zilizomwingia Juvinali na kumwua hapohapo.

Wakati Willy alipomrusha Juvinali kwa Ananie. Haraka aliirukia ile bastola na kumpiga risasi kadhaa Luteni Biniga. Kabla hajafyatua bastola yake, risasi zikampata Luteni Biniga kwenye paja la uso na kumwua pale pale. Ananie naye kwa kutumia nguvu zake zote. Alijaribu kuitoa maiti ya Juvinali ili aichukuwe tena bunduki yake. Lakini hakuwahi. Willy alimpiga tena teke la kichwa na kumtoa fahamu. Willy akaivuta maiti ya Juvinali na kuitoa juu ya Ananie na kuanza kumvuta Ananie ili aweze kumuuliza maswali. Mara akasikia mlio kama wa king'ola. Akajuwa ama yule mwanamke ameripoti au ule mlio wa bunduki na bastola umesikika. Hivyo akajuwa angekutwa pale, kwa hasira aliivunja shingo ya Ananie na kumtupa chini. Akakimbilia ukutani. Akauparamia ukuta na kuangukia kwenye uchochoro wa mtaa wa pili; akakimbilia kwa Col. Rwivanga.

Alipoingia nyumba ya Col. Rwivanga. Ndipo Col. Rwivanga alipojuwa kuwa alipokuwa ameumia sana. Col. Rwivanga alikuwa ameusikia mlio wa bunduki lakini kwa Kigali halikuwa jambo la ajabu, ingawa alikuwa na wasiwasi. Lango la ua wake lilipofunguliwa tu alikuwa nje na ndipo alipomwona Willy akiingia huku akipepesuka. Col. Rwivanga alimsaidia wakaingia ndani. Willy alikuwa anatoka damu puani, Col. Rwivanga akajuwa kuwa alikuwa ameumia sana maana alipoonekana kama ana nyuso mbili kwa vile paji lake lilikuwa limevimba vibaya sana.

"Utadhani umekanyagwa na trekta", Col. Rwivanga alisema baada ya kumwona Willy.

"Nakwambia ni zaidi ya trekta. Sijawahi kupigwa teke lenye nguvu kama lile", Willy alijibu.

Dkt. Daniel Robinson alikuwa daktari mkuu wa Hospitali ya King Faisal mjini Kigali na alikuwa rafiki mkubwa wa Col. Rwivanga kabla Dkt. Robinson hajaja Rwanda alikuwa daktari katika Hospitali ya Mulago mjini Kampala, ambako alikuwa akiishi karibu na Col. Rwivanga. Na kwa muda wote walipokuwa Kampala walikuwa marafiki wa karibu sana.

Kwa hivyo wakati RPF walipoingia tu Kigali, Col. Rwivanga ndiye aliyekuwa kiongozi wa kikosi cha kwanza kabisa kilichoongoza mapambano dhidi ya majeshi ya serikali. Na kituo cha kwanza kabisa ni kuwaokoa watu waliokuwa Hospitali ya King Faisal ambako kuliwa na maelfu ya watu wakiwa pamoja na rafiki yake Dkt. Robinson. walikuwa wamejisalimisha ndani ya Hospita, lakini baada ya Intalahamwe kuwa wamewaua watu wengi Hospitali hapo pamoja na wagonjwa.

Baada ya Col. Rwivanga kuingia na kikosi cha kulinda usalama, watu wengi walipona. Siku zilizofuata majeruhi na wengineo aliponea katika Hospitali hiyo, hivyo Col. Rwivanga alimpigia simu Daktari Robinson ambaye ni Mzungu Mwingereza na kumweleza juu ya Willy kujeruhiwa.

"Niko njiani!", Dkt. Robinson alimweleza Col. Rwivangga, wakati walipokuwa wanamsubiri Daktari, Willy alimweleza Col. Rwivanga yote yaliyotokea nyumbani kwa Luteni Silas Biniga.

"Nini maana ya Inkontanyi?, maana waliniita hivyo", Willy aliuliza baada ya kumaliza maelezo yake.

"Inkontanyi huwa ina maana ya RPF. Maana yake hasa ni mpiganaji mkali na maarufu katika Kinyarwanda. Lilikuwa ni jina lililopewa kikosi kimoja cha Mfalme wa Bugiri katika karne ya kumi na tisa hivyo. Walihisi kuwa wewe utakuwa ni mpelelezi wa RPF", Col. Rwivanga alieleza.

"Kwa hiyo. Inamaana wao siyo RPF", Willy aliuliza.

"Bila shaka, kama ulivyosikia na hili limenitia wasiwasi sana kutambua kuwa katika uongozi wa katikati. Na bila shaka wa juu wa RPF tumeingiliwa na wasalti. Kinachoonekana wazi ni kuwa hawa waliopambana nawe nao ni watu wanaofanya hivi vitendo ni wapenda pesa. Sasa mtu au kikundi hatari ni kile kinachotoa pesa hicho ndicho yafaa tukijuwe na kukiangamiza ili Rwanda iweze kurudi hali yake ya amani", Col. Rwivanga alijibu.

"Basi mtafute yule mwanamke niliyesikia wakimwita Bibiane na jibu lako utakuwa umelipata", Willy alijibu huku akionekana kuwa maumivu yalikuwa yamezidi. Mara akasikia honi ya gari.

"Daktari huyo rafiki yangu, ngoja utubiwe usife maana kazi sasa ndiyo imeaanza", Col. Rwivanga alimtia moyo Willy.

Col. Gatabazi alikuwa kati ya watu wa kwanza kufika kwa Luteni Silas Biniga, maana alikuwa akiishi nyumba ya nne tu kutoka pale. Alipofika hakuamini macho na akili yake ilishindwa kukubali. Watu wote hawa waliouawa walikuwa watu makini katika kundi lake, watu ambao alijua ndio wangemsaidia kuchukua madaraka muda utakapofika. Hili jambo lilimshitua sana. Watu wote hawa walikuwa askari shupavu, jasiri na waliojuwa kazi yao vizuri.

Yeyote yule aliyefanya kitendo hicho hakuwa mtu wa kawaida na kama ni kikundi, hakikuwa kikundi cha kawaida. Hawa watu watatu walikuwa na uwezo wa kuangamiza kikosi kizima cha jeshi la maadui lakini leo wameuawa kirahisi na wote kwa pamoja! Suala hili lilimshitua sana Col. Gatabazi, akaingiwa na woga na wasiwasi.

Gari la jeshi lenye king'ola, lilikuwa tayari limefika pale likiwa na askari wa doria wa sehemu zile, askari hao walifika mara baada ya kusikia milio ya risasi.

"Vipi hamjaona au kukutana na mtu au watu wowote waliofanya kitendo hiki?", Col. Gatabazi aliwauliza wale askari wa doria kwa ghadhabu.

"Hapana afande, kote hapa ni shwari", mmoja wapo alijibu.

"Haiwezekani kuwa shwari wakati maafisa wanaotegemewa kama hawa wameuawa hovyohovyo hivi", Col. Gatabazi alieleza tena kwa ukali.

"Huenda wameuana wao wenyewe afande", askari wa pili wa doria alijibu.

Col. Gatabazi alimwangalia kwa jicho baya mpaka yule askari akarudi hatua moja nyuma.

"Chukueni hizi maiti pelekeni hospitali na poteeni hapa mara moja", Col. Gatabazi aliamrisha mara moja.

Col. Gatabazi alirudi nyumbani kwake ili apige simu Ufaransa. Alipofungua mlango wa mbele aliukuta uko wazi. Alishituka, akatoa bastola yake tayari kukabiliana na lolote ambalo lingetokea mbele yake. Alifungua mlango kwa ghafla huku bastola yake ikiwa tayari tayari.

"Vipi! mbona wasiwasi?", Bibiane alimuuliza huku akiweka mguu mmoja juu ya mwingine pale sebuleni alipokuwa ameketi.

"Hujui kumetokea mauaji mabaya sana usiku huu na vijana wetu watatu wameuawa?", Col. Gatabazi alihoji huku akirejesha bastola yake kwenye mkoba wake na macho yake yakiangalia mapaja ya Bibiane ambayo yalikuwa yameachwa wazi kwa kitendo chake cha kuweka miguu juu ya mwingine na kufanya nguo yake iliyokuwa fupi na ya kubana kuyaacha wazi.

Bibiane Habyarimana alikuwa mtoto wa Kinyarwanda ambaye baba yake alikuwa Mhutu na Mama yake chotara wa Kitutsi na Kifarasa. Alikuwa msichana aliyeumbika kwa sura na mrembo katika warembo. Alikuwa na urefu wa futi tano na inchi nane, hivyo, alikuwa mwanamke na urefu wa kutosha. Alikuwa na nywele ndefu za singa, macho makubwa ya blue, mashavu ya kumimina, pua ya kuchonga, midomo ya tasi, meno meupe yaliyopangika na kuacha mwanya kwenye safu ya juu. Hakika, alikuwa kapendelewa na muumbaji. Mwili wake mzima ulikuwa na muundo wa nyigu, juu mwembamba chini kajaa, akimalizia na miguu minene ivutiayo macho.

Ilimchukua Col. Gatabazi muda mrefu kupata la kusema maana kila alipoonana na msichana huyu alijikuta ulimi wake unakuwa mzito, anashindwa hata kusema. Mara nyingi alipatwa na kigugumizi kwani moyo ulimwenda mbio.

"Aliyewaua mimi nimemwona", Bibiane alieleza bila wasiwasi utafikiri alikuwa anazungumza kitu cha kawaida tu.

"Unasemaje?", Col. Gatabazi alimuuliza kwa mshangao.

"Aliyewaua nimemuona mimi. Nilikuwepo alipofika pale kwa Luteni Biniga", Bibiane alijibu tena kwa utulivu, kisha akasema, "Hamna hata kinywaji humu ndani". Kila wakati Col. Gatabazi alishangazwa na tabia ya huyu binti.

"Kinywaji kipo, huenda kweli tunakihitaji maana sasa wewe unazidi kunichanganya", Col. Gatabazi alisema na kuelekea kwenye kabati la vinywaji akatoa chupa ya whisky na gini, akaleta barafu na glasi mbili.

"Utakunywa nini?".

"Whisky niwekee barafu tu usiiharifu na maji".

"Sawa mama, ehee unamaje eti ulikuwepo kwa Luteni Biniga?", Col. Gatabazi aliuliza kwa shauku ya kutaka kujua.

Bibiane alimweleza kwa kirefu yaliyotokea pale kwa Luteni Biniga na kumalizia, "Watakati natoka ndani walikuwa wakimwuliza maswali pale nje, awaeleze yeye ni nani. Sikuwa na wasiwasi maana nilijuwa yule kaisha. Mbele ya wale wanaume hakuna ambaye angefanya kitu. Niliposikia risasi zinalia ile ya kwanza nilijuwa kauawa, lakini niliposikia milio ya risasi inazidi nikawa na wasiwasi nikarudi haraka kuchungulia na nikaona uliyoyaona, lakini mimi nilikuwa na bahati ya kumwona akiruka ukuta upande ule mwingine, akapotelea gizani. Yule ni mwanaume wa shoka na hapa kazi ipo, sina shaka yule ni Willy Gamba kama Jean alivyomwelezea. Hivyo, umeshindwa mtihani wako wa kwanza huyu mtu hakufa ndani ya ile ndege mliyoitungua. Fanya utafiti, utakuta amekuja na ndege nyingine, kakuzidi maarifa, tayari alishajuwa ni Luteni Silas Biniga aliyeamrisha ile ndege kupigwa. Mtu huyu ni hatari, mbona ni hatari sana! Kazi kwako Gatabazi. Kama unataka Uras kwanza inakubidi huyu mtu ummalize. Hizi habari zitamsikitisha sana Jean, wewe unajua.

"Usipommaliza haraka basi ujuwe wewe umekwisha kwani atakuumbua na RPF watakumaliza na utakuwa umewaangamiza Wahutu", Bibiane alimalizia na tabasamu la mauti.

Woga ulimwingia Col. Gatabazi maana naye alihisi kuwa huenda yule alikuwa Willy Gamba. Rwanda hakukuwa na mtu mwenye uwezo kama huo. Jean alimweleza kwa kirefu uwezo wa huyo Willy Gamba na sasa aliudhihilisha. Vilevile, alijuwa Jean angekasirishwa sana kuona huyu mtu amejipenyeza mpaka kuleta maafa makubwa hivi.

Mtu wa kuweza kumsaidia kumweleza Jean mpaka amwelewe na kumsaidia katika mapambano na mtu huyu alikuwa ni Bibiane. Ingawa alikuwa akimtamani sana Bibiane, lakini alikuwa mwangalifu sana asimguse maana alijuwa siku moja angeweza kumtumia.

Bibiane alikuwa karibu sana na Jean alikuwa mpenzi wake lakini vilevile Bibiane alikuwa mhitimu wa fani ya upelelezi na usalama na akiwa amesomeshwa kwa msaada wa Jean. Jean alikuwa akifanya mambo yake kwa ufasaha. Alihitaji kuwa na mtu Afrika Mashariki na Kati ambaye angeangalia mambo yake bila kuhisiwa. Pamoja na kuwa alikuwa ametumbukia katika lindi la mapenzi na Bibiane, lakini kwa upande mkubwa alimtumia Bibiane kufanikisha mambo yake yaliyokuwa yakimletea maslahi.

Sababu hizi ndizo zilizomfanya Jean amugharamie Bibiane mafunzo ya hali ya juu ya upeleelezi na kweli msichana huyu alifuzu vizuri na alikuwa mjuzi. Idara ya upelelezi na usalama ya Ufaransa inayoshughulikia usalama wa nje (DGSE) ilimuongezea ujuzi msichana huyu na mara nyingi walimtumia katika kazi zake.

Ni huyu msichana, kwa kutumwa na DGSE, alikisambaratisha kikundi cha wanajeshi waliotaka kuipindua serikali ya Hassan Gouled wa Djibouti na kufanya wakamatwe, kwani siri zao zote alitoa wa serikali kupitia DGSE mpaka leo haikujulikana jinsi alivyoweza kupata ushahidi huo ambao hata kikundi hicho cha wanajeshi kilibaki kimepigwa na butwaa. Msaada huo wa Bibiane kwa DGSE ulimwongezea Jean uhusiano wa karibu.

Hivyo hata Bibiane alitumia idara hiyo kwa kumsaidia katika mambo yake. Ni Bibiane aliyekuwa kiungo kikubwa kati ya Jean na familia ya Rais. Ingawaje na yeye aliitwa Bibiane Habyarimana hakuwa na uko na Rais kwani familia za Kinyarwanda hutumia jina lake na siyo jina la ukoo kama jamii zingine.

vilevile, msichana huyu ndiye aliyekuwa kiungo kikubwa na wakubwa wengine wa serikali katika Afrika. Kutokana na umbile na sura yake ya kuvutia, ambayo kila siku ilimuonesha kuwa msichana mdogo asiyezidi umri wa miaka kumi na minane, hakuna aliyeweza kumuhisi kama mmoja ya watu hatari waliokuwa kiungo cha uhaini na ugaidi kati ya wakuu wa serikali, wafanyabiashara na magaidi wa Ulaya. Inasemekana wakati wa mkutano wa amani uliofanyika mjini Arusha, Tanzania, Bibiane alikuwapo kama mkalimani.

Baada ya mkutano huo, rais alimpa nafasi aondoke nae kwenye ndege yake, kwani alikuja kama mkalimani wake lakini Bibiane alikataa na kuondoka na Jean kwa

barabara kupitia Nairobi, nchini Kenya. Inasemekana alijua nini kingetokea, kwani yeye aliingia kwa ndege ya jeshi la Ufaransa akitokea Nairobi, mara tu baada ya marais kuuawa tarehe 6 aprili Bibiane alisaidia kumchukua mke wa rais na familia yake ya watu kumi na watano na kuwapeleka Ufaransa.

Pia. Inasemekana. Kwa kusaidiana na Jean aliwawezesha Protais Naimana na Feldinand Zigilanyilazo kuwapatia visa ya kusafiria na kuwawezesha kwenda Ulaya. Hivyo. yote hii inaweza kukuonyesha jinsi gani msichana huyu mwenye umri wa miaka ishirini na saba tu alivyoweza kufanya mambo makubwa. Alikuwa msichana hatari sana.

Lazima tumweleze Jean hali halisi", Col. Gatabazo alimweleza Bibiane.

"Piga simu!".

"Sawa. Lakini uzungumze nae kwanza".

"Sawa!", Bibiane alijibu. Alimwangalia Col. Gatabazi. Akaona kuwa ameingiwa na woga. Bibiane aliwaponda sana wanaume walioonekana waoga. Kwa mara ya kwanza alimponda Col. Gatabazi, aliwapenda sana watu jasiri mwanaume yeyote shupavu aliifanya damu yake ichemke na kuchochea tamaa zake za mwili. Lakini mwanaume mwoga hata awe mzuri na sifa aina gani alimtia baridi. Mara hii alihisi baridi na kumchukia Col. Gatabazo mawazo yake yalitembea na kumfikiria Jean. Ile kumfikiria tu alihisi damu yake ikichemka. Kwake Jean ndiye alikuwa mfano wa mwanaume ampendaye, jasiri, shupavu anayepata kile anachokitaka hata iwe kwa gharama gani, hata ikibidi kuhatarisha maisha yake.

Ndivyo Jean alivyokuwa. Bibiane alimpenda Jean kikwelikweli. Ingawa Jean alikuwa mzungu, lakini alikuwa mzungu wa aina yake. Alijuwa kupenda na alijuwa jinsi ya kumfurahisha mwanamke mpaka kumaliza haja zake za kimwili. Lakini zaidi ya yote alimpenda kwa ujasiri na ushupavu wake katika mambo yake. Iwe biashara, iwe siasa yeye alikuwa ndie bingwa wa mchezo.

Alifikiria jinsi watu wenye vyeo vikubwa, wakuu wa nchi, matajiri walivyo yeyuka kama barafu mbele ya Jean kila alipopambana nao. Kila siku ndiye aliyetokea kuwa mshindi. Hata rais alipojaribu kumgeuka na kukabiliana na mambo kinyume na matakwa yake, Jean aliibuka mshindi na rais akapoteza maisha. Hata hali ya sasa ya Rwanda, kuwepo RPF, ilikuwa kata ya mbinu zake. Na Bibiane aliamini kabisa kuwa hii ilikuwa ni mipango yake ili baadae aiondoe serikali ya RPF na kumuweka mtu wake Col. Gatabazi. Mwanzo Bibiane alirudi kwa Col. Gatabazi.

Alimfikiria na kisha akatambua mtu kama yeye ndiye angewafaa yeye na Jean, mtu mwoga, mtu anaependa fedha, mtu ambaye anafanya kile ambacho angeambiwa. Kiongozi kama viongozi wengine wa Afrika, mtu anayejifikiria yeye na wala sio nchi au watu wake, mtu mbinafsi, kama walivyo watawala wengi wa kiafrika, Col. Gatabazi alifaa sana kutawala Rwanda.

"Njoo Jean yupo kwenye simu," Col. Gatabazi alimshtua Bibiane kutoka kwenye lindi la mawazo.

"Oh asante sana"" alijibu.

"Mpenzi hujambo?" Bibiane alimsalimia Jean.

"Sijambo, pole na matatizo huko," Jean alijibu.

"Col. amekueleza?"

"Amesema wewe ndiye utanipa safi!"

"Una maana sikupagi safi?"

"Wacha masihara huu si wakati wake. Hebu nieleze imekuwaje?"

"Huwenda na mimi ningekuwepo ningekuwa nimekufa," Bibiane alijibu.

"Sawa tu hiyo ingekuwa kifo kazini," Jean alijibu kwa sauti kavu.

Mara Bibiane akasikia damu yake inasisimka kwani alitaka mwanamume kama huyu asiye na huruma. Huyu ndiye aliyekuwa mwanamume wa kiwango chake.

"Yaani ningekufa asingejali."

"Bila shaka nigejali, lakini kama ungekufa katika mstari wa kazi ni vizuri zaidi kuliko kufa kibudu," Jean alijibu na kuendelea, "Hebu nipe imekuwaje".

Bibiane alichukuwa muda kumwelezea jinsi mambo yalivyotokea.

"Yaani huyu Willy Gamba umemuona kwa macho yako?.

"Ndiyo kwanza sikumtilia maanani sana, nilishtuka kuwa ni yeye baada ya kazi aliyokuwa ameifanya. Mwanzoni nilifikiri ni ka-Inyezi kalikopata fununu ambako vijana walikuwa tayari kushughulika," Bibiane alijibu

"Lazma umsaidie Col. Gatabazi kummaliza huyu mtu, Na mimi nitafanya mipango ya kukupeni msaada wa watu wenye ujuzi wa juu wawasaidie kumuondoa huyu funza anayetaka kula nyama yetu," Jean alijibu.

"Ukisema wewe sisi tutatekeleza, tunaomba hua msaada wako haraka maana hata siye tuna wasiwasi ," Bibiane alijibu.

"Usiwe na wasiwasi, unajua watu kama huyo Willy Gamba ndio nawataka mimi,"

"Najua Jean, wewe tena! Bwana nakuwaza, nataka nije huko unikumbatie, najua huwezi kuja huku sasa!. Bibiane alijibu kwa sauti ya mahaba.

"Baada ya kazi hiyo ya Willy Gamba tuonane Nairobi hata mimi nakutamuni sana," Jean alijibu.

"Haya kazi kwanza."

"Halafu kama kazi," Jean alimalizia na kumuomba Col. Gatabazi tena.

"Kwaheri mpenzi!"

"Kwaheri Bibiane. Col. Gatabazi atakupa mipango yote," Jean alimalizia.

Jean alipozungumza na Col. Gatabazi alimweleza mipango yake ya kummaliza Willy ambayo ilikuwa ikiendelea kichwani mwake.

"Nafikiri mawazo yako ni sahihi tutafanya hivyo. Asubuhi nitawasiliana na wewe," Col. Gatabazi alijibu.

Simu ilipolia ilimshitua sana JKS, maana alikuwa tayari amelala na ilikuwa yapata saa sita za usiku kwa saa za Afrika Mashariki.

"Hallo", JKS aliita.

"Jean".

Mara moja usingizi ulikwisha.

"Ehe, salama huko?", JKS alijibu kwa shauku maana tokea alipopewa taarifa kuwa Willy Gamba alikuwa ameuawa basi roho yake ilikuwa imetulia kabisa.

"Mambo siyo mazuri, rafiki yako hakufa na kaibuka na mambo mapya", kisha akamweleza yote yaliyotokea Kigali.

"Basi huyu ana miguu ya nyuka", JKS alijibu huku sauti yake ikionyesha wasiwasi.

Si wewe mwenyewe ulisema ni mtu hatari, na huu mchezo anaujuwa, sasa basi kazi imefika na inabidi sasa iwe kazi hasa, maana wakati wote tumekuwa tukimchezea", Jean alijibu.

"Sasa mimi nitakusaidia vipi?", JKS aliuliza.

"Utanisaidia mimi au utajisaidia vipi?, unasema kana kwamba wewe haumo kwenye huu mchezo! mchezo huu ni hatari kwako kuliko mimi maana huyu mtu akigundua kuwa wewe umekuwa mmoja wa watu ambao wamekuwa wakiuhujumu mwelekeo wa nchi yako kuhusu suala hili la Rwanda na masuala mengine basi ujuwe umeisha na urais wa Tanzania utauangalia kwenye ndoto zako tu. Kwa hiyo mtu huyu ni hatari kwako kuliko kwangu, hivyo ni kwa faida yako auawe mara moja!!", Jean alimwasa JKS.

"Tufanye nini sasa?", JKS alijibu kwa sauti ya woga.

"Kati ya vijana wetu wazuri na mahiri na wale vijana walioko Arusha ni wazuri sana. Hao ndio saizi ya huyu Gamba kutokana na uzoefu walionao na ujuzi pia ambao wanao. Kwa hiyo. Nataka wote wanne na kiongozi wao, Xavier Nkubana, waende wakaimalize hii kazi. Sasa ninachotaka ufanye ni kuwatafutia pasi mpya za kitanzania waonekane ni Watutsi ambao zamani walikimbilia Tanzania na sasa wanakwenda kuangalia hali ilivyo. Siku zote walikuwa wakifanyakazi yao kwa siri na hakuna atakayewashitukia. Hivyo watafutie hizo pasi na usafiri. Uhakikishe kesho wako Kigali. Wakifika Kigali wawasiliane na Col. Gatabazi atawapa maelekezo ya kufanya. Lazima tusishindwe juu ya jambo hili", Jean alisisitiza.

"Hilo ulilosema hesabu limefanyika, nitatumia nguvu za dola kuhakikisha kesho wako Kigali mapema kabisa. Nkubana amenipigia simu leo na kusema vijana wanasikia kuchoka kukaa tu bila kazi. Hivyo, nikiwaeleza kuwa wanarudi Kigali kwa kazi ngumu, watafurahi sana", JKS alijibu.

"Hiyo safi, basi fanya hivyo na wakishafika nipe taarifa. Hata hivyo, Col. Gatabazi atanipa taarifa, wakiondoka tu mpigie simu Col. Gatabazi", Jean alimalizia na kukata simu.

# SURA YA SITA

Saa ileile JKS alipiga simu Arusha ambako ndiko Xavier Nkubana na wenzake walikuwa wakikaa. Tokea kifo cha Rais wa Rwanda, wao walibaki Tanzania kama wakimbizi na JKS aliwafanyia mipango yote. Hakuna mtu hata mmoja aliyewahisi kwa ubaya, walikuwa wakiishi kwa starehe na kifahari, kama kawaida ya wageni katika Tanzania.

Tanzania ni nchi ya namna ya kipekee kwani wageni ndio wanastarehe kuliko wenyeji. Kwa mtu mgeni kuishi kifahari ilikuwa ni sawa, lakini Mtanzania akitokea kuishi hivyo basi watu humhisi kuwa si mtu mwaminifu na husumbuliwa mara kwa mara na vyombo vya dola mpaka imewafikisha watanzania mahala ambapo hata kama wana uwezo huishi kwa kujibana kwa kuogopa kubuguziwa. Lakini mgeni hata akiishi kifahari vipi alionekana ni sawa na hakuna chombo cha dola ambacho kingeweza kumgusa, na vilevile wananchi hubaki kumsifia kwa ufahari wake.

Hivyo, Nkubana na wenzake waliishi Arusha kwa raha mstarehe wakiwa wameifanya Arusha kama sehemu yao ya kufanyia mipango ya kuihujumu serikali ya RPF. Kusema kweli hawa jamaa walikuwa wauaji katili sana, na si kweli kuwa walikuwa wamebaki Tanzania wakati wa kifo cha Rais, ila walikuwa miongoni mwa watu walioongoza mauaji ya Watutsi. Inasemekana mmoja kati yao, Felician Nzirorera, ndiye aliyekuwa akitangaza na kuchochea watu kwa kutumia radio ya RPLM iliyokuwa ikimilikiwa na Wahutu wenye siasa kali. Radio Televisheni Libre Des Milles Collines (RTLM), iliyokuwa radio ya uchochezi, na mauaji yalipoanza wengi wa watangazaji wake walijiunga katika mauaji na wakubwa wao kukimbilia nje baada ya kuchochea mauaji.

Lakini Nzirorera aliendelea kwa muda mrefu akiwa anatangaza kwa kuhama na stesheni yake ya redio kwenye gari akiwachochea Wahutu kuendelea kuwauwa Watutsi. Na ni mtu huyu pamoja na wenzake aliyekuwa akila starehe hapo mjini Arusha akiendesha magari ya fahari badala ya kuwa amekamatwa kungojea mahakama maalumu ya wauaji hapo Arusha. Kama si JKS kuwasaidia na kuwapa sifa tofauti kuwa wao walikuwa ni maafisa safi wa serikali waliojikuta kwenye mapambano ambayo hawakuwa washiriki, leo hii wangekuwa kati ya watu waliokuwa wakitafutwa na mahakama ya kimataifa ya mauaji ya Rwanda.

Simu ililia chumbani mwa Nkubana, bahati nzuri alikuwa ndio kwanza amerudi toka hoteli Sabasaba kwenye disko ambako alijipatia msichana wa kustarehe naye usiku huo. Simu ilipolia Nkubana alimwacha yule msichana sebuleni na kwenda kuchukua simu chumbani.

"Hello, Xavier".

"JKS".

"Shikamoo, vipi kulikoni".

"Sikiliza kwa makini".

JKS alimweleza yote kuhusu ambavyo yeye na wenzake walikuwa wakitakiwa kwenda Rwanda kumsaidia Bibiane na Col. Gatabazi kummaliza Willy Gamba.

"Hiyo safi sana, tulikuwa tunakaa hapa, tunalewa na kustarehe tu na wanawake maana hatukuwa na kazi. Sisi tuko tayari hata sasa", Nkubana alijibu.

JKS alimweleza mipango yote na jinsi ambavyo wangesafiri mpaka Kigali.

"Hakika mzee, wewe hushindwi kitu. Kweli madaraka ukijuwa kuyatumia ni matamu sana maana kila kitu kinawezekana, sijui bila wewe tungefanya nini. Asante sana. nitawaeleza wenzangu. Hivyo, saa mbili asubuhi tutakuwa tayari. Na hesabu hiyo kazi huko Kigali imeisha maana tuna uchu na damu", Nkubana alijibu kwa majidai.

"Asante na kwa heri".

Nkubana alikuwa amewaacha wenzake kwenye disko. Aliporudi sabuleni alimkuta yule msichana amelala kwenye kiti.

"We, amka turudi kwenye disko".

"Kwanini, mimi nataka kulala, nimechoka".

""Kwani umekuja kulala hapa, kulala ni nyumbani kwako, hapa uko kazini, kazi ya kunistarehesha mimi, kwa vile nasikia nataka kucheza disko tena, utanifuata".

Yule msichana akiwa anashangaa, Nkubana alimuinua na wakaelekea kwenye gari ili kurudi disko sabasaba.

CENTRE CHRISTUS

Ilikuwa yapata saa moja ya usiku wakati Willy alipofika kwenye kituo cha kidini cha Centre Christus. Alikuwa bado anasikia maumivu ya ubavuni yaliyotokana na

mapambano ya juzi yake. Hata hivyo, aliamua kuendelea na kazi kwa vile muda ulikuwa hamruhusu kungoja apone kabisa.

Langoni mwa kituo hiku alimkuta mtawa mmoja aliyemwuliza jina, na baada ya kujitambulisha mtawa huyu alimchukuwa Willy na kumpeleka kwenye nyumba ya Padri Marcel Karangwa ambaye alimkuta akimsubiri.

"Karibu sana Willy Gamba, karibu Kigali. Kigali inanuka mauti; hata nyumba ya Mungu inanuka mauti", Padri Karangwa alimkaribisha sebuleni mwa nyumba yake.

"Nashukuru sana Padri hasa kwa kukubali mimi nije nikuone mara tu baada ya maafa yaliyotokea kwenye kituo chako hiki, nashukuru sana", Willy alijibu.

"Unakaribishwa sana, Bwana Musoke amenieleza kila kitu, nasi tunafarijika sana kukutana na watu kama nyinyi ambao mnaweza kuleta matumaini ya amani ya nchi kama hii. Kweli, tuko tayari kukupa maelezo yoyote unayohitaji kwa shughuli yako", Padri Karangwa alimweleza Willy.

"Asante Padri, mimi nisingependa nichukuwe muda wako mwingi kwa vile una majukumu makubwa ya kukijenga upya kituo hiki na kurudisha imani ya watu katika nyumba ya Mungu", Willy alijibu wakati mmoja wa watawa akileta chai na kahawa.

"Utakunywa chai au kahawa", Padri Karangwa alimuuliza Willy.

"Chai ya rangi", Willy alijibu na kupewa chai ya rangi na kipande cha mkate na Padri Karangwa akapewa kahawa.

"Bwana Musoke alisema ungependa kujuwa kwa kifupi hasa ni nini kiini cha chuki iliyokithiri kati ya makabila haya ya Kitutsi na Kihutu".

"Sawa kabisa", Willy alijibu.

"Kwanza kabisa mimi ni Mtutsi...". Alipoanza kuongea akaingia Padri mwingine. Padri Karangwa alimkaribisha na kumjulisha kwa Willy Gamba. "Huyu Padri Boniface Sibomana na ni mmoja wa watu waliopona mauaji". Kisha akamjulisha Willy Gamba. "Na huyu ni Willy Gamba, mwandishi wa habari kutoka Tanzania, ambaye pia amekuja kama wengine wengi waliomtangulia kutupa pole na kutaka kuelewa vipi watu wa nchi moja wanaweza kugeukiana na kuuana kikatili namna hii.

Willy na Padri Sibomana walipeana mikono na wakaketi chini kuendelea na mazungumzo.

"Kama nilivyokueleza mimi ni Mtutsi, lakini Padri Sibomana ni Mhutu, sasa sema tofauti yetu sisi kimaumbile ni nini?", Padri Karangwa alimwuliza Willy. Willy aliwaangalia wote wawili. kweli kimaumbile kati ya hawa wawili hasa hakukuwa na tofauti.

"Hakuna", Willy alijibu huku mapadri hawa wawili wakitabasamu.

"Kama hakuna jibu la swala zima la mauaji ya Watutsi na Wahutu wenye msimamo wa wastani, basi mauaji haya yalishinikizwa kisiasa na kikundi cha watu wachache wenye madaraka makubwa katika Serikali ya Rwanda. Mara nyingi vita ya wenyewe kwa wenyewe katika Rwanda ikisingiziwa kuwa ni vita ya kikabila. Hii si kweli na inapotosha ukweli, ila yanapotokea mauaji kama haya ndipo ujenzi wa chuki wa kikabila unajengwa. Wahutu na Watutsi wameishi pamoja kwa karne nyingi na tofauti zao si hizi tunazoziona leo, kwani hakukuwa na chuki kati ya makabila haya. Ni utawala wa kikoloni wa kugawa nitawale na baadaye. Serikali zetu zilizoongozwa na ubinafsi na uchu wa madaraka uliohubiri kuwepo tofauti kati ya wahutu na Watutsi, tofauti ambazo awali hazikuwepo. Kwa kifupi ni kwamba ili mbinu za kisasa za kuyatumia makabila haya mawili ili watawala wabaki kwenye madaraka ambayo yamesababisha mauaji haya ya kikatili ambayo tumeyashuhudia", Padri Karangwa alinyamaza kidogo ili anywe kahawa yake wakati Willy na Padri Sibomana wakimsikiliza kwa makini.

Kisha Padri Karangwa aliendelea. "Kama nilivyosema mwanzo, mauaji ya kikatili Rwanda hayakutokea ghafla tu kiwendawazimu eti kwa sababu kabila moja lilikuwa likilichukia kabila lingine. Mauaji ya Rwanda yalikuwa yamepangwa siku nyingi na kwa ufasaha kabisa na watawala wa nchi yetu. Ili kulielewa hili na ili mtu asisingizie kuwa mauaji haya yametokana na ukabila inabidi kwa kifupi tuangalie historia ya Rwanda kwa maana ya makabila haya mawili ya Watutsi na wahutu", Padri Karangwa alieleza.

"Nafikiri kweli ni vizuri tupate historia fupi ya jinsi chuki ilivyojengeka maana mauaji haya ya Watutsi na Wahutu wenye siasa kali ni ya kinyama yaani binadamu ameweza kuwa mharibifu na mkatili kiasi hiki", Willy alisema kwa kusikitika.

"Historia ya Rwanda inaonyesha kwamba watu wa kwanza kuishi Rwanda walikuwa wawindaji ambao ni kizazi cha kabila dogo la Watwa. Inasemekana kuwa wakulima, ambao ni Wahutu, ndio waliofuatia na kisha wafugaji ambao ni

Watutsi, ndio walikuwa wa mwisho kufika, na wote waliishi pamoja kila ukoo ukiwa na utawala wake wa kichifu. Kusema kuwa Watutsi walikuja kama wavamizi na kutaka kutawala kwa nguvu makabila mengine si kweli, kwani wana historia wengi wameupinga usemi huo, ila kitu ambacho kilitokea ni kwamba karibu vizazi ishirini vilivyopita ukoo mmoja wa Kitutsi ulioitwa Nyinginya ulipata sifa katikati ya Rwanda na kuanzisha utawala wa kifalme ambao ulitawanyika kwenda kusini mwa Rwanda ya sasa.

Lakini historia inaonyesha kwa bunge lao la wakati huo lilikuwa linaitwa 'abini', nalo liliwashirikisha Wahutu na Watutsi pamoja. Na kwa vile utawala wa Wanyinginya ulikuwa na nguvu, machifu wa Kihutu katikati ya kusini mwa Rwanda walimezwa na kukubalika kama Wanyinginya. Hapa ndipo swala la ukabila wa Kihutu na Kitutsi ulipotambuliwa, si kutokana na ukoo wa Kihutu au Kitutsi bali kwa kutokana na hadhi mtu aliyokuwa nayo. Ukiwa mtawala, hata ukiwa Mhutu uliitwa Mtutsi. Kama huna mali uliitwa Mhutu, na hivyo hii hali iliashiria kuoana kwingi kati ya Wahutu na Watutsi. Ndiyo sababu hata wewe umeshindwa kututoa tofauti," Padri Karangwa alinena.

"Kama si vitambulisho hivi mara nyingi kweli huwezi kujua Mhutu ni yupi na Mtutsi ni yupi maana vile vile tunazungumza lugha moja, tofauti na nyinyi," Padri Sibomana alidakia.

"Huko ndiko ninakokwenda," Padri Karangwa alisema na kisha kuendelea, "Kusema kweli tofauti halisi ambayo ilibaki ilikuwa kwa wahutu wa kaskazini ambao waliendelea na utawala wao mpaka hapo wakoloni walipofika. Pamoja na kwamba utawala wa Wahutu wa kaskazini haukumezwa na utawala wa ukoo wa Nyiginya, bado wahutu hawa na watutsi waliishi bila matatizo."

"Matatizo yalianza lini? Willy aliuliza.

"Usiwe na haraka, mimi taaluma yangu ni ualimu nakupeleka taratibu uelewe na huko tutafika," Padri Karangwa alimjibu na kisha kuendelea, "Tatizo hasa lilianza wakati wakoloni walipofika Rwanda mwishoni mwa karne ya kumi na tisa. Wamisionari wa Kijerumani na kisha askari wa Kijerumani walipofika Rwanda walikuta utawala uliojengeka wa ukoo wa Nyinginya ambao kama nilivyosema ulikuwa ukoo wa Kitutsi. Kama walivyokuwa wakoloni wote walitumia tawala walizozikuta kuwasaidia kutawala. Hivyo, Wajerumani na kisha Wabelgiji baada ya kukuta utawala wenye nguvu ulikuwa wa kitutsi wakaamua kuutumia huu utawala na kuubadilisha uwe wa kinyanyasaji ili ile sera yao ya gawa utawale iweze kufanikiwa. Kwa kusaidiwa na wakoloni sasa watutsi walifuta nafasi yoyote

waliyokuwa nayo wahutu kabla ya wakoloni na kuwanyang'anya mali na madaraka, na hii yote ilichochewa na wakoloni ili kuwagawa watu wa nchi hii. Na, kwa vile ilikuwa vigumu kuwatofautisha wahutu na watutsi kwa urahisi mnamo mwaka wa 1933-34 vitambulisho vilianzishwa na wakoloni kwa wananchi wote wa Rwanda vikiwatambulisha kikabila yaani Wahutu, Watutsi au Watwa na vitambulisho hivi hivi ndivyo vilivyotumika katika mauaji haya na mengine mengi yaliyokwisha tokea.

"Kwa kutumia vitambulisho hivi basi maendeleo ya Wahutu na Watwa yalizimwa kabisa?", Willy aliuliza.

"Ndiyo, yalizimwa na hata shule nafasi zote zilitolewa kwa Watutsi, kanisani nako baada ya Omwami kubatizwa kuwa mkatoliki hata kanisa liliwabagua Wahutu. Kanisa Katoliki wakati huo ndilo lilikuwa linamiliki karibu shule zote katika Rwanda. Hivyo liliwasomesha Watutsi na kuhakikisha Wahutu hawapati nafasi ya kusoma ila walibaki na haki ya kuhubiriwa tu", Padri Karangwa alijibu.

"Kwa hiyo vitambulisho vilikuwa moja ya mambo yaliyojenga ukabila ndani ya Rwanda?", Willy aliuliza tena.

"Ndiyo, kabla ya vitambulisho ilikuwa vigumu kujuwa huyu ni kabila gani na vitambulisho kama nilivyosema hapo mwanzo, vilianzishwa na wakoloni wa Kibelgiji ili kujenga ukabila ili wautumie huu ukabila kuwagawa Wanyarwanda kwa faida yao ili iwe rahisi kuwatawala. Baada ya kupewa vitambulisho watu wote waliotambuliwa kama Wahutu walinyanyaswa na kunyimwa hazi zozote na elimu na vilevile mali na hata Wahutu wa Kaskazini ambao walikuwa wakijitawala wenyewe, wakoloni mnamo mwaka 1912 walimshinikiza na kumsaidia Omwami atwae madaraka katika sehemu hizi. Kutwaa madaraka Kaskazini mwa Rwanda kwa Watutsi kulikataliwa na Wahutu wa sehemu hii na mapigano makali yalitokea yakiongozwa na Mhutu aitwae Ndugutse. Kwa vile Watutsi walikuwa wakisaidiana na wakoloni, Wahutu walishindwa na wakatawaliwa na Watutsi. Wahutu wengi waliuawa na huo ndio ukawa mwanza wa uhasama na chuki kati ya Wahutu wa Kaskazini na Watutsi. Sasa, ukiangalia mwanzo mwa hii vita ulikuwa umechochewa na wakoloni maana, kama nilivyosema hapo mwanzo, wakoloni walipofika walikuta makabila haya yakiishi kwa amani", Padri Karangwa alijibu.

"Ilikuwaje sasa baadaye Wahutu kuja kutawala Rwanda", Willy aliuliza.

"Baada ya vita kuu vya pili Watutsi walianza kuomba uhuru kama ilivyokuwa katika nchi zingine za kiafrika. Wakoloni wa Kibelgiji kuona hivi, na jinsi Watutsi

walivyokuwa na nguvu na walivyokuwa wamesoma, wakaingiwa na wasiwasi, wakajuwa Watutsi wasingewahitaji iwapo watapata uhuru. Hivyo Wakoloni wa Kibalgiji wakaamua kuwageuka na kuwasaidia Wahutu kuwaunga mkono. Viongozi wa Kihutu walikuwa wachache na wote walikuwa na kisomo kidogo walichopata kwa Wamisionari. Hivyo, kwa vile hawakuwa na nguvu zozote za kiutawala, walipoanza siasa, siasa yao ikawa ya kikabila. Hivyo mwaka 1957 chama cha kupigania haki za Wahutu, kikiongozwa na Gregoire Kayibanda, kilianzishwa kikiitwa Permehutu. Na Wakoloni wa Kibelgiji, wakiwa sasa wamewageuka Watutsi, walianza kukisaidia chama cha Permehutu, huku wakikitafutia nafasi ya kuuangusha utawala wa Watutsi. Nia yao ikiwa kuwaingia kwenye madaraka Wahutu ambao hawakuwa na nguvu ili waendelee kuwategemea kama wangepata uhuru. Hii ingewasaidia wakoloni kuendeleza maslahi yao kwani Wahutu wangewategemea sana kuwalinda dhidi ya Watutsi waliokuwa na nguvu za kijeshi na utawala. Kwa hiyo wakoloni ndio wangeendelea kutawala kiaina kwani watawala wa Kihutu wangekuwepo kama mfano tu.

"Je, viongozi wa Kitutsi hawakushituka?", Willy aliuliza.

"Walianza kushituka lakini mambo yalitokea kwa ghafla sana wakati Omwami Rudahigwa alipofariki kiajabu mjini Bujumbwe mwaka 1959. Jeshi la Ubelgiji lilisimamia kuangushwa kwa utawala wa Kitutsi ambao ulikuwa na umwagaji wa damu vibaya sana. Jeshi la Ubelgiji lililowasaidia Watutsi kuanzia mwaka 1912 sasa liliwasaidia Wahutu na ile chuki ya mwaka 1912 ya Wahutu wa kaskazini ilijitokeza na inasadikiwa kuwa Watutsi wapatao elfu kumi waliuawa na wengi wao wakakimbilia nchi jirani. Hivyo, Wahutu ndio wakawa watawala chini ya Kayibanda baada ya kusaidiwa na wakoloni wa Kibalgiji kuwaweka madarakani", Padri Karangwa alieleza.

"Kwa nini baada ya hapo vitambulisho viliendelea, si Wahutu wangeachana navyo sasa maana vilikuwa vinawabagua?", Willy alitaka kujua.

"Hapana, mambo sasa yaligeuka; Wahutu sasa ndio walikuwa watawala. Hivyo, wakaanza kuwanyanyasa Watutsi. Na vitambulisho hivyo hivyo vilivyowasaidia Wahutu kuwatambua Watutsi na kuwabagua, hata Watutsi wengine wakabadili vitambulisho vyao na kujiita Wahutu maana sasa kibao kilikuwa kimewageukia. Ingawaje Watutsi ndio waliokuwa wamesoma lakini sasa walibaguliwa na Wahutu waliokuwa hawana kisomo maana ndio waliochukua madaraka serikalini. Elimju yote sasa ilitolewa kwa wahutu na Watutsi wakabaki kuangaika na kunyanyaswa. Wengi wao wakaanza kukimbia. Kwa vile jeshi asilimia kubwa lilibaki la Kibelgiji

hivyo hakuna kitu ambacho Watutsi wangefanya. Ingawaje Watutsi waliokimbia walijaribu kuishambulia Rwanda kwa kuunda jeshi la msituni lakini hawakufua dafu. Jeshi zaidi la kuongeza nguvu liliitwa mara moja toka Ubelgiji kuja kutokomeza maasi mara uvamizi wa kitutsi ulipoanza. Kwa hiyo, katika miaka yote ya sitini hali iliendelea kuwa ya wasiwasi nchini Rwanda huku watutsi wakiendelea kuuwawa na kunyanyaswa",

"Ilikuwaje Habyarimana akafanya mapinduzi, maana yeye ni Mhutu na utawala ulikuwa Wakihutu? " Willy aliuliza.

"Swali zuri," Padri Karangwa alijibu na kisha akaendelea, "Serikali ya Kayibanda ilianza kuishiwa mbinu na Wabelgiji wakaanza kuichoka maana sasa ilikuwa inakuwepo kwa sababu ya ukabila tu. Mnamo mwaka 1973 Kayibanda akafanya makosa. Kwa vile Watutsi walikuwa wamenyimwa nafasi yoyote katika serikali, kibiashara na sehemu zingine zozote, sehemu waloyokimbilia ilikuwa ni ndani ya kanisa. Hivyo, Seminari nyingi zilijaa Watutsi pamoja na vyuo vikuu ambavyo viliitwa vyuo vya Watutsi. Kwa hiyo, mwaka 1973 ili kuwaondoa Watutsi katika vyombo vyote vya elimu, serikali ilianza kushambulia seminari, shule na vyuo vikuu. Kwa vile vyombo vyote vya elimu vilikuwa mikononi mwa kanisa katoliki Askofun wa kanisa katoliki akaanza kupiga makelele na kulaani serikali. Hata hivyo, huyu Kayibanda kabla ya kushika madaraka alikuwa katibu wa Askofu huyu na alikuwa akiwaunga mkono wahutu. Hapo ndipo Wabelgiji tena wakapata nafasi na kumtumia Meja Generali Habyarimana kufanya mapinduzi na kumtoa rais Kayibanda.Haybarimana alikuwa Mhutu wa kaskazini na Kayibanda wa kusini. Utawala wake ulipokelewa kwa shangwa na Watutsi na Wahutu ukifikiriwa utakuwa utawala wa haki na usawa lakini hali haikuwa hivyo, badala ya kuwa na mgawanyiko wa Watutsi na Wahutu mambo yalizidi. Sasa kukawa na upendeleo kwa Wahutu wa kaskazini na kuwabagua Watutsi na Wahutu wa kati na kusini. Ndiyo sababu Wahutu wenye siasa ya wastani waliuawa katika mauaji ya aprili wakiwamo wanasiasa, wafanyakazi wa serikali na wafanyabiashara, wote walikuwa wa kusini. hivyo, kufika wakati wa sasa sera ya gawa nitawale iliendelea katika Rwanda."

"Maelezo yako toka mwanzo yameonyesha kuwa Wahutu na Watutsi kama watu hawakuwa na tatizo kati yao. Wamekuwa wakitumiwa na watawala wa kikoloni na watawala wa kizalendo ambao wamekuwa wakiwachonganisha ili wakosane na kwa kukosana kwao wao wafaidike," Willy alieleza.

"Haswa, ndiyo sababu nimeeleza yote haya uweze kulielewa tatizo la Rwanda. Tatizo letu si ukabila, tatizo letu ni uongozi."

"Sasa nini kilifanya hali ifikie mauaji, kama ni tatizo la uongozi nchi nyingi za Kiafrika zina tatizo hilo. Na kama ni kutumiwa na mataifa ya nje nchi nyingi zinatumiwa hivyohivyo, mauaji kama haya ni ya pekee katika dunia, hayana mfano," Willy alimuuliza Padri Sibomana ambaye alikuwa akisikiliza kwa muda mrefu bila kusema kitu.

"Nafikiri hilo swali lako ndilo kila mtu anajiuliza, maana mauaji haya tuliyo yashuudia hayana mfano, hata ya Hitler yalichukua muda mrefu maana vita vilipiganwa kwa miaka, lakini mauaji haya yanashinda fikra kwani yalianza dakika chache tu baada ya kufa Rais na kusambaa nchi nzima utafikiri moto wa petroli," Padri Sibomana alisema.

"Wakati wa Habyarimana kulijitokeza kikundi kidogo cha watu kilichomzunguka ambacho ndicho kilichokuwa kinafaidika na utawala wake. Kikundi hiki kilikuwa cha watu wa kaskazini kutoka sehemu za Gisenyi na Ruhengeri nacho kilijulikana kwa jina la Akazu. Kikundi hiki kilijilimbikizia mali na madaraka, kilijenga ngome ya kukizunguka na hakuna kikundi kingine kilichoweza kupenya ngome hiyo. Hivyo, ili Rais na kikundi hiki waweze kuendelea kujilimbikizia mali na madaraka kilihakikisha kuwa hakuna biashara wala nafasi ya uongozi inayoweza kupatikana mahali popote bila kikundi hicho kutoa ruksa. Kikundi hiki kilikuwa cha Wahutu. Hivyo, uhalali wa serikali ulipoanza kushitukiwa, kwa vile kikundi hiki cha Akazu kilikuwa kimejilimbikizia mali nyingi, kilianza kuitumia mali hii na ya serikali kujenga jeshi lake, redio yake, magazeti na kutumia vyombo hivi kuwachochea Wahutu, ambao ndio wengi, wawachukie Watutsi ambao sasa walikuwa wanausaili uhalali wa serikali hii wakiwemo Wahutu wapendao amani na usawa ambao waliitwa Wahutu wenye msimamo wa wastani. Kufikia mwaka 1990 kulikuwa hakuna Mtutsi mwenye madaraka katika serikali, kwa mfano kati ya wakuu wa mikoa kumi na moja hakukuwa na Mtutsi hata mmoja; kati ya vyeo 143 vya juu serikalini hakukuwa na Mtutsi hata mmoja; kati ya mabalozi wote walioteuliwa kwenda nje Mtutsi alikuwa mmoja tu. Na kati ya wabunge sabini, ni watutsi wawili tu waliokuwa wabunge. Katika jeshi walihakikisha hakuna Mtutsi na hasa jeshi la kumlinda Rais lote lilikuwa na Wahutu na Wahutu hao vilevile walikuwa ni ama ndugu za Rais au wa mkewe", Padri Karangwa alieleza.

"Sijaelewa vizuri jinsi hali hii ilivyoashiria kufikia mauaiji yaliyotokea", Willy alisema huku akionyesha sasa kuwa makini zaidi.

"Huku ndiko ninakokwenda. Hawa Akazu pamoja na familia ya Rais walifikia kujiita miungu wadogo. Walifanya kila walichotaka. Kuna habari za kuaminika kuwa kuna Mzungu mmoja rafiki yake sana na Rais ambaye alikuwa anawatengenezea fedha kwa maana ya kuchapisha na wao wanamlipa mazao kama kahawa kwa bei yake, na mazao mengine yoyote aliyohitaji; na pia kuna tetesi kuwa hata bangi ililimwa na watu hawa na kusambazwa na huyu Mzungu. Kusema kweli, hawa watu walitajirika kuzidi kiasi na wakajisahau kabisa. Ili kubaki katika hali hii kama nilivyosema mwanzo, ilibidi sasa wachochee ukabila. Walikuwa wameshafilisika kisiasa, uhali wa utawala ulikuwa hauna msimamo tena. Hivyo, kimbilio lilikuwa ni ukabila na kuhakikisha Wahutu wananufaika na utawala, na ilikuwa ni rahisi sana kuwachochea na kufanya lolote ambalo viongozi wao wa Kihutu walitaka wafanye. Uchochezi wa Wahutu ulizidi kuanzia mwaka 1988 baada ya kongamano la Watutsi lililofanyika Washington D.C Marekani na kuamua kuiondoa serikali tawala madarakani. Mkutano huo pia ulihuhudhuliwa na Wahutu ambao walikuwa wakipinga mwenendo wa serikali tawala. Haja ya wakimbizi wa Kitutsi kurudi nyumbani kwa njia yoyote ile ndiyo ilikuwa msukumo wa kongamano hili huku Marekani, kwani Rais alikuwa akieleza kuwa wakimbizi hawana haki tena ya kurudi Rwanda kwa kuwa nchi ilikuwa ndogo mno na isingeweza kuwapokea tena". Padri Karangwa alinyamaza kidogo na kuchukua glasi ya maji.

Padri Sibomana akatumia wakati huu kumkata kauli kidogo. akasema, "Padri alilisahau swala la wakimbizi wa Kibanyarwanda Uganda, maana hili lina uhusiano mkubwa mno na hali hii yote anayoieleza".

"Bila shaka Padri Sibomana, nilikuwa bado niendelee huko ila kwanza nilitaka kuonyesha mshikamano wa Wahutu ulikuwaje", Padri Karangwa alijibu.

"Sawa Padri, endelea", Padri Sibomana aliafiki.

"Kama alivyo kumbusha Padri Sibomana, wakimbizi wengi walijiunga na jeshi la NRA la Uganda katika miaka ya themanini. Hao walimsaidia Rais wa sasa wa Uganda kuchukua madaraka. Kwa kawaida, wakimbizi mara kwa mara hujiingiza kiurahisi jeshini kuliko kukaa bure na hii vile vile huwapa tamaa ya kutafuta njia za kijeshi kurudi kwao. Na hivi ndivyo ilivyokuwa kwa wakimbizi wa Kibanyarwanda waliokuwa Uganda, wengi wao wakiwa Watutsi na Wahutu wachache. Makamanda wengi wan NRA walikuwa wakimbizi wa Kibanyarwanda. Baada ya kushika madaraka Uganda ubaguzi ulianza wa wakimbizi wa Kinyarwanda Uganda. Waliwapinga hasa waliokuwa wapinzani wa serikali na raia

wa kawaida wa Kiganda waliona  hawa wakimbizi kama wanaokuja kuwanyang`anya haki zao kwa vile walikuwa wakishika vyeo vya juu katika jeshi la NRA ambali sasa ndilo lililokuwa likitawala Uganda. Ilikuwa ni hali hii na nia ya kurudi kwao kwa hali yoyote sasa, iliyo ashiria kuzaliwa kwa RPF. Hivyo makamanda wa Kinyarwanda walikuwa NRA sasa waliamia RPF.

"Inasemekana Rais wa Uganda, ili asiwe na matatizo nyumbani kwake kwa sababu nilizozisema hapo juu, alikuwa msukumo mkubwa wa kuisaidia RPF ili wakimbizi hawa walazimishe kurudi kwao kwa kutumia nguvu za kijeshi. Kutokana na hali hii mnamo tarehe 1 oktoba 1990 watoto wa wakimbizi wa Kinyarwanda, ambao walikuwa wapiganaji wa NRA, walikusanyika kusini- magharibi mwa Uganda na siku hiyo ya tarehe moja wakaivamia Rwanda. Ingawa hawakufanikiwa, lakini nguvu yao ilifahamika na kusababisha kiwewe kwa utawala wa Rwanda, na hapa ndipo mipigano ya kuwaangamiza Watutsi wote na Wahutu waliokuwa wanaunga mkono jitihada za Watutsi ilipoanza kupangwa na Akazu. Kama nilivyosema hapo mwanzo ili uchochezi kwa Wahutu dhidi ya Watutsi upate kufanikiwa, kundi lililokuwa linafaidika na utawala huu liliunda jeshi lake lililoitwa Interahamwe. Interahamwe maana yake ni "wale wanaovamia na kupigana pamoja". Jeshi hili liliundwa toka sehemu mbali mbali nchi nzima na kufundishwa na kikosi maalumu cha Rais kataka kambi za Gabiro na Bigongwe, na wote waliochaguliwa walikuwa Wahutu isipokuwa kamanda wao alikuwa Mtutsi ambaye baba yake alikuwa amechukua kitambulisho cha Kihutu. Wengi wa Interahamwe walikuwa ni vijana ambao walikuwa hawana kazi, Wakipewa vinywaji na pesa wakifundishwa kuwachukia Watutsi na kufanya maasi ya aina yoyote ile tokea kubaka, kunyang`anya mpaka kuua. Wizara ya ulinzi ndiyo iliyotoa silaha na kutoa sehemu za kufanyia mafunzo ingawa Interahamwe ilibaki mali ya Akazu na cha tawala. Vilevile wakimbizi wa Kirundi nao walichukuliwa na kuingizwa katika jeshi hili Iterahamwe. Inasemekana kuwa hawa wakimbizi wa Kirundi, ambao ni Wahutu, walikuwa wakatili zaidi kuliko hata wenzao wa Rwanda. Wakuu wa Interahamwe hawakuishia hapo tu bali walienda mpaka Goma, Zaire, ambako nako walichukua askari wa kujiunga na Interahamwe. Wazaire waliochukuliwa ni wale wenye asili ya Kihutu lakini Wazaire wanye asili ya kitutsi kwa jina la Wabanyamulenge, wao walikataa kwani wao walikuwa wanaunga mkono harakati za RPF.

"Hawa Interahamwe walikuwa wengi kiasi gani?" Willy aliuliza.

"Hata kufikia tarehe 6 aprili na baada ya kifo cha Rais na mauaji kuanza inasemekana kwamba kila Mhutu sasa alikuwa Interahamwe, lakini Interahamwe waliochukua mafunzo haswa walikuwa wamefikia kiasi cha elfu kumi."

"Inasemekana yalifanyika mauaji mengi kwa silaha hafifu kama rungu, panga na kadhalika.Hii ni kwasababu haya marungu yaliweza kutengenezwa kienyeji na kwa urahisi au vipi?" Willy aliuliza.

"Hapana, marungu na mapanga haya yaliagizwa na kundi la Akazu kutoka China. marungu haya yalipendekezwa na Akazu kwani kila yalipotumiwa yalitoa maumivu ya ajabu kwa adui. Na inasemekana kuwa watu wengi walitoa pesa kununua kuuawa na risasi kuliko kustaimili kifo cha rungu. Marungu haya, kwa mfano yalianza kuingia Rwanda tokea januari 1993 yakipakuliwa toka Mombasa kupitia Nairobi na kuhifadhiwa kwenye maghala Kigali na Kibungo. Lakini, pamoja na marungu haya serikali ya Rwanda, kati ya mwaka 1992 na 1994, iliagiza silaha kubwa kubwa toka Ufaransa. Vile vile silaha zingine zilitoka Ulaya ya mashariki kupitia Zaire. Ufaransa, hata hivyo, ndiyo iliyokuwa mfadhili mkubwa wa siliha kwa serikali ya Rwanda. Inasemekana yule mzungu rafiki wa Rais na Akazu ndiye alipanga mipango yote ya uuzaji wa silaha kati ya Ufaransa na Rwanda. Inasemekanaq kuwa Mfaransa huyu ambaye pia alikuwa na uhusiano wa karibu na Ikulu ya Ufaransa alifikia kuwa mshauri mkuu wa Rais na ndiye aliyekuwa anamshauri Rais afanye nini, aseme nini na hata mauaji mengi inasemekana yalitokana na ushauri wake. Na kwa vile Rais na watu wake walitaka kutawala maisha, huyu mtu ambaye alikuwa akiwapa silaha za hali ya juu ili RPF isiweze kufurukuta, walimwonja kama Mungu, hata ndege ya Rais inasemekana ilitolewa kama zawadi nja mtu maarufu wa huko Ufaransa kwa mipango ya huyu mtu," Padri Karangwa alieleza.

"Kwa hiyo mauaji haya ya Rwanda yalipangwa, na siyo kwamba yalitokea tu kwa bahati mbaya, kwa kuchukizwa na kifo cha Rais?" Willy aliendelea kumdadisi Padri.

"Bila shaka. Hili kundi la Akazu lilikuwa na vyombo vya propaganda vingi ambavyo vilisaidia kuingiza chuki kati ya Wahutu na Watutsi ili iwe rahisi kuwatumia Wahutu katika mpango wao wa kuwamaliza Watutsi ili waweze kutawala milele. Magazeti kama Kangura na Stesheni ya Redio ya RTLM vilikuwa vinamilikiwa na kundi hili. Gazeti hili lilianzishwa katikati ya mwaka 1990 na liliungwa mkono na chama tawala pamoja na Rais na familia yake huku likiongozwa na rafiki wa Rais. Vilevile lilikuwa likifadhiliwa na huyo Mfaransa.

Kazi kubwa, kama nilivyo sema hapo awali , ilikuwa ni kuchochea chuki kati ya Wahutu na Watutsi, huku radio hiyo na gazeti hilo vikiwahamasisha Wahutu wajiweke tayari kuwashambulia na kuwavamia Watutsi ambao kila wakati liliwasema kuwa wanataka kurudisha utawala wao wa kifalme, kila Mhutu amwue Mtutsi aliye karibu nae. Maneno makali kama haya ambayo yaliyotokea kila siku katika vyombo hivi yalikuwa ni chanzo kikubwa kwa mambo yaliyotokea kwanzia tarehe 6 Aprili alipouawa Rais," Padri Karangwa alieleza.

"Naona saa zimeenda, tumezungumza sana maana sasa yapata saa tatu na nusu usiku. Lakini kabla hatujamaliza Padri hasa nani alimuua Rais?" Willy aliuliza.

Sura ya Padri alibadilika na kisha akauliza, "Unataka maoni yangu binafsi?"

"Ndiyo kwani kwa maoni yako kutokana na ulivyonieleza unaweza kuhisi, na hisia zako zinaweza kuwa sahihi,willy alijibu.

"Maoni yangu binafsi ni kwamba Rais aliuawa na Akazu. Ilipoonekana kuwa Rais alikuwa ameamua kutia sahihi ya makubaliano ya Arusha, hiki kikundi chake cha Akazu kikajua huu ndio utakuwa mwisho wao kufaidika. Hivyo wakaamua kumuua Rais ili katika machafuko hayo, waweze kupanga serikali mpya na kusimika utawala wao mpya ambao ungewahakikishia kuendelea kufaidi. Ukweli kuwa watu wake ndio waliomuua kwa kuogopa utawala wa kidemokrasia ambao ungefuata baada kutia saini makubaliano ya Arusha, ulijitokeza katika gazeti lao la Kangura, katika gazeti hilo ilitabiriwa kuwa Rais angeuawa na askari wa jeshi la Rwanda mnamo mwezi wa machi 1994 kufuatia kukubali kwake kusaini makubaliano ya Arusha. Gazeti hilo ambalo lilichapishwa mnamo mwezi wa Januari 1994 liliendelea kusema kuwa atakayemwua Rais atakuwa ni Mhutu. Na likasema kuwa waandishi wa gazeti hilo na rafiki zake na Rais huyo walimuasa asiweke saini makubaliano ya Arusha lakini ilionekana kuwa Rais alikuwa amebanwa sana na serikali zilizokuwa zikisuluisha mgogoro kiasi kuwa alikuwa hana msimamo. Hivyo, gazeti hilo katika toleo hilo, lilisema kuwa Rais atauawa na hapo ndipo vitatokea vita na damu nyingi itamwagika na jeshi la UNAMIR lisingeweza kufanya kitu. Lilizidi kumshauri Rais akatae kutia saini makubaliano hayo vinginevyo kifo chake hakitaepukika. Na yote yaliyoandikwa kwenye toleo hilo ndiyo yaliyotokea. Rais alipokubali tu kutia sahihi makubaliano ya Arusha basi hawa watu wake wakatimizi ahadi yao kwani wao ndio walioshika hatamu zote za serikali kuanzia utawala mpaka jeshini. Kwa hiyo, baada ya kusikia amekubali makubaliano ya Arusha basi walikiamurisha kikosi cha mizinga cha Kanombe, na ndege ya Rais ilipokuwa inakaribia kutua makombora matatu

yalipigwa, mawili yakaipiga ndege; Rais na watu wote waliokuwemo, ikiwa pamoja na Rais wa Burundi, wakauawa. Akazu walipanga kuwa baada tu ya Rais kuuawa basi jeshi lao la Interahamwa lingeanza mauaji mara moja ya kuakikisha kuwa Watutsi wote pamoja na yeyote aliyekuwa anawaunga mkono anauawa. Mbinu hii ilikuwan ni kutaka RPF kukosa watu wa kuwaunga mkono ndani ya nchi hiyo na hivyo kushindwa vita. Lakina ya mungu mengi, mambo hayakwenda moja kwa moja kama walivyotarajia," Padri Karangwa alieleza na kuchukua glasi ya maji na kunywa.

"Lo maelezo yako yameniingia vizuri na nafkiri kutokana na ulivyoeleza kweli Rais aliuawa na mfumo wake mwenyewe wa kung`ang`ania madaraka kwani hata wakati alipokuwa amefikia kubadili mawazo yake, mfumo wake aliokuwa ameuweka haukumpa nafasi. Hivyo, ilibidi ummalize ili ubinafsi wa watu wake waliomzunguka uendelee,"m Willy alisema huku akiwa kama anajisemea mwenyewe.

"Watu ka nyinyi basi ndio mnaotakiwa mueneze habari hizi ili viongozi wengine wajue kuwa utawala wa mabavu, na wakung`ang`ania madaraka ili wewe tu ndio ufaidike una mwisho wake, na mwisho wake ni mbaya ata ufanyeje,"Padri Sibomana alidakia.

"Tutajitahidi kueleza ukweli huu," Willy alijibu.

"Nafikiri itakuwa vizuri kesho kama ukipata nafasi uje nikuonyeshe mauaji yalivyo fanyika, uone ukatili usio kifani,"Padri karangwa alimweleza Willy.

"Nitajitahidi, lakini kwa vile nina shughuli nyingi inabidi nirudi haraka Arusha. Kama sitaweza kufika maelezo yako yanatosha. Na kabla basi sijaondoka nikuulize swali."

"Uliza usiwe na wasiwasi, sisi tumefurahi kuwa nawe hapa wala hatuoni kama muda unaenda" Padri Karangwa alijibu.

"Unafikiri baada ya RPF kuchukua madaraka kutakuwa na maana na uelewano Rwanda? au niulize tena vingine baada ya haya mauaji ya kikatili dhidi ya Watutsi yalivyofanywa na Wahutu, unafikiri kutakuwa na uelewano kati ya makabila haya hata kama RPF itaweka utawala wa demokrasia?"

"Hilo swali gumu lakini nafikiri ndilo swali lenye maana kubwa sana. Uelewano kwa sasa utakuwa mgumu. Vidonda vya mauaji ya ndugu zao Kitutsi bado vibichi na kama binadamu lazima kutakuwa na kisasi, kwa hili tusijidanganye. Pili, baada

ya RPF kuchukua madaraka maelfu ya Wahutu wamekimbia ni wakimbizi huko Tanzania, Zaire, na nchi zinginezo. Kati ya hawa waliokimbia na hasa waliokimbilia Zaire, ni wale Interahamwe na wanajeshi wa serikali ya zamani. Kwa vyovyote, hawa nao wataanza kujikusanya na kuunda tena jeshi la kuja kuvamia tena Rwanda, na Serikali ya sasa haita kubali. Hivyo, vita vitaendelea na itaendelea kwa muda mrefu kama jumuiya ya kimataifa itaendelea kulipa kisogo swala hili la Rwanda. Tatu, miongoni mwa wakimbizi wanaoumia ni wanawake na watoto, na watoto hawa taabu watakazozipata huko watakuwa wanaelezwa kuwa ni sababu ya Watutsi ambao wamewafukuza nchini mwao na hivyo kujenga chuki tena. Watoto wa Kitutsi vilevile watakuwa wanaelezwa ndugu yako fulani aliuawa na Wahutu; na kwa vile kila familia iliathirika chuki hii itazidi kujengeka maradufu. Mimi maoni yangu ni kwa serikali ya RPF isilipize kisasi. Wakimbizi wote warudishwe nyumbani. Wale ambao wanajulikana kabisa ndio waliusika na kuongoza mauaji haya ya kikatili, wakamatwe kokote duniani waliko na wafikishwe maakamani. Kama dunia hii isivyokuwa na usawa, wale wote walioongoza mauaji haya kwa vile wana pesa tayari wapo nchi za nje wanakula starehe. Wanaohangaika sasa ni wanawake na watoto; hii si sawa. Lazima hawa watu wakamatwe hasa kundi la Akazu, wote wakamatwe wafikishwe maakamani,"Padri Karangwa alimalizia huku sasa machozi yakimlengalenga.

"Kwa kweli, hali ya nchi yetu hii itayumba kwa muda mrefu. Wote wanachotegemea sasa ni serikali ya RPF iweze kuwahamasisha wananchi waweze kusameheana ili tujenge taifa jipya. Nakubaliana na Padri Karangwa kuwa ili tukio kama hili lisitokee tena, wote waliohusika na kitendo hiki wafikishwe mbele ya maakama wahukumiwe na adhabu kali itolewe ili kitu kama hiki kisitokee tena popote duniani, maana ni kitu cha kutisha ambacho kinafanya akili isikubali kuwa binadamu anaweza kuwa katili na mharibifu namna hii kama ilivyotutokea sisi hapa. Hapa Willy, dunia isinyamaze mpaka hapo wote waliohusika wameadhibiwa," Padri Sibomana alitoa maoni yake.

Huku akiinuka, Willy alishukuru na kusema, "kusema kweli sina maneno ya kuweza kueleza jinsi ninavyo shukuru kwani naweza kurudi Arusha kesho maana yote nimepata niliyotaka kujua kwenu na nimejifunza mengi, asante sana. Nipatapo nafasi nitawatembelea tena. Nikishindwa kuja kesho mara nyingine nitakuja kwa mapumziko. Asanteni sana, tena sana."

"Nasi tunashukuru sana kwani kuja kwako kumetufariji kumbe kuwa huko duniani kuna watu wanaoyajali matatizo yetu yaliyotupata. Asante sana," Padri Karangwa alimalizia, kisha wakamsindikiza Willy mpaka kwenye gari lake; akaondoka.

# SURA YA SABA

BIBIANE

Ilikuwa yapata saa nne usiku wakati Willy Gamba alipokuwa akielekea nyumbani kwa Col. Rwivanga, akitokea Centre Christus. Walikuwa wamekubaliana na Col. Rwivanga kuonana baada tu ya Willy kutoka kwa Mapadri. Wakati anakaribia kukata kona kuingia Barabara inayoingia sehemu ya Kimihurura ili aelekee nyumbani kwa Col. Rwivanga alipitwa na gari nyingine aina ya Landrover 110, lililokuwa likienda kasi sana na kama asingekuwa makini katika uendeshaji wangeweza kumgonga maana pamoja na kuonyesha ishara ya taa kuwa anahitaji kuingia kushoto lakini gari hilo lilipita kasi bila kujali ishara ya taa.

"Hawa wanajeshi ndio sababu hupata ajali mara kwa mara, uendeshaji wao ni wa ovyo sana", Willy alijisemea moyoni na kisha akakata kushoto kuelekea nyumbani kwa Col. Rwivanga.

"Endesha kwa tahadhali Felician, tungeweza kumgonga yule mtu ikaleta balaa hata kabla hatujaanza kazi. Kazi yetu ni kummaliza Willy Gamba na wala si kugonga magari ya watu ovyo", Xavier Nkubana alikaripia Felician.

Nkubana na wenzake waliwasili jioni ile mjini Kigali kwa ndege ya serikali ya Tanzania ambayo iliwasili na ujumbe wa Serikali ya Tanzania uliofika kuchunguza tukio la kulipuliwa kwa ndege ya Tanzania iliyokuwa inamilikiwa na Kampuni ya ndege ya Tanzaiar. Ndege hii iliwaleta maafisa kutoka idara ya usalama wa anga, mambo ya nje, polisi na waandishi wa habari. Nkubana na wenzake walifanyiwa mpango na kupanda ndege hii kama wafanyabiashara wa kinyarwanda waishio Tanzania walikuwa wakirudi nyumbani Rwanda kuangalia hali ya nchi ilivyo kwa wakati huu ili kama ikiwezekana waanzishe biashara tena kati ya Tanzania na Rwanda. Waliingia Rwanda bila tatizo lolote na kupokelewa vizuri na viongozi wa serikali ya Rwanda na kupelekwa kwenye Hoteli ya Des Mills Collines. Kwa vile walijulikana kama wafanyabiashara, baada ya kufikishwa hotelini waliachwa ili waendelee na mambo yao, na wale maofisa wa serikali ya Tanzania wakaanza kushugulikiwa na wenzao kuhusu mambo ya hotelina mambo mengine ya kiusalama.

Baada ya kuchukuwa vyumba na kuoga. Nkubana aliondoka na kuelekea nyumbani kwa Co. Gatabazi na kuwaacha wenzake wakipumzika, kwani ratiba yao

ya kazi ilikuwa usiku ule ule. Ilikuwa yapata saa moja hivi Nkubana alipowasili nyumbani kwa Col. Gatabazi aliyekuwa akimsubiri.

"Karibu sana", Col. Gatabazi alimkumbatia Nkubana kwani walikuwa hawajaonana kwa muda mrefu.

"Asante, naona mambo mazuri", Nkubana alijibu.

"Mambo mazuri gani haya! Mambo yatakuwa mazuri baada ya sisi wenyewe kuchukuwa madaraka ya nchi hii. Kila siku nasikia uchungu moyoni kuona 'Inyenzi' inazidi kujiimalisha hapa. Lazima mambo yafanyike haraka kabla hawajajizatiti sawasawa, karibu ndani", Col. Gatabazi alijibu huku akiwa ameushikilia mkono wa Nkubana kisha akamwongoza kuelekea sebuleni.

"Utakunywa nini?", Col. Gatabazi alimuuliza.

"Nipe chai kama ipo".

"Tena na mimi sasa hivi nilikuwa nakunywa chai", Col. Gatabazi alijibu na kwenda kuchukuwa chupa ya chai na vikombe viwili vya chai, wakakaa mezani pale sebuleni.

"Karibu".

"Asante sana". Nkubana alichukua kikombe chenye chai na kuanza kunywa.

"Ehee, hamkupata tatizo lolote?".

"Wewe unacheza na mipango ya JKS nini?, atakapokuwa Rais wa Tanzania na wewe hapa mbona tutakula kuku mpaka tuchoke! Tumekuja kwa heshima zote na kupokelewa na 'Inyenzi', na kutupeleka mpaka hotelini. Wangeweza hata kutulipia hoteli lakini sisi tumekataa maana tumekuja kama wafanyabiashara hivyo ni vizuri kujitegemea", Nkubana alijibu.

"Vijana wako katika hali nzuri?".

"Wako na moto kama nini, maana wanataka kumaliza kazi usiku huuhuu, na baada ya hapa tunaelekea Bukavu tukasaidie kupanga mapambano dhidi ya 'Inyenzi', JKS ametueleza mipango yote nasi tumeafiki".

"Hiyo safi, lakini kwanza mambo ya hapa. Huyu Willy Gamba ni mtu hatari kabisa. Inabidi tumfanyie mkakati mzuri. Siyo mtu wa kawaida", Col. Gatabazi alieleza lakini kabla hajajendelea Nkubana alimkata kauli.

"Yaani huna maana sisi watu watano ambao ni sawa na jeshi zima la askari shupavu, bado una wasiwasi? Hivi umesahau kuwa sisi ni makomandoo, tupe mipango tujuwe yuko wapi, kazi ingine tuachie sisi wenyewe", Nkubana alijigamba.

"Imebidi nikutahadharishe kwanza, msije mkamwendea kwa pupa. Ni lazima tupange mipango mathubuti. Inabidi kwanza kueleza nyendo zake kutokana na upelelezi niliofanya toka mambo yaliyotokea juzi usiku", Col. Gatabazi alijibu.

"Sawa endele", Nkubana alijibu huku akionyesha kuwa Col. Gatabazi alikuwa anazidi kupoteza muda kwani anaamini hakuna mtu. Hata awe wa uwezo wa aaina gani asingeweza kutamba mbele ya kikosi chake.

Nkubana alikuwa kati ya askari waliopatiwa mafunzo ya kijeshi na kijasusi kwa pamoja. Alikuwa na cheo cha Meja Jeshini lakini aliingia hata katika kambi za RPF huko Uganda na kuchukuwa habari na ndiye ambaye mara nyingi aliifanya RPF isifanikiwe katika mashambulizi yake kwani yalijulikana mapema. Inasemekana mauaji yote yaliyofanywa kwa watu na wanajeshi waliokuwa wakitoa habari kwa RPF yalifanywa na yeye. Alikuwa jasiri na shupavu lakini uso wake kila siku utadhani wa padri hata namna yake ya kusema akiwa na watu wa kawaida. Pia inasemekana kuwa 'Akazu' walimchagua kufuatilia maofisa ambao baadaye waliwafundisha Intarahamwe, na kuwapa amri kumi ili wazieneze kwa Wahutu. Mhutu yeyote ambaye asingezifuata na kuzitekeleza basi auawe hapohapo.

Na hizi amri kumi za Wahutu zilikuwa kama ifuatavyo.

1. Kila Mhutu ajue kuwa mwanamke wa Kitutsi kokote aliko, yuko kwa manufaa ya watutsi. Kwa hiyo mtu yeyote atakayeoa, kufanya urafiki au kumwajiri mwanamke wa Kitutsi kama mfanyakazi wake au mkewe basi Mhutu huyo ni msaliti, lazima auawe.

2. Kila Mhutu ajue kuwa ni mwanamke wa Kihutu tu anjayefaa kama mke, kama rafiki na kama mfanyakazi wake ofisini.

3. Wanawake wote wa Kihutu lazima wewe imara na wawahamasishe waume zao, kaka zao na watoto wao wa kiume kumchukia Mtutsi.

4. Kila Mhutu lazima ajue kuwa Mtutsi yeyote si mwaminifu katika biashara. Hivyo, Mhutu anayefanya biashara na Mtutsi, anayewekeza fedha zake au za

serikali katika kampuni za Kitutsi, anayekopesha ama kukopa kwa Mtutsi, anayewasaidia wafanyabiashara wa Kitutsi ni msaliti, anatakiwa kuuawa.

5. Kazi zote za juu katika siasa, utawala, uchumi, jeshi na usalama lazima wapewe Wahutu.

6. Katika sekta ya elimu (walimu, watoto wa shule na nguo), lazima wengi wawe Wahutu.

7. Jeshi la Rwanda liwe kwa Wahutu tu. Na mwanajeshi haruhusiwi kuona Mtutsi.

8. Wahutu waache kuwaonea huruma Watutsi, unyama unyama tu dhidi ya Watutsi.

9. Wahutu popote walipo duniani lazima wawe na umoja kwa kila njia na wajaribu kuzima propaganda za Watutsi na kuungana katika kuwaangamiza Watutsi.

10. Mapinduzi ya kijani ya mwaka 1959 na itikadi za Kihutu lazima zifundishwe kwa kila Mhutu. Na Mhutu yeyote anayemwonea Mhutu mwenzake kwa kueneza itikadi hizi basi huyo Mhutu auawe, maana ni msaliti.

Kwa kutumia askari wa vikosi alivyovifundisha Nkubana alihakikisha kuwa amri hizi zinatekelezwa na zinachochea chuki ya Wahutu dhidi ya Watutsi kama alivyoagizwa na Akazu.

Huyu ndiye Nkubana, mtu jasiri, aliyehitimu katika shule mbalimbali za kijeshi, kijasusi na kikomandoo ulimwenguni, lakini mafunzo yake yote yalikuwa ya dhamira moja tu, ya kuhakikisha kuwa utawala wa Kihutu uliokuwa madarakani unaendelea kutawala milele na milele kwa njia moja tu kuhakikisha Watutsi wote wanafyekwa ili wasiwepo tena duniani. Hivyo, kwake mtu yeyote aliyemuunga mkono Mtutsi lazima afe na yeyote aliyesaidia Mhutu basi yeye Nkubana alimsaidia kwa lolote. Hivyo ndivyo walivyoweza kuelewana na kundi la Jean kwani lilikuwa upande wa Akazu. Na habari za Willy Gamba kuwa alikuwa anajaribu kuharibu mipango ya Wahutu kurudi madarakani, zilimuudhi sana na kusikia hasira isiyo kifani dhidi ya Willy Gamba.

"Lazima usiku huu huu afe", Nkubana alijishitukia amesema kwa hasira hata Col. Gatabazi aliyekuwa ameanza kueleza mipango akashituka. Akashtuka.

"Haya sasa endelea, huyu mtu ameniudhi sanasana, tayari hukumu yake ya kifo imeshapita".

Col. Gatabazi ilibidi aanze upya kumpa mipango ya usiku ule kama walivyokuwa wamepanga na Jean na JKS.

Willy Gamba alimkuta Col. Rwivanga anakula chakula. Alipomuona Willy alionekana kufurahia "Nimekusubiri sana mpaka nikaamua bora niendelee na chakula maana ni zaidi ya saa nne sasa na unajuwa mimi nakula mara moja tu kwa siku, njaa ilikuwa inauma sana", Col. Rwivanga alijitetea.

"Usijali Kamanda", Willy alijibu huku akielekea jikoni kuchukua sahani na kisha akaketi kwenye meza pamoja na Col. Rwivanga na kupakuwa chakula.

"Hiki chote kilikuwa chako peke yako", Willy alimkejeli Col. Rwivanga.

"Hapana, nilijuwa tu utanikuta nakula", Col. Rwivanga alijibu huku akicheka. Willy alichota kijiko cha kwanza na kukitia mdomoni, chakula kilikuwa wali na mchemsho wa nyama.

"Lo, mpishi ni wewe?".

"Kwani vipi?".

"Kitamu sana chakula hiki", Willy alijibu.

"Wapi, na wewe una njaa vilevile, upishi wangu mimi ni mchemsho tu".

"Hapana si njaa ila wali umepikwa vizuri na nyama ya mchemsho, napenda sana mimi", Willy alieleza.

"Ehe vipi huko, umewakuta?".

"Bwana nimewakuta wale mapadri na nimewekwa shule hasa, na sasa hivi naijua historia ya utawala wa nchi vizuri sana kuanzia kabla ya ukoloni".

"Wacha bwana".

"Nakuambia wale mapadri wanaijua nchi hii kuliko viganja vya mikono yao", Willy alimweleza Col. Rwivanga, kisha akamgusia kwa muhtsari mambo muhimu aliyoelezwa.

"Kumbe hili swala la Akazu hata hawa wazee wanalifahamu sana?", Col. Rwivanga aliuliza baada ya maelezo ya Willy.

"Sana, na wamesema bila hawa watu kukamatwa hakuwezi kuwa na amani katika nchi hii".

"Hilo ni kweli kabisa na sisi tunalijua na ninafikiri ndio walio nyuma ya hili swala la kutaka kukuua maana hawa watu wana mahusiano dunia nzima na pesa nyingi. Hivyo, tunajua wanajipanga kuja kutuhujumu, hilo tunajua. Ila hatujui kwa sasa hivi wanafanya shughuli zao kutoka wapi. Nia yetu imekuwa ni kuimarisha serikali yetu, halafu ndipo tuangalie habari yao", Col. Rwivanga alieleza.

"Ni sawa, lakini mimi nafikiri jambo hili mgelishughulikia sasa hivi wakati bado nao wamechanganyikiwa, lakini mkisubiri watakusanya nguvu halafu itakuwa shida tena", Willy alishauri.

"Kutokana na matokeo ya siku hizi mbili nasi tumeshituka sana, maana inaonekana hawa watu bado wana watu ndani ya serikali yetu na wameanza kutuhujumu. Kama unavyosema, nasi tumeamua kulishughulikia mara moja swala hili na tutakuwa na mkutano na makamanda wote wa jeshi pamoja na baraza la mawaziri kesho saa moja na nusu asubuhi", Col. Rwivanga alieleza.

"Hivyo itakuwa vizuri. Ingawaje mimi kazi iliyonileta haikuwa ya mapambano, lakini kwa sababu wao ndio wamenianza na mimi naomba ruksa yako unilinde mbele ya wakubwa wako, kwani nataka nami kwa kiasi fulani nijuwe habari ya watu hawa na vipi wameamua kutaka kuniangamiza. La maana hasa nataka nijuwe nani hasa anahusika na kutaka kuniua mimi. Hilo Col. Rwivanga ningependa sana unipe hiyo nafasi nifanye kazi yangu", Willy alijieleza.

"Ni sawa lakini tungeomba na sisi utufahamishe kila hatua unachofanya ili tuweze kukusaidia itakapobidi kwani ukweli ni kuwa kazi hii ni yetu na wala si yako", Col. Rwivanga alijibu.

"Asante Col. Rwivanga. Vipi yule msichana wa jana usiku, Bibiane umepata habari zake?".

"Ahaa, ndio nilikuwa nakusubiri nikueleze. Hivi usingewahi ungenikuta nimeshaenda kumfuata. Huyu msichana inasemekana ni mkalimani, anajuwa lugha kama nane hivi na amekuwa akifanya kazi serikalini kama mkalimani hivyo, alikuwa akisafiri na Rais au mawaziri ama maafisa wakubwa wa serikali wanaposafiri nje ya nchi na vilevile ndiye aliyekuwa mkalimani wa serikali kama wageni wasiojuwa kifaransa wakija nchini hapa. Inasemekana wakati wa mauaji yeye hakuwepo. Alikuwa Nairobi, lakini ni kati ya watu wa kwanza kabisa kurudi na amekaa katika nyumba yake aliyokuwa akiishi toka zamani mtaa uleule wa Silas Biniga, lakini nyumba ya nne mbele kwenye kona watu wamekuwa hawana wasiwasi nae kwani inasemekana ana asili ya Kitutsi ingawa ni chotara na uzuri

wake watu wengi wameuchukulia tu kuwa huenda ni chakula ya wazee. Kwa hivyo hakuna ambaye amediliki kumgusa. Hivyo nataka nikajuwe habari zake", Col. Rwivanga alieleza.

"Hapana, usiende wewe, maana wewe ni afisa wa ngazi za juu na unajulikana hapa la pili wewe ni mwanajeshi. Kazi hii ni ya mpelelezi kama mimi. Tatu, nina kisasi naye. Naomba uniachie, usiku huu lazima nitapambana naye kama bado yuko hapa mjini na nitakujulisha habari zake baadae".

"Sawa Willy, kazi kwako, mzee naye alinieleza ndio zako hizo ikibidi msichana au mrembo".

"Zamani siyo sasa, sasa nimestaafu maana nimeoa lakini kwa msichana kama yule ambaye hatishiki na mtu kuuawa, nataka mimi mwenyewe nijuwe habari zake. Habari ulizonazo ni kwamba bado yuko mjini?".

"Jioni hii ameonekana akiendesha gari lake aina ya MB 190E. Na hilo ni gari lake hata kabla ya mauaji na kabla sisi hatujaingia hapa. La ajabu si sisi wala si Intarahamwe aliyegusa gari lake, ni jambo la kushangaza na limefanya nitaka kujuwa huyu binti vipi mambo yake".

"Basi niachie maMBO yake utayapata. Si bure huyU binti ni mtu hatari, na hatari sana".

Baada ya Col. Gatabazi kumwelezea mipango yote kama walivyokuwa wamepanga na Jean, Nkubana aliomba gari ili akawachukuwe wenzake na kuanza kazi ya kumsaka Willy. Col. Gatabazi aliwapa gari aina ya Landrover 110 ya Jeshi ambayo hutumika kwa ajili ya wageni wa Serikali. Kwa sababu ya kazi maalum iliyokuwa ikiwakabili, kutokana na unyeti wa kazi hiyo, Col. Gatabazi aliwaachia gari hilo waendeshe wenyewe. Nkubana alikwenda, moja kwa moja akawaamsha wenzake, baada ya mazoezi makali, walioga na kupata chakula pale hotelini, kisha wakaanza kazi ya kupeleleza habari za Willy Gamba.

Kutokana na maelezo waliyokuwa wamepewa na Col. Gatabazi, mara moja walijua kuwa Willy yuko Meridien Hoteli, mara baada ya kupata namba ya chumba chake cha kulala waliamua kwanza wakafanye shughuli nyingine ili wasubiri wakati mzuri wa kupambana na Willy Gamba ambaye pia walikuwa wakimhofia kwa kiasi fulani.

Baada ya kupanga vyema mipango yao ya kuhakikisha wanamuua Willy Gamba usiku huo. Walirudi hotelini wakapata kinywaji kidogo kwa ajili ya kujiweka safi.

Ilipotimia saa nne hivi usiku wakaamua kwenda kwa wote kwa Col. Gatabazi kwa ajili ya mikakati ya ziada. Ni wakati huo walipokuwa wakielekea kwa Col. Gatabazi ndipo walipokaribia kuligonga gari la Willy Gamba bila wao kujuwa kuwa ndiye mtu anayepanga kumuangamiza usiku huo.

Kwa kasi ileile, gari hilo liliingia nyumbani kwa Col. Gatabazi, aliyekuwa nje ya nyumba yake akitafakari jinsi Willy alivyokuwa akiwanyima usingizi. alipowaona akawapokea kwa tabasamu kisha akawaongoza hadi kwenye sebule ya nyumba yake.

"Vipi mmepata habari zozote kuhusu Willy Gamba?", Col. Gatabazi aliwauliza baada tu ya kuketi kwenye makochi.

"Habari za Willy zote tunazo, huyo tutaanza biashara yake, atakuwa marehemu baada ya saa sita usiku", Nkubana alijibu kwa majidai na kujiamini.

"Nasema tena lazima muwe makini sana, huyo mtu ni hatari sana, na amri ni kwamba mara hii isishindikane, akionekana tu ua mara moja", Col. Gatabazi alisisitiza.

"Col. tafadhali usitutishe na huyo mtu wako, atakuwa hatari gari mbele yetu! Vipi una matatizo nini Col. Gatabazi?", Nkubana alijibu kwa mshangao huku vijana wake wote wanne wakicheka kwa dharau.

"Acha wasiwasi mzee, kazi ya Willy hesabu imeisha, amezoea kucheza na wafanzi leo atakutana na waalimu wa kazi", Felician alimhakikishia Col. Gatabazi.

"Ehe, Bibiane umemtaarifu kuwa tutakwenda nyumbani kwake leo?", Nkubana aliuliza.

"Bibiane ana taarifa zenu, na wakati ndio huu, twendeni basi mara moja, hiyo gari acheni hapa maana anakaa ileile nyumba yake", Col. Gatabazi alijibu.

"Ahaa, kweli gari tuache tu hapa, tutalipitia wakati wa kwenda mjini", Felician alijibu.

"Haya twendeni anatusubiri, lakini mjuwe kutokana na mipango ilivyo mimi nitawaacha pale nyinyi mtaendelea nae", Col. Gatabazi aliwaelza.

"Sawa hamna tabu", wote walijibu kwa pamoja na kuondoka kuelekea kwa Bibiane.

Wakati Willy anafika nyumbani kwa Bibiane. Col. Gatabazi alikuwa akifunguliwa lango la mbele nyumba hiyo akatoka na kuondoka akihofia matatizo aliyokumbana nayo kwa Luteni Biniga. Willy alichukuwa hadhari kubwa sana maana alichukuwa vifaa vya kazi si mchezo. Kwa vile nyumba ya Bibiane ilikuwa kwenye kona ya barabara mbili, Willy alibana kwenye kona moja na kuchungulia mbele ya nyumba na kuona lango likifunguliwa. Alimuona mtu mmoja akitoka na kukatisha barabara na kuelekea kwenye uchochoro na kutokomea. Willy alirudi nyuma kidogo na kuhisi kuwa sehemu ile ndiyo ilikuwa nyuma ya nyumba hii. Kwa hadhari sana alikwea ukuta uliozungishiwa vyuma vilivyochongoka juu. Kwa vile Col. Rwivanga alimweleza kuhusu hilo. Willy alikuwa amejitayarisha vizuri kabisa kwa lolote. Alikwea na kuchungulia ndani, baada ya kuangaza vizuri macho yake aliweza kuona kivuli cha mtu amebana kwenye ukuta wa nyumba hii karibu na upande wa pale alipokuwa yeye. Mtu huyu alikuwa amebeba bunduki kubwa. Hivyo, Willy alihisi ni mlinzi wa pale nyumbani.

Baada ya muda kidogo, Willy alimuona mtu mwingine anakuja akitokea upande wa mbele kuja upande huu ambao huyu mwingine alikuwa amebana. Willy alijining'iniza juu ya ukuta kwa nje ili asionekane huku macho yake yakiwa usawa wa ukuta. Yule mtu alikuja moja kwa moja mpaka usawa wa yule mwingine alipokuwa amesimama.

"Unataka sigara?", yule aliyekuja eneo hilo alimuuliza mwenzake.

"Sitaki, hao jamaa ndani si wamalize mambo yao haraka ili waondoke na sisi twende zetu, maana hapa tunapoteza muda na huku kazi yenyewe bado", yule wa pili ajibu.

"Mbona kama una wasiwasi, vipi unaogopa?".

"Kwanini nisiogope, mimi si binadamu bwana?".

"Acha woga wewe, wajuwa Kaisari alisema watu waoga mara nyingi hufa kabla ya tarehe ya vifo vyao kufika, komaa mtoto wa kiume", mwenzake alisema kwa kujiamini.

"Bwana, hebu nenda kalinde sehemu yako na umwambie huyo Nkubana aharakishe kutoka sehemu hii".

Baada ya kuelezwa, yule mtu aliyekuja sehemu hii kutoka mbele aliondoka kimyakimya kurudi kule alikotoka huku mwenzake akimsindikiza. Willy akatumia nafasi hiyo. Kama tumbili aliukwea ule ukuta haraka sana. Kufumba na kufumbua

akaruka juu ya vile vyuma na kujitosa ndani bila hata kusababisha kishindo na kujibanza kwenye ukuta. Kwa vile Willy alikuwa amevaa nguo nyeusi pale alipokuwa amejibanza ilibidi umsogelee karibu sana ndipo uweze kumtambua maana upande huu wa nyumba hapakuwa na mwanga. Mara akamsikia yule mlinzi akirudi upande wake, kutokana na mazungumzo aliyokuwa ameyasikia alihisi hawa nao bila shaka walikuwa kundi lilelile kama alilopambana nalo kwa Luteni Biniga. Bila shaka walikuwa wamekuja kwa malipo kwa huyu mwanamke. Willy alijitayarisha na kujibanza kwenye ukuta utafikiri buibui. Yule mtu alikuja akinyata taratibu utafikiri alikuwa amehisi kitu. Willy alikuwa amebana kwenye kona kabisa ya upande wa pili wa nyumba. Huyu mtu alipofika hapo tu, kama Simba anapomrukia Swala, Willy alimtia kabali kwa nguvu zake zote. Yule mtu hakuweza hata kuguna maana kabali ile ilikuwa kali, na huku akitumia utaalam kumuua kimyakimya kwa kumnyonga, Willy alimuua yule mtu. Kisha, alimvuta mpaka kwenye ua wa nyumba na kumvua shati, akavua lake na kuvaa la yule mtu kwani ukubwa wa mwili na urefu walikuwa wanalingana. Akatwaa silaha yake ya AK 47 'Machinegun' ya Kirusi na kuelekea mbele.

Alipofika kwenye kona ya mbele, Willy alimuona yule mtu mwingine akichungulia dirishani, si mbali na aliposimama Willy. Willy alikohoa kidogo na yule mtu akageuka kuangalia. Alionyesha ishala ya kumwita. Na yule, akijuwa fika kuwa alikuwa mwenzake, alikuja haraka bila hadhari. Alipokaribia, na kwa ajili ya giza aliamini ni yule mwenzake, alianza kusema, "Huko ndani naona mambo yanaa...", kabla hajamalizia sentesi yake, Willy alimrukia na kumpiga karate ya shingo na kumuua palepale. Alianguka chini kwa kishindo, na Willy alipomrukia pale chini akammaliza. Baada ya Willy kumkagua alimkuta na Bastola mbili, moja yenye kiwambo cha sauti na nyingine ya kawaida. Vilevile alimkuta na kisu ambacho ukikibonyeza kinachomoka na kutoka urefu wa nchi tisa. Kile kisu kilikuwa silaha hatari sana ikitokea watu wanapigana huku mmeshikana. Willy alijihisi mtu mwenye bahati kwani silaha kama hii kama ingebidi kumenyana bila kujuwa kuwa mtu anayo anakuondoa duniani haraka sana.

Sasa Willy alikimbia mbele kuangalia kama kulikuwa na mtu mwingine, lakini hakukuwa na kitu. Alipozunguka upande mwingine tena hakuna kitu. Kisha akachukua dakika chache kuhakikisha kuwa hakuna hatari nyingine, na alipohakikisha ndipo alipokwenda pale dirishani alipokuwa anachungulia yule mtu wa pili. Dirisha lile lilikuwa sebuleni na lilikuwa wazi kidiogo. Pazia la dirisha lilikuwa limerudishiwa kidogo kiasi kwamba ungeweza kuona ndani na kusikia maneno yote yaliyokuwa yanazungumzwa.

Willy alishangazwa kuwaona wanaume watatu na mwanamke mmoja ambaye mara moja alimtambua kwani alikuwa Bibiane. Hawa wanaume wote walikuwa wametoa Bastola zao wakizungumza na yule mwanamke. Wawili walikuwa wamesimama na mmoja ameketi kwenye kiti kilichokuwa kinaangaliana uso kwa uso na alichoketi Bibiane.

"Nakwambia hivi, sisi tumetumwa kuja kukuua na huyo huyo bwanako Jean. Faida yako kwake imesisha sasa wewe ni mzigo na yeye hataki kubeba mzigo", yule aliyeketi alimweleza yule mwanamke huku akionyesha kwenye sura yake maudhi na usongo wa ajabu.

"Wewe unatania. Jean! hawezi kusema hivyo. Kwa yote niliyomtendea na jinsi tunavyopendana, Xavier sema jingine kama wewe na Col. Gatabazi mmeamua kuniua basi niuweni, msimsingizie Jean, Jean ni wangu wa kufa na kuzikana", Bibiane alijibu huku akionyesha sura ya hofu maana aliwajuwa hawa jamaa ni wauaji.

"Wanawake ni watu wa ajabu. Epa", yule mtu ambaye Bibiane alimwita Xavier alimwita mmoja wa wale waliosimama.

"Eee", yule mtu alijibu kwa woga vilevile.

"Siku zote nakwambia wanawake ni wajinga, wewe huamini. Huyu anafikiri eti Jean alikuwa anampenda, Jean alikuwa anamtumia tu kama chombo. Kwanza alikuwa anakutumia kwa mambo yake ya kazi zake za kumwingizia pesa na pili, anapokuwa huku Afrika alikuwa akijisaidia kutimiza haja zake za kimwili; hata siku moja hajawahi kukupenda. Pale tu wewe na Col. Gatabazi mlipomweleza kuwa wewe umemwona Willy Gamba na Willy Gamba kukuona mara moja alijuwa Willy Gamba atakutafuta na akikupata utatoa siri, na ukitoa siri si ndiyo mambo yetu yameisha! kwa hiyo, mara moja ametoa hukumu ya kifo kwako na sisi tumekuja kutekeleza amri. Kwa kweli ni uhalibifu kwa kiumbe kizuri kama wewe kuuawa, lakini wewe sasa ni mzigo kwetu nasi hatubebi mzigo," Xavier alieleza.

Kwa maelezo haya Bibiane alijua kweli hukumu imetoka kwa Jean na huo ndio ulikuwa mwisho wake. Pamoja na ujuzi wake wote wa kupigana hakuthubutu mbele ya Xavier na wenzake kwani aliwajuwa vizuri, walikuwa wabaya mara kumi yake, na alijuwa kuwa hao hawabembelezeki hivyo, alikata tamaa na hasira zikampanda dhidi na Jean na machozi yakaanza kumtoka.

"Ukionana naye mwambie atakufa kifo kibaya sana. Nami naamini kuwa huyo Willy Gamba anayemuogopa kweli ndiye atakayenilipia kisasi", Bibiane alisema huku akitetemeka kwa hasira.

Xavier alisimama na kurudisha kiti chake nyuma. Bibiane naye akataka kusimama. "Hapana, kaa hapohapo, usilete ujanja hapa. Huyo Willy baada ya muda si mrefu mtaonana ahera, nasikia huko watu huonana tena. Hamtapishana zaidi ya masaa mawili na yeye atakuwa marehemu kama wewe".

Willy, ambaye alikuwa anasikia na kuona yote haya akiwa dirishani, alipoangalia usoni mwa yule aliyeitwa Epa, akajuwa huyu ndiye akayemuua Bibiane. Aliangalia nafasi aliyokuwa, akajuwa angeweza kumpiga risasi Epa na yule mwingine, lakini si Xavier. Kwa vyovyote Xavier angemmaliza Bibiane, lakini hakukuwa na njia. Hawa walikuwa ni wauaji wataalam, tena huenda wa kulipwa. Hivyo, ilikuwa ni afadhali kwake kupambana na mmoja kuliko watatu na kwa maajabu ya Mungu angeweza kumponyesha Bibiane ambaye akili yake ilimweleza kuwa angeweza kuwa mtu muhimu kwake.

Xavier alimkonyeza Epa. Yeye akavuta kiti na kuanza kugeuka. Bibiane akafumba macho, lakini kabla Epa hajafyatua risasi, palepale Willy akiwa dirishani na mikono yake yote ikiwa na Bastola, alimpiga risasi ya kichwa Epa na yule mwingine kifuani, na Bibiane akajirusha nyuma ya kiti, Nkubana kama umeme akamimina risasi dirishani. Lakini Willy alikuwa tayari amejitupa chini na kujiviringisha na kisha kuchukua AK 47 akamimina risasi kama hamsini hivi kumtia kiwewe Nkubana. Haya mambo yote yalitokea haraka sana kama kufumba na kufumbua. Nkubana alipoangalia akajuwa Epa na Karekezi walikuwa wamekufa na hakujuwa wamezungukwa na watu wangapi. Alijirusha kwenye dirisha upande wa pili ambalo lilikuwa la kioo kitupu na kuangukia nje na kisha kujiviringisha tena. Bibiane alichukua Bastola iliyodondoka kutoka kwa Epa na kujaribu kumpata Xavier lakini naye alijitosa nje akaurukia ukuta wa mbele kwa nanma ya ajabu na kuangukia uapnde wa barabarani. Willy alipokimbia upande ule wa pili ili kumuwahi Nkubana alikuwa amechelewa, Xavier naye alikuwa ndio anaishia baada ya kuruka ule ukuta.

Bibiane alipoinuka pale alipokuwa amejitupa kumfuata Xaviar akajikuta anaangalia kwenye mdomo wa AK 47.

"Tupa silaha yako mama, uko chini ya ulinzi", Willy alimweleza Bibiane.

"Aheri ya Musa kuliko ya Firauni, Bila shaka wewe ni Willy Gamba".

"Naamini wewe ni Bibiane".

Willy alimshika mkono Bibiane na bila hata kumwelezana wanaelekea wapi, wakakimbia kwa tahadhari kuwa kutoka eneo hilo kabla askari na watu wengine hawajafika kuangalia kilichotokea hapo kwani mlio wa risasi za Ak 47 ulikuwa umetikisa eneo hilo na kusikika vibaya sana wakati huo wa usiku

# SURA YA NANE

NGUVU YA RUSHWA

Nkubana, huku damu zikimtoka, alikimbia moja kwa moja mpaka nyumbani kwa Col. Gatabazi. Alipolisukuma lango la mbele alikuta likiwa wazi. Akaingia ndani, moja kwa moja kwenye mlango wa mbele ambao ulikuwa umefungwa. Aligonga kwa nguvu mpaka Col. Gatabazi aliyekuwa anaoga, alitoka haraka huku akiwa amejifunga taulo na bastola mkononi. "Nini", aliuliza kwa shauku baada ya kuona hali aliyokuwanayo Nkubana.

"Vaa tuondoke hapa, mambo yameharibika.

"Nini?", Col. Gatabazi aliuliza tena.

"Nakwambia vaa twende, mambo yameharibika", Nkubana alimjibu huku akielekea sebuleni, akafungua friji akatoa maji baridi na kunywa huku Col. Gatabazi akimwangalia kwa mshangao.

"Huyu mtu wako ni mchawi. Kawaua vijana wangu wote na sasa yuko na Bibiane. Kwa kuwa ilikuwa tumuue Bibiane, sasa atakuwa upande wa Willy Gamba. Hivyo, lazima tayari mambo yako yataelezwa, na Jeshi la RPF litakuwa hapa sasa hivi. Lililopo tuondoke hapa tufuate majeshi yetu Kihumba".

"Hebu nieleze vizuri imekuwaje, maana siamini kabisa mtu mmoja kufanya kazi kubwa namna hiyo, tena kwa watu wenye uwezo mkubwa kama wewe?", Col. Gatabazi aliuliza kwa hofu huku akielekea chumbani kujitayarisha kwa ajili ya kuondoka eneo hilo. Nkubana alimweleza kila jambo lilivyotokea kwa Bibiane na jinsi alivyopoteza vijana wake.

Willy Gamba akifuatana na Bibiane usiku huo, huku mkononi mwake ameshika bunduki kubwa aina ya AK 47, walitembea kwa tahadhari kubwa kuelekea nyumbani kwa Col. Rwivanga. Walipofika hawakumkuta na nyumba yake ikiwa imefungwa. Kwa vile Willy alikuwa amepewa ufunguo wa ziada, walikuwa wameamua kwa ajili ya swala la kiusalama Willy awe analala pale, Alifungua mlango na kumvuta Bibiane ndani. Aliwasha taa ya sebuleni na kumsukumia Bibiane kwenye kochi.

Kwa mara ya kwanza ndipo Willy alipomwangalia Bibiane vizuri. Alistaajabu kuona kiumbe kizuri kama hiki kilivyojiingiza kwenye vitendo vya ugaidi wa

ajabu. Hakika huyu msichana alikuwa mzuri. Ukisikia mrembo, urembo hio huu. Willy katika maisha yake alishawaona wasichana warembo lakini huyu alikuwa msichana mrembo kwelikweli.

"Asante kwa kuniokoa", Bibiane alimshukuru Willy Gamba huku akiwa amelegeza macho yake na kuonyesha tabasamu la aina yake mbele ya Willy ambaye alikaa kimya akimwangalia bila kujibu.

"Sasa niko upande wako, usipate taabu kunilinda, kwa jinsi ulivyookoa maisha yangu sasa nifanye vyovyote upendavyo", Willy kwa kumwangalia Bibiane machoni aliamini kuwa anasema ukweli.

"Nenda kaoge", Willy alimweleza Bibiane huku akielekea kwenye chumba alichokuwa akilala. Bibiane aliinuka taratibu na kumfuata Willy. Chumba alichokuwa akilala kilikuwa na maliwato ya ndani. Hivyo, alimuonyesha ishara Bibiane alifungua mlango na kuingia ndani.

Wakati Bibiane anaoga, Willy aliingia jikoni na kutayarisha kahawa. Alipoangalia saa yake ilikuwa yapata usiku wa manane. Alishangaa kwa nini Col. Rwivanga alikuwa hajarejea,  akajiuliza ameelekea wapi wakati huo.

Simu ilipoita Jean alikuwa amelala. JKS alikuwa amemweleza kuwa vijana walikuwa wamefika salama na kazi ya kumsaka na kumuua Willy Gamba ilikuwa ifanyike usiku ule. Alikuwa amefikiria jinsi Bibiane angeshangaa sana baada ya kuelezwa kuwa Jean ndiye aliyetoa amri ya yeye kumuua. Jean alikuwa mtu aliyefurahia uovu, alikuwa mtu katili afadhali ya mnyama. Alifurahi kusikia mtu akipata maumivu, na hapo ndipo roho yake ilipopata faraja. Pamoja na miaka yoye sita aliyokaa na Bibiane, utafikiri walikuwa mtu na mke wake, yaani mume na mke, bado alipomweleza Col. Gatabazi kuwa lazima Bibiane auawe moyoni mwake hakusikia masikitiko. Kilichomfurahisha na kumridhisha ilikuwa ni pesa na nguvu ya pesa, na si mapenzi. Jean aliabudu pesa kwani aliamini kuwa pesa ndizo zilizompatia uwezo alionao duniani.

Kwa kutumia pesa, Jean aliweza kuwakamata wakuu wa nchi nyingi duniani, hasa katika Afrika na Asia, lakini vilevile viongozi wa ngazi za juu katika serikali za nchi za Ulaya. Alipata kila alichokitaka kwa kutumia pesa. Hivyo, simu ilipolia alijua analetewa habari njema za kuuawa kwa Bibiane na Willy Gamba maana alikuwa amesema alikuwa amesema wakishauawa aelezwe. Kila alipopewa taarifa ya kuuawa kwa mtu alipata faraja ndani ya moyo wake, Ndio sababu maelfu ya

Watutsi walipouawa alisikia raha isiyo kifani. Hakika mtu huyu alikuwa mgonjwa, tena mgonjwa sana!.

"Jean", aliitikia kwenye simu.

"Col. Gatabazi hapa".

"Sema Col. Gatabazi".

"Kazi imeharibika".

"Nini?".

"Kazi imeharibika. Vijana wote wameuawa. Bibiane yuko hai na ameokolewa na Willy Gamba. mimi na Nkubana tunaondoka kwenda Kibunda, hatuna muda maana wakati wowote wataanza kutusaka, afadhari tuyaandae majeshi yetu tayari kwa vita", Col. Gatabazi alimwambia Jean.

"Ilikuwaje", Jean aliuliza kwa sauti ya kukata tamaa. Col. Gatabazi alimweleza kwa ufupi kama Nkubazi alivyomweleza.

"Basi tuonane kesho Goma, saa tisa mchana nitakuwa huko, natarajiwa kuja na ndege yangu, lakini nitampitia rafiki yetu Kinshasa", Jean alieleza na kukata simu kabla hata Col. Gatabazi hajajibu kitu.

Jean alipokata simu ya Col. Gatabazi, alitumia muda huo kupiga simu Zambia, Zaire, Afrika Kusini, Angola, Kenya na kumalizia Tanzania.

"Umenipata JKS?", Jean alimuuliza JKS baada ya kumweleza yote yaliyotokea na maelekezo mengine huku JKS akipatwa na shinikizo la damu.

"Nimekupata", JKS alijibu kwa sauti ya kutetemeka.

Bibiane alipomaliza kuoga alimkuta Willy amemtengea kikombe.

"Kahawa au chai?"

"Kahawa."

Willy alimmiminia kahawa na alipotaka kumwekea sukari Bibiane alikataa.

"Bila sukari," alisema.

Kwa mara ya kwanza vilevile Bibiane alimuangalia Willy vizuri na kumuona mwanaume mzuri sana, na alipofikiria namna alivyowasambaratisha akina Xavier na kundi lao, mwili wake mara moja ulisisimuka. Halafu, palepale akamfikiria

Jean na jinsi alivyompenda na kumfanyia kila kitu lakini akaamua kumuua. Hasira ilimpanda sana, na akaapa kiroho kuwa kwa vile yupo hai atalipiza kisasi.

"Unafikiri nini?" Willy alimwuliza Bibiane.

"Ahera."

"Umeshapona sasa?".

"Xavier alisema mimi na wewe tutaonana ahera baada ya masaa machache, akili yangu inafikiri huenda tupo ahera." wote walicheka.

"Uko tayari kuzungumza lolote," Willy alimuuliza Bibiane huku sauti yake ikiwa imebadilika ghafla na kuwa sauti yenye uzito fulani.

"Niko tayari, nimekuambia kila unachotaka," Bibiane alijibu kwa sauti ya mahaba.

"Wewe ni nani?" Willy alimwuliza.

"Mimi naitwa Bibiane Habyarimana, ni Mnyarwanda, na wewe?".

Willy alishtuka namna alivyo mjibu na kuzidi kuimarisha hisia zake kuwa huyu msichana vilevile alikuwa si mtu wa hivihivi ila alikuwa mtaalamu katika nyanja kama yake. Mara ya kwanza alipohisi, ilikuwa jinsi alivyojirusha nyuma ya kochi pale nyumbani kwake baada ya yeye kuwapiga risasi wale watu wawili, na alivyochupa dirishani kumfuata Xavier. Kwanza alifikiri alikuwa na mafunzo ya kijeshi tu, lakini kutokana na jinsi ya majibizano yao aligundua alikuwa na utaalamu zaidi.

"Willy Gamba, Mtanzania," alijibu na wote wakaangaliana kama wanapimana saizi. "Ningependa nijue historia yako nzima, na usinifiche kitu, mpaka kufikia uhusiano wako na hawa wauaji na hasa huyu aliyekuhukumu kifo bwana Jean", Willy alimwambia Bibiane.

"Nimeshatoa kauli yangu kuwa nitakueleza kila kitu unachotaka niseme. Hivyo, usiwe na wasiwasi nitakueleza, ila itabidi uwe na subira maana ni hadithi ndefu", Bibiane alijibu.

Bibiane alimweleza Willy kwa kirefu maisha yake ya utoto, maisha ya shule, juu ya baba yake na mama yake na akaendelea, "Mwaka nilipoanza kazi baada ya kuhitimu digirii ya kwanza ya lugha katika Chuo Kikuu cha Kigali, wazazi wangu wote wawili walikufa kwa ajali. Nilikuwa nimeanza kazi Wizara ya Mambo ya Nje kama mkalimani.

"Inasemekana kuwa wazazi wangu hawakufa kwa ajali ya kawaida ila waliuawa na vikaragosi vya Watutsi ambao walifikiri kuwa baba yangu alikuwa ndugu yake na Rais. Hivyo waliwaua wazazi wangu ili kumkomoa Rais. Kitendo hicho kiliniuma sana nikawachukia sana Watutsi", Bibiane alieleza.

"Pole sana", Willy alisema kwa sauti ya huruma.

"Kwa kunisikitikia kutokana na yaliyowakuta wazazi wangu, serikali ikanihamishia ofisi ya Rais, huko ndiko nilipokutana na Jean Yves Francois, yeye ni Mfaransa anaishi Paris lakini alikuwa rafiki kipenzi na Rais. Tulionana naye nyumbani kwa Rais ambako alikaribishwa na tulianza urafiki siku hiyohiyo", Bibiane alieleza Willy huku akimwangalia kwa jicho la kuiba.

"Huyu Jean Yves Francois ndiye aliyekufundisha ujasusi?", Willy alimuuliza.

"Umejuaje?".

"Nimehisi".

"Jean ni mfanyabiashara na alikuwa akifanya biashara na kundi la marafiki wa Rais pamoja na familia ya Rais, wakati mimi nafahamiana naye serikali ilikuwa imeanza kuwa na matatizo kwani Watutsi waliokuwa humu ndani na nje, nchini kwenu na Uganda walikuwa wakipigana ili waiangushe serikali. Jean ndiye aliyekuwa akimsaidia Rais kwa kumjenga kijeshi, kiusalama na kiutawala. Huyu Jean ana utajiri usio kifani, kwani ndiye anayezifadhili serikali na wakuu wengi wa nchi za Afrika. Kwa vile mimi pia nilikuwa kwenye himaya yake alinipeleka kwenye mafunzo ya kiusalama sehemu mbalimbali duniani".

"Na ukahitimu vizuri", Willy alidakia.

"Vizuri sana".

"Ehee, endelea".

"Si ni wewe unanikatisha".

"Huu utajiri aliupataje?", Willy aliuliza.

"Sijui mwenyewe ameupataje, ila anashughulika na mambo ya silaha. Hapa alikuwa analeta silaha, halafu anachukua chai yote na kahawa inayolimwa katika nchi. Hili suala ni moja ya malalamiko mengi ya wananchi maana Jean ndiye aliyekuwa akipanga bei anayotaka, na hakukuwa na mtu wa kusema kitu, maana alikuwa akifanya biashara na Rais na kundi lake, lililokuwa likiitwa Akazu.

Kusema kweli Jean na hilo kundi la Akazu ndio waliokuwa wanatawala na si baraza la mawaziri au Bunge", Bibiane aliendelea huku sasa Willy akimsikiliza kwa makini zaidi.

"Huoni kuwa hiyo haikuwa sawa?", Willy aliuliza.

"Mimi ningefanya nini, nilibaki kufanya kila nilichoagizwa kama ilivyokuwa kwa wengine wengi maana sasa hii ndio ilikuwa namna ya maisha. Ama uko na Akazu, vinginevyo hupati kitu cha aina yoyote, iwe mali, elimu au kazi ya aina yoyote Rwanda".

"Kwa hiyo rushwa ndio ilitawala utawala uliopita?", Willy aliuliza.

"Inategemea unavyotafasiri rushwa", Bibiane alijibu huku akiwa kama haelewi anasema nini.

"Rushwa ni pale vyombo vya serikali vinaposhindwa kufanya kazi zake, kwa sababu hiyo kushindwa kutoa haki kwa wananchi wake, na kuwafanya wananchi wengi wapoteze imani, utu, uhuru na maadili kwa serikali yao kwani wote sasa huishi kama wanyama ambapo mwenye nguvu na pesa ndiye anayepata anachohitaji", Bibiane alisema.

"Hivyo ndivyo, maana nchi inakosa maendeleo kwani mapato yote ya nchi badala ya kuendeleza watu wote huingia kwenye mifuko ya watu wachache. Na kama ulivyosema uhalali wa serikali kama chombo cha watu unakwisha, badala yale wale wanaofaidika ndio wanakuwa na nguvu zaidi ya serikali yenyewe", Willy alitafasiri rushwa.

"Kwa tafasiri hiyo nakubali kuwa rushwa ndiyo imetawala. Na sasa Watutsi na Wahutu walipoanza kudai demokrasia isingewezekana maana Jean na Akazu hawakutaka kusikia kitu kama hicho kwa vile kingeweza kuingila maslahi yao. Na ndio sababu Watutsi walipokazana na kusikia eti wako tayari hata kupigana na Akazu, kwa kufadhiliwa na Jean, walianza kulifundisha jeshi la wahutu lililoitwa Intarahamwe ili liweze kuwadhibiti Watutsi wa ndani na nje ya Rwanda".

"Kwa hiyo huyu bwanako Jean ndiye alikuwa Rais hapa?".

"Si hapa tu, mimi najuwa nchi nyingi ambako amewakamata wakuu wa nchi na viongozi wa ngazi za juu serikalini na anawajaza mapesa kila wakati".

"Huoni kuwa yeye ndiye ananufaika zaidi, maana anajaza mapesa watu wachache lakini yeye anachukuwa mali za wananchi wengi", Willy alijaribu kumwelimisha Bibiane.

"Najuwa, maana hata huko kwenu Tanzania pia amewakamata wakubwa, ndio sababu nchi yenu imekuwa ikisita juu ya suala hili la Rwanda".

Willy alisitushwa na taarifa hii lakini hakutaka kujionyesha maana kweli msimamo wa serikali ya Tanzania ulikuwa unalegalega kabla na hata baada ya mauaji.

"Ina maana maamzi yoyote ilikuwa lazima Jean akubaliane nao?".

"Ndiyo, na mapesa yalitembea sana kuhusu swala hili na viongozi wengi wamenufaika. Unafikiri kama swala hili lingefanyiwa maamuzi mapema mauaji yangetokea!", Bibiane alimwambia Willy kwa njia ya kushangaza.

"Kwa hiyo huyu Jean ndiye aliamru mauaji haya?".

"Baada ya Rais kuonekana kwamba angekubali mkataba wa Arusha. Jean na Akazu walikasirika sana maana hawakutaka, kama nilivyosema mwanzo, kugawana madaraka na mtu mwingine. Hii ingegusa maslahi yao. Kwa hiyo, kwanza ndio waliamru Rais auawe na pili tayari walikuwa wamewatayarisha na kuwahamasisha Wahutu kuwamaliza Watutsi wote asibaki mtu ili wajihakikishie uwezo wa kutawala milele. Mpango ulikuwa kwamba hata kama jeshi la RPF la Watutsi lingeshinda jeshi lao lazima baada ya kuchukuwa nchi wangeshindwa kutawala maana wangemtawala nani huku Watutsi wote wakiwa wameshauawa, waliobaki ni Wahutu watupu ambao hawawaungi mkono. Hivyo, ingewachukuwa siku chache kuuangusha na kuutokomeza kabisa utawala wa RPF. Hii ingebaki nchi ya Wahutu chini ya utawala wa Jean na Akazu.

Bibiane alipofika hapa ndipo Willy alipoanza kuelewa kwa undani mambo yalivyokuwa. Kumbe mauaji yote haya yalitokana na watu wachache kutaka kulinda maslahi yao ya kunyonya mali ya wananchi, na kutumia hiyo mali kuweza kuwachochea wananchi kuuana!.

Kwa mara ya kwanza Willy aliona jinsi ambavyo nchi zote za Afrika zilivyo hatarini kutokana na rushwa. Kwa vile viongozi wa nchi hizi kuabudu rushwa, hivyo Willy akaamini kuwa tukio kama la Rwanda kumbe linaweza kutokea mahali pengine katika Afrika!.

"Baada ya RPF kushinda na mipango ya Jean kushindwa, wana mikakati gani sasa?", Willy alihoji.

"Kama nilivyosema hawajashindwa. Wewe ndiye umeingilia ndani ya mipango yao, kuna mpango kabambe wa kuisambaratisha serikali ya RPF kutokea jimbo la Kivu, Zaire. Akazu wamekuwa wakiliimarisha jeshi lao katika makambi ya wakimbizi kule Goma na Bukavu, Zaire, huku Jean akiwatumia rafiki zake kutoka Afrika Kusini hasa waliowahi kuwa katika idara ya ujasusi ya makaburu, alikokuwa akinunua silaha na kuzipitishia Angola ya UNITA, Zaire na Zambia kwa kutumia viongozi wa ngazi za juu za serikali za nchi hizo ambao wako kwenye orodha ya malipo kutoka kwa Jean. Kwa hiyo mambo bdo sana Willy, vita ndio sasa karibu vitaanza".

"yaani dunia inafikiri kuwa kambi zilizoko Zaire ni za wakimbizi kumbe ni kambi za jeshi".

"Ni kambi za jeshi na serikali ya Zaire inajua na ndio inayosaidia hata mafunzo. Hata katika kambi zilizoko kwenu Tanzania kuna wanajeshi wa jeshi la zamani na Intarahamwe, na kuna watu wazito katika serikali yenu ambao wanalipwa na huyu Jean ili kuwasaidia hawa watu, kwa hiyo hili si dogo. Kama ulivyosema pesa ni kitu kibaya sana, watu hawaoni tena madhara ya mauaji yaliyotokea bali wanaona pesa tu".

"Swala la rushwa ni swala linalohujumu haki za binadamu, yapaswa lichukuliwe hatua kimataifa katika uzito huo wa haki za binadamu", Willy alijibu kwa hasira.

Bibiane alikaa kimya bila kujibu kitu.

"Wewe ulikuwa uwasaidie vipi Jean na Akazu katika kutekeleza huu mpango wao wa kuivamia tena Rwanda", Willy aliuliza.

"Usije ukanipeleka kwenye mahakama ya mauaji ya Arusha maana mauaji yale sikuyajuwa pia sikushiriki, nilikuwa Nairobi nikitokea kwenye mkutano Arusha. Ila juu ya hili la sasa Jean amekuwa akinituma kupashana habari kati ya kambi za wakimbizi ambazo ni kambi za jeshi lao huko Zaire, yeye na Akazu. Vilevile kuna wanajeshi na viongozi wa RPF ambao tayari wamenunuliwa na wako upande wa Akazu, mmoja wao ndiye anayetarajiwa kuchukua madaraka mara tu jeshi la Akazu litakapotwaa madaraka tena".

Willy hakuamini masikio yake kuwa tayari hata ndani ya RPF kuna wasaliti.

Mara moja Willy alielewa jinsi alivyotaka kuuawa na akagudua kuwa kweli kama anavyosema Bibiane kuna kiongozi wa juu na karibu sana katika serikali ya Tanzania amabye anamtumikia Jean na kundi la Akazu.

"Utasaidia kunipa majina ya watu wote unaowajuwa kuwa wanahusika, maana hiyo ndio njia pekee tunaweza kulikosha jina lako", Willy alimuasa Bibiane.

"Swala la Jean kunisaliti mimi, na kunihukumu kifo, bila kujali yote niliyomtendea kwa hali na mali ikiwa pamoja na kumpa mwili wangu auchezee atakavyo, na jinsi nilivyojitoa kumstarehesha. Willy mimi niko upande wako, kama uko tayari kupambana nao nihesabu na mimi. Jean akishaambiwa kuwa umenichukua ninavyomjua atataka apambane na wewe yeye mwenyewe, ikifika hapo niachie mimi. Majina na mipango yao yote ni juu yako na uongozi wa RPF mjuwe la kufanya kwani jeshi la Akazu, likisaidiwa na viongozi wa nchi kadhaa ambao ni marafiki na Jean watakuwa tayari kuingilia kati. Ni lazima liwahiwe mapema kabla halijajiimarisha sawasawa", Bibiane alieleza.

"Nafikiri swala la vita si letu, ni la serikali ya Rwanda na RPF, mimi nipe hayo majina na kutokea hapo ndipo nitajua kama kazi yangu imeisha au ndio kwanza inaanza", Willy alieleza taratibu.

Bila kuwa ameandika mahali popote, Bibiane alitoa kichwani jina hadi jina akianza na kundi la Akazu mpaka viongozi wa nchi mbalimbali wanaolipwa na Jean huku Willy akiyaandika chini kwa mshangao mkubwa, kwani watu waliokuwa wanatarajiwa wengi wao ni viongozi wanaoheshimika Afrika na kote duniani. Alishangaa zaidi Bibiane alipotaja jina la yule waliyekuwa wakimwita JKS wa Tanzania.

"JKS, hii imenishangaza sana, maana huyu ndiye anayetegemewa kugombea urais wa Tanzania katika uchaguzi mkuu unaokuja," Willy alimweleza Bibiane.

"Najua kabisa, na tayari Jean ameshamtengea mamilioni ya dola za Kimarekani zitakazo msaidia katika kampeni hiyo ya uchaguzi kuusaka urais. Nia ya Jean ni kuwa na marais vibaraka kote Afrika ili yeye na wenzake huko Ulaya, waweze kufanya vile wanavyotaka katika nchi hizi. Jean anaongoza kundi la wafanyabiashara wakubwa wanaomiliki makampuni makubwa ya kimataifa. Na nia yao ni kuhakikisha kuwa Afrika inakuwa soko lao tu, na hata siku moja Afrika isisimame kiuchumi. Ingawaje nchi zao zinapigia kelele rushwa, lakini nchi hizohizo ndizo zinazoyasaidia makampuni makubwa kwa madogo kutoa rushwa kwa nchi zinazoendelea, maana makampuni hayo yakitoa hongo, hongo hii huchukuliwa kama gharama na kutolewa kwenye kodi ya mapato. Hii yote inaonyesha unafiki wa nchi za magharibi, na kila wakati Jean alikuwa akinieleza kuwa kelele zote hizi kuhusu rushwa, demokrasia na soko huria ni kelele za kinafiki tu, lakini huku nyuma katika vikao vya viongozi wa nchi za magharibi ni

kuchochea rushwa. Wanajuwa kuwa rushwa ikiisha Afrika basi demokrasia na soko huria vitashamiri na hivyo uchumi wa nchi hizo utakua haraka sana, kitu ambacho hawataki kitokee. Jean anasema, rushwa ndiyo sera inayotumiwa kuendeleza umaskini katika nchi za Afrika ili nchi zilizo endelea ziendelee kuitawala Afrika kiuchumi. Kwa hiyo, iwapo JKS ataitawala Tanzania rushwa itazidi mara dufu, na kutokana na fedha alizotengewa na Jean lazima atashinda, kwani kila walipoweka mtu wao hajawahi kushindwa uchaguzi", Bibiane alieleza.

Sasa Willy alikuwa na picha kamili namna JKS alivyokuwa anahusika na swala zima la Rwanda. na sababu za Tanzania kutokuwa na msimamo dhabiti juu ya swala hili na kuweza kuyumbisha mikutano kule Arusha kiasi cha kutofikia maamzi kwa muda mrefu maana swala hili la Rwanda kwa muda mrefu lilikuwa chini ya Tanzania kwa muda mrefu na JKS alikuwa mmojawapo wa viongozi walioonyesha kuchoshwa na mauaji ya Rwanda. Na alifanya hivyo kwa shinikizo la Jean aliyekuwa akimlipa pesa nyingi na uchu wake wa kutaka madaraka kwa njia ya ruswa ili aweze kuyatumia kwa faida yake na kujinifaisha yeye na rafiki zake. Na ni hii rushwa iliyowanyima Wanyarwanda haki yao mpaka kufikia hatua ya kuuawa vibaya namna ile kweli ni aibu! Aibu sana kwa Afrika nzima.

"Vizazi vijavyo vitakapoyasoma na kuyaelewa matukio haya, hakika hawataamini, watajuwa sisi wote tulikuwa wendawazimu kabisa, kwani ni sisi wote ndio tulioachia hali hii ikafikia hapo ilipo, kwa kuwapa walarushwa madaraka kwa gharama ndogo ya kuuza kura zetu na wao kutumia madaraka tuliyowapa kwa malipo ya fedha kidogo, lazima wayatumie kutuangamiza", Willy alisema kwa uchungu huku akikuna kichwa chake.

Mara moja Willy alimkumbuka Malisa wa Arusha, aliyekuwa mshauri wa JKS katika masuala ya uhusiano wa Kimataifa kabla hajarudi Chuo Kikuu. Hivyo basi, alijuwa Malisa ndiye aliyemweleza JKS kuhusu msimamo na mipango ya PAM na kuteuliwa kwa Willy kufuatilia jambo hili. Willy aliamini kuwa JKS ndiye aliyetoa taarifa za safari ya Rwanda kwa Jean na kundi lake na ndi sababu ndege aliyopanda ikapigwa kabla ya kutua uwanja wa ndege wa Kigali.

"Kwa hiyo JKS ndiye aliyotoa habari zangu zote kwa Jean?", Willy aliuliza kwa shauku.

"Ndio, na ndio sababu Col. Gatabazi aliamru ndege hiyo ipigwe kabla ya kutua uwanja wa ndege, lakini kwa bahati na umahiri wako ukawaponyoka", Bibiane alijibu huku akimwemwesa. Mara mlango wa mbele ukafunguliwa na Col. Gatabazi akaingia ndani.

Willy alipoangalia saa yake ilikuwa yapata saa tisa usiku. Wote walisimama, na Willy akawatambulisha.

"Pole Kanali, leo tumepata mgeni na anaitwa Bibiane, na Bibiane huyu ndiye mwenyeji wetu. Col. Rwivanga, kiongozi katika serikali mpya ya RPF".

"Nashukuru kumfahamu", Col. Rwivanga alijibu.

"Nami nimefurahi kukuona leo, nimekuwa nikisikia sifa zako nyingi kwa muda mrefu, toka kwa Col. Gatabazi kuwa wewe ni mpiganaji hodari, hongera", Bibiane alijibu kwa tabasamu akimwangalia Col. Rwivanga.

"Asante kwa sifa hizo zilizotoka katika kinywa cha msichana mrembo kama wewe", Col. Rwivanga alijibu akaendelea, "Ehe, imekuwaje Willy, hebu nipe habari kamili, maana kazi tumeiona kwa Bibiane, sasa halafu ikawaje hivi", Col. Rwivanga alionekana kuwa wasiwasi na Bibiane.

"Mimi naomba nikalale ili mzungumze vizuri, nionyeshe chumba cha kulala", Bibiane aliomba.

Willy na Col. Rwivanga aliangaliana na Willy ndiye alikuwa wa kwanza kujibu, "Kwa vile nyumba hii ina vyumba viwili tu vya kulala, basi kalale chumbani kwangu, maana tayari hata kuoga umeoga huko. Mimi nitalala hapa sebuleni kwenye kochi hamna taabu".

"Asante", Bibiane aliwaaga na kuelekea chumbani huku wote wakimwangalia. Kisha wakatazamana na kutabasamu.

"Ehe, hebu nipe mambo".

Willy alichukua muda mrefu kumweleza mambo yalivyotokea na mambo mengine yote aliyoelezwa na Bibiane. Col. Rwivanga akasimama na kumshika mkono Willy kwa hatua aliyofikia haraka na kwa umakini mkubwa.

Simu ilipoita Jean alikuwa amelala. JKS alikuwa amemweleza kuwa vijana walikuwa wamefika salama na kazi ya kumsaka na kumuua Willy Gamba ilikuwa ifanyike usiku ule. Alikuwa amefikiria jinsi Bibiane angeshangaa sana baada ya kuelezwa kuwa Jean ndiye aliyetoa amri ya yeye kumuua. Jean alikuwa mtu aliyefurahia uovu, alikuwa mtu katili afadhali ya mnyama. Alifurahi kusikia mtu akipata maumivu, na hapo ndipo roho yake ilipopata faraja. Pamoja na miaka yoye sita aliyokaa na Bibiane, utafikiri walikuwa mtu na mke wake, yaani mume na mke, bado alipomweleza Col. Gatabazi kuwa lazima Bibiane auawe moyoni

mwake hakusikia masikitiko. Kilichomfurahisha na kumridhisha ilikuwa ni pesa na nguvu ya pesa, na si mapenzi. Jean aliabudu pesa kwani aliamini kuwa pesa ndizo zilizompatia uwezo alionao duniani.

# SURA YA TISA

Kwa kutumia pesa, Jean aliweza kuwakamata wakuu wa nchi nyingi duniani, hasa katika Afrika na Asia, lakini vilevile viongozi wa ngazi za juu katika serikali za nchi za Ulaya. Alipata kila alichokitaka kwa kutumia pesa. Hivyo, simu ilipolia alijua analetewa habari njema za kuuawa kwa Bibiane na Willy Gamba maana alikuwa amesema alikuwa amesema wakishauawa aelezwe. Kila alipopewa taarifa ya kuuawa kwa mtu alipata faraja ndani ya moyo wake, Ndio sababu maelfu ya Watutsi walipouawa alisikia raha isiyo kifani. Hakika mtu huyu alikuwa mgonjwa, tena mgonjwa sana!.

"Jean", aliitikia kwenye simu.

"Col. Gatabazi hapa".

"Sema Col. Gatabazi".

"Kazi imeharibika".

"Nini?".

"Kazi imeharibika. Vijana wote wameuawa. Bibiane yuko hai na ameokolewa na Willy Gamba. mimi na Nkubana tunaondoka kwenda Kibunda, hatuna muda maana wakati wowote wataanza kutusaka, afadhari tuyaandae majeshi yetu tayari kwa vita", Col. Gatabazi alimwambia Jean.

"Ilikuwaje", Jean aliuliza kwa sauti ya kukata tamaa. Col. Gatabazi alimweleza kwa ufupi kama Nkubazi alivyomweleza.

"Basi tuonane kesho Goma, saa tisa mchana nitakuwa huko, natarajiwa kuja na ndege yangu, lakini nitampitia rafiki yetu Kinshasa", Jean alieleza na kukata simu kabla hata Col. Gatabazi hajajibu kitu.

Jean alipokata simu ya Col. Gatabazi, alitumia muda huo kupiga simu Zambia, Zaire, Afrika Kusini, Angola, Kenya na kumalizia Tanzania.

"Umenipata JKS?", Jean alimuuliza JKS baada ya kumweleza yote yaliyotokea na maelekezo mengine huku JKS akipatwa na shinikizo la damu.

"Nimekupata", JKS alijibu kwa sauti ya kutetemeka.

Bibiane alipomaliza kuoga alimkuta Willy amemtengea kikombe.

"Kahawa au chai?"

"Kahawa."

Willy alimmiminia kahawa na alipotaka kumwekea sukari Bibiane alikataa.

"Bila sukari," alisema.

Kwa mara ya kwanza vilevile Bibiane alimuangalia Willy vizuri na kumuona mwanaume mzuri sana, na alipofikiria namna alivyowasambaratisha akina Xavier na kundi lao, mwili wake mara moja ulisisimuka. Halafu, palepale akamfikiria Jean na jinsi alivyompenda na kumfanyia kila kitu lakini akaamua kumuua. Hasira ilimpanda sana, na akaapa kiroho kuwa kwa vile yupo hai atalipiza kisasi.

"Unafikiri nini?" Willy alimwuliza Bibiane.

"Ahera."

"Umeshapona sasa?".

"Xavier alisema mimi na wewe tutaonana ahera baada ya masaa machache, akili yangu inafikiri huenda tupo ahera." wote walicheka.

"Uko tayari kuzungumza lolote," Willy alimuuliza Bibiane huku sauti yake ikiwa imebadilika ghafla na kuwa sauti yenye uzito fulani.

"Niko tayari, nimekuambia kila unachotaka," Bibiane alijibu kwa sauti ya mahaba.

"Wewe ni nani?" Willy alimwuliza.

"Mimi naitwa Bibiane Habyarimana, ni Mnyarwanda, na wewe?".

Willy alishtuka namna alivyo mjibu na kuzidi kuimarisha hisia zake kuwa huyu msichana vilevile alikuwa si mtu wa hivihivi ila alikuwa mtaalamu katika nyanja kama yake. Mara ya kwanza alipohisi, ilikuwa jinsi alivyojirusha nyuma ya kochi pale nyumbani kwake baada ya yeye kuwapiga risasi wale watu wawili, na alivyochupa dirishani kumfuata Xavier. Kwanza alifikiri alikuwa na mafunzo ya kijeshi tu, lakini kutokana na jinsi ya majibizano yao aligundua alikuwa na utaalamu zaidi.

"Willy Gamba, Mtanzania," alijibu na wote wakaangaliana kama wanapimana saizi. "Ningependa nijue historia yako nzima, na usinifiche kitu, mpaka kufikia uhusiano wako na hawa wauaji na hasa huyu aliyekuhukumu kifo bwana Jean", Willy alimwambia Bibiane.

"Nimeshatoa kauli yangu kuwa nitakueleza kila kitu unachotaka niseme. Hivyo, usiwe na wasiwasi nitakueleza, ila itabidi uwe na subira maana ni hadithi ndefu", Bibiane alijibu.

Bibiane alimweleza Willy kwa kirefu maisha yake ya utoto, maisha ya shule, juu ya baba yake na mama yake na akaendelea, "Mwaka nilipoanza kazi baada ya kuhitimu digirii ya kwanza ya lugha katika Chuo Kikuu cha Kigali, wazazi wangu wote wawili walikufa kwa ajali. Nilikuwa nimeanza kazi Wizara ya Mambo ya Nje kama mkalimani.

"Inasemekana kuwa wazazi wangu hawakufa kwa ajali ya kawaida ila waliuawa na vikaragosi vya Watutsi ambao walifikiri kuwa baba yangu alikuwa ndugu yake na Rais. Hivyo waliwaua wazazi wangu ili kumkomoa Rais. Kitendo hicho kiliniuma sana nikawachukia sana Watutsi", Bibiane alieleza.

"Pole sana", Willy alisema kwa sauti ya huruma.

"Kwa kunisikitikia kutokana na yaliyowakuta wazazi wangu, serikali ikanihamishia ofisi ya Rais, huko ndiko nilipokutana na Jean Yves Francois, yeye ni Mfaransa anaishi Paris lakini alikuwa rafiki kipenzi na Rais. Tulionana naye nyumbani kwa Rais ambako alikaribishwa na tulianza urafiki siku hiyohiyo", Bibiane alieleza Willy huku akimwangalia kwa jicho la kuiba.

"Huyu Jean Yves Francois ndiye aliyekufundisha ujasusi?", Willy alimuuliza.

"Umejuaje?".

"Nimehisi".

"Jean ni mfanyabiashara na alikuwa akifanya biashara na kundi la marafiki wa Rais pamoja na familia ya Rais, wakati mimi nafahamiana naye serikali ilikuwa imeanza kuwa na matatizo kwani Watutsi waliokuwa humu ndani na nje, nchini kwenu na Uganda walikuwa wakipigana ili waiangushe serikali. Jean ndiye aliyekuwa akimsaidia Rais kwa kumjenga kijeshi, kiusalama na kiutawala. Huyu Jean ana utajiri usio kifani, kwani ndiye anayezifadhili serikali na wakuu wengi wa nchi za Afrika. Kwa vile mimi pia nilikuwa kwenye himaya yake alinipeleka kwenye mafunzo ya kiusalama sehemu mbalimbali duniani".

"Na ukahitimu vizuri", Willy alidakia.

"Vizuri sana".

"Ehee, endelea".

"Si ni wewe unanikatisha".

"Huu utajiri aliupataje?", Willy aliuliza.

"Sijui mwenyewe ameupataje, ila anashughulika na mambo ya silaha. Hapa alikuwa analeta silaha, halafu anachukua chai yote na kahawa inayolimwa katika nchi. Hili suala ni moja ya malalamiko mengi ya wananchi maana Jean ndiye aliyekuwa akipanga bei anayotaka, na hakukuwa na mtu wa kusema kitu, maana alikuwa akifanya biashara na Rais na kundi lake, lililokuwa likiitwa Akazu. Kusema kweli Jean na hilo kundi la Akazu ndio waliokuwa wanatawala na si baraza la mawaziri au Bunge", Bibiane aliendelea huku sasa Willy akimsikiliza kwa makini zaidi.

"Huoni kuwa hiyo haikuwa sawa?", Willy aliuliza.

"Mimi ningefanya nini, nilibaki kufanya kila nilichoagizwa kama ilivyokuwa kwa wengine wengi maana sasa hii ndio ilikuwa namna ya maisha. Ama uko na Akazu, vinginevyo hupati kitu cha aina yoyote, iwe mali, elimu au kazi ya aina yoyote Rwanda".

"Kwa hiyo rushwa ndio ilitawala utawala uliopita?", Willy aliuliza.

"Inategemea unavyotafasiri rushwa", Bibiane alijibu huku akiwa kama haelewi anasema nini.

"Rushwa ni pale vyombo vya serikali vinaposhindwa kufanya kazi zake, kwa sababu hiyo kushindwa kutoa haki kwa wananchi wake, na kuwafanya wananchi wengi wapoteze imani, utu, uhuru na maadili kwa serikali yao kwani wote sasa huishi kama wanyama ambapo mwenye nguvu na pesa ndiye anayepata anachohitaji", Bibiane alisema.

"Hivyo ndivyo, maana nchi inakosa maendeleo kwani mapato yote ya nchi badala ya kuendeleza watu wote huingia kwenye mifuko ya watu wachache. Na kama ulivyosema uhalali wa serikali kama chombo cha watu unakwisha, badala yale wale wanaofaidika ndio wanakuwa na nguvu zaidi ya serikali yenyewe", Willy alitafasiri rushwa.

"Kwa tafasiri hiyo nakubali kuwa rushwa ndiyo imetawala. Na sasa Watutsi na Wahutu walipoanza kudai demokrasia isingewezekana maana Jean na Akazu hawakutaka kusikia kitu kama hicho kwa vile kingeweza kuingila maslahi yao. Na ndio sababu Watutsi walipokazana na kusikia eti wako tayari hata kupigana na

Akazu, kwa kufadhiliwa na Jean, walianza kulifundisha jeshi la wahutu lililoitwa Intarahamwe ili liweze kuwadhibiti Watutsi wa ndani na nje ya Rwanda".

"Kwa hiyo huyu bwanako Jean ndiye alikuwa Rais hapa?".

"Si hapa tu, mimi najuwa nchi nyingi ambako amewakamata wakuu wa nchi na viongozi wa ngazi za juu serikalini na anawajaza mapesa kila wakati".

"Huoni kuwa yeye ndiye ananufaika zaidi, maana anajaza mapesa watu wachache lakini yeye anachukuwa mali za wananchi wengi", Willy alijaribu kumwelimisha Bibiane.

"Najuwa, maana hata huko kwenu Tanzania pia amewakamata wakubwa, ndio sababu nchi yenu imekuwa ikisita juu ya suala hili la Rwanda".

Willy alisitushwa na taarifa hii lakini hakutaka kujionyesha maana kweli msimamo wa serikali ya Tanzania ulikuwa unalegalega kabla na hata baada ya mauaji.

"Ina maana maamzi yoyote ilikuwa lazima Jean akubaliane nao?".

"Ndiyo, na mapesa yalitembea sana kuhusu swala hili na viongozi wengi wamenufaika. Unafikiri kama swala hili lingefanyiwa maamuzi mapema mauaji yangetokea!", Bibiane alimwambia Willy kwa njia ya kushangaza.

"Kwa hiyo huyu Jean ndiye aliamru mauaji haya?".

"Baada ya Rais kuonekana kwamba angekubali mkataba wa Arusha. Jean na Akazu walikasirika sana maana hawakutaka, kama nilivyosema mwanzo, kugawana madaraka na mtu mwingine. Hii ingegusa maslahi yao. Kwa hiyo, kwanza ndio waliamru Rais auawe na pili tayari walikuwa wamewatayarisha na kuwahamasisha Wahutu kuwamaliza Watutsi wote asibaki mtu ili wajihakikishie uwezo wa kutawala milele. Mpango ulikuwa kwamba hata kama jeshi la RPF la Watutsi lingeshinda jeshi lao lazima baada ya kuchukuwa nchi wangeshindwa kutawala maana wangemtawala nani huku Watutsi wote wakiwa wameshauawa, waliobaki ni Wahutu watupu ambao hawawaungi mkono. Hivyo, ingewachukuwa siku chache kuuangusha na kuutokomeza kabisa utawala wa RPF. Hii ingebaki nchi ya Wahutu chini ya utawala wa Jean na Akazu.

Bibiane alipofika hapa ndipo Willy alipoanza kuelewa kwa undani mambo yalivyokuwa. Kumbe mauaji yote haya yalitokana na watu wachache kutaka kulinda maslahi yao ya kunyonya mali ya wananchi, na kutumia hiyo mali kuweza kuwachochea wananchi kuuana!.

Kwa mara ya kwanza Willy aliona jinsi ambavyo nchi zote za Afrika zilivyo hatarini kutokana na rushwa. Kwa vile viongozi wa nchi hizi kuabudu rushwa, hivyo Willy akaamini kuwa tukio kama la Rwanda kumbe linaweza kutokea mahali pengine katika Afrika!.

"Baada ya RPF kushinda na mipango ya Jean kushindwa, wana mikakati gani sasa?", Willy alihoji.

"Kama nilivyosema hawajashindwa. Wewe ndiye umeingilia ndani ya mipango yao, kuna mpango kabambe wa kuisambaratisha serikali ya RPF kutokea jimbo la Kivu, Zaire. Akazu wamekuwa wakiliimarisha jeshi lao katika makambi ya wakimbizi kule Goma na Bukavu, Zaire, huku Jean akiwatumia rafiki zake kutoka Afrika Kusini hasa waliowahi kuwa katika idara ya ujasusi ya makaburu, alikokuwa akinunua silaha na kuzipitishia Angola ya UNITA, Zaire na Zambia kwa kutumia viongozi wa ngazi za juu za serikali za nchi hizo ambao wako kwenye orodha ya malipo kutoka kwa Jean. Kwa hiyo mambo bdo sana Willy, vita ndio sasa karibu vitaanza".

"yaani dunia inafikiri kuwa kambi zilizoko Zaire ni za wakimbizi kumbe ni kambi za jeshi".

"Ni kambi za jeshi na serikali ya Zaire inajua na ndio inayosaidia hata mafunzo. Hata katika kambi zilizoko kwenu Tanzania kuna wanajeshi wa jeshi la zamani na Intarahamwe, na kuna watu wazito katika serikali yenu ambao wanalipwa na huyu Jean ili kuwasaidia hawa watu, kwa hiyo hili si dogo. Kama ulivyosema pesa ni kitu kibaya sana, watu hawaoni tena madhara ya mauaji yaliyotokea bali wanaona pesa tu".

"Swala la rushwa ni swala linalohujumu haki za binadamu, yapaswa lichukuliwe hatua kimataifa katika uzito huo wa haki za binadamu", Willy alijibu kwa hasira.

Bibiane alikaa kimya bila kujibu kitu.

"Wewe ulikuwa uwasaidie vipi Jean na Akazu katika kutekeleza huu mpango wao wa kuivamia tena Rwanda", Willy aliuliza.

"Usije ukanipeleka kwenye mahakama ya mauaji ya Arusha maana mauaji yale sikuyajuwa pia sikushiriki, nilikuwa Nairobi nikitokea kwenye mkutano Arusha. Ila juu ya hili la sasa Jean amekuwa akinituma kupashana habari kati ya kambi za wakimbizi ambazo ni kambi za jeshi lao huko Zaire, yeye na Akazu. Vilevile kuna wanajeshi na viongozi wa RPF ambao tayari wamenunuliwa na wako upande wa

Akazu, mmoja wao ndiye anayetarajiwa kuchukua madaraka mara tu jeshi la Akazu litakapotwaa madaraka tena".

Willy hakuamini masikio yake kuwa tayari hata ndani ya RPF kuna wasaliti.

Mara moja Willy alielewa jinsi alivyotaka kuuawa na akagudua kuwa kweli kama anavyosema Bibiane kuna kiongozi wa juu na karibu sana katika serikali ya Tanzania amabye anamtumikia Jean na kundi la Akazu.

"Utasaidia kunipa majina ya watu wote unaowajuwa kuwa wanahusika, maana hiyo ndio njia pekee tunaweza kulikosha jina lako", Willy alimuasa Bibiane.

"Swala la Jean kunisaliti mimi, na kunihukumu kifo, bila kujali yote niliyomtendea kwa hali na mali ikiwa pamoja na kumpa mwili wangu auchezee atakavyo, na jinsi nilivyojitoa kumstarehesha. Willy mimi niko upande wako, kama uko tayari kupambana nao nihesabu na mimi. Jean akishaambiwa kuwa umenichukua ninavyomjua atataka apambane na wewe yeye mwenyewe, ikifika hapo niachie mimi. Majina na mipango yao yote ni juu yako na uongozi wa RPF mjuwe la kufanya kwani jeshi la Akazu, likisaidiwa na viongozi wa nchi kadhaa ambao ni marafiki na Jean watakuwa tayari kuingilia kati. Ni lazima liwahiwe mapema kabla halijajiimarisha sawasawa", Bibiane alieleza.

"Nafikiri swala la vita si letu, ni la serikali ya Rwanda na RPF, mimi nipe hayo majina na kutokea hapo ndipo nitajua kama kazi yangu imeisha au ndio kwanza inaanza", Willy alieleza taratibu.

Bila kuwa ameandika mahali popote, Bibiane alitoa kichwani jina hadi jina akianza na kundi la Akazu mpaka viongozi wa nchi mbalimbali wanaolipwa na Jean huku Willy akiyaandika chini kwa mshangao mkubwa, kwani watu waliokuwa wanatarajiwa wengi wao ni viongozi wanaoheshimika Afrika na kote duniani. Alishangaa zaidi Bibiane alipotaja jina la yule waliyekuwa wakimwita JKS wa Tanzania.

"JKS, hii imenishangaza sana, maana huyu ndiye anayetegemewa kugombea urais wa Tanzania katika uchaguzi mkuu unaokuja," Willy alimweleza Bibiane.

"Najua kabisa, na tayari Jean ameshamtengea mamilioni ya dola za Kimarekani zitakazo msaidia katika kampeni hiyo ya uchaguzi kuusaka urais. Nia ya Jean ni kuwa na marais vibaraka kote Afrika ili yeye na wenzake huko Ulaya, waweze kufanya vile wanavyotaka katika nchi hizi. Jean anaongoza kundi la wafanyabiashara wakubwa wanaomiliki makampuni makubwa ya kimataifa. Na

nia yao ni kuhakikisha kuwa Afrika inakuwa soko lao tu, na hata siku moja Afrika isisimame kiuchumi. Ingawaje nchi zao zinapigia kelele rushwa, lakini nchi hizohizo ndizo zinazoyasaidia makampuni makubwa kwa madogo kutoa rushwa kwa nchi zinazoendelea, maana makampuni hayo yakitoa hongo, hongo hii huchukuliwa kama gharama na kutolewa kwenye kodi ya mapato. Hii yote inaonyesha unafiki wa nchi za magharibi, na kila wakati Jean alikuwa akinieleza kuwa kelele zote hizi kuhusu rushwa, demokrasia na soko huria ni kelele za kinafiki tu, lakini huku nyuma katika vikao vya viongozi wa nchi za magharibi ni kuchochea rushwa. Wanajuwa kuwa rushwa ikiisha Afrika basi demokrasia na soko huria vitashamiri na hivyo uchumi wa nchi hizo utakua haraka sana, kitu ambacho hawataki kitokee. Jean anasema, rushwa ndiyo sera inayotumiwa kuendeleza umaskini katika nchi za Afrika ili nchi zilizo endelea ziendelee kuitawala Afrika kiuchumi. Kwa hiyo, iwapo JKS ataitawala Tanzania rushwa itazidi mara dufu, na kutokana na fedha alizotengewa na Jean lazima atashinda, kwani kila walipoweka mtu wao hajawahi kushindwa uchaguzi", Bibiane alieleza.

Sasa Willy alikuwa na picha kamili namna JKS alivyokuwa anahusika na swala zima la Rwanda. na sababu za Tanzania kutokuwa na msimamo dhabiti juu ya swala hili na kuweza kuyumbisha mikutano kule Arusha kiasi cha kutofikia maamzi kwa muda mrefu maana swala hili la Rwanda kwa muda mrefu lilikuwa chini ya Tanzania kwa muda mrefu na JKS alikuwa mmojawapo wa viongozi walioonyesha kuchoshwa na mauaji ya Rwanda. Na alifanya hivyo kwa shinikizo la Jean aliyekuwa akimlipa pesa nyingi na uchu wake wa kutaka madaraka kwa njia ya ruswa ili aweze kuyatumia kwa faida yake na kujinifaisha yeye na rafiki zake. Na ni hii rushwa iliyowanyima Wanyarwanda haki yao mpaka kufikia hatua ya kuuawa vibaya namna ile kweli ni aibu! Aibu sana kwa Afrika nzima.

"Vizazi vijavyo vitakapoyasoma na kuyaelewa matukio haya, hakika hawataamini, watajuwa sisi wote tulikuwa wendawazimu kabisa, kwani ni sisi wote ndio tulioachia hali hii ikafikia hapo ilipo, kwa kuwapa walarushwa madaraka kwa gharama ndogo ya kuuza kura zetu na wao kutumia madaraka tuliyowapa kwa malipo ya fedha kidogo, lazima wayatumie kutuangamiza", Willy alisema kwa uchungu huku akikuna kichwa chake.

Mara moja Willy alimkumbuka Malisa wa Arusha, aliyekuwa mshauri wa JKS katika masuala ya uhusiano wa Kimataifa kabla hajarudi Chuo Kikuu. Hivyo basi, alijuwa Malisa ndiye aliyemweleza JKS kuhusu msimamo na mipango ya PAM na kuteuliwa kwa Willy kufuatilia jambo hili. Willy aliamini kuwa JKS ndiye aliyetoa

taarifa za safari ya Rwanda kwa Jean na kundi lake na ndi sababu ndege aliyopanda ikapigwa kabla ya kutua uwanja wa ndege wa Kigali.

"Kwa hiyo JKS ndiye aliyotoa habari zangu zote kwa Jean?", Willy aliuliza kwa shauku.

"Ndio, na ndio sababu Col. Gatabazi aliamru ndege hiyo ipigwe kabla ya kutua uwanja wa ndege, lakini kwa bahati na umahiri wako ukawaponyoka", Bibiane alijibu huku akimwemwesa. Mara mlango wa mbele ukafunguliwa na Col. Gatabazi akaingia ndani.

Willy alipoangalia saa yake ilikuwa yapata saa tisa usiku. Wote walisimama, na Willy akawatambulisha.

"Pole Kanali, leo tumepata mgeni na anaitwa Bibiane, na Bibiane huyu ndiye mwenyeji wetu. Col. Rwivanga, kiongozi katika serikali mpya ya RPF".

"Nashukuru kumfahamu", Col. Rwivanga alijibu.

"Nami nimefurahi kukuona leo, nimekuwa nikisikia sifa zako nyingi kwa muda mrefu, toka kwa Col. Gatabazi kuwa wewe ni mpiganaji hodari, hongera", Bibiane alijibu kwa tabasamu akimwangalia Col. Rwivanga.

"Asante kwa sifa hizo zilizotoka katika kinywa cha msichana mrembo kama wewe", Col. Rwivanga alijibu akaendelea, "Ehe, imekuwaje Willy, hebu nipe habari kamili, maana kazi tumeiona kwa Bibiane, sasa halafu ikawaje hivi", Col. Rwivanga alionekana kuwa wasiwasi na Bibiane.

"Mimi naomba nikalale ili mzungumze vizuri, nionyeshe chumba cha kulala", Bibiane aliomba.

Willy na Col. Rwivanga aliangaliana na Willy ndiye alikuwa wa kwanza kujibu, "Kwa vile nyumba hii ina vyumba viwili tu vya kulala, basi kalale chumbani kwangu, maana tayari hata kuoga umeoga huko. Mimi nitalala hapa sebuleni kwenye kochi hamna taabu".

"Asante", Bibiane aliwaaga na kuelekea chumbani huku wote wakimwangalia. Kisha wakatazamana na kutabasamu.

"Ehe, hebu nipe mambo".

Willy alichukua muda mrefu kumweleza mambo yalivyotokea na mambo mengine yote aliyoelezwa na Bibiane. Col. Rwivanga akasimama na kumshika mkono Willy kwa hatua aliyofikia haraka na kwa umakini mkubwa.

Baada ya Col. Gatabazi kuvaa nguo vizuri, walichukua silaha mbalimbali na fedha zilizokuwa pale ndani. Wote walivaa mavazi ya kijeshi na kutumia gari ndogo aina ya MB 230E, ambalo awali Nkubana alikuwa amepewa na Col. Gatabazi kwa ajili ya Operesheni ya usiku. Gari hii ni mojawapo ya magari yaliyokuwa yameachwa na viongozi wa serikali iliopita, baada ya kukimbia mji wa Kigali, wakati RPF inaingia madarakani.

Nkubana alikaa kwenye usukukani kwa ajili ya kuendesha gari, Col. Gatabazi akakaa upande wa kulia, maana gari hili lilikuwa na usukani upande wa kushoto.

"Aha, kumbe gari limejaa mafuta kwenye tenki".

"Ndio, nilijaza kwa sababu kama hizihizi kama dharura itatokea", Col. Gatabazi alijibu.

"Tuchukue njia gani?", Nkubana aliuliza.

"Najua sasa hivi wataanza kututafuta. Hivyo, twende na barabara kubwa iendayo Ruhengeri. Kwa vile bado mawasiliano ni shida kati ya vikosi, tunaweza kupata bahati tukafika Gisenyi kabla habari zetu hazijaenea. Kwa vile vikosi vya RPF vinanifahamu na kuniheshimu njiani hatutaulizwa wala kupata tatizo lolote, watajua kuwa niko kazini. Kwa hiyo tutumie barabara kubwa mpaka Ruhengeri, halafu moja kwa moja mpaka Gisenyi, halafu tutavuka mpaka na kuingia Goma. Upande ule Jean ameshafanya mipango, hatutakuwa na shida. Nimemweleza amweleze Mkuu wetu wa Majeshi Col. Marcel Bazimaziki atukute mpakani"Col. Gatabazi alieleza.

"Sasa hivi ni saa sita na robo, itatuchukua masaa kama manne kwa gari hii, kwa hiyo saa kumi na moja alfajiri tutakuwa Goma?", Nkubana aliuliza huku akitia gea na kuondoa gari kwa kasi kuelekea Goma.

Baada ya Jean kumweleza JKS mambo yote yaliyokea Kigali, palepale JKS usingizi ulimtoka. Aliona na kuamini kuwa huo ndio ulikuwa mwisho wake. Ndoto zake za kuwa Rais wa Tanzania zilianza kuyeyuka mfano wa seluji. Hakujua afanye nini. Aliamini kuwa Willy Gamba akipata habari zake kuwa yuko kwenye mtandao wa kuisaliti Afrika haitamchukua zaidi ya siku mbili kabla mambo yake hayajabainika na kuanikwa hadharani.

JKS alimjua vizuri Willy Gamba alivyokuwa makini na hodari katika kufanya kazi zake. Alifikiri asubiri Willy arudi kwanza nchini ndio amkabiri yeye mwenyewe au aieleze serikali ya Tanzania kilichokuwa kinafanyika Rwanda. Aliona kashifa kubwa inakuja mbele yake. Ingawaje Rais wa sasa wa Tanzania alikuwa rafiki yake mkubwa, lakini ingekuwa vigumu sana kuizuia kashifa hii, maana vyombo vya habari vingemmaliza kabisa. Kisha, akakumbuka kuwa alikuwa na mapesa mengi ambayo Jean alimwekea kwenye akaunti zake katika mabenki ya huko Uswisi na Cyprus.

Baada ya kutafakari kwa muda mrefu huku jasho jembamba likimtoka. JKS akaamini kuwa mapesa hayo yangeweza kuzuia kashifa hii kwa kuwanunua wamiliki wote wa vyombo vya habari Tanzania kama Radio, magazeti na taasisi zingine kama polisi, usalama wa Taifa na idara zingine nyeti za serikali ambazo zingeonekana kumletea madhara kwenye safari yake ya kuelekea Ikulu.

"Watanzania karibu wote wana njaa, nitawanunua kwa mapesa tu. Hapo ndipo Willy atajuwa jeuri na nguvu ya pesa. Hakuna mtu atakayemsikiliza tena Willy Gamba, mimi nitaendelea na mambo yangu bila hofu. Uchu wangu wa kuwa Rais wa Tanzania utafanikiwa", JKS alijisemea mwenyewe huku akiwa amelala mfano wa mtu aliyeko katika usingizi mnono akiota ndoto.

Hivyo, baada ya kutafakari hili na lile kwa mapana na marefu, JKS aliamua kuwa atamfuata Rais ili amuombe ruhusa na kusafiri kwenda Ulaya kwa ajili ya kuangaliwa afya yake kwa madaktari wake walioko Uingereza, na angemwambia daktari mkuu wa Hospitali ya Muhimbili atoe ushauri wa haraka. Akiwa amejiwekea malengo kuwa akifika Ulaya akusanye mapesa yake halafu ndipo ajue kitu cha kumfanyia Willy Gamba aliyemwona mchawi wa safari yake ya kuelekea Ikulu ya Tanzania.

JKS aliamini kuwa akiwa na mapesa mkononi, ataweza kufanya chochote atakavyo. Akapiga moyo konde, akamkumbuka tena Willy Gamba moyo wake ukapata maumivu makali, akahisi mtu huyu ni mchawi. Hata hivyo akaapa kuwa hatarudi nyuma.

# SURA YA KUMI

GISENYI

Ilikuwa yapata saa kumi na mbili alfajiri wakati Willy Gamba na Bibiane walipokuwa wakiondoka nyumbani kwa Bibiane kuelekea Goma, nchini Zaire. Baada ya Bibiane kwenda kulala usiku na kumwacha Willy akimpa habari Col. Rwivanga kuhusu yote aliyoelezwa na Bibiane, usiku, uleule Willy na Col. Rwivanga waliamua kwenda haraka kumkamata Col. Gatabazi nyumbani kwake, baada ya kuchunguzi wa kina waligudua kuwa nyumba hiyo imefungwa na hakuna mtu. Mara moja Col. Rwivanga akahisi kuwa Col. Gatabazi alikuwa ameelekea kwenye majeshi yake huko Kibumba karibu na Goma kama ambavyo walikuwa wameelezwa na Bibiane. Hivyo, waliafikiana kuwa asubuhi na mapema Willy aondoke na Bibiane kwenda Goma, kuwasaka Col. Gatabazi, Nkubana na Jean.

Wakati huo Col. Rwivanga alikuwa akijiandaa kwenda kutoa taarifa za uhalifu huo kwa serikali ya RPF ili iandae jeshi la kushambulia sehemu ya Kibumba na kuliangamiza jeshi la Akazu pamoja na Jean kabla halijaishambulia Rwanda tena. Hivyo, Willy Gamba na Col. Rwivanga walirudi nyumbani na Willy akatafuta usingizi wa saa moja kwa ajili ya kujiweka sawa. Ilipofika saa kumi na moja alifajiri Willy alimuamsha Bibiane ili waanze safari.

Willy akilipokuwa akijipumzisha, Col. Rwivanga alitoka usiku huo kwenda kumwona mkuu wa shirika la Msalaba Mwekundu ambaye alikuwa rafiki yake na kumwomba gari. Col. Rwivanga alipewa gari ya Msalaba Mwekundu aina ya Toyota Land Cruser GX ambalo alipanga Willy na Bibiane walitumie kwenda mpakani kwenye kambi ya wakimbizi ya Kibumba. Vilevile Col. Rwivanga aliwatanguliza vijana wake watatu askari wa kikosi maalumu cha upelelezi kutoka jeshi la RPF ili wawahi kufika Gisenyi na kutoa taarifa za Col. Gatabazi kwa makamanda wa RPF walioko Gisenyi. Pia alituma taarifa ya siri kwa Meja Tom Kabarisa, kiongozi wa waasi wa Banyamulenge kikundi kilichokuwa kikipigana kupinga serikali ya Zaire, kilichokuwa na makao makuu yake sehemu za milimani, karibu na mji wa Goma. Hawa Banyamulenge walikuwa ni watu wa asili wa Kitutsi ambao walihamia miaka mingi eneo hili na Mashariki mwa Zaire kutokana na misukosuko ya muda mrefu ndani ya Rwanda.

Kwa muda mrefu watu hawa waliishi kama wananchi wa Zaire, lakini miaka ya hivi karibuni serikali ya Zaire ilianza kuwabagua kiasi cha kuwanyima haki hata ya

kupiga kura na kisha kuwataka wahame maeneo waliyokuwa wakiishi ndani ya Zaire ili warudi kwao Rwanda. Lakini walikataa katakata kutii amri hii ya serikali ya Zaire na kuanzisha kikundi chao cha wapiganaji ili kiweze kulinda maslahi yao. Kikundi hiki kilikuwa na mahusiano mazuri na maofisa wa jeshi la RPF. Wakati na baada ya mauaji ya Watutsi na Wahutu kukimbilia eneo hili la Ziwa Kivu, uhusiano wa Banyamulenge na uongozi wa RPF uliimarika zaidi kwa sababu za kiusalama kwa pande zote mbili.

"Mimi niko tayari kwa safari, lakini naomba tupite pale nyumbani kwangu ili nipate nguo za safari ya namna hii na nyenzo nyingine ambazo zinaweza kutusaidia katika safari yetu", Bibiane ambaye alikuwa ametokea chumbani na kujiegemeza kwenye ukuta alisema.

Willy na Col. Rwivanga waliokuwa wanapanga mikakati huku wameupa mgongo ule upande wa chumba waligeuka na kumwangalia. Alfajiri hii Bibiane alionekana mrembo hata zaidi ya jana yake.

Willy na Col. Rwivanga walitazamana tena na kutabasamu huku macho ya Col. Rwivanga yakimweleza Willy kuwa. "Haya kazi unayo".

"Mmenisikia?", Bibiane aliuliza tena.

"Sawa", Willy alijibu kisha kama amekumbuka kitu akahoji, "Lakini sijui kama pale kwako tutaweza kuruhusiwa kuingia".

"Tutaenda wote", Col. Rwivanga alijibu.

Kisha Col. Rwivanga alimmalizia Willy maelezo na mipango yote, wakaondoka kuelekea nyumbani kwa Bibiane.

Kwa vile kulikuwa bado hakujapambazuka, walipofika nyumbani kwa Bibiane ilibidi Col. Rwivanga atoke na kujitambulisha kwa askari wapatao wanne waliokuwa wamejitokeza baada ya kusikia mwungurumo wa gari. Kisha lango la mbele lilifunguliwa wakaingiza gari ndani. Baada ya maelezo mengine mafupi, Bibiane aliruhusiwa kuingia ndani.

"Karibuni", Bibiane aliwakaribisha Willy na Col. Rwivanga ndani.

Bibiane aliingia chumbani na kuwaacha Col. Rwivanga na Willy sebuleni. Nyumba ilikuwa bado kabisa haijakaguliwa. Hivyo, kila kitu kilikuwa kimebaki kama kilivyokuwa isipokuwa maiti za wale tu ndizo zilikuwa zimeondolewa.

"Willy njoo", Bibiane alimwita Willy chumbani kwake. Willy na Col. Rwivanga waliangalia na kutabasamu, baada ya sekunde kadhaa Col. Rwivanga alimuonyesha Willy ishara aende chumbani kama alivyoitwa.

Willy alipoingia chumbani alimkuta Bibiane anavaa suluali lakini sehemu ya juu yote ilikuwa bado iko wazi yaani hajavaa kitu hata sidiria.

"Hatuna muda wa kukaa hapa hivyo itabidi unisaidie vitu vingine ili tuweze kuondoka mapema", Bibiane alimwambia Willy ambaye alikuwa kama amepigwa na butwaa. Hakika msichana huyu alikuwa mzuri, umbo lake jinsi alivyoumbika hutaamini kama alizaliwa kutoka tumboni kwa mwanamke isipokuwa alishushwa kutoka juu. Hakukuwa na maelezo ya kutosha kueleza urembo wa msichana huyu bali ujitahidi kumtafuta ili uthibitishe mwenyewe kama Willy alivyojionea.

Usinitie majaribioni", Willy alisema huku akirudisha mlango.

"Aaa mshirika, mapigo yangu nikitaka utayaweza?. Kazi kwanza mambo mengine baadaye. Nimekuita kwa sababu hatuna muda wa kukaa hapa nataka kukuonyesha kitu", Bibiane alisogea kwenye ukuta akabonyeza sehemu na ukuta ule ukafunguka. Willy alishangazwa kuona kumbe ule haukuwa ukuta isipokuwa kabati la siri lililojificha likiwa na zana mbalimbali za kazi za kisasa kabisa.

"Pale mwisho kuna makasha mawili makubwa yameandikwa 'hatari', yatoe", Bibiane alimwambia Willy huku akichukua sidiria na kuendelea kuvaa.

Willy aliyatoa na kuyaweka chini.

"Fungua", alisema huku akiendelea kuvaa. Willy alipofungua alikuta ni mabomu aina ambayo hakuwahi kuyaona wala kuyatumia kabisa.

"Haya ni mabomu aina ya teknolojia ya kisasa kabisa, ambayo Jean aliniletea siku chache tu zilizopita, akanielekeza niyahifadhi mpaka nitakapopata maelekezo zaidi. Lakini yule mtu wa DOSE aliyeleta silaha hizi alinieleza jinsi zinavyotumika na kweli ni aina ya mabumu ya kisasa na hatari sana", Bibiane alieleza huku akivaa viatu na kutengeneza nywele zake. Alimweleza Willy jinsi mabomu hayo yanavyofanya kazi na kumalizia. "Hayo mabomu mawili yana uwezo wa kulipua nusu ya mji wa Kigali, na kwa kutumia saa hii ninayokupa unaweza kulipua mji wa Kigali huku umeketi mahali unakunywa chai.

"Ili mradi tu usiwe umetega na nyumba yako au ya majirani zako", Willy alitania na wote wakacheka.

Willy alikubaliana na Bibiane kuwa waende na makasha yote mawili, maana kutokana na maelezo ya Bibiane, Jean na Akazu walikuwa wameandaa jeshi kamili kwa ajili ya kuivamia Rwanda, wakiwa na silaha kali na za kisasa kutoka Ufaransa na Afrika Kusini, huku wakitumia kisingizio cha wakimbizi. Kisha Bibiane alitoa bastola nne, mbili zikiwa ndogondogo sana alizoziweka kwenye mkoba na mbili kubwa alizomkabidhi Willy, vilevile alichukua risasi nyingi sana.

"Nafikiri sasa tuko tayari", Bibiane alisema huku akimsaidia Willy kubeba kasha moja na mfuko wake wa nguo.

"Ehe, vipi huko ndani?", Col. Rwivanga aliuliza.

Kabla Willy hajajibu Bibiane alijibu."Salama kabisa".

Wote wakacheka, kisha kwa kifupi, Willy akamweleza Col. Rwivanga kuhusu kilichokuwa ndani ya yale makasha waliyotoka nayo ndani.

Baada ya hapo, Willy na Bibiane waliingia ndani ya gari na kumtakia Col. Rwivanga heri ya kuonana, kisha wakaanza safari ambayo hawakuwa na uhakika kama mambo yangeendaje huko.

"Mungu awe pamoja nanyi, naamini atawasaidia", Col. Rwivanga aliwaaga, askari waliokuwa wakilinda nyumba ile waliwafungulia lango wakatoka na kutokomea kuelekea Kibunda.

Ilipofika saa nne asubuhi JKS alikuwa tayari ameshapata kibali kutoka kwa Rais ili aweze kwenda Uingereza kwa matibabu. Daktari alikuwa ameiandikia serikali barua kufanya haraka na kila njia JKS aondoke siku ileile kwani alihisi kuendelea kusubiri kungeweza kumletea shinikizo la damu lenye nguvu kubwa ambalo huenda wao wasingeweza kumsaidia kabisa.

Ni barua hii ya Daktari iliyomfanya Rais akubali kutoa kibali harakaharaka na kuamru kuwa ifikapo jioni ile JKS awe ameondoka kwenda Uingereza kwa matibabu. Hadi saa saba mchana Wizara ya Afya ilikuwa imefanya mipango yote na ikawa wamempatia usafiri kuondoka na ndege ya shirika la ndege la Uingereza usiku ule.

JKS alikataa kusindikizwa na maofisa wa serikali kwa kisingizio kuwa atapokelewa na watoto wake walioko mjini London, Uingereza ambao alisema watamwangalia kwa karibu zaidi wakati wa matibabu yake. Bila watu kujua, alifanya mipango yake mwenyewe ili usiku uleule aweze kuunganisha ndege kwenda hadi Geneva, Uswisi, kitu ambacho alifanikiwa. "Hakika Willy Gamba

hataniweza, nikirudi na mapesa yote yale, hakika naamini ataiona dunia na ardhi ya Tanzania chungu", JKS alijisemea mwenyewe huku mapigo ya moyo yakimwenda mbio.

..........................................................................................................................

III

Wakati Willy na Bibiane wanaondoka Kigali kuelekea Goma, saa kumi na mbili asubuhi. Col. Gatabazi na Nkubana walikuwa wanapokelewa na Col. Marcel Bazimaziki na kikundi cha wanajeshi wa jeshi la Zaire kikiongozwa na Meja Massamba kwenye mpaka wa nchi hizo za Rwanda na Zaire.

"Pole sana na safari, ulipokaribia kufika Gisenye natumaini umepita ile njia yetu na nadhani hukupata shida", Col. Bazimaziki aliwasalimia kuwapa wageni wake mkono huku kila kikundi cha askari kikijiweka sawa kutoa heshima kwa gwaride rasmi lililoandaliwa kwa ajili ya Col. Gatabazi ambaye kama walivyokuwa wameelekezwa kuwa baada ya muda si mrefu ndiye atakuwa kiongozi wa Rwanda.

"Safari ilikuwa safi kabisa na hizi Benz ni gari imara sana ha hata kile kinjia tulichopita hatukupata taabu sana. Asante kwa kutuma mtu wa kutuongoza, maana tungeweza kubabaika kufika hapa", Col. Gatabazi alijibu.

"Jean tulizungumza kwenye simu yetu aliyoleta hivi karibuni ya Satellite. Sasa mawasiliano ni mazuri sana kati yake na sisi. Hata kabla ya kuja kukupokea tulizungumza nae, alikuwa akielekea uwanja wa ndege, nae tayari amepanda ndege na imeondoka Paris tangu saa kumi na mbili.

"Anatumia ndege yake ile ya Falcon, atakuwa hapa saa kumi na mbili jioni, maana atapitia Kinshasa kuonana na viongozi wa serikali kule, mkutano utafanyika uwanja wa ndege ili waweke msimamo, halafu watakuja na Jenerali Kasongo ili kuangalia hali pamoja na wewe mwenyewe ukiwepo ili mkiridhika na hali kazi ianze", Col. Bizimaziki alieleza na kisha Col. Gatabazi akaelekea kwenye gwaride ili apokee heshima zake kutoka kwa kikundi cha wanajeshi wa Zaire.

Baada ya kupokea heshima na kukagua gwaride. Col. Gatabazi na wenyeji wake waliamua kuondoka kuelekea Kibumba kwanza na kisha jioni ndio waelekee Goma kwenda kuonana na Jean na maofisa wengine wa juu.

"Acheni hilo gari hapa mpakani, hakuna matatizo askari wa jeshi la Zaire wapo wataliangalia maana kule kwenye makambi lazima kwenda na magari ya jeshi la

Zaire ndio idara na taasisi za Kimataifa zinazoshughurikia wakimbizi haziwezi kushituka", Col. Bizimaziki alieleza.

"Sawa, vipi minong'ono kwamba watu wetu wanajitayarisha kuishambulia tena Rwanda huku wakitumia kinga ya wakimbizi?", Col. Gatabazi aliuliza.

"Usijali kabisa kuhusu hilo, serikali ya Zaire itakanusha vikali huku sisi tumetia pamba masikioni. Na kama ujuavyo kiongozi wa baraza la Akazu, Anatoile Kabuga. Alitusihi tusisikilize propagada za vyombo hivi isipokuwa tujiimarishe kijeshi tayari kwa kuikomboa nchi yetu kutoka kwa wavamizi wa Kitutsi. Kwanza nilitaka kusahau, vilevile Bwana Kabuga anakuja pamoja na Jean ili maamuzi yaweze kufanyika, ameeleza kuwa mjumbe mwingine wa Akazu ambaye anaweza kufika ni John Ngeze ambaye sasa yuko Afrika Kusini, lakini ameambiwa apande ndege ya shirika la ndege la Afrika Kusini inayoingia mjini Kinshasa saa sita na kama akiwahi atawasubiri pale uwanjani na wao wakiwahi watamsubiri|.

"Lo, kumbe tutakuwa na mkutano mkubwa", Col. Gatabazi alinena.

"Wakati umefika kwa wewe Col. Gatabazi kuchukua nchi kutoka mikononi mwa wavamizi wa Kitutsi. Siri zote za adui yetu unazijua, nguvu ya RPF yote unaijua, ya kijeshi na kisiasa. Sasa nini kitazuia?, wao hawajui nguvu yetu wanafikiri tunacheza. Utaenda sasa hivi kujionea mwenyewe salaha za kisasa, magari, vifaru. Tuna silaha ambazo zina uwezo wa kupiga masafa marefu hadi kilomita mia mbili, na kuna mafunzo makali yanayoendelea kutoka kwa askari wale tuliowakodi kutoka Afrika Kusini na wana kazi kubwa na vijana wetu wana ari kubwa maana wanajua tusiposhika nchi tena maisha yao yako hatarini. Ni kweli kama ulivyosikia wakimbizi tumewazuia kurudi ili siku tutakapoamua kuanza kazi ndiyo siku ambayo wakimbizi wote wanaume tutaandamana nao. Wakirudi wakati huu uhalali wa kuivamia tena Rwanda hatutakuwa nao. Hii vurugu ya wakimbizi kwanza inaficha mambo yote tunayoyafanya, pili itatupa uhalali na nguvu za kuvamia. Rafiki zetu wote watasema. "mlitaka wafanye nini, yaani mamilioni ya watu yabaki kuwa wakimbizi nje ya nchi yao", Col. Bazimaziki alieleza, kisha wakaelekea kwenye kambi.

Walipofika huko kambini walitumia muda mrefu kuangalia aina mbalimbali za silaha za kisasa kabisa, mafunzo makali ya kijeshi, ari ya vijana wa Kihutu, hasa wale Intarahamwe waliotaka siku hiyohiyo kwenda kuvamia Inyenzi na kurejesha madaraka yao. Kutokana na aina ya silaha walizonazo na mafunzo waliyokuwa wakipata na moto waliokuwa nao wa kutaka kupigana na adui. Col. Gatabazi aliamini kabisa kuwa wakisaidiwa na Wahutu waliokuwa ndani ya Rwanda ushindi

ulikuwa wao asilimia mia. Col. Gatabazi alipandwa na mori akatamani kama vita vingeanza saa ile. Kisha, wakaondoka kuelekea Goma.

Ilikuwa saa kumi na moja na nusu jioni, Jeana na wenzake walipowasili kwenye uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Goma. Baada ya kuwasiliwa, walipokelewa na Col. Gatabazi aliyesindikizwa na askari wake. Jean aliwasili akiwa pamoja na kiongozi wa Akazu, Bwana Anatoile Kabuga, Bwana John Ngeze, ambaye ni Mjumbe wa Baraza la Akazu, Jenerali Kasongo, ambaye ni mshauri wa Rais wa Zaire, Meja Karongo, Mkuu wa kikosi cha jeshi linalomlinda Rais wa Zaire, Bwa, George Karikutis, ambaye ni dalali wa mamluki aliyefanya mipango yote ya kuwawezesha Jean na wenzake wa Akazu kupata askari wa kukodi.

Baada ya kuwasili uwanja wa ndege walipelekwa moja kwa moja hadi Ikulu, ambako Rais alitoa kibali Jean na wenzake wafikie kwenye jumba hilo. Ikulu hii ilikuwa ya kifahari sana. Ili uweze kuelewa kwa kifupi, vyoo, bafu na vyumba vya kulala alivyokuwa akitumia Rais vilijengwa kwa vito vya dhahabu tupu. Sasa naamini utakuwa umeelewa maana yake. Karibu na Ikulu hii kulikuwa na Jumba jingine kubwa ambalo Majemedari wa jeshi wa ngazi za juu walikuwa wakifikia. Ndani ya jumba hilo ambalo pia lilikuwa la kifahari sana, ndimo alipofikia Col. Gatabazi na wenzake. Kisha, wakaenda kukaa kwenye sebule ya kifahari ajabu. Wasichana warembo sana wapatao kumi hivi walijitokeza kwa ajili ya kutoa huduma, wakiwa wamevaa kaputula fupi, matiti nje, yaani asilimia tisini walikuwa uchi.

"Hivi ndivyo mzee anavyoishi hapa duniani Jean, hapa panaweza kuwa peponi ukitaka. Mzee ameyafanya maisha yake hapa duniani kuwa sehemu ya peponi. Hivyo, na wewe onja pepo kidogo ukiwa hapa", Jenerali Kasongo alimweleza Jean, ambaye wakati huo alikuwa akitikisa kichwa, maana pamoja na utajiri wake mkubwa usio kifani alikuwa hajawahi kukalia viti na meza za kahawa vilivyotengenezwa kwa dhahabu tupu, ukiacha sehemu za kukaa ambazo zilivishwa kwa ngozi ambazo hata yeye hakuwahi kuziona kabisa duniani.

Huku wale wasichana wakiendelea kuwahudumia, kila mmoja alikuwa amejichagulia mrembo wa kumhudumia, wakileta vinywaji vya kila aina vilivyokuwa ndani ya jumba hilo. Baada ya muda mazungumza yalianza.

"Ehe, hebu Nkubana tueleze ilikuwaje hata huyu Willy Gamba akachafua mipango yetu namna hii, maana inaniuma sana kufikia hatua ya Bibiane kuwa mikononi na mshenzi huyu. Hebu tueleze", Jean aliuliza kwa hasira.

Huku akitetemeka Nkubana alieleza jinsi mambo yalivyokuwa huku wote wakimsikiliza kwa makini sana, kisha akamalizia kwa kusema, "Tulichukua tahadhali ya kila aina, lakini nafikiri huyu Willy Gamba alikuwa na bahati kuliko sisi. Katika biashara kama hii yetu, wakati mwingine ni bahati tu inaweza kukusaidia", Nkubana alijitetea.

"Unafikiri huyu mtu ana mipango gani sasa?", Jenerali Kasongo aliuliza.

"Sijui, lakini naamini Bibiane anaweza kumleta huku. Hizi ni hisia zangu, maana Bibiane atakuwa na uchungu wa kutaka kulipiza kisasi na siri zetu zote anazijua. Hivyo, atataka amtumie Willy Gamba baada ya kuona umahiri wake, alipize kisasi", Nkubana alijibu.

"Mbona hiyo itakuwa raha, maana nitaua ndege wawili kwa jiwe moja, Col. Bazimaziki na Meja Massamba, moja ya kazi zenu ni kuweka kikosi imara chenye wapiganaji jasiri cha kuweza kuwakamata hawa watu wawili, nataka Nkubana akiongoze kikosi hicho, Nkubana, ukiweza kuwakamata usiwaue hao ni halali yangu. Nataka niwafanyie kitu ambacho wakiwa ahera wasinisahau milele", Jean aliamru.

"Sawa bosi", Nkubana alijibu hku Col. Bazimaziki na Meja Massamba wakiitikia kwa vichwa vyao.

"Ratiba ikoje?", Jean alimuuliza Col. Gatabazi.

"Nafikiri kwanza twendeni wote tukaangalie hali ya vikosi vyetu ilivyo, hasa hapa Kibumba, maana mtapata mwanga baada ya kuona jinsi tulivyojiandaa tayari kwa vita. Tumetuma habari kwa vikosi vyetu vingine vilivyoko karibu na Bukavu, navyo vijiweke tayari. Ile simu moja kati ya simu nne za Satellite ulizoleta tuliwapelekea na sasa tunawasiliana vizuri sana kati ya hapa na sehemu zingine zote ambako kuna vikosi vyetu, lakini kwa kuwa nguvu yetu kubwa iko hapa nafikiri twende mara moja Kibumba mkajionee wenyewe, kwani ni kilomita thelathini tu kutoka hapa Goma. Halafu tukirudi tutakula chakula hapa na baadaye kidogo tutaanza mkutano wetu. Mimi naamini kuwa mkishaona kama nilivyoona mimi mkutano wa leo utaruhusu tuanze uvamizi leoleo", Col. Gatabazi alimalizia.

Wote walikubaliana naye. Kabla hawajaondoka alichukua simu ya Satellite akapiga simu Tanzania. Nia yake ilikuwa kumpata JKS ili ampatie habari za wakati ule kuhusu nyendo za Willy Gamba kama alikuwa amezipata kutoka kwenye vyanzo vyake vya habari. Kwa mshangao alipata habari kutoka kwa mke wa JKS kuwa alikuwa ameumwa ghafla na kuondoka jioni ile Tanzania kuelekea

Uingereza kwa ajili ya matibabu. Na mama huyo alieleza kuwa mumewe aliondoka kwa ndege ya shirika la ndege la Uingereza. Mara moja Jean alihisi kuna tatizo. huku akitingisha kichwa huku wengine wakimwangalia kwa kustaajabu, Jean aliwaambia wenzake wote wamsubiri nje.

Walipotoka nje Jean alipiga simu zingine tatu zilizomchukua dakika kama kumi hivi na baada ya kuzipiga aliagua kicheko kwa sauti mpaka askari aliyekuwa karibu akashangaa akifikiri kuwa huyu mzungu alianza kupata uchizi kwa kucheka peke yake hivi. Jean alipoangalia saa yake ilikuwa yapata saa moja na nusu jioni, hivyo aliungana na wenzake wakaondoka kuelekea Kibumba.

Mjini Kigali baada ya Willy Gamba na Bibiane kuondoka wakielekea mpakani mwa Zaire, Col. Rwivanga alikwenda moja kwa moja kuonana na Mkuu wa Majeshi mnamo saa mbili, akamweleza yote aliyoyapata kutoka kwa Willy kutokana na maelezo ya msichana mrembo Bibiane.

"Kamanda, hali ni mbaya, tusipofanya haraka tunaweza kuvamiwa," Col. Rwivanga alimuasa Mkuu wa Majeshi.

"Sasa tunafanyaje?" Mkuu wa Majeshi, Jenerali Bunyenyezi, alimuuliza Col. Rwivanga.

"Nafikiri mpigie simu Rais aitishe kikao cha Baraza la Mawaziri na makamanda wa vikosi vyote haraka ili tuliangalie swala hili kwa undani zaidi, maana tukifanya mchezo hawa Interahamwe wanaweza kutuvamia, wamepania sana kufanya hivyo, wanaweza kutuvamia, silaha wanazo tena kali na za kisasa, mafunzo wanapewa na askari wa kukodi, maana wapiganaji wao hawana njia nyingine ila kupigana tu ili warudi. Wamekataza hata wakimbizi halali wanawake kwa watoto wasirudi Rwanda kwa hiari yao ili wawatumie katika uvamizi huu. Kamanda, hii ni hatari na ni hatari sana lazima uamuzi upatikane leo", Col. Rwivanga alishauri.

Jenerali Bunyenyezi alimpigia simu Mkuu wa nchi, nae aliposikia uzito wa swala lenyewe aliamua kuitisha mkutano saa sita na nusu ili watu wote wanaohusika waweze kuwepo maana swala hili lilikuwa na maana ya kuanzisha vita dhidi ya Interahamwe waliokuwa mpakani mwa Zaire na Rwanda.

Baada ya Col. Rwivanga kuona umuhimu wa mkutano huu aliwasiliana na Col. Tom Kabalisa, Kiongozi wa Banyamulenge, Baada tu ya kuwasiliana na Mkuu wa Majeshi kwa njia ya simu ya Satellite ambayo serikali ya Rwanda ilikuwa imewapa kurahisisha mawasiliano na kumweleza ajitayarishe kuja Kigali kwenye mkutano muhimu na kwamba angemtumia helikopta ya kumchukua awe Gisenyi

saa nne na watu wasiozidi watatu wa ngazi za juu katika uongozi wao wanaoweza kufanya maamuzi. Kwa miezi mingi Col. Tom Kabalisa alikuwa anasubiri huo muda hivyo alifurahi sana kupata habari hizi.

Baada ya kupata habari hizi walikubaliana kuitisha mkutano wa dharura mnamo saa sita na nusu mchana. Rais alipiga simu tena kwa Jenerali Bunyenyezi na kumwambia afike ofisini kwake haraka akiwa pamoja na kiongozi wa upinzani wa Zaire, aliyekuwa akiunganisha vyama vyote vya upinzani na ambaye askari wake waliwahi kupigana vita bega kwa bega na majeshi ya RPF, wakati wa mapambano dhidi ya Serikali ya Rwanda ili wapate uzoefu kutoka kwao. Bwana Mpinda ambaye nae alikuwa mjini Kigali kwa mazungumzo.

Haikuchukua zaidi ya saa moja wote walifika ofisini kwa Rais.

"Bwana Mpinda karibu sana. Nimekuita pamoja na Kamanda hapa ili tuzungumze kama uliyonieleza juzi, maana naona hali imegeuka, sasa inakupendelea wewe", Rais alicheka kidogo na wote wakatabasamu.

"Asante sana Mheshimiwa Rais, nashukuru Mungu, kama umegeuza uamuzi wako na uko tayari kutuunga mkono sisi", Mpinda alijibu.

"Kama nilivyosema naona hali inakupendelea, kuna mambo ambayo yametokea na kuashiria tulifikirie kwa makini ombi lako. Askari wako wote bado wako kwenye ardhi ya Rwanda?", Rais aliuliza.

"Hapana Mheshimiwa, wengine wengi bado wapo lakini baadhi yao wamevuka wapo mpakani, wakisaidia kufundisha jeshi la Wabanyamulenge", Mpinda alimwambia Rais.

"Kamanda Bunyenyezi, nataka basi ufanye mpango na kiongozi wa Banyamulenge nae awepo kwenye mkutano wa saa sita na nusu", Rais aliagiza.

"Na hilo tumelifikiria, na Col. Rwivanga ameshatuma Helikopita kwenda kumchukua", Kamanda Bunyenyezi alijibu.

"Oh, vizuri sana. Sasa bwana Mpinda unakaribishwa kwenye kikao saa sita na nusu, na naomba ujieleze vizuri, na kama ukiweza kuwashawishi mawaziri na makamanda wangu, basi utakuwa umefanikiwa. Hii ni nafasi nzuri sana kwako kwani na sisi sasa tunalazimika kutumia mpango wako ili nasi tukidhi lengo letu. Hivyo, kazi kwako kukishawishi kikao kama kweli una mipango thabiti ya kuweza kufanya kazi", Rais alimalizia.

"Mheshimiwa Rais, naenda kukaa na makamanda wangu, na kwa vile viongozi wa Banyamulenge nao watakuwepo na wako upande wenu na wetu, basi naamini nitaweza kukiridhisha kikao kuwa tuko tayari kufanya kweli", Mpinda alijibu.

"Haya Bwana Mpinda kwa heri. Kamanda Bunyenyezi, wewe ngoja kidogo".

Walimtoa nje Bwana Mpinda na wakamrudisha kwenye nyumba ya wageni ya Serikali alikokuwa amefikia na makamanda wake. Rais na makamanda wake walipobaki nyuma, walitafakari swala zima kwa undani. Wakaangalia jinsi ambavyo wangeweza kufaidika kwa kuwatumia wapinzani wa Serikali ya Zaire ili waweze kutimiza lengo lao kuwaondoa Intarahamwe na Wahutu wote wenye siasa kali pale mpakani kwao ili wasije wakaivamia Rwanda, huku bila kulaumiwa na Jumuia ya Kimataifa kuwa wamevamia nchi nyingine na kuwaua wakimbizi.

"Nafikiri hii ndio nafasi yetu ya pekee kumaliza tatizo hili. Kwa hiyo, inabidi tulieleze kwenye mkutano vizuri", Kamanda Bunyenyezi alieleza.

"Je, hawa wapinzani na waasi wa Banyamulenge wakishindwa, itakuwaje? si siri itavuja?", Rais aliuliza.

"Hilo litakuwa jambo jingine, sisi tutakuwa tumetimiza lengo letu na tutakuwa tumewaondoa na kuwamaliza kabisa hawa Intarahamwe karibu na mipaka yetu. Tutakuwa tumewatokomeza mstuni huko Zaire. Shida na wasiwasi kwetu vitakuwa vimemalizika kabisa. Kazi yako itabaki kujenga nchi na si kupigana tena", Kamanda Bunyenyezi alijibu.

"Kweli, sasa tumepata kisingizio; Mungu yuko pamoja nasi, maana chochote tungefanya serikali ya Zaire na Jumuia ya Kimataifa visingetupa nafasi. Basi nenda kajitayarishe, Mkutano utakuwa mgumu sana, maana najua mawaziri wengi itakuwa vigumu kukubali", Rais alijibu.

"Asante Mheshimiwa Rais, nafikiri watatuelewa kwa sababu hii ni kwa faida ya Taifa la Wanyarwanda ambalo limeteseka sana, lazima wananchi wapate muda wa kupumua na si vita kila siku", Kamanda Bunyenyezi alijibu na kueondoka kwenda kujitayarisha.

Mpinda alipofika kwenye nyumba aliyokuwa amefikia, aliteremka haraka kutoka ndani ya gari na kuingia ndani ya nyumba hii, akawagongea wenzake waliokuwa ndani ya vyumba, akiwataka kwenye mkutano pale sebuleni.

Alifikiria na kuona kwamba Mwenyezi Mungu alikuwa ameyajibu maombi yake. Hii ilikuwa nafasi aliyoisubiri kwa muda mrefu sana. Na yeye vilevile kama

wenzake wa Rwanda aliona nafasi hii ilikuwa inazifaa pande zote tatu zilizokuwa zinahusika kwenye harakati hizi za mapambano. Kati ya wote waliokuwa katika sakata hilo, alijiona ndiye mwenye fursa ya kufaidika zaidi ingawaje Serikali ya Rwanda ndio ingefaidika zaidi kwa kuhakikisha kuwa haina mgogoro au wasiwasi wa kushambuliwa na Wahutu wenye msimamo mkali chini ya wanamgambo wa Intarahamwe na Banyamulenge ambao nao wangefaidika kwa kutobuguziwa tena na Serikali ya Zaire, na wangeendelea na maisha yao raha mstarehe.

Makamanda hawa walipokusanyika pale sebuleni Mpinda aliwaeleza kila kitu jinsi mambo yalivyokuwa wamejipa.

"Tunachotakiwa kufanya ni kukishawishi na kukikahakikishia kikao cha Serikali ya Rwanda na viongozi wa Banyamulenge kuwa tutakapoanzisha vita hii ni kweli uwezo wa kushinda tunao?. Pande zote zimekubali kuwa sababu tunayo na nia tunayo, swala hapa ni uwezo, wakiridhika kuwa uwezo upo, basi mambo tayari", Mpanda aliwaeleza wenzake.

"Mkuu, wala tusipoteze muda wa kufikiri, sisi tumekuwa hapa tukijaribu kuwashawishi siku zote, tusingekuwa na uhakika na uwezo wetu kivita tusingekuja kuomba watuunge mkono, uwezo tunao. Nenda kawaeleze kwa uhakika kama watatoa msaada kidogo tu, basi nchi yetu tumeikomboa kutoka kwenye mikono ya utawala wa Kidikteta na kifashisti", Col. Mkengeri, mmoja wa makamanda wa wapinzani wa serikali ya Zaire alijibu. Wenzake wote walitingisha vichwa kukubali maneno yake.

"Azimio, tunakwenda wote kushiriki kikao hicho", Mpinda alijibu.

Willy Gamba na Bibiane walisafiri salama kutoka Kigali mpaka Gisenyi bila kukutana na kituko cha aina yoyote Barabarani. Lile gari lenye alama ya Msalaba Mwekundu liliwafanya wasafiri bila kupata usumbufu na habari zilikuwa zimetumwa mapema na wale askari watatu waliotumwa kutangulia mbeke ili lile gari la maofisa wa Msalaba Mwekundu lisibugudhiwe.

Walipofika Ruhengeri walipumzika huku kila mmoja wao akili yake ikifanya kazi jinsi ya kukabiliana na jambo lililokuwa mbele yao.

Baada ya mapumziko ya saa moja hivi, Willy na Bibiane waliendelea na safari yao na kuwasili Gisenyi saa nane za mchana. Moja kwa moja walikwenda Hoteli Meridien-Izuba, ambako walipanga kuonana na maofisa ambao Col. Rwivanga alikuwa amewapasha habari waonane nao na wawape habari kamili kuhusu uhalifu

unaofanywa huko Gisenyi na Kibumba, ili kama walikuwa wamebahatisha kupata habari zozote wazipate hapo.

Meridien Hoteli Izuza ilikuwa moja ya hoteli nzuri sana ingawa vita vya wenyewe kwa wenyewe nchini Rwanda vilikuwa vimeiathiri kidogo hoteli hii, lakini ilibaki kuwa safi pamoja na misukosuko ilivyokuwa sehemu hii. Ikiwa kwenye ufukwe wa Ziwa Kivu, mpakani mwa Zaire, huku kwa mbali ukiangalia milima ya volkano ya Virunga, kweli Meridien-Izuda palikuwa mahali pazuri sana pa kupumzika.

"Umepapenda hapa?", Bibiane alimuuliza Willy Gamba.

"Mbona wewe unapenda kusoma mawazo yangu?", Willy aliuliza.

"Ubaya uko wapi Willy, fikiri kama tungekuwa tunakuja hapa kwa ajili ya mapumziko na si hii kazi ya hatari, huoni kuwa ingekuwa raha sana, mimi naona tungestarehe sana", Bibiane alijibu.

Huku akitabasamu Bibiane alitoa mkoba wake ndani ya gari huku Willy akijibu. "Sawa mama umeshinda".

Baada ya gari la Msalaba Mwekundu lililokuwa likitumiwa na Willy na Bibiane kusimama, askari wanne walielekea kwenye gari hilo, walipofika karibu mmoja wao moja kwa moja akauliza. "Natumaini nyinyi ni Bwana na Bibi George Mambo wa Msalaba Mwekundu kutoka Makao Makuu Nairobi?".

"Bila shaka", Willy alijibu bila kusita huku Bibiane amejikausha utafikiri kweli alikuwa mke wake, baada ya kutambulishwa vile, Willy alitambua kuwa huyu mwanamke alikuwa kweli amefundishwa vizuri mambo ya upelelezi maana Willy hakumweleza mapema jinsi ambavyo wale askari wangetambulishwa hapa. Kazi yote hii ilikuwa imefanywa na Col. Rwivanga.

"Kamanda Kasubuga anawasubiri pale ofisini kwake", yule askari alimweleza Willy Gamba.

"Twende", Willy alimweleza Bibiane.

"Hapana, wewe nenda tu, mimi nitakusubiri hapa", Bibiane alijibu na Willy akaelewa maana na sababu ya Bibiane kubaki pale, akafurahi moyoni kuwa kweli alikuwa amepata mshirika katika kazi.

Kamanda Kasubuga alikuwa mtu mwenye rika la Willy na baada ya Willy kuingia ofisini kwake aliinuka kwenye kiti alichokuwa amekaa akisoma faili moja hivi, huku akitabasamu akamlaki Willy.

"Karibu sana", Kamanda Kasubuga alimkaribisha Willy.

"Asante", Willy alijibu huku wakishikana mikono na Kamanda Kasubuga alimwonyesha ishara yule askari aliyemleta Willy awape faragha kidogo, yaani aondoke awaache peke yao.

Baada ya yule askari kutoka Kasubuga alisema, Lo! Bwana Willy Gamba ni wewe huyu, Sifa zako na wewe mwenyewe hufanani. Col. Rwivanga amenieleza yote na mimi nikamweleza kuwa nimekusikia sana nilipokuwa Tanzania. Mimi nimefanya kazi na Jeshi la Tanzania na vyeo vyangu vyote mpaka hiki cha umeja nimevipata nikiwa Tanzania".

"Alaa! nashukuru sana", Willy alijibu na kuketi kwenye kiti.

"Oke, bila kupoteza wakati, habari kutoka kwa kijana wetu ambaye juzi tu tumeweza kumnunua kutoka katika jeshi la Zaire linalolinda mpaka na sisi zinaeleza kuwa leo hii yapata saa kumi na mbili na nusu asubuhi waliwasili watu wawili upande ule wa Zaire na kupokelewa kwa heshima zote za kijeshi na kisha wakaondoka kuelekea kwenye makambi ya wakimbizi kule Kibumba. Baada ya maelezo ya jinsi wale watu walivyofanana tulielewa mara moja kuwa mmoja wao alikuwa Col. Gatabazi. Hivyo, Col. Gatabazi kafika na yuko Kibumba", Meja Kasubuga alieleza.

"Hizo ni bahari njema sana, sasa ngoja na sisi tupumzike halafu giza likiingia na sisi tutakwenda Kibumba", Willy alijibu huku Meja Kasubuga akimwemwesa.

"Sawa mzee, ila tumewawekea chumba kimoja maana ni mimi tu ninajua wewe ni nani, hawa askari wengine wote wanajua kweli wewe ni afisa wa Msalaba Mwekundu na kwamba kwa vile unajua utakaa Rwanda kwa muda mrefu umekuja na mke wako", Meja Kasubuga alimweleza Willy.

"Hapa taabu", Willy alijibu kwa mkato.

"Safari ya Kibumba, tumeagizwa na Mkuu wetu kuwa tufuatane, maana siku zote nimetaka kuvuka na kikosi changu cha hapa lakini nimekuwa nakatazwa, lakini leo nimeamriwa tufuatane wote, sijui safari itakuwa saa ngapi?".

"Sijui, tutaangalia wakati huo si na wewe unakaa hapa hapa hotelini?".

"Ndiyo mzee, niko chumba namba 110, nyie mtakuwa nambari 220 kwenye vyumba vinavyofuata".

"Sawa", Willy alijibu na kuaga. Aliporudi pale kwenye gari alimkuta Bibiane anapiga soga na wale askari.

"Tupelekeni chumba namba 220", Willy aliwaeleza wale askari.

Askari mmoja aliingia ndani ya gari baada ya kushusha mizigo yao, akawapeleka kwenye banda lililokuwa na chumba nambari 220. Yule askari alipoondoka Bibiane akasema, "Kwa vile kuna kitanda kimoja tu wewe utalala ng'ambo ile na mimi ng'ambo hii".

"Lo, kumbe ulikuwa unajidai bure, sasa umeanza masharti".

"Si tulisema kazi kwanza?", Bibiane alijibu huku akifunga mlango kwa funguo na kuanza kuvua nguo huku akiendelea kusema, "mimi nitaoga kwanza.

"Sawa mama", Willy alijibu huku mawazo yake yakiwa tayari yameanza kupanga mipango ya usiku ule. "Tukimaliza wote kuoga tuitishe chakula kidogo halafu tupumzike angalau kwa masaa mawili ndipo safari ya Kibumba ianze", Willy alimwambia Bibiane.

"Amri itatoka kwako baba, mimi kazi yangu ni kutii amri tu", Bibiane alijibu huku sasa akiwa amevua nguo zote pale kitandani.

Meja Kasubuga baada ya kuachana na Willy Gamba, alimtafuta Col. Rwivanga akitumia simu ya Satellite na kumweleza kuwa Willy alikuwa amefika salama na kwamba Willy na Bibiane walipanga kuelekea Kibumba usiku uleule.

Col. Rwivanga alifurahi kupata simu ya Meja Kasubuga lakini akakataa Willy na mwenzake wasiondoke, "Hapana mwambie Willy na mwenzake wasiondoke mpaka kesho, kuna mabadiliko ya mipango ya kazi huku, waambie wapumzike tu hakuna tatizo. Meja Tom Kabalisa atakuja kumuona Willy kesho asubuhi, nami nitafika huko kesho asubuhi. Hivyo, mambo yote tutapanga kesho baada ya sisi kufika huko".

"Nimekusoma, nitamweleza kuhusu taarifa hii afande".

Kasubuga aliona si vyema kumweleza Willy wakati ule, bali amwache mpaka baadaye ili apumzike kidogo, lakini muda si mrefu alikuja askari mmoja na kusema kuwa wale wageni wa Msalaba Mwekundu walikuwa wakihitaji chakula. Meja Kasubuka akaona huo ulikuwa muda mwafaka vilevile kuwaeleza kuhusu maagizo kutoka kwa Col. Rwivanga. Hivyo, akaamua yeye mwenyewe ndiye awapelekee chakula kitakapokuwa tayari ili awaeleza kama alivyoagizwa.

"Chakula kilipokuwa tayari Meja Kasubuga aliwapelekea yeye mwenyewe na kuwaeleza kuhusu maagizo aliyopewa kutoka kwa Col. Rwivanga.

"Sawa tumekusikia", Willy alijibu bila kuonyesha kama alikuwa na maana gani au alipanga kufanya nini usiku ule.

# SURA YA KUMI NA MOJA

KASHESHE

Ilikuwa yapata saa tatu na nusu usiku wakati Willy na Bibiane walipokuwa wakijiandaa kuelekea Kibumba, walivalia sare za Msalaba Mwekundu huku wakiwa wamebeba silaha mbalimbali ndani ya mifuko ya nguo na mikoba waliyokuwa wamebeba yenye alama ya Msalaba Mwekundu. Walibeba silaha zote za hatari yakiwemo mabomu ya kisasa yaliyotolewa na Bibiane.

Willy alikuwa amevaa saa iliyoendana na yale mabomu akiwa tayari kuyatumia wakati wowote wakati wa safari yao. Walipofika kwenye gari na kufungua mlango ili waweke mikoba yao tayari kwa safari, mara moja Meja Kasubuga alijitokeza akitoka gizani akiwa ameshika bastola yake mkononi akawauliza. "Mnakwenda wapi Willy, hamkusikia maagizo ya Col. Rwivanga kwamba msifanye chochote wala msiende Kibumba mpaka mtakapowasiliana nae kesho, haraka ya nini Willy?, mimi sintaruhusu muondoke".

"Sisi hatuendi Kibumba Meja, tuko hapa hapa sehemu ya mpakani ili kufanya utafiti wa hali ya usalama katika maeneo hayo", Willy alijibu.

"Siamini, huenda mnataka kuvunja amri ili mvuke mpaka, hilo sintaruhusu na nimeamru kikosi changu hapa kiwazuie msiondoke hapa hotelini mpaka hiyo asubuhi, mimi nina amri zangu. Willy naomba tafadhali rudini ndani tusije tukavunjiana heshima kwa kuwakamata na kuwaweka chini ya ulinzi mpaka Col. Rwivanga atakapofika hapa", Meja Kasubuga alionya.

Willy na Bibiane waliangaliana, maana wao walikuwa wameamua kuendelea na kazi yao usiku ule. Hawakuona sababu ya kusubiri kesho yake kwani wao walikuwa na mipango yao tofauti ambayo haikuwahusu akina Col. Rwivanga. Nia yao ilikuwa kuwasaka Col. Gatabazi, Nkubana na Jean. Wakati lengo la Col. Rwivanga na jeshi la RPF ilikuwa kuliangamiza jeshi zima la Akazu.

"Naona kama hutuamini Meja, hakuna tatizo tutarudi ndani tukalale", Willy alijibu kwa sauti ya unyonge sana.

"Samahani bwana Willy, mimi natii amri niliyopewa na wakubwa wangu wala msijaribu kunitoroka maana hiyo haiwe.....", kabla hajamaliza kusema sentensi hiyo, milio ya bunduki aina ya AK 47 ilisikika upande mwingine wa hoteli.

"Tumeingiliwa", Meja Kasubuka alisema huku akikimbia kuelekea sehemu ulipotokea mlipuko huku akitoa amri kwa wanajeshi wake kujitokeza tayari kwa mapambano dhidi ya wavamizi.

II

Wakati Jean na wenzake wanatoka Goma kuelekea Kibumba saa moja na nusu ya jioni ile, Nkubana akiwa na kikosi cha askari shupavu wenye mafunzo thabiti wapatao thelathini hivi, walielekea mpakani kutafuta habari za Willy na Bibiane, kwani walikuwa na hisia kuwa lazima wangewatafuta kwa vile Bibiane aliijua mipango yao yote.

Nia ya Nkubana ilikuwa kupeleleza ili amuwahi Willy kabla Willy hajawawahi, maana hii ndio sheria ya mchezo wao huu. Nkubana na kikosi chake walipofika mpakani upande wa Zaire ilikuwa yapata saa mbili na nusu na ndipo walipoelezwa na vikaragosi wao waliokuwa wamejipenyeza ndani ya vikosi vya jeshi la RPF pale Gisenyi kuwa mtu mgeni aliyekuwa amefikia pale Meridien Hotel alikuwa ofisa wa Msalaba Mwekundu na mkewe.

"Huyo mkewe alifananaje?", Nkubana aliuliza kwa shauku.

"Afande, ni mwanamke mrembo ajabu, utanisamehe afande lakini kusema kweli nilipomwangalia yule mwanamke mara moja nilizini afande, ni mzuri sanasana chotara yule?", askari alijibu huku mawazo yake yakiwa yamerudi kwa yule mwanamke na kuanza kumfikiria huku mwili wake unasisimka.

Hata Nkubana alipokuwa anakieleza kile kikosi chake. "Watu wetu wamefika yafaa tupange mipango madhubuti tuwashambulie na kuwakamata hai kama bosi alivyoagiza", yule askari hakusikia kabisa mpaka Nkubana alipomshitua tena. Wewe vipi, una tatizo la kifafa", maana alianza kutetemeka.

"Hapana afande, hapana, nafikiri ukame umetuathiri sana mawazo".

"Ukame gani, wewe ni mwehu nini?, hetu tufahamishe huyu jamaa na mkewe wanakaa upande upi pale hotelini?".

Yule askari alieleza kila kitu kwa ufasaha jinsi hotelini ilivyo na akawaelekeza namna ya kuingia mpaka kwenye chumba walichofikia akina Willy bila kushukiwa na askari wa RPF waliokuwa wakilinda eneo hilo.

"Inapofika saa tatu mara nyingi askari wengi wanaondoka kuelekea mpakani na wale wanaobaki mara nyingi wanakuwa upande wa Ziwa. Hivyo itabidi tuvuke

mpaka kabla ya saa tatu na nitawaonyesha sehemu salama ya kupita, halafu tutajibanza sehemu mpaka hapo askari wengi watakapotawanyika kuelekea kwenye malindo ya usiku halafu ndipo tutavamia kwani askari watakaobaki tutaweza kuwamudu", yule kikaragosi alielekeza.

"Maelezo yako ni safi sana, unafikiri kutakuwa na askari kama wangapi, yaani watakaokuwa wamebaki kwa ajili ya kulinda hoteli?", Nkubana alihoji.

"Hawawezi kuzidi hamsini pamoja na mimi, maana leo ni zamu yangu kulinda hoteli", yule askari alieleza.

"Ulikuwa ulinde upande gani?", Nkubana aliuliza kwa shauku.

"Unande ule niliokueleza kuwa tutapita halafu tujibanze maana askari anayelinda sehemu hiyo ni mtu wetu, anajuwa kila kitu", yule askari alibainisha.

Nkubana alimwangalia kwa makini yule askari na akaridhika kuwa alisema ukweli na akamwamini.

"Kwanza nenda na askari wangu mmoja mkavinjari, halafu mrudi. Kama kila kitu kiko tayari na mambo shwari ndipo tutaanza kazi", Nkubana aliwatuma ili kuwa na uhakika wa mambo na kuthibitisha maneno ya yule askari alivyoeleza. Baada ya wale askari wawili kuondoka. Nkubana alibaki akiwaweka sawa askari wake tayari kwa kuishambulia hoteli ya Meridien-Izuda ili waweze kuwakamata Willy na Bibiane.

Wale askari waliporudi na kumweleza Nkubana kuwa mambo yalikuwa shwari na vilevile kupata habari kuwa yule mtu wa Msalaba Mwekundu na mke wake walikuwa wamelala baada ya safari ndefu habari hizi zilimfurahisha sana Nkubana, akafikiri kuwa angeweza kumteka Willy na Bibiane wakiwa wamelala na huenda wakiwa wanafanya mapenzi. Alisikia hasira inampanda na palepale akakiamru kikosi chake. "Haya sasa tunakwenda kazini".

Willy aliangaliana na Bibiane. "Unasemaje tuwasaidie hawa ama vipi?", Bibiane aliuliza.

"Hapana tuendelee na mipango yetu. Hii imekuwa bahati nzuri kwetu, naamini Meja Kasubuga ana uwezo wa kuukabiri uvamizi huu, na nahisi walengwa wa uvamizi huu ni sisi tunatafutwa, huenda kikosi cha Col. Gatabazi kimesikia ama kuhisi kuwa tuko hapa. Wakati wao wanatusaka hii itatupa nafasi nzuri, kwanza kumtoroka Meja Kasubuga na pili kuendelea na mipango yetu. Panda gari twende

zetu Kibumba tukawasake hawa majahiri", Willy alieleza huku wakipanda gari na kuondoka kwa kasi kuelekea Kibumba.

IV

Wakati kikosi cha Nkubana kikisonga mbele kuelekea hoteli Meridien-Izuda kilishitukiwa na askari mmoja wa doria ambaye baada ya kusikia nyayo za watu zisizo za kawaida akapanda juu ya mti na kuchungulia chini ya kjinjia kilichotelemka kutoka mlimani kuelekea hotelini. Akisaidiwa na mbalamwezi askari hjuyu aliweza kukiona kikundi cha askari kadhaa kikielekea hotelini hapo, baada ya kuthibitisha kuwa walikuwa askari wa adui na jinsi walivyokuwa wakisonga mbele kwa tahadhari kubwa huku silaha zao zikiwa zimewekwa tayari kwa mashambulizi.

Huyu askari wa doria alitelemka kwenye mti haraka haraka na kimya ili asiwagutue wale wavamizi waliokuwa hatua kumi tu karibu na ule mti na kwa kutumia uzoefu wa sehemu ile alikimbia kwa kutumia njia za mkato na kwenda kutoa taarifa kwa kikosi kilichokuwa kwenye maandalizi ya kuondoka kuelekea mpakani kisiondoke kwani kulikuwa na uvamizi.

"Kuna kikosi cha adui kinaweza kutushambulia sasa hivi, kimetumia kichochoro namba tatu na kitafika hapa sasa hivi, askari huyo alimweleza Mkuu wa kikosi hicho Sajenti Ibrahim.

"Oke, wewe kimbia kwa Afande Kasubuga umweleze wakati sisi tunaelekea huko kuwasimamisha mpaka tupate msaada", Sajenti Ibrahim aliamru na palepale akawaamru askari wake waweke silaha zao tayari na kusonga mbele kuelekea kichochoro namba tatu. Njia zote zilizokuwa zinaelekea kwenye hoteli hii zilipewa namba ili iwe rahisi kuzitambua kwani zilikuwa nyingi. Yule askari wa doria alikimbia mpaka ofisini kwa Meja Kasubuga lakini hakumkuta, kwani ndio wakati Meja Kasubuga alikuwa amewasimamisha Willy na Bibiane wasiondoke, na kabla hajajuwa ampate wapi na yeye alisikia milio ya bunduki akajuwa tayari mapambano yameanza.

Sajenti Ibrahim na kikosi chake walifanikiwa kuwaona wale askari wavamizi wakisonga mbele kuelekea hotelini na kwa vile hakujuwa walikuwa na nguvu kiasi gani aliamru askari wake waanze kushambulia hata bila kulenga shabaha kwa uhakika ili kuwatia kiwewe. Na kweli hii ilimshitua Nkubana kwani hakutegemea kukutana na upinzani haraka kiasi hicho kutokana na maelezo ya yule askari muasi.

"Luteni Nyamboma", Nkubana alimwita msaidizi wake, "Wewe endelea kukabiliana na hawa adui zetu ili mimi na askari watano tuweze kupata mwanya wa kwenda kumkamata Willy. Fanya mashambulizi makubwa ili askari wote wafikiri kuwa wanashambuliwa na kikosi kikubwa ili wote waje upande huu na sisi tupate urahisi pale Willy alipo".

"Sawa, nimekusoma Kamanda", Nyamboma alijibu.

Nkubana aliwachagua askari watano wazuri pamoja na yule kikaragosi wao. "Wewe tupeleke chumba cha yule mtu, tumia uzoefu wako wa hapa".

"Sawa afande, yule askari alijibu huku akitetemeka maana alistaajabu namna walivyokuwa wamebainika na kuonekana kwa adui mapema namna ile.

Mapigano makali yalianza na, kama Nkubana alivyotaka, askari wengi wa kambi ile walielekea upande wa mapigano kuongeza nguvu wakiongozwa na kiongozi wao Meja Kasubuga. Nkubana na askari wake hawakupata kikwazo mpaka walipofika kwenye chumba alichopangiwa Willy.

Baada ya Nkubana kushuhudia umahiri wa Willy Kigali, hakutaka kufanya makosa tena. Aliwapanga askari wake vizuri na kwa hadhari kubwa, walipofika kwenye chumba cha Willy na kwa amri moja wakaupiga mlango kwa nguvu zao zote na askari wawili wakaingia na mlango ndani ya kile chumba. Chumbani hawakumkuta mtu isipokuwa mikoba miwili iliyokuwa na nguo, Nkubana akautambua mkoba mmoja kuwa ulikuwa wa Bibiane, maana alipata kuuona pale sebuleni kwa Bibiane mjini Kigali.

"Watakuwa wapi hawa?", Nkubana alihoji, kisha akaendelea. "Wanaweza kuwa wamejiunga na askari wa hapa wanaopigana na kikosi chetu au wamevuka mpaka".

Yule askari kikaragosi alikuwa ametoka nje na akarudi na kusema. "Gari lao halipo, nafikiri wamekimbia mapigano".

Nkubana aliposikia hivyo woga ulimwingia kwani alijua mtu huyu amevuka mpaka. "Itatubini na sisi tuvuke mpaka sasa hivi. Wao wameondoka na gari sisi itabidi twende kwa miguu sasa", Nkubana aliamru huku ule upande wa mapigano makali yalikuwa yakiendelea.

"Itabidi turudi kuongeza nguvu", askari mmoja alishauri.

"Hapana, Luteni Nyambona ana ujuzi wa kutosha, akiona amezidiwa atarudi nyuma na kukimbilia mpakani. Huu ni wakati mzuri kwetu kuondoka kuwafuata hawa washenzi", Nkubana alijibu huku wakiondoka kuelekea mpakani.

V

Usiku ule Willy na Bibiane walipokuwa wakielekea kwenye mpaka wa Rwanda na Zaire, mbalamwezi iling'aa sana na kuyaonyesha mandhari safi ya milima ya Volkano ya Virunga.

Milima hii ilijulikana toka zama za kale, ambapo hata Wagiliki wa zamani waliizungumzia sana milima hii wakiita milima ya mwezi. "Sasa wewe mwenyewe unaweza kuona kwanini waliita hivyo", Willy alimsimulia Bibiane.

"Inaonekana wewe umesoma sana historia", Bibiane alieleza.

"Unajuwa kitu chochote hakiwezi kuwa kitu bila historia. Ili uijue dunia hii lazima ujue historia. Hata binadamu hawezi kuwa binadamu kama hana historia. Ndio maana mimi nikikwambia naitwa Willy, lazima utaniuliza Willy nani, nitakujibu Willy Gamba. Halafu utataka kujuwa baba yangu anatoka wapi halafu nitakwambia. Hii yote ni kutaka kujua historia yangu ili uweze kujua namna utakavyoniweka. Hata nchi. Nchi isiyokuwa na historia si nchi. Haiwezi kuwa na maendeleo. Sijui kama umenielewa vizuri mpaka hapo?", Willy alijibu na kuhoji.

"Nimekuelewa vizuri sana Willy. Kwa muda huu mfupi nitakaokuwa na wewe hakika nitajifunza mambo mengi", Bibiane alimwambia Willy.

"Sasa walikuwa wanakaribia sana mpakani, na Bibiane akasema.

"Tukivuka mpaka tu, lazima tutakutana na kikosi cha jeshi la Zaire, Unasemaje?".

"Unazijuwa njia nyingine tunazoweza kukwepa mambo ya mpakani?", Willy aliuliza.

"Ndiyo Willy, na ndio sababu nimesema hivyo, hapo mbele utakata kulia nitakuonyesha njia ya siri wanayotumia wapelelezi wa Akazu, lakini tuwe na tahadhari kubwa. Willy akakata kulia baada ya mwendo wa dakika kadhaa mara njia iliisha. Kukawa na njia ya majani tu. "Endelea tu. Ukikata tena kushoto. Tutakuwa tayari tuko Zaire. ni kilomita kama moja tu kutoka hapa", Bibiane alimwambia Willy, baada ya kutembea mwendo wa kilomita moja na baada ya kupita sehemu ya miti mingi walitokea mahali pa wazi na upande wa kushoto wakaona taa zinawaka.

"Pale ndio mpakani upande wa Zaire na ile ni kambi ya jeshi la Zaire", Bibiane alieleza.

"Tunaweza kupata magari ya jeshi pale?", Willy alimuuliza Bibiabe.

"Lazima. Unataka tukaibe gari moja la jeshi?", Bibiane alihoji.

"Unasoma sana mawazo yangu. Tusiibe, tukachukue tu?", Willy alijibu na kuendelea. "Ili tusije tukatia shirika la Msalaba Mwekundu dosari, yafaa tusiwe na gari lao kwenye uwanja wa mapambano. Hapa tutapata mahali pazuri pa kulificha halafu tukachukue gari la jeshi la Zaire. Itakuwa vilevile vigumu kusimamishwa na askari hovyohovyo".

"Je kuhusu nguo itakuwaje?", Bibiane alihoji tena kwa shauku.

"Kuhusu nguo tutawavua askari walioko mpakani". Willy alisema huku Bibiane akicheka sana.

"Wewe una mambo. Mbona naanza kusikia raha, usiku huu naona itakuwa kasheshe tupu", Bibiane alinena.

Walitafuta sehemu iliyokuwa na msitu wakalificha gari la Msalaba Mwekundu na kuitoa mizigo yao. Gari lilifichika vizuri sana kiasi kwamba ingekuwa vigumu mtu kuligundua mara moja.

"Tutalipitia kabla jua halijachomoza", Willy alinena.

"Kama tukiwa hai", Bibiane alijibu.

"Ili uweze kubaki hai fikiri kuwa utakuwa hai. Na ukiwa hai ukifikiri utakufa. Utakufa tu", Willy alifafanua.

"Sawa bosi. Tutarudi hapa kwenye gari letu tukiwa hai", Bibiane alisema.

"Mawazo safi kabisa", Willy aliongeza. Wakiwa wamebeba silaha zao na kila kitu walichohitaji kwa mapambano usiku ule walianza kuinyemelea ile kambi ya jeshi mpakani Zaire. Walipofika pale kituoni waliyaona magari matatu ya jeshi aina ya Landrover ya wazi nyuma yakiwa yameegeshwa. Walipoangalia vizuri waliwaona askari watatu. Kila mmoja akiwa ameegemea kwenye gari lake.

"Hao watakuwa madereva wa hayo magari", Bibiane alibobota kwa sauti ya chini.

"Hata mimi nafikiri hivyo, nahisi yalikuwa yamewachukua wale askari walioshambulia kule Meridiane hoteli, maana inaonekana hawa askari wanaosubiri watu", Willy alijibu.

Kwa vile yale magari yalikuwa karibu na ua wa michongoma na pale mahali. Willy alifikiri namna ya kuwashambulia bila ya kuwagutusha watu wengine pale kikosini. Mara akawaona askari wote wanakuja kuzungumza na yule askari aliyekuwa kwenye gari la mwisho karibu kabisa na ua.

"Bibiane kazi kwako, hapohapo wewe mshambulie yule wa kushoto. Mimi nitamalizana na wale wawili. Wa kati na kulia", Willy aliagiza huku hawa askari wakiwa sasa wameegemea kwenye magari yao huku wameipa visogo sehemu ile waliyokuwa wamejibanza akina Willy.

"Wale tutumie bastola zenye kizibo tusipoteze muda", Bibiane alishauri.

"Hapata, tunahitaji kila risasi tuliyonayo isipotee bure, pale ambapo tunaweza kulinda risasi nashauri tutumie njia nyingine, au unaogopa hutaweza kumkaba sawasawa?", Willy alimuuliza Bibiane.

"La, hasha! naweza sana Willy na wewe mwenyewe utanishuhudia leo; haya twende", Bibiane aliamru.

Huku wakitambaa chini kama nyoka, waliwanyemelea wale askari. walipofika usawa wa gari la kwanza Willy alisema. "Sasa", wote wawaili walirukia na bila kuwapa nafasi hata ya kushituka, Willy aliwapiga wawili karate kwenye vichwa akitumia mikono yake miwili na kupasua vichwa vyao palepale. Bibiane alimrukia yule wa kushoto na kumbana shingo na kisha kuikata kwa mikono yake. Hawa askari waliuawa kama kondoo. Hawakutoa upinzani wa aina yoyote, huenda kwa vile hawakutegemea kushambuliwa kama lile mahali pale. Kisha walizivuta maiti zao mpaka nyuma ya ua, wakawavua zile sare za jeshi na kuzivaa haraka haraka. Bibiane alichekelea sana maana zilikuwa kubwa. Hata hivyo akazifungafunga zikamwenea hivyohivyo.

"Utaweza kukimbia ama kupigana na adui ukiwa na magwanda haya?", Willy alimuuliza Bibiane huku akicheka.

"Tena ndio mazuri zaidi hasa kwa judo na karate", Bibiane alijibu.

Willy na Bibiane walibeba mizigo yao na kisha wakachungulia ndani ya magari na kukuta la gari la katikati likiwa na funguo. Waliweka mizigo yao ndani na kuliwasha na kisha kuondoka. Walipoangalia saa ilikuwa yapata saa nne na nusu

usiku. Waliondoka bila mtu yeyote pale kuhisi kitu. "Moja kwa moja Kibumba", Bibiane alisema.

Ilikuwa saa nne na nusu usiku, wakati Jean na kundi lake walipoondoka Kibumba kuelekea Goma.

"Hakika nimeridhika na ari ya wanajeshi wetu na uwezo mkubwa wa vikosi vyetu, pia nimefurahishwa sana na aina ya silaha tulizonazo, hii inaonyesha ni jinsi gani tumedhamilia kufanya kweli", Jean alisema kwa kujiamini.

"Nilikwambia toka mwanzo kuwa ukifika na kuona lazima utaamua tuingie vitani, kwani hakuna sababu wala haja ya kusubiri, vita vianze moja kwa moja, tuchukue madaraka", Col. Gatabazi alitamba huku Jean akitingisha kichwa kukubaliana nae.

"Twendeni Goma tukafanye maamuzi. Sijui kwa upande wa wenzangu, lakini mimi nafikiri tuanze mashambulizi alfajiri na mapema ila kwanza tukamate vikosi vya hapa Gisenyi kabla ya jua kuchomoza, maana adui hajui nguvu zetu, sisi nguvu yake tunaijua", Jean alishauri, wote kwa pamoja wakakubaliana.

"Mimi niko tayari wakati wowote, hata sasa vijana wangu wako tayari, uamuzi wenu tu ndio unasubiliwa", Col. Gatabazi alijibu.

"Haya twendeni Goma tukafanye uamuzi mara moja", Jean alijibu wakaondoka haraka kuelekea Goma.

# SURA YA KUMI NA MBILI

Ilipofika saa tano kamili za usiku, Willy Gamba na Bibiane walikuwa tayari wamewasili Kibumba. Bibiane alizijua vizuri njia za vichochoro za sehemu hii. Hivyo, walifika bila tatizo lolote. Bibiane alimuonyesha Willy sehemu yalipo maghala makubwa ya silaha ambayo baada ya Willy kuyaona, alitaka waanzishe mapambano dhidi ya watu wakiwa kwenye maghala hayo kwani aliamini hapo ndipo nguvu kubwa ya Akazu ilikuwa imewekwa.

"Sehemu hii inalindwa sana", Bibiane alimwambia Willy baada ya kutoka kwenye msitu na kuona kambi kubwa ya kijeshi ambayo ilimshangaza hata Willy.

"Walijenga lini kambi kubwa ya jeshi kama hii?", Willy aliuliza kwa mshangao.

"Hapa kulikuwa na kambi ya jeshi la Zaire, na Akazu walipewa kambi hii baada ya matukio makubwa ya Rwanda, na mara moja wakaleta vifaa vyao vya kivita na kuifanya kuwa kambi ya jeshi ya kisasa kabisa. Ina kila kitu kama unavyoona, taa, maji, mawasiliano, yaani kuna kila kitu cha kisasa nakwambia. Hata maafisa wa mashirika ya kimataifa yanayoshughulikia wakimbizi wanapotokea hapa kwa bahati mbaya wanaamini ni kambi ya jeshi la Zaire, maana kambi za wakimbizi ziko kilomita moja tu kutoka hapa upande ule wa kilima, hata wakiuliza basi huambiwa kuwa hii ni kambi ya jeshi la Zaire, na raia hawaruhusiwi kabisa kusogea karibu na kambi hii", Bibiane alimwambia Willy, ambaye wakati huo alikuwa ameshikwa na mshangao.

"Maghala ya silaha ni yapi?", Willy alihoji huku akichungulia kuangalia vizuri kambi hii akitumia kiona mbali. Bibiane alitumia nafasi hiyo kumwelekeza kila kitu. Kwa vile kambi ilikuwa ikiwaka taa utafikiri mchana waliweza kuona kila kitu vizuri kabisa.

"Kambi hii yote imezungukwa na seng'enge yenye umeme wenye nguvu kubwa unaoweza kumuua hata tembo haraka kama inzi, yaani ukigusa tu unakaushwa kwa umeme kama nyama", Bibiane alieleza.

Willy aliamua kwanza walifiche gari la jeshi walilokuwa wakitumia kwenye msitu ule, wakachukua mizigo yao ya kazi na kasha wakatafuta njia ya siri kwa ajili ya kuingia pale kambini.

"Hii kambi inaweza kuwa na askari kama wangapi kwa kukisia kwako?", Willy alimuuliza Bibiane.

"Eeeh… wanafika elfu tano na zaidi, wenye mafunzo ya juu sana, wale askari wa kikosi cha Rais wako hapa pia na askari wenye ujuzi mkubwa. Kuna makomandoo waliofuzu vizuri kama mia tano, halafu kuna askari wa kawaida wenye mafunzo mazuri vilevile zaidi ya elfu nne na mia tano. Hivyo, kuna askari kama elfu kumi hapa, na ndilo tegemeo kubwa la Akazu kurudi madarakani. Lakini kusema kweli wanaweza kushika tena madaraka, ukichukulia ari, uwezo na vifaa vya kijeshi walivyo navyo", Bibiane alimweleza Willy.

KKwa kweli kambi hii ilikuwa kubwa sana kiasi cha kumtia hofu Willy Gamba, kwani hakutegemea kabisa kukutana na kambi kubwa ya adui yenye idadi kubwa ya askari kama hii.

"Hebu nipe muda nifikiri kabla ya kujitumbukia huko", Willy alimwambia Bibiane.

"Hatuna muda Willy, hatuna muda kabisa kabisa, lazima ufahamu kuwa tunatafutwa na adui, na wakihisi tuko huku hakika tumekwisha", Bibiane alilalamika wakati Willy akimwangalia tu bila kusema kitu.

Baada ya Willy kutafakari kwa dakika kadhaa alilazimika kumwambia Bibiane. "Nikisema nahitaji muda wa kufikiri nina maana dakika tano tu, lakini niwe peke yangu, naamini sasa umenielewa?", Willy alimwambia Bibiane huku akielekea kwenye kichaka kilichokuwa hatua chache kutoka walipokuwa wamesimama.

"Kumbe unaamini uchawi, wewe unakwenda kuloga, mimi nifanyeje sasa?", Bibiane alimkebehi Willy.

"Jifanyie lolote kwa imani yako", Willy alijibu huku akipotelea kwenye kichaka. Inasemekana katika hali kama hii ya hatari Willy husali sana akimuomba Mungu. Baada ya dakika kadhaa Willy alirudi alimkuta Bibiane akiwa amebeba silaha za kiasi chake akiwa tayari kwa kusonga mbele kwa ajili ya mapambano dhidi ya jeshi la Akazu.

"Ehe, sema sasa tunasonga mbele ama tunarudi nyuma kumsubiri Col. Rwivanga?", Bibiane aliuliza.

"Tunaendelea", Willy alijibu kwa mkato huku akitoa vifaa vyake vya kazi kwenye mkoba wake.

Willy alibeba silaha na vifaa vilivyokuwa vimebaki, na kwa hadhari kabisa wakaanza kuelekea kwenye ile seng'enge yenye umeme.

"Mara nyingi ulinzi si mkali sana upande wa ua kwa kuwa wanaamini hakuna kitu kinachoweza kuzipenya hizi seng'enge bila kufa kwa umeme, maana kila siku wanyama wanakutwa wamejikaanga wenyewe. Vilevile, kitu chochote kinachokaribia mita moja ishara inaonekana kwenye chumba maalum kinachodhibiti usalama wa kambi hii kama kuna kitu kinasogelea seng'enge mara moja hatua za haraka za usalama wa kambi zinachukuliwa.

"Yote haya yamefanywa lini?", Willy alitaka kujua.

"Sababu ya pesa Willy, pesa, askari wa kukodishwa kutoka Afrika Kusini ndio wameleta vifaa na teknolojia hii iliyopo hapa kambini. Tukifanikiwa utajionea mwenyewe", Bibiane alidokeza.

Walipokuwa mita kumi kutoka usawa wa seng'enge walisimama na Willy alitoa kifaa maalum kwenye mkoba wake. "Tutapita chini ya seng'enge, baada ya kuchimba handaki".

"Itatakiwa liwe mita mbili kwenda chini, vinginevyo tutakaushwa kama mikaa", Bibiane alisema huku akionyesha wasiwasi.

"Hili bomu", Willy alisema akiwa ameshika bomu dogo lenye ukubwa wa yai la kuku. "Lina uwezo wa kuchimba handaki la urefu wa mita kumi na upana wa mita tatu, na kina cha mita tatu unasemaje?".

"Sikupingi, kwa teknolojia ya sasa hata mimi nimeona maajabu mengi katika vifaa vya vita, teknolojia imeendelea sana. Haya chimba tuone".

Willy alishika kisu na kuanza kuchimba shimo la mita moja kwenda chini, kisha akawasha lile bomu na kulitumbukiza pale shimoni na kulifukia.

"Litalipuka baada ya nusu dakika turudi nyuma haraka tulale chini".

"Halitasikika baada ya kulipuka?".

"Hapana, bomu hili limetengenezwa mahususi kwa ajili ya matumizi kama haya, ili kuziba mlio ndio sababu tunalizika chini ya ardhi", Willy alimwambia Bibiane na kumtoa hofu.

Baada ya nusu dakika bomu lile lililipuka na kutoma sauti kidogo, hii yote ilitokana na kazi ya Willy na kukatokea handaki zuri kwa ajili ya wao kupita bila kikwazo.

"Bwana, hakika kazi yako nimeipenda, sasa tuingie ndani tukafanye kazi iliyotuleta, kikwazo hiki ndicho kilikuwa kinanipa wasiwasi mkubwa", Bibiane alisema wakati wakiingia ndani ya handaki ili wapite kwa ajili ya kuwakabiri wanajeshi zaidi ya elfu kumi ndani ya kambi yao.

Nkubana na wale askari watatu walifika mpakani yapata saa tano na robo usiku. Walishangaa kukuta moja ya magari yao halipo na wale madereva wa magari hayo pia hawaonekani. Kwanza walifikiri huenda baada ya wao kuchelewa wale askari waliona waondoke, lakini askari mmoja aliona damu mahali gari moja lilikuwa limeegeshwa.

"Hebu angalieni vizuri huenda Willy Gamba kafika hapa na kufanya uharibifu tena", Nkubana alieleza huku mikono yake ikiwa imeshika nyonga.

Wakati Nkubana na askari wake wakitafakari, ndipo mmoja wa wale askari alipoona maiti za wale madareva wa magari zikiwa zimetupwa nyuma ya ua palepale kituoni.

"Shenzi kabisa huyu ni WIlly Gamba alikuwa hapa, na kachukua hata gari pamoja na sare zetu. Mtu huyu ni mshenzi sana, ole wake nikimuona sintangoja kumpeleka kwa Jean, nitamuua mwenyewe keshanisumbua sana. Twende haraka Kibumba, lazima atakuwa ameelekea huko", Nkubana aliwaamru askari wake.

Walitafuta funguo za magari haya na kwa bahati nzuri. gari moja lilikuwa na funguo zilizoachwa ndani. Hivyo wakaliwasha gari hilo na kwa kasi kubwa wakaondoka kuelekea Kibumba, wakiamini kuwa watamkuta Willy huko.

..........................................................................................................

IX

Mapigano makali kati ya kikosi cha Luteni Nyamboma na jeshi la Meja Kasubuga yaliendelea kwa kila upande kutumia mbinu kuukabiri upande mwingine. Kwa muda wa saa moja na nusu, Luteni Nyamboma hakurudi nyuma, lakini alikuwa amewapoteza askari wake wapatao kumi na watano, lakini nao pia walikuwa wamefanikiwa kuwaua askari zaidi ya arobaini wa jeshi la Meja Kasubuga. Luteni Nyamboma alipoona anaelemewa na risasi zinamwishia aliwaamru askari wake

waliobaki kurudi nyuma ili wakimbilie mpakani ambako waliamini kuwa wangepata msaada zaidi.

Walirudi nyuma kwa hadhari na walipoona sasa wanaweza kukimbia ili kuwatoroka wanajeshi wa jeshi la Meja Kasubuga walifanya hivyo. Meja Kasubuga alimru jeshi lake liwafukuze na kuwakamata. yeye mwenyewe alirudi ofisini kwake ili aweze kupeleka habari Makao Makuu Kigali kueleza mambo yaliyokuwa yametokea. Col. Rwivanga ndiye aliyepokea simu na alipoangalia saa yake ilikuwa saa tano usiku.

"Afande, tumevamiwa hapa na jeshi la Intarahamwe na Wahutu wenye msimamo mkali, tumepoteza askari kama arobaini hivi, lakini tumefanikiwa kumrudisha adui nyuma, amekimbilia mpakani mwa zaire", Meja Kasubuga alimweleza Col. Rwivanga na kisha kueleza kwa kirefu mapigano yalivyokuwa.

"Hivyo, inaonekana hao ni askari wenye ujuzi mkubwa?", Col. Rwivanga aliuliza.

"Sana afande, mpaka mimi nimeshangaa, nafikiri fununu tulizonazo kuwa kuna kambi kubwa ya mafunzo yenye wakufunzi wenye utaalamu wa hali ya juu kuhusu mambo ya kijeshi ni kweli kabisa".

"Willy yuko wapi?".

"Katika prukushani hii Willy na mwenzake wamechomoka, naamini wamekwishavuka mpaka. Huyu mtu ataleta kasheshe kubwa, nadhani niruhusu sasa mimi na kikosi changu tuvuke mpaka ili tuwasaidie, maana alitaka kwenda Kibumba na huko ndiko kunasemekana kuna jeshi zima la Intarahamwe. Kwa vyovyote hawezi kurudi, kwani taarifa za siri tulizonazo kama ni kweli kuna askari zaidi ya elfu kumi katika kambi hiyo, na wakimbizi wote katika sehemu hiyo wamepewa mafunzo ya hali ya juu ya kijeshi. Kwani wale wakimbizi wanaokataa kushiriki mafunzo ya kijeshi wanauawa, elewa kuwa kuna wakimbizi zaidi ya laki moja wanaume, achilia mbali wanawake na watoto. Hivyo, Willy yuko katika hatari kubwa, huenda hakujua vizuri nguvu ya adui", Meja Kasubuga alimwambia Col. Rwivanga.

"Wewe fanya kazi moja kwanza, wafukuze hao wavamizi mpaka mpakani, wakivuka mpaka wewe na jeshi lako msivuke, mtusubiri hapo hapo mpakani. Mimi, Meja Tom Kabalisa wa Banyamlenge na Bwana Mpinda wa vikosi vya vyama vinavyopinga serikali ya Zaire tutakuja usiku huu kwa helkopita, naamini saa nane usiku tutakuwa tumefika hapo mpakani, msivuke mpaka tufike", Col. Rwivanga aliagiza.

"Sawa afande, mimi naendelea na mapambano, jeshi langu sasa linaelekea mpakani hivi sasa. Mkifika helkopita itue ile sehemu ya kawaida, tutakuwa tumeimalisha ulinzi eneo hilo, nitawasubiri", Meja Kasubuga alisema.

"Asante na kwaheri, msifanye chochote kwanza", Col. Rwivanga alisisitiza na palepale akajiweka tayari kisha akatoka kwenda kuwafuata akina Mpinda na Kabalisa kwa ajili ya kuelekea kwenye uwanja wa mapambano.

Willy na Bibiane walitambaa chini kwa chini kama nyoka na hatmaye wakayafikia majengo yaliyokuwa upande wa pili kutoka sehemu waliyotokea.

"Haya ni maghala ya kuhifadhia silaha, ni makubwa sana yana silaha nyingi za kisasa na vifaa vya kila aina vya kijeshi, zikiwemo silaha mpya za kisasa kabisa kwa ajili ya vita", Bibiane alieleza.

"Itabidi tuingie ndani kwanza ndio tutajua cha kufanya", Willy alieleza.

"Mlango uko upande ule kabisa, yaani unatazamana na majengo ya upande ule kabisa, ambako ndiko kuna ofisi na nyumba za kulala askari. Ulinzi upande ule ni mkali sana na lango la upande ule linafunguliwa kwa chombo maalumu ambacho kinahifadhiwa kwa mmoja wa makamanda wa juu wa jeshi lao", Bibiane alieleza.

"Kuta za maghala haya zimejengwa kwa teknolojia gani, au wametumia nini kujenga, tofali za simenti ama mabati?", Willy aliuliza.

"Kampuni moja ya Afrika Kusini iitwayo Super Frame ndiyo iliyojenga maghala haya pamoja na mabanda yote unayoyaona tena kwa muda wa mwezi mmoja tu. Kila kitu kililetwa hapa kwa helkopita kubwa zilizokodishwa kutoka Urusi na hapa waliunganisha tu hizi kuta na kuezeka. Wakati wa joto kuta zake zinaleta ubaridi na wakati wa ubaridi kuta hizi zinaleta joto, hivyo sijui zimetengenezwa kwa teknolojia gani?", Bibiane alijibu.

"Nimeelewa, baada ya hayo maelezo yako, teknolojia hii imetoka Marekani na inatumika kwa kujenga nyumba za gharama nafuu, lakini zenye kudumu kwa muda mrefu hata zaidi ya matofali ya saruji", Willy alijibu.

"Wewe kuna kitu usichokijua katika Ulimwengu huu", Bibiane alitania kisha akaendelea. "Sasa tunafanyaje Bwana kujua?".

"Utaona, sasa hivi tutaingia ndani", Willy alijibu kisha akafungua na kupekua kwenye mkoba wake, akatoa kifaa kimoja kilichofanana na kalamu lakini hiki ni kinene kidogo. alikifungua akatoa mfuniko wa mbele na kukifungua tena nyuma,

baada ya kukifungua zilitoka betri mbili ndogo sana, Willy akazikagua kuona kama ziko sawa, kisha akazirudisha.

"Haya, rudi nyuma hiki chombo kinatoa miale aina ya leza bimu na hii miale ina nguvu za ajabu na miale hii inakata huu ukuta utadhani kisu ndani ya siagi, rudi nyuma yangu kabisa", Willy alisema Bibiane akarudi nyuma kwa hofu.

"Nasubiri kuona", Bibiane alitania.

"Subiri utaona japokuwa umeingiwa na hofu, lakini usiogope maana hapa hakuna ujanja zaidi ya kumuomba Mungu".

Willy alisukuma nyuma ya kile chombo kama mtu anavyosukuma kalamu wakati anataka kuandika, na mara moja miale myekundu ilijitokeza Willy akaielekeza kwenye ukuta na taratibu alikata saizi ya mlango sehemu ile walipokuwa, alipomaliza akakizima kile kifaa chake.

"Mbona hujakata chochote?", Bibiane aliuliza.

"Subiri kidogo, hii ni sawa na sayansi inayotumiwa na madaktari siku hizi kupasua mwili wa binadamu, wewe uko wapi mama, wenzio twaelekea karne ya ishirini na moja, karne ya sayansi na teknolojia wewe bado upoupo tu. Siku hizi mtu anafanyiwa opresheni, anapasuliwa tumbo, halafu baada ya saa moja anarudi nyumbani mwenyewe na haoni sehemu iliyopasuliwa", Willy alimkoga Bibiane aliyekuwa anashangaa.

Willy aliiangalia saa yake kisha akaufungua mkoba wake akatoa kitu kama bawaba kisha akaipachika kwenye ukuta kikanasa.

"Hiyo ni sumaku?", Bibiane alihoji.

"Ndiyo, inashika kitu chochote hata kama ni mbao".

"Ama kweli wewe mkali Willy, sikutegemea kabisa".

"Au vipi", Willy alijibu. Huku akiitumia ile bawaba alivuta taratibu na ile sehemu ikachomoka na kuacha uwazi wenye ukubwa wa mlango.

Willy na Bibiane walijikuta wanaangalia ndani ya ghala kubwa sana lililojaa silaha.

"Ingia sasa, mbona kama umepigwa na radi!" Willy alimweleza Bibiane.

"Bado nashangaa, hakika mambo uliyonionyesha ama kweli ujuzi huzidiana", Bibiane alijibu huku akiingia ndani ya ghala la silaha.

Willy akitumia chombo kingine kwa kukishikanisha na ile bawaba, ile bawaba ilitoka akaiweka upande mwingine wa kipande cha ukuta alichokuwa amekata, kisha na yeye alipoingia ndani ghala alivuta kile kipande cha ukuta kwa nguvu zake zote na kukipachika mahali pale tena. Mtu yeyote angepita pale kwa macho tu bila darubini asingejua kuwa pale pamekatwa. Bibiane hakuna na neno la kusema isipokuwa kuangalia ile sehemu tu.

"Wewe ni mkali kwelikweli", Bibiane alirudia kusema.

"Kwa mambo mengi si hili tu", Willy alisema kwa kumwemwesa.

wakiwa ndani Willy alishangaa kuona ghala kubwa sana la silaha. Kwa vile taa zilikuwa zikiwaka kwa ndani hawakuamini macho yao. Hata Bibiane hakujuwa kuwa Akazu walikuwa wamejiimarisha kiasi hiki. Mara ya mwisho Bibiane kufika hapa ilikuwa kama miezi mitatu iliyopita na katika hii miezi mitatu silaha nyingi, yakiwemo makombora ya masafa marefu na mafupi, vifaru, ndege aina ya MIG 21 na 23. mizinga, magari ya kivita, helkopita za kivita zilikwishaletwa eneo hili! Hakika ilikuwa ajabu na kweli.

"Hawa watu wanajipanga kupigana na Rwanda tu ama nchi nyingine jirani?", Willy aliuliza kwa mshangao.

"Nia yao ni kupigana na serikali ya Rwanda basi, hakuna kingine", Bibiane alijibu na kuongeza. "ila wanataka kuyapiga majeshi ya RPF kipigo kitakatifu, wasijejaribu tena mara baada ya kufukuzwa Rwanda".

"Fedha za kununulia vifaa hivi vyote watakuwa wamepata wapi?", Willy aliuliza.

"Miaka yote hii unafikiri walikuwa wakifanya nini?, wamewaibia wananchi mali zao zote. Akazu na Jean ni matajiri ajabu. Wana uhusiano na Rais wa Zaire na kiongozi wa waasi wa UNITA kule Angola. Almasi za Angola na Zaire dalali wake ni Jean. Sasa wewe fikiria wana utajiri wa kiasi gani?", Bibiane alijibu.

"He, sasa nimekuelewa mama".

"Kila kitu kilipangwa kwa ustadi wa hali ya juu. Hii ingewezekana kuchukua silaha zao kwa kutumia muda mfupi sana kwama wangeshambuliwa. Willy aliamini kuwa hii kweli ilikuwa kazi ya askari wa kukodishwa kwani hakika hili

lilikuwa ghala la silaha lililotayarishwa na kupangwa na watu wenye ujuzi wa juu sana.

Willy na Bibiane walitembea kwa hadhari lakini kwa haraka wakijificha ndani ya vivuli vya zile silaha. Waliziangalia silaha hisi kiasi kwamba walianza kusahau kilichowaleta hapa.

"Unayaona makombora haya Willy", Bibiane alimwonyesha Willy makombora yaliyotengenezwa Urusi. Kisha akaendelea. "Haya makombora ni aina ya SAM 16 yalitekwa na majeshi ya Ufaransa wakati wa vita vya Ghuba, Februari 1991 na kupelekwa kwenye maghala ya silaha huko Ufaransa lakini kutokana na mahusiano wa karibu kati ya Jean na viongozi w ngazi za juu wa Ufaransa waliamua kumuuzia Jean makombora hayo. Katika makombora haya yamo yaliyotumika kuipiga ndege iliyokuwa imewabeba marais wa Rwanda na Burudi Aprili 6, 1994. Ni Jean na Akazu ndio waliamru rais auawe kwa sababu alikuwa ameanza kwenda kinyume na maagizo yao wakati wa mkutano wa Arusha, nakumbuka niliwahi kukueleza".

"Kama ndivyo, basi hawa Akazu na Jean ni wabaya kwelikweli, sasa naamini", Willy alisema huku hasira zikimpanda dhidi ya watu hawa.

"Lililobaki sasa ni kuziteketeza silaha hizi zote, naamini kuwa jeuri na nguvu ya Jean na Akazu tutakuwa tumeimaliza", Bibiane alieleza.

"Mkuki wa nguruwe, kwa binadamu mchungu, itabidi sasa tutumie yale mabomu yako aliyokuletea Jean, maana kazi kama hii ndio saizi yake", Willy alishauri.

"Unafikiri kwanini nilisema tuyachukue, nilijua. Kwanza ni madogo, na pili yana nguvu kubwa ya ajabu. Ghala kubwa kama hili, matano au sita yanaliteketeza kabisa na hakibaki kitu. Hili senduku linatosha kuiteketeza Kigali nzima. Nia ya Akazu ilikuwa wakishindwa mpango huu basi waiteketeze Kigali nzima na vyote vilivyomo bila kujali maisha ya watu", Bibiane alieleza.

Willy alimwangalia Bibiane kwa jicho kali, baada ya kutafakari akaelewa kwanini Willy alibadilika vile, ikamlazimu Bibiane kubadili maneno. "Haya tuyatege, nafikiri ulikuwa unasoma maelezo sasa unajua nini cha kufanya".

"Bila shaka", Willy alijibu sasa akiwa makini tayari kwa kazi. Kwa hesabu zake alitega mabomu ambayo alihakikisha angeteketeza kila kitu ndani ya lile ghala. Bila kushitukiwa walitoka kwa kupitia sehemu ileile na kisha wakairudishia ile

sehemu ya ukuta kiasi kuwa hakuna ambaye angefikiria kuwa kuna mtu aliyewahi kupitia pale.

"Umesema kama ukitumia hii saa ya kulipua haya mabomu unatakiwa kuwa umbali gani, nina maana haya mabomu tuliyotega", Bibiane aliuliza huku wakiambaa na ukuta kuelekea kwenye mabweni ya kulala askari.

"Umbali usizidi kilomiota moja", Willy alijibu.

Nkubana aliamua kuwasiliana na Col. Gatabazi kwa simu ya upepo. Alipompata alikuwa tayari amewasili Goma na walikuwa wameanza mkutano. Nkubana alieleza kwa kirefu yote yaliyotokea na kisha akashauri. "Huyu Willy Gamba hajui nguvu zetu. Hivyo, ameamua kwenda kujinyonga huko Kibumba, mimi naelekea huko kwenda kuongeza nguvu na kuwashitua makamanda wetu ili tumkamate kabla hajaleta kasheshe zake".

"Sawa, fanya hivyo, Jean anahitaji kumuona akiwa hai", Col. Gatabazi alikubaliana na Nkubana na kumweleza shabaha ya bosi wao Jean.

"Vilevile nitazungumza na makamanda hapa ili waniruhusu tupeleke jeshi mpakani kumsaidia Luteni Nyamboma kudhibiti mpaka wa Zaire, mpaka hapo amri ya kuishambulia Rwanda itakapotoka. Sisi tuko tayari, naamini uamzi utatoka haraka ili kazi ianze alfajiri ya leo. Hebu ngoja kidogo usizime radio yako", Col. Gatabazi aliwaeleza wenzake mambo yalivyokuwa Gisenyi na jinsi ambavyo Nkubana alikuwa akihisi kuwa Willy ameelekea Kibumba. Mara moja Jean alisimama baada ya kusikia habari hii ya Willy kuelekea Kibumba. Haraka alichukua radio na kutoa maagizo kwa Nkubana.

"Sikia, sisi tunakuja huko sasa hivi, tutakuja kwa ndege yangu na mimi nitaondoka. Sasa hivi bado tunawasiliana na Kamanda Bazimaziki awahi uwanja wa ndege. Waeleze wakiwakamata Willy na Bibiane wasiwaue kwanza mpaka tufike, hao ni halali yangu", Jean alitoa amri.

"Unafikiri ni busara sisi viongozi wa juu kwenda huko?", Anatoile kabuga alihoji.

"Bila shaka, huko ndiko yaliko majeshi yetu na ndiko tutakapotoa amri", Jean alieleza msimamo wake.

"Mimi pia nafikiri tuwe pale wakati wanajeshi wanaelezwa kukaa tayari kwa ajili ya kuanza vita alfajiri, hii itawaongezea mori", Jenerali Kasongo alijibu.

"Na mimi nimefurahi sana kwa uamzi huo, kuanzia sasa ofisi yetu kubwa ya kuratibu shughuli za vita itakuwa hukohuko Kibumba, maana ndiko kwenye vifaa vyote, sioni sisi tutafanya nini hapa wakati kila kitu chetu kiko kule", Col. Gatabazi alieleza kwa sauti ya juu.

"Sawa, wengi wape", Kabuga alijibu.

Kisha wakawasiliana na Col. Marcel Bizimaki, ambaye ni Kamanda wa jeshi la Akazu wakitumia njia ya simu ya satellite, wakamweleza kuwa wote walikuwa wanarudi hapo tena, kwa ajili ya kutoa mwongozo na ruksa ya kuanza mapambano dhidi ya adui alfajiri ile. Vilevile, alielezwa aweke vikosi vyake vyote kwenye tahadhari ili waweze kumsaka na kumkamata Willy Gamba akiwa hai.

"Karibuni, nitawapokea na nitawaweka kwenye nyumba ya mkufunzi wetu mkuu. Kamanda Moris ambayo ina ulinzi mkali pia inalindwa na mitambo ya kisasa ya usalama. Na mtakapokuwa pale kwake itakuwa rahisi kwenu kuona kwa macho jinsi majeshi yetu yanavyosonga mbele kupitia mitambo ya kisasa kabisa", Col. Bizimaziki alitamba.

Kundi zima liliondoka kuelekea uwanja wa ndege, likiwa tayari kuelekea Kibumba, ambako kuna umbali usiozidi dakika kumi kwa ndege, Jean alifikiria kuwa ni vizuri kuwa na ndege yake karibu, ikiwa kwa bahati mbaya kikatokea kitu na kutakiwa kuondoka ghafla na kujisalimisha aweze kufanya hivyo kwa ndege yake. Wakati wanaelekea uwanja wa ndege. Co. Gatabazi aliwasiliana tena na Nkubana.

"Uko wapi sasa?".

"Nimekwisha kuwasili Kibumba na sasa naelekea kwenye lango kuu la kuingilia ndani, nimewasiliana nao kwa radio wananisubiri", Nkubana alimweleza Col Gatabazi.

"Sawa, kazi yako kubwa ni kumkamata huyo Willy na kikaragosi chake huyo Bibiane na uwalete kule mlimani ilipo nyumba ya Kamanda Moris, sisi tutakuwa huku muda si mrefu", Col. Gatabazi aliagiza.

"Nitafanya hivyo afande. Mara hii kaingia mkenge yeye mwenyewe", Nkubana alijibu.

"Lakini mtu huyu ni hatari sana, naomba umwambie Kamanda Bizimaziki mchukue tahadhari kubwa sana. Hata tulipofika sitaki makosa yatokee", Col. Gatabazi alisisitiza.

"Sawa afande, tutafanya hivyo, lakini mtu mmoja na mwanamke mmoja wanaweza kufanya nini mahali kwenye kambi kubwa ya jeshi kama Kibumba?", Nkubana alihoji.

"Wewe chukua hadhari ya hali ya juu huyu mtu si wa kawaida", Col. Gatabazi alisisitiza na kuzima radio.

Nkubana alifahamu kuwa viongozi wake walikuwa na mashaka na Willy, lakini Nkubana yeye hakuna na wasiwasi. Aliamini kuwa huu ndio ulikuwa mwisho wa Willy Gamba. Ulinzi na uwezo wa kambi ya Kibumba ulikuwa mkali mno, kiasi kwamba ilikuwa vigumu sana kwa mtu mmoja kuingia na kutoka salama. Gari lilisimama na kumwondoa Nkubana katika mawazo yake. Walikuwa wamefika kwenye lango kuu na kusimama kama ilivyo sheria ya kusimama na kukaguliwa kabla ya kuingia ndani ya ngome hii.

Nkubana alipoangalia saa yake ilikuwa yapata saa sita na nusu usiku.

"Saa ngapi sasa?" Bibiane alimwuliza Willy Gamba.

"Imefika saa sita na nusu sasa", Willy alimjibu.

# SURA YA KUMI NA TATU

Walikuwa tayari wana saa moja ndani ya kambi hii ya kijeshi na bado walikuwa hawajapata tatizo lolote. Sasa ndio walikuwa wanaanza kutega mabomu kwenye bweni la mwisho ili baada ya hapo kama itawezekana watafute namna ya kutoka nje, kwani mabomu waliyokuwa wameyatega na kuyaprogramu kwa saa ya Willy ili kuyalipuwa lazima wawe mbali, maana yalikuwa na uwezo wa kuharibu kambi nzima na vitu vyote vilivyomo kama yangefanya kazi kama ilivyotarajiwa. Wakati wanafikiri hivi, ghafla taa za kiwanja cha ndege zikawashwa.

"Aha, kumbe ule ni uwanja wa ndege!" Willy alinong'ona.

"Ndio, unafikiri zile ndege za kijeshi zinaruka kutokea wapi!", Bibiane ambaye naye hapo awali alikuwa hajui uwanja ulikuwa wapi, alijibu.

"Kwanini wanawashwa taa wakati huu?", Willy alijiuliza.

Wakiwa wameduwazwa na kitendo hiki na wakiwa sasa wameondoka kwenye ukuta wa bweni la mwisho na kujibanza kwenye kivuli cha lori kubwa la jeshi lililokuwa limeegeshwa pale, Bibiane alijibu. "Huenda ndege za kivita zinatolewa ili zikashambulie mahali ama ndege ya Jean inataka kutua".

"Nafikiri hilo la pili ni sawa. Hii itakuwa raha sana mimi kukutana uso kwa uso na huyu bwana yako", Willy alikejeli Bibiane akafadhaika.

"Si bwana yangu tena, bwana yangu ni wewe Willy, maana wewe ndiyo uko na mimi sasa, sema, fanya kila unachotaka nifanye", Bibiane alijibu kwa sauti ya mahaba. Willy alimwangalia, kisha akamshika na kumbusu.

Mara wakasikia king'ola na askari wakatoka na kuanza kuelekea kwenye kiwanja cha ndege.

"Hapa kuna hatari, nafikiri wametushitukia", Willy alisema huku ile kengere yake ya hadhari ikilia kichwani mwake. Kisha akaendelea. "Kinachotokea hapa ni sisi kutoka ndani ya kambi hii. Wataanza kutusaka sasa hivi".

Mara tena wakasikia mwungurumo wa ndege na magari sita aina ya Landrover ya wazi yakiwa yamebeba askari yakielekea karibu na uwanja, yalipokaribia yakasimama. Kisha, yakafika magari mengine mawili aina ya Landcruiser GX nayo yakasimama pale vilevile kusubiri ile ndege itue. Pale kwenye uwanja mkubwa, vikosi vya askari vilizidi kujipanga kwa ajili ya mapokezi.

Ile ndege ilipotua watu wanne walitoka ndani ya Land Cruiser zilizokuwa zimesimama kando na kusogea karibu ili kuilaki ile ndege. Wakiwa bado wamefichwa na kivuli cha lile Lori walitumia viona mbali vyao na kuwaangalia kwa makini wale watu waliotoka kwenye yale magari.

"Yule aliyetangulia ni Col. Marcel Bazimaziki, huyu ndiye kamanda mkuu wa majeshi yote ya Akazu. huyo wa kushoto ni Kapten Nkubana aliyekutoroka Kigali, ndiye aliyetumwa kuniua, kumbe naye keshafika huku. Wa kulia ni kamanda Morris huyu ni mkuu wa vikosi vya kukodiwa ambavyo vinafundisha majeshi ya Akazu. Huyu wa nyuma simfahamu".

Ndege ilisimama na milango ikafunguliwa na watu wakaanza kutoka. Jean ndiye alikuwa wa kwanza kutoka ndani ya ndege hii.

"Aha huyu ndiye Jean nafikiri?", Willy aliuliza.

"Bila shaka huyo ndiye Jean, ambaye ndiye mzizi wa fitina katika Rwanda. na yule anayemfuatia ni Anatoile Kabuga, huyo ndiye kiongozi wa Akazu, anayefuata ni Jenerali Kasongo, kamanda wa majeshi ya Rais wa Zaire, rafiki mkubwa wa Jean, anayetokea sasa pale mlangoni ni Col. Gatabazi na huyo anayetokea mwisho simfahamu, maana sijawahi kumuona", Bibiane alieleza.

"Asante, sijui bila wewe ingekuwaje, umefanya kazi yangu iwe rahisi kiasi fulani".

"Ni kweli, lakini ungetumia njia nyingine, wewe si wa kushindwa jambo".

Baada ya kutoka ndani ya ndege, kundi la Jean liliingia ndani ya zile Landcruiser wakaondoka huku wakisindikizwa askari kwa ulinzi mkali.

"Unadhani watakuwa wanaelekea wapi sasa?", Willy alimuuliza Bibiane.

"Sijui, nilitegemea huenda wanataka kuzungumza na vikosi vilivyofanya gwaride pale uwanjani, lakini wameondoka moja kwa moja kuelekea upande ambao ndiko kuna lango kuu. Huenda wanakwenda kupumzika kwa kamanda Morris, nyumba na ofisi ya kamanda Morris iko juu ya hicho kilima, huwezi kuona ukiwa hapa kwa vile kumefichika kwa miti", Bibiane alieleza.

Kati ya magari yaliyobeba askari moja halikuendelea na msafara isipokuwa lilielekea kwenye gwaride. Gari hilo lilipofika hapo lilisimama na watu waliotoka ndani walikuwa Nkubana na askari wengine watano. Kisha Nkubana akaanza kuhutubia hilo gwarinde na kikosi kimoja wapo kikapiga hatua moja mbele na vingine vikatawanyika. Willy na Bibiane hawakuelewa nini kilikuwa kinaendelea.

"Lililopo ni sisi kuondoka hapa kambini haraka iwezekanavyo. Vinginevyo tutakamatwa hata kabla hatujamaliza kazi iliyotuleta", Willy alieleza.

"Mimi bila kummaliza huyu Jean siendi kokote ng'o", Bibiane alijibu kwa hasira.

"Lazima ufahamu kuwa hatuwezi kukabiliana na watu wote hawa, lazima kutumia akili ya ziada, wewe unajua katika kazi yetu hii swala ni kuendelea kuishi; lazima uhakikishe unajilinda ili ubaki salama. Hapa tukitaka kuanza mapambano ni sawa na kujinyonga sisi wenyewe. Pili ili tuweze kulipua mabomu tuliyotega ni lazima tutoke nje kabisa ya eneo hili, la sivyo sisi pia tutakuwa tumejiteketeza pamoja na adui", Willy alimuasa Bibiane kisha wakaona wale askari wa kikosi wanakabidhiwa silaha na kuelekea kwenye seng'enge ya ua wa kambi.

"Ehe, umeona kazi hiyo, hawa jamaa wanategemea tutakuja hapa, lakini hawajui kama tumeingia ndani na kazi imefanyika", Willy alieleza.

"Lakini wakifika pale tulipoingilia lazima watajuwa tuko ndani", Bibiane alijibu.

"Ndio sababu nikasema tutafute njia tutoke humu ndani", Willy alisisitiza.

Wakati wote Willy alikuwa akipanga mbinu za kuweza kutoka ndani ya kambi hii wakiwa salama.

"Hebu nifuate tuangalie hali ikoje upande wa lango kuu", Willy alimwambia Bibiane.

"Kule hatuwezi kupita, afadhari tuwahi palepale mahali tulipotumia mwanzo", Bibiane alisema na Willy akamuunga mkono na kuona alikuwa na mawazo sahihi hivyo, haraka haraka wakaelekea sehemu waliyokuwa wameingilia, huku askari wa doria wakizidi kujipanga na kupewa silaha ili kuzidi kujipanga kando ya ua huu wa seng'enge wakiwa tayari kulinda kambi yao. Ile tembetembea ya hawa askari kiasi fulani iliwasaidia sana akina Willy na Bibiane kutobainika mapema kwani walikuwa wamevaa mavazi ya kijeshi kama wale askari. Nkubana na watu wake waliweka ulinzi mkali upande la lango kuu wakiamini kuwa Willy angeweza kujaribu kuingia pale kambini kwa kutumia lango kuu.

Hakuna askari wala kiongozi katka kikosi chicho aliyefikiri kuwa adui wangeweza kupitia sehemu nyingine yoyote kwani waliamini kwamba hakuna kitu ambacho kingeweza kupita ua ulioizunguka kambi hii. Hivyo, hata hawakuweka askari kuzunguka ua ilikuwa ni kwa hadhari tu. Kumbe kitu ambacho hawakujua ni kwamba teknolojia yototе inaweza kushindwa na teknolojia nyingine yenye

maarifa ya juu zaidi. Willy alikuwa ndani na tayari alikuwa ametega mabomu kila upande.

Huyu Willy Gamba lazima atakuwa kaingia hapa, hatujui kapita njia ipi na yuko sehemu gani?", Nkubana alimwambia Col. Gatabazi kwa njia ya radio.

"Haiwezekani, hakikisha kwanza", Col. Gatabazi alijibu kwa hofu.

"Hakika ni yeye Willy Gamba, tumekuta sehemu imechimbwa chini ya ua mita kama tatu hivi kwenda chini, hata hatujui imetumika nini kuchimba ardhi. Kwa maana hiyo, tumeanzisha operesheni kali ya kumsaka ndani na nje ya kambi, japokuwa hatuna uhakika kama bado yuko ndani ama ametoka. Hakika mtu huyu ni hatari sana, itabidi kuongeza ulinzi katika eneo hilo hususan mahali mlipo, nitatuma askari zaidi kuimarisha ulinzi hapo", Nkubana aliahidi.

"Kuna madhara yoyote kafanya huyo Willy", Col. Gatabazi alihoji kwa wasiwasi.

"Mpaka sasa hakuna, tumekagua sehemu zote ni salama isipokuwa hapa kwenye ua palipochimbwa ardhi, ni sehemu hii tu".

"Nani kagundua eneo hilo limechimbwa na muda gani umepita toka hali hiyo itokee", Col. Gatabazi aliuliza tena kwa shauku.

"Niko hapa katika eneo husika afande", Nkubana alijibu. Baada ya ukimya wa sekunde kadhaa akaendelea. "Askari wetu mmoja wa doria aliyepangwa kulinda eneo hili la ua anasema haiwezi kuwa zaidi ya dakika kumi na tano hivi zilizopita. Nafikiri bado hajaingia ndani, anasubiri ama ameona ndege wakati mnaingia, anaweza kuwa anajipanga kujaribu kuanzisha mashambulizi. Ujue yuko pamoja na Bibiane ambaye anaijua sehemu hii vizuri sana".

"Bibiane anataka kulipa kisasi, kwa hiyo lazima watakuwa wanaelekea hapa baada ya kuona tumetua kwa ndege, ongeza ulinzi, nafikiri umebashiri sawasawa", Col. Gatabazi alijibu.

Baada ya kuzungumza na Nkubana kwa radio, Col. Gatabazi aliwafahamisha wenzake kuhusu maelezo ya Nkubana. "Huyu mtu ni hatari sana, lazima atakuwa anaelekea hapa, nimeagiza ulinzi uongezwe zaidi. Nia yake ni kutuangamiza sisi kwani Bibiane atakuwa amemweleza yote kuhusu uongozi wetu. Naomba wote tuwe katika hadhari, huyu mtu ananitia wasiwasi maana anaonekana amepania ni mjuzi na haogopi kitu. Watu wa aina hii ni hatari sana", Col. Gatabazi alieleza.

"Hapa hawezi kuingia, ajaribu aone moto, hii itasaidia kumkamata kirahisi maana nyumba hii inalindwa na mitambo maalumu ya kisasa, kuna kamera zimetegwa eneo hili. Na tunaweza kuona sehemu zote zinazoizunguka nyumba hii kwa mara moja, kwenye chumba chetu kuna vifaa vya kuangalia usalama wa nyumba hii, kuna televisheni nne ambazo zinaangalia mzunguko wa eneo hili kwa umbali wa kilomita moja. Hii ina maana hata sehemu ya upande huu wa kambi tunaona. Halafu pale kambini kuna mitambo kama hii, sijui imekuwaje hawakuweza kumuona!", Kamanda Morris alieleza kwa mshangao.

"Hebu twende kwenye hicho chumba chako", Jean ambaye pia alianza kuingiwa na hofu, alieleza. Wakaelekea kwenye chumba cha mawasiliano na usalama wa kambi hiyo.

Walipoingia ndani ya chumba hiki waliwakuta askari kama sita hivi waliokuwa wakisimamia kuendesha ile mitambo ya ulinzi mle ndani. Wakiwa ndani waliweza kuona picha za maeneo yote yaliyozunguka ile nyumba, waliwaona pia askari waliokuwa wakilinda eneo hilo. Kwa kweli, kulikuwa na askari wengi kila mahali wakiwa tayari kupambana na adui kwa njia yoyote. Kupitia mitambo hiyo waliweza kuwaona askari wengine zaidi wakiongezeka na kujipanga kwa ulinzi zaidi.

Kwa vile kambi hii inao komandoo zaidi ya mia tano waliofuzu vizuri mafunzo yao, hii ilimpa jeuri Jean na Col. Gatabazi kuwa na imani kuwa hakuna adui anayeweza kuleta rabsha mbele ya vijana hao ambao pia walikuwa sehemu ya ulinzi wakati huo.

"Kukitokea kitu chochote cha hatari, sisi tutakuwa wa kwanza kukiona hata kabla ya askari wa hapo nje hawajakiona. Tumeweka taa kali za ulinzi ili eneo hili lionekane kama mchana na kamera zetu zichukue picha kwa ufasaha zaidi", Kamanda Morris aliwaeleza na kufanya wageni wake waridhike na maelezo hayo na kuamini kuwa hakuna madhara.

"Lakini ikitokea bahati njema Willy Gamba akamatwe, huyu atakuwa mfungwa mikononi mwangu, msimuue tafadhari, nileteeni hapa nimle nyama taratibu. Nasisikia kuonja nyama yake", Jean aliagiza.

"Na Bibiane?", Col. Gatabazi aliuliza huku akimwangalia Jean.

"Huyu nitapenda kufanya naye mapenzi kwa mara ya mwisho kabla hajaenda ahera", Jean alijibu huku uso wake ukionyesha uovu wa ajabu na mate yakimjaa mdomoni.

"Huyu mtu ni mgonjwa", Col. Gatabazi alijisemea moyoni.

"Tunaweza kuendelea na mkutano", Jean aliagiza baada ya kujiridhisha na hali ya usalama wa kambi, wakarudi kwenye chumba cha mkutano walikokuwa Kamanda Morris, Bizimaziki na wataalamu wengine wa kijeshi waliokodishwa, waliendelea kuwaeleza jinsi mipango ya mashambulizi ilivyokuwa imepangwa.

Meza moja ilikuwa na ramani ya nchi za Zaire, Rwanda na Burundi na baadhi ya nchi zote za maziwa makuu zikitumiwa kuonyesha jinsi ambavyo jeshi la Akazu lilivyojiandaa kusonga mbele katika kuivamia Rwanda, wakitumia askari wa miguu, magari ya kisasa ya kivita, vifaru, makombora ya masafa mafupi na marefu pamoja na ndege za kivita, yote ni kuivamia nchi hiyo kijeshi.

Wakiwa ndani ya kambi hii, Willy na Bibiane walijificha kwenye vichaka vilivyokuwa kando ya njia ambayo magari ya jeshi yalikuwa yanapita kuelekea kwenye jumba analoishi Kamanda Morris.

Walikuwa wamefanikiwa kuvuka kizuizi cha kwanza kutoka kambini bila kushitukiwa, na moja kwa moja walitumia vichaka kujificha huku wakiua askari waliokuwa wakilinda maeneo hayo, mpaka wakafika sehemu hii wakitafuta nafasi nzuri ya kuishambulia nyumba ya Kamanda Morris ili waweze kuukabiri uongozi wa juu wa Akazu.

"Ikitokea gari lisilo na askari wengi nyuma au hata likiwa na askari wawili ama watatu tulivamie na kulifanya letu ili tulitumie litupeleke kule juu bila kuwashtua walinzi. Kwa vile tumevaa sare zao tunaweza kujaribu kuingia mpaka ndani bila shida ndipo tuanze mapambano, kama tutakuwa bado hatujashitukiwa", Willy alimwambia Bibiane.

"Kama nilivyowahi kukwambia nyumba hii inalindwa kwa mitambo maalumu ya kisasa. Nje kuna kamera nne zinazopeleka picha kwenye televisheni ndani ya chumba cha udhibiti wa mitambo, ambamo kuna askari wanaangalia mitambo hii kwa zamu, kwa saa ishirini na nne kila kinachotokea nje kinaonekana kwenye televisheni hizi, kamera hizi ninafanya kazi katika mzunguko wa kilomita moja kutoka eneo la kambi. Vilevile ndani ya chumba hicho kuna vifaa vya kisasa kwa ajili ya kunanasa sauti na mazungumzo yoyote ya radio kwa radio kwa umbali wa zaidi ya kilomita mia moja. Pia wanaweza kunasa picha zinazoletwa kwa rada kama kuna kitu kinaruka sehemu hii. Hivyo, tukijaribu kufanya chochote lazima tutaonekana moja kwa moja", Bibiane alimuasa Willy.

Baada ya kutafakari kwa sekunde kadhaa, Willy alitoa kile kitochi chake chenye miali ya leza akampatia Bibiane.

"Sikia, mimi ninacho kingine, kama tutafanikiwa kuikaribia ile nyumba tutagawana njia, wewe utaelekea mashariki mimi nitapita magharibi, kitu cha kwanza kabisa ni kuua zile kamera za upande wako kwa kutumia miali ya chombo hiki. Ukiwasha tu na kuelekeza miali hii kwenye hizo kamera basi zinakufa papohapo, hazifanyi kazi tena. Harafu unaweza kukitumia haraka kukata ukuta kama tulivyofanya wakati tunaingia kwenye maghala ya silaha, Pia unaweza kukitumia chombo hiki kupofua mtu yeyeto macho. Tukifanikiwa kuifikia ile nyumba basi tuivamie na kuanza mapambano, hapo ndipo kuna kufa ama kupona. Jean na wenzake ama sisi. Tukifanikiwa tutaonana ndani, nataka umuonyeshe Jean mafunzo yote aliyokupeleka ulihitimu vizuri na unao iwezo mkubwa wa kutumia nafasi kama ulivyofundishwa".

Wakati Willy bado anaeleza waliona gari aina ya Landrover la jeshi linakuja, nyuma ya gari hilo kulikuwa na askari wawili waliokuwa wamesimama wakiwa wamevalia mavazi ya kijeshi kama wao.

"Gari hilo, kazi kwako Bibiane", Willy alitoa amri, na gari lilipokaribia wote walilirukia kwa nyuma na kuingia ndani bila kutoa kishindo. Wale askari wawili walikuwa wakizungumza huku wakiangalia mbele. Willy alimuonyesha ishara Bibiane, na kwa kutumia vipaji vyao vya karate, waliwavamia wale askari na kuwaua palepale na kisha kuwainamisha chini ndani ya lile gari bila kutoa kishindo cha kuwashitua wale waliokuwa mbele ya gari. Wakawalaza vizuri na kuwafunika kwa turubai lililokuwa ndani ya lile gari.

Kisha wakajifanya ndio wale askari kwani walivaa kofia za chuma za wale askari waliowaua. Gari lilipopunguza mwendo na kusimama, Willy alitoa ishara wote wakaruka na kuelekea pande mbili tofauti. Bibiane akaelekea kulia, Willy kushoto. Kwa vile wote walikuwa wamevaa nguo za kijeshi kama wale askari wengine, hakuna aliyewashitukia. Willy aliongoza kwenye ile nyumba bila wasiwasi huku akipigiana saluti na askari wengine wa pale. Alipofika karibu kabisa na nyumba ile aliona ile kamera. Wakati Willy anaiona ile kamera ya upande huu wa kushoto, Bibiane naye alikuwa akijipenyeza upande wa kulia, akaiona ile kamera wa upande wake.

Kama vile walivyoambizana, wote walitoa zile tochi zao zenye miali ya leza na kuzielekeza kwenye kamera hizo. Macho ndani ya zile kamera yalikufa palepale na kukatisha mawasiliano ya kutuma picha za pande zote mbili kwenye televisheni.

Na baada ya kufanya hivyo tu Willy alijipenyeza na kwenda kuitafuta ile kamera ya upande wa kusini.

Mle ndani ya chumba maalumu kilichokuwa na mitambo walishituka baada ya televisheni zinazopokea picha kutoka kulia na kushoto kushindwa kutuma picha.

"Tumeingiliwa, hii si bure", Kiongozi wa wale askari waliokuwa wakiendesha mitambo ndani ya chumba alisema na kwenda kumweleza Kamanda Morris. Kamanda Morris na wenzake walikuwa katikati ya mkutano wakati yule askari alipofungua mlango na kuingia ndani.

"Kuna nini?". Kamanda Morris alimuuliza kwa shauku huku kundi zima likisimama kumwangalia yule askari kwa taharuki.

"Televisheni zote za kulia na kushoto hazileti picha, inawezekana zimeharibiwa", yule askari alisema.

"Tayari yuko hapa", Col. Gatabazi alijibu na kuinuka kutoka kwenye kiti. Kabla mtu mwingine hajasema lolote, mlango ulifunguliwa na askari mwingine kutoka chumba cha kingine mitambo nae akaingia na kueleza. "Sasa kamera zote hazileti picha".

Kundi zima la Akazu na mamluki wao wakaingiwa na hofu.

"Huyu mtu ameweza kufika mpaka kutuingilia hivi kwa namna gani, Nyinyi hamna ulinzi wa kutosha hapa", Jean alifoka kwa hasira huku akionyesha hofu.

"Usitahayali Jean, lazima ufurahi kuwa mtu wetu kajileta mwenyewe na hataweza kuondoka hapa akiwa hai", Col. Gatabazi alijibu huku akielekea mlangoni na kwenda nje akifuatiwa na Kamanda Morris.

"Twende zetu tukamsake, mambo yameiva sasa", Col. Gatabazi alimwambia Kamanda Morris.

Nkubana ambaye naye alikuwa amefika kwenye eneo la nyumba hii akiwa anahisi Willy na Bibiane wangekuwa wamefika, alizunguka eneo hili kwa hadhari kubwa huku akiwachunguza kwa makini kila askari waliokuwa karibu yake, aliwaangalia machoni mwake. Kutokana na kitendo cha pale mpakani alijuwa kuwa Willy na Bibiane walikuwa wamevaa sare za jeshi sawa na wao. Wakati Bibiane anapiga miali ya leza kuua ile kamera ya kusini Nkubana alikuwa karibu nae kabisa lakini alikuwa bado hajamtambua. Ile miale ilipotoka kwenye tochi ya Bibiane na

kuunguza jicho la kamera likatoa mwanga wa kati baada ya sekunde kadhaa jicho lake likaungua.

Nkubana alisitushwa na mwanga uliotokea na kuua kamera. Akamwangalia Bibiane na macho yao yalipokutana mara moja wakatambuana. Kama umeme Nkubana alitoa bastola yake kiunoni ili awahi kummalize Bibiane. Bila hata kufikiri kuwa Bibiane alikuwa fundi zaidi, alimuelekezea ile mionzi ya leza machoni na palepale akajitupa chini kukwepa risasi, Nkubana alipiga risasi hovyo kwani alikuwa amekwisha pofuka macho na kupiga makelele, "Bibiane huyu hapa kanipofua macho".

# SURA YA KUMI NA NNE

Risasi zote alizorusha Nkubana hazikumpata Bibiane ambaye alijiviringisha na kuinuka mahali penye mlango ambao Col. Gatabazi na Kamanda Morris walikuwa wanaufungua ili kutoka nje, baada ya kumsikia Nkubana akipiga kelele. Hivyo, mlango ulipofunguliwa tu, Bibiane alijitupa pale mlangoni na kuwakumba Col. Gatabazi na Kamanda Morris, kitu ambacho hawakukitegemea na wote wakaangukia ndani huku wakifuatiwa na risasi zilizoelekezwa kwa Bibiane.

"Acheni acheni kupiga risasi, mtaleta madhara makubwa", Ofisa mmoja wa jeshi la Akazu aliamru baada ya kuona kilichotokea. Bibiane ndiye aliyekuwa wa kwanza kuinuka na alipoinuka huku katoa Bastola yake, askari mmoja aliyekuwa analinda mle ndani alimpiga kichwani kwa kitako cha bunduki; Bibiane alianguka chini na kuzirai.

Jean, aliyekuwa anaangalia yaliyokuwa yanatokea huku akiwa amezugukwa na kundi la viongozi wa Akazu na marafiki zake wa jeshi la Zaire, aliagiza, "Msimuue. Nasema mpelekeni bafuni mmwagieni maji. Kwanza mfungeni kamba, sikujua mtoto huyu ni hatari kiasi hiki. Kumbe sikupoteza fedha zangu bure nilipompeleka kwenye mafunzo ya kijeshi. Nilikuwa nasikia sifa zake tu leo nimemuona mwenyewe akiwa kazini, nimefarijika sana".

Col. Gatabazi na Kamanda Morris sasa walikuwa wamesimama huku wakiwa na hasira ya kutaka kummaliza Bibiane.

"Wewe huna akili nzuri kweli, huyu mwanamke ni mtu hatari halafu unasema umefarijika, huyu ni mtu wa kuuawa sasa hivi si mtu wa kusubiri". Col. Gatabazi alihamaki.

"Poa, Col. tulikubaliana kuwa kabla sijamuua ni lazima nifanye naye mapenzi mara ya mwisho. Hakuna mwanamke aliyewahi kuniridhisha kimwili kama huyu. Ngoja azinduke halafu nitimize ahadi yangu ndipo nitakuachia umuue", Jean alieleza.

Willy aliposikia purukushani na milio ya risasi upande ule wa kusini na kelele alizopiga Nkubana alijua kuwa kwa Bibiane mambo tayari yameharibika. Alitumia hii vurugu na yeye akakimbilia ule upande wa kusini. Alipofika akamuona mtu anataka kubebwa ili aingizwe ndani, alikuwa haoni na hakujua yule ndiye alikuwa mtu aliyepambana na Bibiane na kupofuliwa macho. Kwa vile nia ya Willy ilikuwa

kuingia ndani na kuwaangamiza viongozi wa Akazu, aliona amepata upenyo wa kuweza kufanya hivyo. Huku akijifanya kama mmoja wa askari wa pale, aliwahi na kumuondoa askari aliyekuwa anataka kumbeba Nkubana kumpeleka ndani na kumuonyesha ishara ambayo yule askari hakuelewa lakini akafikiri huenda yule ni askari mwenzake ndiye aliyeamriwa kufanya vile.

Willy alimshika Nkubana kiunoni na kumweleza. "Afande ngoja nikuongoze ndani ukapumzike, huyu mshenzi Willy atatutambua leo".

"Nia aibu kwangu, mimi Nkubana kufanywa hivi na mwanamke, mimi nia yangu ilikuwa kumuangamiza kabisa Willy kwa mikono yangu, nasikia uchungu sana", ndipo Willy alipotambua kuwa huyu aliyekuwa amemshika alikuwa Nkubana. Alifurahishwa sana na kazi ya Bibiane.

"Usihofu Afande, tutakulipizia, hapa huyo Willy kafika, atawezaje kutoka hapa, huyu mtu ni mwendawazimu. wakati Willy akieleza hayo walikuwa wamefika mlangoni na kuingia ndani ya sebule kubwa ya nyumba hiyo.

Bila kuhisi kuwa huyu aliyekuwa akimuongoza Nkubana alikuwa ni Willy Gamba, Col. Gatabazi alimweleza.

"Mkarishe pale kwenye kiti, halafu askari toka haraka mkamsake huyo Willy Gamba".

"Ndio Afande", Willy alijibu huku akielekea kwenye pembe nyingine ya ile sebule kulipokuwa na makochi. Wakati huo Willy alimsikia Kamanda Morris akitoa amri kwenye kipaza sauti kuwa askari wote walioko pale wapange mstari mara moja kuizunguka nyumba na kila mmoja amnong'oneze afisa wake lile neno la siri wanalotumia wakati wa usiku. Wakati huo huo Willy aliliona kundi la Akazu na Jean likizunguka meza na mmoja wao kutamka, "Nafikiri tuyaamrishe majeshi yetu yaanze kusogea, tunapoteza muda kwa huyu Willy, mtu mmoja asitupotezee muda hata kama ni hodari atakua wangapi, sanasana hawazidi mia, ndio atakuwa amefanya nini?", Kabuga alieleza.

"Namuunga mkono bwana Kabuga. Askari wachache wabaki wamshughulikie huyo Willy, wengine waanze kuelekea mpakani, huku kusubirisubiri kunaweza kutuletea madhara. Tumeshaona tuko tayari kabisa, hakuna wakati tumekuwa tayari kama wakati huu", Col. Gatabazi alieleza.

"Oke, nami nakubali, kwanza huyu Bibiane kesha fufuka?", Jean aliuliza.

Willy alikuwa amekwisha mkalisha Nkubana huku akili yake ikipiga hesabu za haraka namna ya kuwateka hawa Akazu na vibaraka wao.

"Wewe askari njoo hapa, na wewe uninong'oneze neno la siri tunalitumia usiku", Kamanda Morris alimwita Willy wakati alipotaka kutoka nje. Willy alikuwa hajui hilo neno la siri, hivyo mtego huo ulikuwa umemnasa. Karibu na Kamanda Morris alikuwepo Jean akaagiza chumba cha mitambo askari wamlete Bibiane aweze kuulizwa alipo Bibiane.

"Willy alimsogelea Kamanda Morris na ghafla alimrukia Jean na kumkaba na kuvuta kwenye ukuta, bastola kichwani kwa Jean na kusema, Jean huna haja ya kumtafuta Willy, niko hapa. Kundi zina lilisimama huku askari wote wakiwa wamepigwa na butwaa. Kamanda Morris, Jenerali Kasongo, Meja Masamba, wale askari wa kukodiwa na hata Nkubana, japo alikuwa kipofu walitoa bastola zao.

"Msifanye mchezo wowote, wekeni silaha zenu zote hapo kwenye meza, mkifanya mzaha huyu bwana yenu Jean atakuwa historia nitamwangamiza", Willy Gamba alieleza kwa ukali. Wote walijua hatari. "Na mtu asisogee hapa wala asiondoke humu ndani. Ila wamlete Bibiabe", Willy aliendelea kuamru.

"Fanyeni anavyosema", Jean alieleza huku akitetemeka huku mkojo ukimtoka chapachapa.

Kamanda Morris alitaka kutoka ili kwenda kumleta Bibiane, lakini Willy alikataa, "Mtu hatoki huku ndani, nimesema kwa lugha inayoeleweka, umenipata wewe Kaburu".

"Kampuni yenu ya mamluki naijua safari hii mmeingia hasara, mmetengeneza faida kubwa katika biashara hii, lakini leo nasema tena, safari hii mmeingia hasara".

Kamanda Morris alimwagiza askari mmoja amlete Bibiane, ambaye alikuwa tayari amepata fahamu. Na Kamanda Morris akawa amesema na neno moja ambalo Willy hakulielewa. "Umesema nini wewe kibaraka?", Willy alihoji huku macho yake yakionekana mekundu.

"Nimeita mwisho jina la yule askari", Kamanda Morris alijibu. Lakini Willy machale yalimcheza. Wakati bado anafikiria lile neno aliwahi kulisikia wapi, ghafla ukuta aliokuwa ameuegemea ukapitishwa umeme na yeye akamsukuma Jean upande mwingine na kuruka nyuma ya makochi.

Nguvu ya ule umeme ilikuwa kubwa kiasi cha kumfanya Willy kupoteza fahamu baada ya kuanguka chini. Kamanda Morris alikuwa amejiwekea usalama wa kila aina na alikuwa amemzidi Willy maarifa, mara moja kila mmoja alichukua silaha yake, na Bibiane kabla hajafanya lolote alikuwa ameshikiliwa vizuri na askari watatu.

"Mfungeni kwenye hicho kiti, sasa tutamla nyama vizuri", Col. Gatabazi aliagiza. Bwana Kabuga akiwa bado anatetemeka kwa kuwa mambo kama haya yalitokea kama miujiza alidai arudi kwenye ndege ili waondoke eneo hilo.

"Hapana, kaa uone maana ya utawala", Jean alijibu baada ya kuinuka kutoka mahali alipokuwa amedondoka na macho ya chuku akiwa ameyaelekeza kwa Bibiane aliyekuwa anafungwa kwenye kiti. Kisha, akamwendea Bibiane na kumnasa kibao, akisema "Mbio za sakafuni huishia ukiongoni, janja yako kwisha. Lakini kabla mwisho wako haujafika niliahidi nitafanya mapenzi na wewe kwa mara ya mwisho".

"Utawahi, kwani na wewe unadinda", Bibiane alijibu.

Jean alimnasa tena kibao na kusema, "Umesahau nilivyokuwa nakunyanyasa kitandani".

"Wewe ni mgonjwa na huu ndio mwisho wako", Bibiane alijibu kwa dharau.

"Unachekesha, huu ndio mwanzo wangu na mwisho wako", Jean alijibu na kugeuka nyuma, kwani wakati mawazo yake yakiwa kwa Bibiane, Kamanda Moris alileta kifaa cha umeme na kumfunga Willy kwenye kiti na kumtingishatingisha ili azinduke.

"Willy alipozinduka tu, Jean alikuwa wa kwanza kumfikia na kuanza kumpiga vibaya sana mpaka Willy akaanza kutoa damu puani.

"Wewe mwanaume gani, mpaka mwanaume mwenzako afungwe ndio umpige, si umfungue tuone nani mwanaume hapa, kati yako Jean na Willy", Bibiane alisema kwa dharau.

"Ngoja amalize hasira zake, huyu mshenzi hatufanyia mambo mabaya sana", Col. Gabatazi alidakia huku akisogea na kumchakaza Willy kwa makofi yaliyomfanya azirai tena.

"Basi inatosha, kabla hajala umeme nataka nimpe maneno yake. Nikimaliza kusema Kamanda Morris fanya kazi yako. Huyu tayari tumemhukumu kifo, na

atakufa si kwa risasi bali kwa umeme, kama wahalifu waliohukumiwa kunyongwa kule Marekani.

"Kufa si tatizo, kila mtu atakufa", Willy alisema baada ya kuzinduka na kuongeza, "Ila hata mkitumaliza leo, lakini hamfiki popote".

"Wewe ni mwehu, sisi tuna jeshi la kuikamata Rwanda chini ya wiki moja, unasema nini mwehu wewe, utapata habari utakapokuwa ahera", Col. Gatabazi alitamba.

"Wewe ndiye nani", Willy aliuliza.

"Mimi ndiye Col. Gatabazi".

"Nijulishe basi kwa wengine maana kata anayehukumiwa kifo hujui majaji waliomhukumu", Willy alihoji akiwa na maana ya kuvuta muda kama kuna njia nyingine ya kujiokoa aweze kufanya hivyo.

"Huyu hapa ni Anatoire Kabuga, ndiye kiongozi wa Akazu. Najua unafahamu Akazu ni nini. Wale rafiki zetu toka jeshi la Zaire. Anayeingiza ni Col. Marcel Bizimaziki, ambaye ni kamanda wa Akazu anayesaidiwa na huyu mzungu. Kamanda Morris kutoka kampuni ya kijeshi ya Afrika Kusini. Na waheshimiwa huyu ndiye adui yetu namba moja Willy Gamba, kutoka Tanzania lakini na yeye tuna habari kuwa kazi hii anaifanya kwa kukodishwa. Hivyo, hawakilishi msimamo wa Tanzania hata kidogo katika suala hili; yeye na Kamanda Morris hawana tofauti na huyu Bibiane ni msalti kama mnavyomjua. Niliwahi kumshawishi Jean kuwa karibu sana na mwanamke akajua siri zake ni balaa kwani wao fikira zao zinatoka chini na si juu kichwani. Si watu hawa, lakini hakunisikia, sasa ona madhara aliyotufanyia", Col. Gatabazi alilalamika.

"Kazi na dawa, bila kuwa karibu na mwanamke mzuri anayekupa mapenzi vizuri huwezi kufikiri sawasawa, usisahau Col. Gatabazi hata sisi tumenufaika sana na huyu kiupmbe, mimi binafsi nilikuwa na bahati ya kufaidi mwili wake hivyo usinionee wivu, ngoja nikafaidi mara ya mwisho", Jean alijibu. Akimuonyesha ishara askari aliyekuwa karibu amfungue kamba ili ampeleke chumbani. Willy sasa fahamu zake zilikuwa zimerudi na akili yake ilikuwa ikifanya kazi ya ziada namna ya kuponyoka toka ndani ya balaa hii.

Aliona azidi kununua muda kidogo wa kuomba.

"Huenda nimefanya yote haya bila kujua undani wa suala zima hili, kwa sababu kwa akili ya mtu yeyote haya mauaji mliyofanya na kuyatekeleza yanafanya akili

isikubali maana yalikuwa ya kikatili na kunyama. Kabla sijanyongwa naweza angalau kuelezwa sababu zilizowafanya mkatekeleza mauaji mabaya ya aina hii ambayo ni ya kipekee baada ya Dikteta Hitler?".

Wakati Willy anamuuliza Col. Gatabazi, Jean na Kamanda Morris walikuwana wananong'onezana na Kamanda Bizimaziki ili askari waondoke kuelekea mpakani. Willy, huku macho yakifunguka kwa shida kutokana na kipigo aliweza kuwaona jinsi wanavyonong'onezana na vilevile akaweza kuona jinsi Bibiane anavyofunguliwa kamba kutoka kwenye kiti na kupelekwa kwenye mlango uliokuwa ukielekea chumbani. Aida, alihisi Jean alikuwa anataka kufanya nini. Yote haya yalifanyika wakati Willy akiongeza kasi ya kuwaza jinsi ya kujinasua ili aweze kukamilisha kazi yake iliyomfikisha haba badala ya kukata tamaa.

Acha mimi nimjibu, wewe endelea na shughuli inayotusubiri, ambayo ni muhimu zaidi. Nimefurahi kuona kuwa huyu Willy anataka kujua sababu na sababu nitazitoa mimi", Anatoile Kabuga, Kiongozi wa Akazi, alijibu huku akiangalia saa yake iliyoonyesha kuwa ilikuwa saa nane na nusu usiku.

Meja Kasubuga alipigana vikali na jeshi la Luteni Nyamboma na kufanikiwa kuwazidi nguvu na hivyo askari wa jeshi hilo walilazimika kukimbilia mpakani. Luteni Nyamboma alikuwa amepoteza askari wengi sana, walipfika mpakani wakitegemea kumkuta Nkubana ili awaongezee nguvu ya askari warudi kuendeza mapambano, lakini hakumkuta Nkubana. Hivyo, Luteni Nyamboma akaamua kuelekea Kibumba na masalia ya askari wa kikosi chake waliobaki. Luteni Nyamboma alipoangalia saa yake ilikuwa saa nane usiku. Walitumia magari waliyoyakuta pale mpakani, Luteni Nyambona na askari wake waliondoka kuelekea Kibumba.

Hata hivyo, Luteni Nyamboma alilazimika kuwaacha askari wa jeshi la Zaire pale mpakani kwa ajili ya ulinzi ili baada ya kazi ya Gisenyi Luteni Nyamboma awafuiate Kibumba.

Meja Kasubuga alipofika mpakani aliyaona magari yanaondoka kasi eneo la mpakani. Meja Kasubuga akagundua kuwa magari yale yalikuwa yakielekea Kibumba. Asingekuwa ameamriwa na Col. Rwivanga awasubiri pale mpakani hakika Meja Kasubuga angeyafuata magari yaliyoondoka na kikosi kile. Baada ya kufika mpakani, jeshi la Meja Kasubuga lilifanikiwa kukitwaa kikosi cha jeshi la Zaire kilichokuwa kikiwasaida wanajeshi la Intarahamwe na hii ikawa ngome ya jeshi lake kwa muda.

Kikosi hiki kilichokuwa mpakani mwa Zaire na Rwanda kilikuwa kimejijenga vizuri kivita, kikiwasaidia wanajeshi wa Intarahamwe na kundi la Akazu lililokuwa likifanya jitihada ya kuivamia serikali ya RPF ili kutwaa madaraka ya kuiongoza Rwanda kijeshi.

Baada ya kuhakikisha usalama wa eneo hili, Meja Kasubuga alielekea sehemu iliyoandaliwa, ambayo Col. Rwivanga alimweleza kuwa angetua hapo kwa Helikopta akiwa na kiongozi wa kikundi cha Banyamulenge na kiongozi wa vikosi vya vyama vinavyoipinga serikali ya Zaire. Meja Kasubuga alipoangalia saa yake ilikuwa saa nane na dakika kumi. Muda ambao Col. Rwivanga aliahidi kuwa atafika Gisenyi. Hivyo, Meja Kasubuga na kikosi chake wakaamua kusubiri.

Col. Rwivanga alikuwa na matumaini makubwa na kikosi cha Meja Kasubuga, hivyo baada ya kuondoka Kigali kwa Helikopta ya jeshi, walisafiri moja kwa moja usiku huo kuelekea Gisenyi. Col. Rwivanga hakuwa na papala wakati wote alikuwa akitafakari jambo kabla ya kulifanyia kazi. Alikuwa mmoja wa maofisa wa jeshi walioheshimiwa na kutegemewa sana na serikali ya Rwanda. Alikuwa mtu mwadilifu asiyependa kuisalti nchi yake, kutokana na msimamo wake dhabiti aliogopwa sana na vibaraka hususan wanaotaka kuigawa Afrika.

Alikuwa akijitosheleza kiulinzi, kutokana na hali hiyo nyumba yake haikuwekewa ulinzi kutoka jeshini, kama ilivyo kwa maofisa wengine wa ngazi za juu kama yeye. Alikuwa mmoja wa makomandoo wa jeshi waliofuzu vizuri mafunzo yake, lakini kutokana na cheo chake jeshini alibaki kuwa ofisa wa jeshi aliyeheshimiwa sana. Alikuwa mpole asiyependa makuu, alikuwa na subira, hata ukimchoma kidole machoni hatakufanya kitu. Lakini akilazimika kuchukuzwa na upuuzi alifanya kitu ambacho hakuna awezaye kuamini, hakuwa na mchezo tena. Huyo ndiye Col. Thomas Rwivanga, Afisa wa jeshi mwandamizi.

Anatoile Kabuga alimwangalia Willy kwa jicho baya sana, alimuona kuwa ndiye kikwazo na adui wao namba moja kwa kuwachelewesha Inyenzi na washirika wao kushika madaraka ya nchi ya Rwanda. Hata hivyo aliamini kuwa hakuna mtu mwingine zaidi ya Willy atakayeweza kupena na kuingia katika ngome yao.

"Nitakupa historia kidogo", Anatoile Kabuga alianza kumweleza Willy Gamba. "Willy Gamba, lazima ufahamu kuwa sehemu hii ya Maziwa Makuu katika Afrika watu wa kwanza wa asili ni wabantu. Wabantu ndio walioishi eneo hili la Maziwa Makuu kwa karne nyingi sana tena wakiishi kwa raha mstarehe bila migogoro wala matatizo mpaka walipokuja watu wenye asili ya Kihemetiki ambao baada ya kufika eneo hili walianza kuleta chokocoko, vita wakitokea Kaskazini na

Mashariki mwa Afrika. Kwa ufupi, Watutsi wamo kwenye kundi hilo. Tangu wafike katika sehemu hii amani imekosekana kabisa. Karne mbili zilizopita walianza kuweka Ufalme wao katika eneo hili baada ya vita vikali na wabantu wa sehemu hii na kuwashinda. Waliweka wafalme wao waliowaita wafalme wa Kihima ambao walitawala kutoka Bahari ya Hindi mpaka Atlantiki, sehemu ambayo sasa ni Zaire, Rwanda, Burundi, Tanzania, Uganda na Kenya", alinyamaza kidogo kisha akaendelea.

"Willy Gamba. Nitakueleza kwa kifupi sana maana hatuna muda wa kupoteza. Lakini kwa sababu wao walikuwa wachache na wakawa wanaendeleza utawala wa mabavu na unyanyasaji kwa wabantu ambao ndio waliokuwa wengi, hali inayoendelea mpaka sasa, mapigano ya kuukataa utawala huo yaliendelea sehemu zote, hatmaye ufalme huo ukaangushwa katika sehemu zingine na kubaki sehemu ambayo sasa ni Rwanda na Buurundi. Na hali hii iliendelea mpaka wakati wa Ukoloni ambapo katika Rwanda utawala wa ukandamizazi wa Watutsi dhidi ya Wahutu na wabantu ambao ndio wengi katika Rwanda, uliendelea. Miaka yote hii mpaka vita vya pili vya dunia Watutsi wachache waliendelea kutawala na kuwanyanyasa Wahutu wakihakikisha kuwa hawapati elimu, madaraka na hata mali. Ni mpaka juzi tu, mwaka 1957, Wahutu walipojikomboa na kushika madaraka, na hawa Inyenzi wakakimbilia nchi jirani ikiwemo Tanzania. Wakati wa utawala wetu tulijaribu sana kuwaweka karibu lakini siyo wote waliotaka kutawaliwa na walio wengi sababu wao walijiona wana hadhi ya juu kuliko sisi. Vilevile, waliapa kuwa lazima watatafuta njia mbadala warudi kututawala maana sisi ni watumwa wao. Na kwa taarifa yako kila Mtutsi anamuona kila Mbatu kama mtumwa wake. Ndivyo wanavyokuona wewe hata kama unawasaidia kwa sababu wewe ni Mbantu na ndivyo wanavyoniona hata mimi. Sasa basi tatizo kubwa lilikuja wakati nchi jirani ilipopata kiongozi mwenye asili hiyohiyo ya Kitutsi, na akawa na nguvu na akaahidi kuwasaidia Wahutu ili wautoe utawala wa wabantu katika Rwanda, Yaani watu wenye asili ya Kitutsi tu ndio watawale sehemu hii ya maziwa makuu ikiwemo Zaire, Rwanda, Burundi, Tanzania, Uganda na Kenya. Sisi tulipopata habari hizi tukajua eneo lote hili la maziwa makuu halitapata amani ikiwa hawa Watutsi wanazidi kuzaliana na kuwa wengi eneo hili. Njia pekee ya kuleta amani ni kuhakikisha mmewaua waume, wake kwa watoto, ili kuua kabisa nguvu yao. Leo hawa tusipowaangamiza nakueleza wewe Willy Gamba, Tanzania haitakuwa na amani na wala Zaire, Uganda na Kenya hawana amani maana hawa wana asili ya kujipanua. Ni watu hatari ajabu, na kama mngejuwa kuwa hawa ni watu wa kuteketezwa kabisa hata mmoja asionekane katika sehemu hii".

"Ngoja nikukata kauli, umesema watu wengi katika eneo hili la maziwa makuu ni wabantu, hawa Watutsi wachache watatawala vipi", Willy aliuliza huku akisogeza vidole vya mkono wake wa kulia kujaribu kama vingeweza kuifikia saa yake aliyovaa mkono wa kushoto.

"Unasema nini, tunavyozungumza nani anatawala Rwanda, Burundi na Uganda, watu wengi katika nchi hizi ni watu gani, sisi wabantu, sasa nini kitawashinda kutawala Zaire, Tanzania na Kenya kama wameweza katika nchi hizo, njia pekee ni kuwateketeza ili waishe, wasiendelee kutunyanyasa na kuleta vita vya mara kwa mara katika eneo letu. Hawa na Wayahudi hawana tofauti. Ngoja nikwambie Willy Gamba, hawa Watutsi hata kama ukiona Mtutsi amezaa na wewe lazima atatembea na Mtutsi mwenzie ili azae Mtutsi, kazi yako wewe itakuwa ni kukuza damu isiyokuwa yako. Na wamehakikisha wanawake wao wamesambaa dunia nzima, lakini kila mwanamke wa Kitutsi ahakikishe mahali alipo anapewa mimba na Mtutsi mwenzie tu. Huku wanawake wao kusambaa ni njia mojawapo ya kujipanua ili waweze kufanya kampeni yao kwa kuhurumiwa na mataifa mengine. Hivyo, mauaji haya tuliyofanya ni kwa niaba ya wabantu wote na sasa hivi tuko tayari kuurudisha utawala wetu Rwanda na Burundi ili heshima ya mbantu katika eneo hili ipatikane. Baada ya kuichukua tena Rwanda mara hii tutataka viongozi wote katika eneo hili waelewe ukweli huo na watuunge mkono kuwatokomeza Watutsi hawa. Vinginevyo nakwambia Willy Gamba watatawala tena sehemu yote hii, la sivyo hakuna amani katika eneo hili. Vita vitaendelea kwa miaka mingi. Sisi Akazu ndio tumaini pekee la sehemu hii, bila sisi kesho tawala zote za sehemu hii zinazotawaliwa na wabantu zitatikiswa na kumalizwa. Hivyo, wewe Willy ni msaliti, unawasalti wabantu kwa kuwasaidia Inyenzi ili waweze kutawala ardhi halali ya wabantu. ndio sababu tumekuhukumu kifo. Na, wote wawe wabantu au taifa lingine, wakibainika wanasaidia Inyenzi lazima wauawe. Na sasa wewe utauawa ili Akazu ifanye kazi yake ya kuwakomboa wabantu", Kabuga alisema kwa sauti nzito iliyoashiria hasira ya ajabu ambayo kila mtu pale ndani alihisi kapagawa.

"Yote hayo uliyoyasema yanaweza kuwa na ukweli mwingi tu, lakini ukweli huwa hautoi uhalali wa kuangamiza kabila zima. Hii ni kinyume na haki za binadamu. Njia nyingine itafutwe kuwadhiti na si kuwaangamiza", Willy alijibu huku kidole chake cha karibu na gumba kwenye mkono wa kulia kikiwa kimefika kwenye ufunguo wa saa yake na kukandamiza ufunguo wa saa na kusubiri kuona kifo chake ama kifo cha jeshi la Akazu.

"Unasema haki za binadamu, sisi wabantu hatuna haki mbona...........", Kabuga hakumaliza sentensi yake teknolojia ilianza kufanya kazi yake.

Col. Rwivanga, Mpinda na Meja Tom Kabalisa waliwasili mpakani mwa nchi za Rwanda na Zaire katika sehemu waliyokuwa wamekubaliana na Meja Kasubuga mnamo saa nane na dakika arobaini usiku.

Hali ya usalama ilikuwa imeimalishwa katika eneo hili, ambapo vijana wa Meja Kasubuga walikuwa makini kwa kila jambo, baada ya Helikopta ya jeshi la Rwanda waliyosafiri hadi mpakani kutua, Col. Rwivanga alikuwa wa kwanza kushuka akifuatiwa na Mpinda, kasha Meja Kabalisa.

"Mambo yakoje hapa", Col. Rwivanga alimuuliza Meja kasubuga wakati wakisalimiana baada ya heshima ya kijeshi.

Meja Kasubuga alieleza kwa urefu jinsi mapambano yalivyokuwa, kisha akamalizia, "Huyu Willy atakuwa kauawa kule Kibumba maana kajipeleka mahali ambapo panatakiwa vikosi vyote husika, huyu Willy ingawaje Afande unamsema ni hatari lakini hana akili ya tahadhari, angesubiri twende wote, ndipo angeweza kuwa msaada kwetu maana maiti haina msaada wowote.

"Nakubaliana na wewe lakini yule ni mtu mwenye maisha mengi, unaweza kumuona kaibuka", Col. Rwinga alisema wote wakacheka kwa utani huo.

"Kweli, akiibuka tena atakuwa mtu wa maisha mengi", Meja Tom Kabalisa wa Banyamulenge alijibu kwani na yeye alijua nguvu za Intarahamwe kule Kibumba na ndio sababu alikuwa hajathubutu kufanya lolote. Kisha akaendelea. "Col. Rwivanga, nafikiri sasa tumweleze Meja Kasubuga mipango ikoje ili....", Kabla Meja Kabalisa hajamaliza kusema sentesi yake, mripuko mkubwa usio kifani ulisikika mpaka huko walikokuwa.

"Ooh Willy Gamba, kweli u-hatari", Meja Kasubuga aligwaya.

Wakati huo Jean alikuwa ameanza kumvua nguo Bibiane ili atimize ahadi yake kama alivyoahidi kuwa atafanya nae mapenzi kabla ya kumuua, wakati akikaribia kutimiza ahadi yake, ghafla mlipuko mkubwa ulitokea eneo hilo na kuleta hofu, palepale nyumba ile ikasambaratika vipande. Bahati nzuri nyumba hii ilikuwa imetengenezwa kwa mbao tupu ili likitokea tatizo kama hili Kamanda Morris asihatarishe maisha yake.

Kwa vile Bibiane alikuwa akiutegemea mlipuko kama huo, ulipotokea tu hakuzirai kama wengine. Alizitupa mbao zilizomwangukia mwilini mwake, akainuka na

kuanza kumsaka Willy ambaye wakati huo alikuwa amefungwa kwenye kiti pale ukumbini. Kumbe mlipuko ulipotokea kile kiti kilirushwa pamoja na Willy Gamba mpaka nje kwenye bustani. Bibiane aliangalia huku na huko kwa tahadhari kubwa, maana watu wote walikuwa wamelala chini kwa hofu. Vilio vilisikika eneo lote la kambi hii mara akamuona Willy Gamba na kiti chake akiwa nusu amezirai.

Milipuko ile iliendelea kuleta hofu na kusababisha mwanga mkubwa katika eneo lote. Milio na mwanga ilionekana na kusikika mpaka Goma, Gisenyi na sehemu nyingine kwani sasa mizinga na makombora nayo nayo yalianza kulipuka bila mpangilio na kusababisha Jean na wenzake kupatwa na taharuki. Bibiane alitoa kisu chake kidogo alichokuwa amekifika kwenye nywele zake, akiwa tayari kabisa kummaliza Jean. Na kwa kutumia hiki kisu alifanikiwa kuzikata kamba alizokuwa amefungwa Willy Gamba kisha akamtingisha hadi Willy akapata fahamu. Baada ya Willy kuzinduka Bibiane akamshika mkono. Willy alisimama wakakimbia kuelekea sehemu ile ya Magharibi ya kambi mahali ambapo kulikuwa na mstu mkubwa.

Walipokimbia kama mita hamsini hivi Bibiane alitoa bomu la kurusha kwa mkono akalitupa kwenye ile nyuma kisha wakajitupa chini. Bomu hilo liliporipuka likasambaratisha eneo hilo halikubakiza mtu wala kitu kilichokuwa ndani ya nyumba hii au mita thelathini kuzunguka nyumba hii. Wakati wanaelekea kwenye ule mstu mabomu, mizinga na makombora yaliyokuwa ndani ya maghala makubwa ya kuhifadhia silaha yaliendelea kuripuka yenyewe.

"Kazi ipo Willy, wamelikoroga acha walinywe sasa", Bibiane alisema kwa kebehi.

"Kazi yenyewe si kidogo, wamelala matajiri wataamka masikini", Willy alijibu wakiwa wemeingia kwenye msitu.

"Naona sasa tumechoka, kazi hii inatosha kabisa kwa siku moja ya leo", Willy alieleza wakiwa wametokeza kwenye sehemu ya majani mazuri chini ya mbaramwezi. "Hapa panafaa kupuzika,  au vipi", Willy aliuliza.

"Hapa tumetafutiwa na Mwenyezi Mungu ili tupumzike baada ya hii kasheshe. Nilikuwa natamani ufike muda nipate mahali ambapo dunia itakuwa mimi na wewe tu. Na mahali hapo ni hapa, yaani mimi, wewe, mbaramwezi, nyota, malaika na Mungu", Bibiane alieleza.

Willy alivua gwanda lake la juu akatandika chini kwenye majani, Bibiane akavua pia na kusema. "Hili tutajifunika".

Willy akamwinua na kumbeba mikononi kisha akambusu na kumlaza juu ya gwanda lake.

KAMPALA

JKS aliamka mapema asubuhi huku roho yake ikiwa na furaha nyingi sana. Sasa hivi alikuwa akielekea benki kwa ajili ya kuchukua pesa zake. Hisia za urais wa Tanzania zilimjia katika mawazo yake, akatamani kuwa kiongozi wa Tanzania ili atimize ndoto yake ya kuwa mheshimiwa rais wa Tanzania.

Baada ya kustafutahi kwa chai nzito, alipiga simu kwenye benki yake hapo Geneva na kuuliza mahali ilipo. Baada ya kupata maelekezo sehemu na mtaa ambao benki ipo, alipiga simu mapokezi na kumuomba mhudumu amletee teksi saa tatu kamili ili impeleke benki.

Baada ya kujiweka sawa, alitelemka chini taratibu ilikuwa majira ya saa tatu kamili, akiwa amebeba mkoba wake wa ngozi ya mamba mkononi aliokuwa amepewa kama zawadi na rafiki yake Jean.

Alipofika chini alikuta teksi inamsubiri mbele ya hoteli. Alifungua mlango wa nyuma kama VIP akaingia, akampa dereva anuani ya benki, baada ya kuthibitisha ni eneo gari dereva aliondoa gari huku mawazo ya JKS yakiwa juu ya baraza lake la mawaziri baada ya kuukwaa  urais.

Jean alikuwa amempa jina la meneja wa benki na kumweleza kuwa akifika benki amwone meneja huyo. Alipofika benki alitelemka na kumwambia mwenye teksi amsubiri akaingia ndani ya benki na kuelekea mapokezi. alimwonyesha yule msichana wa mapokezi jina la meneja. Asubuhi ile meneja alikuwa bado hana watu wengi, hivyo akamkaribisha vizuri sana.

"Karibu Mheshimiwa, nikusaidie nini?", meneja wa benki aliuliza JKS baada ya kuingia ofisini kwake.

"Asante", JKS alijibu na kutoa bahasha yenye maelezo yake yote. Meneja aliipokea kwa tabasmu na kuifungua bahasha na kuanza kusoma. Alivuta Kompyuta yake na kuanza kushughulika. Meneja, akiwa anatabasamu tena alimgeukia JKS na kumweleza, "Samahani, hii akaunti imefungwa jana na aliyeifunga ametoa pesa zote na kusema mtu yeyote akifika hapa kuuliza juu ya akaunti mwenye kitambulisho namba hii, aelezwe kuwa akaunti hiyo imefungwa maana mkataba umeisha. Samahani sana mheshimiwa, nina wateja wengine wananisubiri".

JKS alichanganyikiwa. Aliinuka, mara akamuona yule meneja wa benki anakuwa mkubwa zaidi na yeye JKS anakuwa mdogo na chumba kinazidi kuwa kidogo, akasikia anakosa pumzi halafu giza nene likamuingia mara akaanguka chini na kupoteza fahamu.

Ilikuwa yapata saa moja asubuhi Willy aliposhituka kutoka usingizini baada ya kuota ndoto mbaya ya vita ambayo aliota Bibiane akipigwa risasi sita kifuani na kupoteza maisha, alipotaka kupiga kelele alishituka kutoka usingizini, akamwona Bibiane amemlalia kifuani wakiwa kitandani akakumbuka kuwa kumbe walikuwa Hoteli ya Sheraton, iliyoko mjini Kampala, baada ya kuletwa hapa jana jioni kwa ndege ya serikali ya Rwanda baada ya kuchukuliwa na helikopita ya jeshi ya akina Col. Rwivanga kutoka kule porini Kibumba walikolala baada ya usiku wa kasheshe walipofanikiwa kuiteketeza ngome ya Akazu. Taratibu Willy alimwondoa Bibiane kwenye kifua chake na kumlaza kwenye mto. Alichukua chombo cha kuwashia televisheni ili kusikia taarifa ya habari ya saa moja.

Baada ya kuwasha televisheni mtangazaji alisoma taarifa ifuatayo.

"Zaire. Vikosi vya wapinzani wa serikali ya Zaire, vikiongozwa na mpinzani mkuu Bwana Mpinda vimeanzisha mapigano makali dhidi ya serikali hiyo vikisaidiwa na vikosi vya waasi wa kabila la Banyamulenge vikiongozwa na Meja Tom Kabalisa Mubanyamulenge, aliyeasi kutoka jeshi la Zaire. Bwana Mpinda amekaririwa na vyombo vya habari kuwa nia yao ni kuuondoa utawala wa kidikteta wa serikali iliyoko madarakani Kinshansa. Wamejigamba wakisema usiku wa kuamkia jana walishambulia kambi kubwa ya kivita iliyoko Kibumba, karibu na Goma na kuteketeza silaha nyingi, vikiwemo vifaru, ndege za kivita, mizinga mkibwa na midogo na kuua askari wapatao elfu kumi".

"Pamoja na kwamba habari hizi hazijathibitishwa na vyombo vingine vya habari vya ndani na nje, raia wa sehemu hiyo wamethibitisha kutokea kwa milipuko mkubwa ya ajabu ambayo hawajawahi kuisikia katika kambi hiyo. Na wanasema wanajeshi karibu wote na silaha zilizokuwa kwenye kambi hiyo zimeteketezwa kwa milipuko hiyo iliyosikika mpaka Gisenyi na Goma".

"Habari zilizotufikia hivi punde katika chumba chetu cha habari zinasema waasi tayari wamekamata miji wa Goma na Bukavu na bado wanasonga mbele kuchukua maeneo mengine. Vilevile, kuna habari ambazo hazijathibitishwa kuwa vikosi hivyo vya wapinzani vinasaidiwa na vikosi vya jeshi la RPF la Rwanda".

"Hii ina maana kuwa wapinzani wamekusudia kuung'oa utawala wa sasa ambao umedumu madarakani kwa zaidi ya miaka thelethini sasa ambao wameupachika jina kuwa utawala wa mabavu, unyanyasaji uliojaa rushwa na udikteta. Bado hakuna taarifa yoyote ya kukanusha habari hizo kutoka kwa serikali ya Zaire, mji Kinshansa".

"Na huko Jijini Dar es Salaam, Tanzania kuna habari kuwa waziri wa ngazi ya juu nchini humo kwa jina maarufu la JKS amefariki dunia akiwa katika benki moja huko Geneva, Uswisi baada ya kupatwa na shinikizo la damu. Kiongozi huyo aliondoka nchini Tanzania siku mbili zilizopita na kuelekea London kwa ajili ya matibabu ya moyo, bado haijabainika kwa nini alikwenda Geneva, na alifuata nini kwenye benki hiyo. Waziri huyo ndiye aliyekuwa akitegemewa kuwania urais wa Tanzania baada ya rais wa sasa kumaliza muda wake".

Willy alitabasamu baada ya taarifa hii iliyonoga. Kisha, akachukua simu na kumpigia Mzee Musoke na kumwomba waonane mchana kama walivyokuwa wamepanga wakati akiwa mjini Kigali ili ampatie ripoti ya kazi yake aliyoifanya kwa mafanikio.

"Nimefarijika kusikia kazi yako kwenye taarifa ya habari ya asubuhi hii, wewe ni mwanaume wa shoka", Musoke alimsifu Willy.

"Asante mzee, tutaonana hiyo saa nane", Willy alimjibu Musoke na kukata simu. Kisha akapiga simu nyingine.

"Pepe mpenzi".

"Uko wapi", Pepe aliuliza.

""Niko Kampala narudi kesho".

"Ooh Mungu wangu, toka umeondoka sijapata usingizi. Njoo mume wangu nina hamu sana na wewe, nakupenda sana".

"Na mimi zaidi, kesho mama, kwaheri", Willy akakata simu.

Bibiane alikuwa akisikia lakini alijifanya kama hamsikii alimgeukia Willy na kusema. "Uko wapi Willy?, njoo ulale, najua siku yangu ni leo tu, hivyo lazima niitumie siku hii kikamilifu".

"Katika nafsi yangu hupenda mtu anayeelewa mambo kama wewe", Willy alijibu huku akirudi ndani ya shuka na kumkumbatia Bibiane.

# MWISHO